**Disclaimer : Ministry of Finance and Planning repository shall be regarded as a publisher and bears no liability for any damage upon using contents of the repository.**

National Economic Survey The Economic Survey

1987

# Hali ya Uchumi wa Taifa,1987

## Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Wizara ya Fedha

https://repository.mof.go.tz/handle/123456789/734
*Downloaded from Ministry of Finance and Planning Repository*

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# *Hali ya Uchumi wa Taifa Katika Mwaka 1987*

Juni, 1988
*Kimetolewa na:* WIZARA YA FEDHA, UCHUMI NA MIPANGO DAR ES SALAAM—TANZANIA

1988
KIMEPIGWA CHAPA NA MPIGACHAPA WA SERIKALI
DAR ES SALAAM—TANZANIA

*Bei Sh. 130/-*

*Hali ya Uchumi wa Taifa*
*Katika Mwaka*
*1987*

# YALIYOMO


UKURASA

ORODHA YA MAJEDWALI ........ iv

SURA YA I—Hali ya Uchumi kwa Jumla ........ 1

SURA YA II—Maendeleo Muhimu katika Uchumi ........ 8

1. Pato la Taifa ........ 8
2. Ukuzaji wa Rasilimali ........ 16
3. Biashara na Hali ya Malipo na Nchi za Nje ........ 21
4. Maelekeo ya Fedha za Serikali ........ 35
5. Fedha, Mabenki na Mashirika Mengine ya Fedha ........ 39
6. Uajiri, Mishahara na Bei ........ 55
7. Mashirika ya Umma ........ 67
8. Sayansi na Teknolojia ........ 71
9. Idadi ya Watu Nchini ........ 76
10. Hali ya Uchumi Duniani na Ushirikiano wa Kiuchumi wa Kimataifa ........ 78

SURA YA III—Maendeleo katika Sekta Mbalimbali

1. Kilimo na Mifugo ........ 87
2. Maliasili na Mazingira ........ 106
3. Madini ........ 114
4. Viwanda ........ 118
5. Biashara ya Ndani na Utalii ........ 127
6. Ujenzi, Ardhi na Maendeleo ya Nyumba ........ 133
7. Usafirishaji na Mawasiliano ........ 137
8. Maji na Nishati ........ 155
9. Elimu ........ 160
10. Afya ........ 166
11. Kazi na Ustawi wa Jamii ........ 172
12. Maendeleo Vijijini ........ 180

## ORODHA YA MAJEDWALI


*Jedwali Na.* *Ukurasa*

A. Takwimu muhimu katika Uchumi ..... 7
1. Pato la Taifa (GDP) kisekta kwa gharama zake (Bei za miaka inayohusika) ..... 12
2. Jumla ya Pato la Taifa (GDP) kisekta kwa gharama zake (Bei za miaka inayohusika—Asilimia) ..... 13
3. Jumla ya Pato la Taifa (GDP) kisekta kwa gharama zake (Bei za mwaka 1976) ..... 14
4. Jumla ya Pato la Taifa (GDP) kisekta kwa gharama zake (Bei za mwaka 1976—Asilimia) ..... 15
5. Ukuzaji wa Rasilimali (Bei za miaka inayohusika) ..... 18
6. Ukuzaji wa Rasilimali (Bei za mwaka 1976) ..... 19
7. Uzalishaji wa Rasilimali: Sekta ya Binafsi na ya Umma ..... 20
8. Thamani ya Biashara baina ya Tanzania na Nchi Nyingine ..... 25
9. Aina za Bidhaa zilizoagizwa toka Nchi za Nje ..... 26
10. Mizania ya Malipo na Nchi za Nje ..... 27
11. Aina na Thamani ya Bidhaa zilizoagizwa kutoka Nje ..... 28
12. Thamani ya Bidhaa zilizoagizwa kutoka nchi zilizotajwa ..... 29
13. Thamani ya Bidhaa zilizopelekwa kwa nchi zilizotajwa ..... 30
14. Biashara kati ya Tanzania na Nchi za Soko Nafuu za Mashariki na Kusini mwa Afrika ..... 31
15. Kiasi na Thamani ya Bidhaa muhimu zilizouzwa Nchi za Nje ..... 32
16. Bei za Bidhaa muhimu zilizouzwa Nchi za Nje ..... 33
17. Fahirisi ya Bei za Bidhaa muhimu zilizouzwa Nchi za Nje ..... 34
18. Mwenendo wa Mapato na Matumizi ya Serikali ..... 37
19. Mgawanyo wa Huduma za Serikali ..... 38
20. Hali ya Fedha kwa Jumla: katika Mwaka 1984—1988 (Tanzania Bara) ..... 50
21. Benki ya Taifa ya Biashara: Amana na Karadha ..... 51
22. Benki ya Taifa ya Biashara: Mikopo kufuatana na Sekta za Uchumi ..... 52
23. Benki ya Ushirika na Maendeleo Vijijini—Mgawanyo wa Mikopo ..... 53
24. Shirika la Akiba ya Taifa ya Wafanyakazi ..... 54
25. Uajiri na Mishahara katika sekta mbali mbali za Uchumi: 1984—1987 (Tanzania Bara) ..... 57
26. Uajiri na Mishahara katika Mikoa: 1984—1987 (Tanzania Bara) ..... 58
27. Fahirisi ya Bei za Rejareja ya Bidhaa zitumiwazo na watu wa Kipato cha Chini, Dar es Salaam (1977 = 100) ..... 59

*Jedwali Na.* *Ukurasa*

28. Fahirisi ya Bei za Bidhaa na Huduma zitumiwazo na Wafanyakazi wa Kima cha Kati, Dar es Salaam (1977 = 100) ........ 60
28A. Fahirisi ya Bidhaa na Huduma zitumiwazo na Wafanyakazi wa Kima cha Kati, Dar es Salaam (1977 = 100) ........ 61
29. Fahirisi ya Gharama ya Maisha ya Wenye Kipato cha Juu, Dar es Salaam (1977 = 100) ........ 62
30. Fahirisi ya Gharama ya Maisha ya Wenye Kipato cha Juu, Dar es Salaam (1977 = 100) ........ 63
31. Fahirisi ya Bei za Bidhaa na Huduma zitumiwazo na Wakazi wa Mijini—Tanzania Bara (1977 = 100) ........ 64
32. Fahirisi ya Bei ya Bidhaa na Huduma zitumiwazo na Wakazi wa Mijini—Tanzania Bara (1977 = 100) ........ 65
33. Fahirisi mbali mbali za Bidhaa na Huduma zitumiwazo na Wakazi wa Mijini—Tanzania Bara (1977 = 100) ........ 66
34. Vipimo mbali mbali vya mafanikio ya Mashirika ya Umma ........ 69
35. Muhtasari wa takwimu za Mashirika ya Umma ........ 70
36. Uzalishaji wa Miwa na Sukari Nchini ........ 95
37. Pamba iliyonunuliwa na Mauzo Nchini ........ 96
38. Eneo lililopandwa michai na majani mabichi yaliyopatikana ........ 97
39. Kahawa iliyonunuliwa na Mauzo Nchini ........ 98
40. Eneo lililopandwa Mkonge na Katani iliyopatikana ........ 99
41. Tumbaku iliyonunuliwa na Mauzo Nchini ........ 100
42. Maua ya Pareto yaliyonunuliwa na Mauzo ya Bidhaa za Pareto Nchini ........ 101
43. Korosho zilizonunuliwa na Mauzo Nchini ........ 102
44. Muhtasari wa Mazao muhimu ya Biashara yaliyonunuliwa . 103
45. Mazao muhimu ya chakula yaliyonunuliwa na Shirika la Taifa la Usagishaji ........ 104
45A. Kiasi cha mazao ya Mbegu za Mafuta na Iliki kilichonunuliwa na GAPEX ........ 105
46. Upandaji Miti (Hekta) ........ 111
46A. Shirika la Mbao Tanzania (TWICO)—Uzalishaji ........ 112
46B. Shirika la Mbao Tanzania (TWICO)—Mauzo ........ 113
47. Uchimbaji wa Madini: Kiasi kilichopatikana ........ 116
48. Madini yaliyouzwa ........ 117
49. Matumizi ya Saruji Nchini ........ 121
50. Uzalishaji wa Baadhi ya Bidhaa za Viwanda ........ 122
51. Idadi ya Watu walioajiriwa ........ 123
51A. Viwanda: Gharama za Kazi ........ 124
52. Viwanda: Muhtasari wa Matokeo ........ 125

*Jedwali Na.* *Ukurasa*


52A. Viwanda: Muhtasari wa Matokeo Kimkoa .................... 126
53. Idadi ya Watalii, Siku zao Hotelini na Makadirio ya Fedha za Kigeni zilizopatikana .................... 129
54. Safari katika Mbuga za Wanyama .................... 130
55. Nafasi katika Hoteli na Matumizi yake .................... 131
56. Idadi ya Watalii na siku za kulala wageni .................... 132
57. Huduma za Usafiri Dar es Salaam .................... 144
58. Kampuni ya Mabasi ya Taifa (KAMATA) .................... 144
59. Shirika la Reli Tanzania .................... 145
59A. Reli ya Uhuru—TAZARA .................... 146
60. Usafirishaji kwa Meli .................... 147
61. Huduma za Posta .................... 151
61A. Huduma za Simu .................... 152
61B. Huduma za Simu .................... 153
52. Shirika la Ndege Tanzania .................... 154
63. Uwezo wa Mitambo ya Umeme .................... 157
64. Uuzaji wa Nguvu za Umeme .................... 158
65. Uuzaji wa Umeme kwa Watumiaji mbali mbali .................... 159
66. Shule za Sekondari za Serikali: Idadi ya Wanafunzi kwa Vidato .................... 162
66A. Shule za Sekondari za Binafsi: Idadi ya Wanafunzi kwa Vidato .................... 163
67. Wanafunzi Watanzania katika Vyuo Vikuu vya Dar es Salaam na Sokoine .................... 164
68. Muhtasari wa Takwimu za Elimu .................... 165
69. Vyombo vya Afya Nchini .................... 168
70. Waliofaulu Mafunzo .................... 169
71. Matumizi ya Vyombo vya Afya: Idadi ya Wagonjwa .................... 170
72. Idadi ya Wafanyakazi wa Afya .................... 171

A. Kiwango cha kujitosheleza Kiutalaam na Kujitegemea Kiutalaam .................... 175
B. Mchanganyo wa Utaalam (Skill Mix) .................... 176
C. Makadirio ya Mahitaji ya Watumishi 1987—1991 .................... 176

# SURA YA I

## HALI YA UCHUMI KWA JUMLA

Katika mwaka 1987, hali ya uchumi wa taifa haikuwa tofauti sana na ilivyokuwa katika mwaka 1986. Uzalishaji kwa jumla uliongezeka zaidi kidogo na japokuwa bei kwa wastani ziliendelea kuwa za juu, upatikanaji wa bidhaa muhimu uliendelea kuwa nafuu ingawaje upungufu wa baadhi ya bidhaa bado uliendelea. Upande wa huduma muhimu, upungufu uliendelea kutokana na uhaba wa vifaa vya kutolea huduma na pia upanukaji wa haraka wa mahitaji ya huduma zenyewe kutokana na ongezeko la haraka la idadi ya watu.

**Pato la Taifa:**

2. Ongezeko la uzalishaji katika mwaka 1987 limedhihirishwa na matokeo yake katika Pato la Taifa halisi lililoongezeka kwa asilimia 3·9 (kwa bei za mwaka 1976) ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 3·6 mwaka 1986. Huu ni mwaka wa pili mfululizo ambapo pato la wastani la Mtanzania (per capita income) limeongezeka licha ya ongezeko la wastani la idadi ya watu la asilimia 3·3 kwa mwaka. Sekta zote isipokuwa madini ziliongeza mchango wake katika Pato la Taifa. Mwenendo huo umeonyesha dhahiri kuwa hatua zilizochukuliwa katika Mpango wa Kufufua Uchumi zimeanza kuleta mafanikio. Hata hivyo ni dhahiri kuwa juhudi zaidi zinahitajiwa ili kufikia lengo la ukuaji wa Pato la Taifa la wastani wa asilimia 4·5 la Mpango wa Kufufua Uchumi na pia ukuaji wa asilimia 5 katika kipindi cha Mpango wa Miaka Mitano unaoanza hapo Julai 1988.

**Ukuzaji wa Rasilimali:**

3. Kulikuwepo upungufu wa Sh. 400 milioni, au asilimia 5·3 (kwa bei za mwaka 1976) katika ukuzaji wa rasilimali kwa jumla mwaka 1987 kwa kulinganisha na upungufu Sh. 49 milioni, au asilimia 0·6 uliotokea mwaka 1986. Kushuka kwa ukuzaji wa rasilimali mwaka 1986 kulisababishwa na upungufu katika vifaa na shughuli za ujenzi mbali na majengo. Kwa upande wa majengo, unafuu katika upatikanaji wa zana za ujenzi, zikiwemo saruji na vyuma ndio uliosababisha ongezeko la mwaka 1987. Vifaa vya usafiri, mitambo na vifaa vingine vilikuwa na upungufu wa Sh. 451 milioni, au asilimia 8·8, mwaka 1987 hasa kutokana na upungufu wa uagizaji kutoka nje. Shughuli za ujenzi wa barabara, madaraja, ardhi, mifereji, n.k. zilikuwa na upungufu wa asilimia 26 toka Sh. 1,069 mwaka 1986 (kwa bei za mwaka 1976) hadi Sh. 791 milioni mwaka 1987. Hii ilitokana hasa na uhaba wa zana nzito za kusukuma ardhi (kama makatapila) kwani hizi zinategemea hasa fedha za Serikali yenyewe ambazo hazikutosheleza mahitaji yote muhimu.

**Maendeleo ya Sekta Mbali mbali:**

4. Katika mwaka 1987, sekta zote isipokuwa madini ziliongeza mchango wake katika Pato la Taifa. Zipo dalili za kuridhisha zinazoonyesha kwamba sekta zilizopewa kipaumbele katika Mpango wa Kufufua Uchumi (ERP) yaani kilimo, viwanda na mawasiliano ziliweza kufanya vizuri zaidi kuliko hapo awali.

5. Pato la Taifa kutokana na sekta ya kilimo iliongezeka kwa asilimia 4·4 katika mwaka 1987. Kama ilivyokuwa msimu wa mwaka 1986/87, mazao ya pamba na mahindi yameendelea kuongezeka. Matarajio ni kwamba katika msimu wa 1987/88 mavuno ya pamba yatafikia marobota 465,000 ikilinganishwa na marobota 400,000 katika msimu wa 1986/87. Uzalishaji wa baadhi ya mazao mengine ya biashara uliongezeka pia. Uzalishaji wa mahindi kwa mwaka wa pili mfululizo uliongezeka na matarajio ni kwamba Shirika la Taifa la Usagishaji (NMC) litanunua tani 237,682 katika msimu wa 1987/88 ikilinganishwa na tani 215,600 katika msimu wa 1986/87. Hali hii nzuri imewezesha NMC kuuza nje (export) tani 100,000 za mahindi. Uzalishaji wa mpunga, ngano na maharage vile vile uliongezeka. Hata hivyo matatizo yalijitokeza katika zao la mhogo kutokana na ugonjwa wa "Mealie bug". Matarajio ni kuwa hatua zilizochukuliwa zitafanikiwa na kurejesha hali nzuri ya ulimaji wa zao hili kwa msimu wa 1988/89.

6. Uzalishaji katika sekta ya viwanda uliokuwa ukipungua kila mwaka kwa miaka saba mfululizo umeongezeka katika mwaka 1987. Mchango wa sekta hii katika Pato la Taifa katika mwaka 1987 uliongezeka kwa asilimia 4·2 ikilinganishwa na kushuka kwa asilimia 4·2 mwaka 1986. Unafuu wa upatikanaji wa fedha za kigeni kutokana na Mpango wa Kufufua Uchumi ndio uliosababisha ongezeko hili hasa kwa kutoa kipaumbele kwa baadhi ya viwanda muhimu kwa kuvipatia malighafi zaidi. Baadhi ya viwanda hivyo ni viwanda vya magurudumu, saruji, zana za kilimo, sabuni n.k. Hata hivyo, viwanda kadhaa vimeendelea kuwa na matatizo makubwa ya spea kutokana na kwamba spea zake hazitengenezwi tena. Mkazo mkubwa bado unahitajiwa katika sekta hii.

7. Pato la Taifa litokanalo na sekta ya usafirishaji na mawasiliano liliongezeka kwa asilimia 4·5 katika mwaka 1987. Ongezeko hili lilitokana na ongezeko katika jumla ya mizigo na abiria waliobebwa. Karibu nyanja zote za uchukuzi ziliongeza kiasi cha mizigo na idadi ya abiria waliobebwa isipokuwa mabasi ya KAMATA yaliyopunguza sana idadi ya abiria wake waliobebwa toka abiria 1,165,000 mwaka 1986 mpaka abiria 62,000 mwaka 1987, upungufu wa asilimia 94·7. Upatikanaji wa kuridhisba wa mafuta hasa dizeli, spea na magari ulichangia kwa kiasi kikubwa matokeo hayo mazuri. Hata hivyo sekta

hii bado inakabiliwa na matatizo makubwa ya ubovu wa barabara, uchakavu wa reli hasa reli ya kati na uhaba wa vyombo vya uchukuzi. Matokeo yake yameendelea kuwa mlundikano wa mazao, pembejeo na bidhaa nyingine na hivyo kusababisha upungufu hata pale ambapo bidhaa zipo nchini. Mipango mingi inaendelea kutekelezwa kupambana na hali hii.

8. Katika sekta nyingine vile vile maendeleo yalikuwa ya kuridhisha. Sekta ya umeme na maji iliongezeka kwa asilimia 7·5 kutokana na usambazaji wa umeme hasa kwenda bara (National Grid) na matengenezo katika baadhi ya miji mikubwa. Biashara pia iliongezeka kwa asilimia 4·8 kutokana na unafuu katika uzalishaji pamoja na ongezeko la bidhaa kutokana na kulegeza masharti ya uagizaji bidhaa. Sekta ya huduma haikuonyesha maongezeko makubwa (0·8) kama ilivyokuwa hapo awali kwani kigezo muhimu katika sekta hiyo kimebadilishwa na kuwa ongezeko la ajira badala ya ongezeko la mishahara hasa ya kima cha chini kama ilivyokuwa hapo awali.

Biashara

**~~Mishahara~~ na Hali ya Malipo na Nchi za Nje:**

9. Biashara baina ya Tanzania na nchi za nje iliendelea kukabiliwa na hali ngumu katika mwaka 1987. Thamani ya mauzo yetu nchi za nje inategemewa kufikia Dola za Marekani 347 milioni ikilinganishwa na Dola 347·6 milioni mwaka 1986. Urari wa biashara ya bidhaa inatarajiwa kuwa na nakisi ya Dola 745 milioni.

10. Tofauti na ilivyokuwa katika mwaka 1986 kiasi (volume) cha bidhaa nyingi zilizouzwa nje kilishuka. Mazao ambayo uuzaji wake nje uliongezeka ni pamba, katani na chai. Hali kadhalika bei ya mazao zilishuka isipokuwa bei ya korosho zisizobanguliwa iliyoongezeka toka Dola 250·30 kwa tani mwaka 1986 hadi Dola 990·80 kwa tani mwaka 1987. Kwa upande wa uagizaji bidhaa uliofikia Dola 1,092 milioni, ijapokuwa mapato ya mauzo yetu na misaada ya uagizaji (Import Support) ililipia sehemu kubwa, ni wazi kuwa kiasi cha fedha za watu binafsi zisizopitia Benki Kuu zilichangia pia. Inakadiriwa kuwa uagizaji bidhaa usiopungua Dola 300 milioni ulifanywa na watu binafsi katika mwaka 1987. Kutokana na hali hiyo, ni dhahiri kuwa mikopo na ruzuku toka nje haifidii pengo lote la Dola 745 milioni katika urari wa biashara ya bidhaa.

11. Kwa jumla, urari wa biashara ya bidhaa ulikuwa na nakisi ya Dola 745 milioni ikilinganishwa na Dola 670 milioni mwaka 1986. Urari wa huduma ulikuwa na nakisi ya Dola 124 milioni na urari wa uhamisho wa mali ulikuwa na ziada ya Dola 583 milioni. Nakisi ya urari wa malipo yote, unaojumlisha urari wa bidhaa, huduma na uhamisho wa mali ulikuwa Dola 286 milioni ikilinganishwa na Dola 312 milioni mwaka 1986.

**Mapato na Matumizi ya Serikali:**

12. Ijapokuwa takwimu halisi za mapato na matumizi kwa mwaka 1987/88 hazijakamilishwa, ni dhahiri kuwa pameendelea kuwepo pengo baina ya mapato na matumizi. Hata hivyo, tofauti na miaka mingine, kiasi kikubwa cha pengo kimefidiwa na fedha za misaada ya kuagizia bidhaa (Import Support) na hivyo kupunguza kiasi cha mikopo ya mabenki ambayo ndiyo ilikuwa chanzo kikubwa cha kuziba mapengo ya bajeti katika miaka iliyotangulia.

13. Katika mwaka 1987/88 mapato ya kawaida yalikadiriwa kufikia Sh. 46,600 milioni na matumizi ya kawaida Sh. 60,071 milioni. Inatarajiwa kwamba mapato ya kawaida yatafikia Sh. 46,828·5 milioni kutokana hasa na jitihada nzuri za kukusanya kodi ya mapato. Matumizi ya kawaida yanatarajiwa kufikia Sh. 61,764·7 milioni ikilinganishwa na makadirio ya Sh. 60,071 milioni na hivyo kupita makadirio kwa kiasi cha Sh. 1,693·7 milioni. Kwa upande wa matumizi ya maendeleo yaliyokadiriwa kufikia Sh. 17,255 milioni, matarajio ni kuwa ifikapo mwisho wa Juni, 1988, kiasi cha Sh. 15,091 milioni au asilimia 88 ya makadirio kitakuwa kimefikiwa.

14. Baada ya kujumlisha mapato yote na matumizi yote, bajeti ilikadiriwa kuwa na pengo la Sh. 28,490 milioni lililotarajiwa kufidiwa na misaada ya uagizaji. Matarajio sasa ni kwamba misaada ya uagizaji itafikia Sh. 26,126 milioni na mikopo ya mabenki inakadiriwa kufikia Sh. 613·4 milioni ikilinganishwa na lengo la Sh. 236 milioni. Hali hii inadhihirisha jinsi Tanzania inavyozidi kutegemea nchi za nje kwa maendeleo yake, jambo ambalo likiachwa kuendelea litaathiri sana maendeleo na uhuru wa Taifa.

**Hali ya Fedha na bei:**

15. Matarajio ya kubana karadha ili kupunguza ongezeko la ujazi wa fedha ambao ni chanzo muhimu cha kuchochea ongezeko la bei hayakufanikiwa ipasavyo. Japokuwa karadha kwa Serikali ilipungua sana kufikia Sh. ~~913·4~~ milioni ikilinganishwa na Sh. 1,656·3 milioni mwaka 1986/87, karadha iliyoelekezwa kwa Bodi za mazao hasa Bodi ya Pamba, Bodi ya Tumbaku na Shirika la Taifa la Usagishaji (NMC) ilivuka viwango vilivyowekwa kwa kiasi kikubwa sana. Matarajio ya awali yalikuwa kwamba NMC ingerekebishwa ili ipunguze gharama na vile vile usindikaji wa pamba na usafiri vingekuwa bora zaidi ili pamba iweze kuuzwa mapema. Haya hayakuweza kukamilika na matokeo ya mavuno mazuri, matatizo ya usindikaji na usafiri yalisababisha ongezeko la karadha.

16. Ongezeko la karadha mwaka 1987/88 lilikadiriwa kufika Sh. 11,326·8 milioni. Matarajio sasa ni kwamba karadha itafikia Sh. 22,655·8 milioni ongezeko la asilimia 34·6 ikilinganishwa na lengo la asilimia 17. Hili pia ni sawa na ongezeko la asilimia 20·1 la ujazi wa fedha ikilinganishwa na lengo la asilimia 10·7 lililopangwa.

17. Matokeo haya vile vile kwa kiasi fulani yamejionyesha katika ongezeko la bei. Katika mwaka 1987, ongezeko la bei linalopimwa na fahirisi ya bei kwa wakazi wa mijini Tanzania Bara (CPI) lilikuwa asilimia 28·9, ikilinganishwa na asilimia 33·2 mwaka 1986 na asilimia 33·3 mwaka 1985. Lengo kwa mwaka 1987 lilikuwa asilimia 25. Sehemu kubwa ya ongezeko hilo la asimilia 28·9 ilitokea katika robo ya nne ya mwaka kutokana hasa na ongezeko la bei la asimilia 17 kwa chakula peke yake. Jumla ya ongezeko kati ya Januari na Septemba 1988 lilikuwa asilimia 14·7 tu. Ni dhahiri kuwa chakula cha kutosha pamoja na usambazaji wake haraka kwa walaji ni moja ya mambo muhimu katika kupunguza kasi ya upandaji wa bei.

**Hali ya Uchumi Duniani na Ushirikiano wa Kiuchumi Kimataifa:**

18. Katika mwaka 1987, hali ya uchumi duniani ilikuwa ya mchanganyiko ambapo kulikuwa na tofauti kubwa katika ukuaji wa uchumi baina ya nchi mbali mbali, zilizoendelea na zinazoendelea. Uchumi wa nchi zinazoendelea uliendelea kuathirika kutokana na matatizo sugu hususan malimbikizo ya madeni, bei duni kwa bidhaa zinazouzwa na nchi zinazoendelea na kuyumba kwa thamani ya fedha. Pato la taifa (GDP) duniani liliongezeka kwa asilimia 3·2 katika mwaka 1987 ikilinganishwa na asilimia 3·5 katika mwaka 1986. Pato la Taifa la nchi zilizoendelea za Magharibi lilikua kwa asilimia 2·7 ikiwa ni sawa na kiwango cha mwaka 1986. Pato la Taifa la nchi zinazoendelea liliongezeka kwa asilimia 2·1 katika mwaka 1987 ikilinganishwa na asilimia 3·2 mwaka 1986. Pato la nchi za Kiafrika liliongezeka kwa asilimia 0·8 ikilinganishwa na asilimia 0·5 katika mwaka 1986.

19. Wingi wa biashara uliongezeka kwa asilimia 4 katika mwaka 1987. Thamani ya mauzo ya bidhaa nje iliongezeka kwa asilimia 15·5 na kufikia dola za Kimarekani bilioni 2.450 katika mwaka 1987. Wastani wa fahirisi ya bei katika fedha za SDR ulishuka kwa asilimia 1·8. Katika mwaka 1987, bei za bidhaa katika dola za Kimarekani zilizouzwa na nchi zilizoendelea zilipanda kwa asilimia 13·4 wakati ambapo bei za bidhaa zinazouzwa na nchi zinazoendelea zilipanda kwa asilimia 3·3. Ongezeko la bei kwa wastani katika nchi zilizoendelea lilikuwa asilimia 2·9 katika mwaka 1987 kutoka asilimia 2·4 mwaka 1986. Ongezeko la bei kwa wastani katika nchi zinazoendelea lilikuwa kubwa na kuwa asilimia 47·2 katika robo ya tatu ya mwaka 1987 ikilinganishwa na asilimia 29·4 katika robo ya tatu ya mwaka 1986.

20. Malimbikizo ya madeni ya nchi zinazoendelea yaliongezeka kwa asilimia 6·25 na kufikia dola za Kimarekani bilioni 1,190. Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) lilianzisha Mfuko wa Nyongeza wa Kurekebisha Uchumi (Enhanced Structural Adjustment Facility) mnamo Desemba 1987 kuzisaidia nchi zinazoendelea zinazotekeleza mipango ya kurekebisha uchumi wao. Mfuko huo umeongezea dola za Kimarekani

bilioni 8·4 (SDR bilioni 6) kwenye Mfuko wa Kurekebisha Uchumi (Structural Adjustment Facility). Maafikiano yalifikiwa mnamo Novemba 1987 kuupatia Mfuko wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (African Development Fund) kiasi cha dola za Kimarekani bilioni 2.700. Mwishoni mwa mwaka 1987 Jumuiya ya Uchumi ya Ulaya (EEC) ilitoa ECU milioni 100 za nyongeza kuzisaidia nchi za Kiafrika maskini sana na zenye madeni katika kuimarisha na kurekebisha uchumi wao.

21. Hapakuwepo maendeleo makubwa katika juhudi za kuleta Mfumo Mpya wa Uchumi Duniani (N.I.E.O.). Kikao cha saba cha Mkutano wa Umoja wa Mataifa kuhusu Biashara na Maendeleo (UNCTAD VII) kilimalizika bila mafanikio ya kuleta msukumo mpya. Awamu mpya ya majadiliano ya biashara baina ya Mataifa (Uruguay Round of Multilateral Trade Negotiations) iliendelea kwa vikao mbali mbali vya kamati zake. Tume Teule ya Ushirikiano wa Nchi Zinazoendelea (South Commission) ilifanya vikao viwili na kutayarisha malengo na misingi ya kazi ya Tume hiyo pamoja na kutoa mkakati wa awali wa kulikabili tatizo la madeni duniani. Juhudi za kukuza ushirikiano wa kiuchumi na kiufundi baina ya nchi zinazoendelea hazikuleta mafanikio makubwa vile vile. Kikao cha mawaziri wa nchi zinazoendelea kilichofanyika Machi 1988 huko Belgrade, Yugoslavia kilitia saini kuanzishwa kwa mkataba wa Mfumo wa Biashara baina ya nchi zinazoendelea (GSTP). Ushirikiano wa Kiuchumi baina ya nchi zilizo Kusini mwa Afrika (SADCC), Soko Nafuu la Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika (PTA) na Tume za Ushirikiano kati ya Tanzania na Nchi rafiki (Joint Commissions) viliendelea kutekeleza mipango yao katika nyanja mbali mbali za ushirikiano.

Jedwali A

| | |
|---|---|
| Idadi ya Watu | N |
| *Takwimu za Uzalishaji* | |
| 1. *Pato la Taifa* | |
| (i) Kwa bei za miaka inayohusika | S |
| (ii) Kwa bei za mwaka 1976 | S |
| 2. *Wastani wa Pato kwa kila mtu:* | |
| (i) Kwa bei za miaka inayohusika | S |
| (ii) Kwa bei za mwaka 1976 | S |
| 3. *Mazao ya Kilimo (1):* | |
| (a) *Mazao ya Chakula (2):* | |
| (i) Mahindi | T |
| (ii) Mpunga | T |
| (iii) Ngano | T |
| (b) *Mazao ya kuuza (3)* | |
| (i) Kahawa | T |
| (ii) Pamba yenye mbegu | T |
| (iii) Chai (Majani mabichi) | T |
| (iv) Tumbaku | T |
| (v) Katani | T |
| (vi) Korosho | T |
| 4. *Hali ya Malipo na Nchi za Nje* | |
| (i) Bidhaa zilizouzwa Nchi za Nje | S |
| (ii) Bidhaa zilizoagizwa toka Nje | S |
| (iii) Urari wa Biashara ya Bidhaa | S |
| (iv) Urari wa Bidhaa, Huduma na Uhamisho wa mali | S |
| (v) Urari wa Malipo yote | S |
| (vi) Kiwango cha Wastani cha ubadilishanaji wa Fedha kwa mwaka Sh/US $ (Annual average Exchange rate) | |
| 5. *Ujazi wa Fedha:* | |
| (i) Fedha Mikononi mwa watu | S |
| (ii) Amana za Muda Mfupi | S |
| (iii) Amana za Akiba na za Muda Maalum | S |
| Jumla | S |
| 6. *Fahirisi za bei (1977 = 100)*:* | |
| (i) Fahirisi za bei kwa walaji wa Mijini Tanzania Bara | |
| (ii) Fahirisi za bei ya rejareja kwa watu wa kipato cha Chini Dar es Salaam | |
| 7. *Fedha za Serikali:* | |
| (a) Mapato ya Kawaida | S |
| (b) Matumizi ya kawaida | S |
| (c) Matumizi ya Maendeleo | S |
| (i) Mapato ya Ndani | S |
| (ii) Mapato ya Nje | S |

*Tanzania Bara

(1) Mazao ya Kilimo yameonyeshwa kwa miaka ya mavuno.
(2) Kiasi kilichonunuliwa na Shirika la Usagishaji (NMC).
(3) Kiasi kilichonunuliwa na Mamlaka za Mazao.
(4) Msiegemeo Halisi.

## SURA YA II

# MAENDELEO MUHIMU KATIKA UCHUMI

## 1. PATO LA TAIFA

1. Takwimu za awali zinaonyesha kuwa Pato la Taifa katika mwaka 1987 lilikuwa Sh. 26,142 milioni kwa bei za mwaka 1976 ikilinganishwa na Sh. 25,158 mwaka 1986. Hili ni ongezeko la asilimia 3.9 katika Pato la Taifa mwaka 1987, ikilinganishwa na miaka miwili iliyotangulia, yaani 1986 na 1985. Pato la Taifa liliongezeka kwa asilimia 3.6 mwaka 1986 na asilimia 2.6 mwaka 1985.

2. Ingawa ukuaji wa Pato la Taifa uliotokea mwaka 1987 ni mkubwa kuliko uliotokea miaka ya 1986 na 1985 na vile vile kuliko ongezeko la wastani la idadi ya watu la asilimia 3.3 kwa mwaka, ongezeko hilo bado ni pungufu ya lengo la ukuaji uliokadiriwa katika Mpango wa Kufufua Uchumi la asilimia 4.5. Hata hivyo, tofauti na miaka ya 1986 na 1985, sekta zote ukiondoa madini zimechangia katika ukuaji wa Pato la Taifa ambapo katika miaka ya 1986 na 1985, mbali na sekta ya kilimo, ukuaji ulitokana hasa na sekta za huduma.

3. Sekta ya kilimo (ikijumuisha mazao, ufugaji na maliasili yaani misitu, uvuvi na uwindaji) iliendelea kuchangia sehemu kubwa ya Pato la Taifa kuliko sekta nyingine (asilimia 46.2 katika bei za mwaka 1976). Thamani yake ilikuwa ni Sh. 12,066 milioni kwa kulinganisha na Sh. 11,557 milioni mwaka 1986, likiwa ni ongezeko la Sh. 509 milioni au asilimia 4.4. Kwa jumla, nyanja zote ambazo huchangia katika Pato la Taifa litokanalo na kilimo zilikuwa na maongezeko mwaka 1987. Ingawa uzalishaji wa baadhi ya mazao, hasa mazao ya biashara ulipungua, mchango wa mazao kwa jumla ulikuwa Sh. 9,431 milioni ikiwa ni ongezeko la Sh. 464 milioni au asilimia 5.2 kwa kulinganisha na mwaka 1985.

4. Kama ilivyokuwa mwaka 1986, Serikali iliendelea kutoa kipaumbele kwa uzalishaji wa mazao ya biashara na chakula katika mwaka 1987 kwa kuongeza bei zake na vile vile upatikanaji na usambazaji wa pembejeo. Aidha, hali ya hewa iliendelea kuwa nzuri hasa katika kipindi cha Januari—Septemba. Shughuli za ufugaji zilichangia sh. 1,474 milioni ikiwa ni ongezeko la Sh. 45 milioni au asilimia 3.0 kwa kulinganisha na mwaka 1986. Serikali imekuwa ikijitahidi kuendeleza sekta ya mifugo miaka ya karibuni ili kuiwezesha kutoa mchango mkubwa zaidi katika uchumi. Nyanja za maliasili kwa pamoja zilichangia

Sh. 1,161 milioni katika Pato la Taifa mwaka 1987 kiasi ambacho kinalingana na mchango wa mwaka 1986. Nyanja za uvuvi na uwindaji zilikuwa na maongezeko, ingawa kwa kiwango kidogo kwa kulinganisha na mwaka 1986.

5. Sekta ya madini ilichangia sh. 165 milioni katika Pato la Taifa mwaka 1987 kwa kulinganisha na Sh. 167 milioni mwaka 1986. Upungufu uliotokea mwaka 1987 wa Sh. 2 milioni au asilimia 1.5 ni mdogo kuliko uliotokea mwaka 1986 wa Sh. 7 milioni au asilimia 4.2 na ulisababishwa hasa na kushuka kwa mauzo ya almasi, chumvi na mawe ya thamani. Mauzo ya madini mengine yakiwemo dhahabu yaliongezeka, na kwa jumla bei za madini mengi hazikutofautiana sana na mwaka 1986. Kama ilivyokuwa katika miaka iliyotangulia, tatizo kubwa la sekta ya madini limeendelea kuwa uhaba wa rasilimali ya kuendeleza sekta hii na kuiwezesha kutoa mchango mkubwa zaidi katika uchumi.

6. Baada ya upungufu wa Sh. 87 au asilimia 4.2 uliotokea katika uzalishaji wa sekta ya viwanda mwaka 1986, kulikuwepo ongezeko la asilimia 4.2 katika mwaka 1987. Ikizingatiwa kuwa uzalishaji wa viwanda kwa jumla umepungua mwaka hadi mwaka tangia mwaka 1980, ongezeko lililopatikana mwaka 1987 ni dalili kwamba sekta ya viwanda imeanza kuibuka, ingawa kiwango cha uzalishaji kilichofikiwa ni sawa na ilivyokuwa mwaka 1985. Haya ni matokeo ya Mpango wa Kufufua Uchumi ulioanza kutekelezwa hapo Juni 1986 ambao moja ya malengo yake ni kuongeza matumizi ya uwezo wa viwanda kwa kuzitengea nyanja muhimu fedha za kigeni zitakazoweza kupatikana ili kuagizia malighafi na spea. Matazamio ni kwamba uzalishaji wa viwanda utaendelea kuwa ahueni kadri matatizo ambayo yamekuwa yakiathiri sekta hii, yaani uhaba wa malighafi, spea na mitambo na vile vile ukatikaji wa mara kwa mara wa maji na umeme yatakavyoendelea kutafutiwa ufumbuzi.

7. Sekta ya umeme na maji ilikuwa na ongezeko la asilimia 7.5 mwaka 1987 ambalo ni pungufu ya ongezeko la asilimia 18.0 lililopatikana mwaka 1986. Kama ilivyokuwa mwaka 1986, ongezeko la mwaka 1987 lilitokana hasa na umeme. Utekelezaji wa miradi ya umeme ikiwemo usambazaji wake ambayo ndiyo ilisababisha ongezeko kubwa la mwaka 1986 uliendelea mwaka 1987. Serikali iliendelea pia na azma yake ya kutoa maji safi kwa kila mwananchi. Licha ya juhudi zinazofanywa kuongeza upatikanaji wa huduma za maji na umeme kwa sehemu mbali mbali za uzalishaji, tatizo la ukatikaji wa mara kwa mara wa maji na umeme liliviKumba viwanda kadhaa katika nyakati mbali mbali.

8. Shughuli za ujenzi zilikuwa na ongezeko la Sh. 22 milioni au asilimia 2.9 mwaka 1987 ambapo mwaka 1986 kulikuwepo ongezeko la Sh. 151 milioni au asilimia 25.1 lililotokana hasa na ujenzi wa maghala na shughuli nyinginezo zikiwemo barabara na mifereji. Upatikanaji wa vifaa kadhaa vya ujenzi vikiwemo saruji, mabati na rangi sasa ni nafuu kidogo

kutokana na baadhi ya viwanda vya ujenzi kufanyiwa ukarabati (hasa viwanda vya saruji) au kupata malighafi zaidi (viwanda vya mabati na rangi). Hata hivyo, uwezo wa sekta ya ujenzi kuhudumia kikamilifu nyanja nyingine za uchumi zinazoitegemea haujaimarika kwa kiasi cha kuridhisha, jambo ambalo linasababisha rasilimali za umma (barabara n.k.) kutofanyiwa matengenezo yanayohitajika kwa wakati.

9. Uuzaji wa jumla na rejareja pamoja na maboteli ulikuwa na ongezeko la asilimia 4.8 mwaka 1987 kwa kulinganisha na mwaka 1986 ambapo kulikuwepo ongezeko la asilimia 10.9. Kwa jumla, upatikanaji wa baadhi ya bidhaa umeendelea kuwa nafuu mwaka hata mwaka kuanzia mwaka 1984 ambapo utaratibu wa kuruhusu watu binafsi wenye fedha za kigeni kuingiza nchini bidhaa fulani fulani ulipoanzishwa. Pamoja na utaratibu huo, miaka iliyofuatia vile vile imeshuhudia juhudi za Serikali kuongeza uzalishaji wa bidhaa muhimu na pia kuthibiti usambazaji wake.

10. Sekta ya uchukuzi na mawasiliano ilikua kwa asilimia 4.5 katika mwaka 1987. Kwa kutambua umuhimu wake katika juhudi za kufufua uchumi, Serikali imeendelea kutoa kipaumbele kwa shughuli za uchukuzi kwa kuthibiti usambazaji wa mafuta na vile vile upatikanaji wa matairi na spea. Pamoja na kwamba uwezo wa uchukuzi umeimarika kidogo, matatizo ya siku nyingi ya uchakavu wa barabara na reli na vile vile uhaba wa mabogi na mabehewa yameendelea kukwamisha usombaji wa mazao katika sehemu mbali mbali nchini.

11. Kulikuwepo ongezeko la Sh. 79 milioni au asilimia 2.4 kutokana na huduma za fedha na bima, mali na huduma za biashara. Mwaka uliotangulia yaani 1986 ongezeko lilikuwa Sh. 237 milioni. Tofauti na mwaka 1986 ambapo nyanja zote zilichangia kwa kiwango kikubwa kwa ongezeko lililotokea, katika mwaka 1987 sehemu kubwa ya ongezeko (asilimia 80) ilitokana na mali. Huduma za fedha na bima zimekuwa zikichangia nusu ya Pato la Taifa linalotokana na sekta ya fedha, bima, mali na huduma za biashara. Kwa upande wa huduma za biashara, maongezeko katika miaka ya karibuni yamekuwa madogo hasa kutokana na hali mbaya ya biashara iliyosababishwa na kutetereka kwa uchumi. Inategemewa kuwa kuibuka kwa uchumi kunakoanza kuonekana kutabadili hali hiyo katika miaka inayokuja.

12. Katika sekta ya uendeshaji wa serikali na huduma nyingine, takwimu za miaka iliyotangulia zilikuwa zikionyesha kuwa ukuaji halisi wa Pato la Taifa kutokana na sekta hii ulikuwa ukiongezeka sana na wakati mwingine kuchangia sehemu kubwa ya ukuaji wa Pato la Taifa kwa jumla, hasa katika miaka ya 1984—86. Msingi wa takwimu hizo ulikuwa ni fahirisi ya mshahara wa kima cha chini, ambacho kilipandishwa mara kwa mara tangu mwaka 1980. Kwa kutumia fahirisi ya uajiri na tija, maongezeko ya ukuaji wa huduma za serikali yalikuwa

ya kadiri, kwa kulinganisha na ukuaji wa zaidi ya asilimia 10 uliokuwa ukitokea karibu kila mwaka kwa fahirisi ya kima cha chini cha mshahara. Mwaka 1987, kulikuwepo ongezeko la asilimia 0·8 tu. Serikali imejitahidi kubana kasi ya ongezeko la uajiri tangu zoezi la kupunguza wafanyakazi lililofanyika mwaka 1985. Mtazamo mkubwa wa serikali kwa sasa ni kujenga mazingira ya kumwezesha kila mfanyakazi kuongeza tija.

Takwimu kuhusu Pato la Taifa zinaonyeshwa katika majedwali Na. 1 hadi 4.

## PATO LA TAIFA (GDP) KISEKTA KWA GHARAMA ZAKE

(Bei za miaka inayohusika)

Jedwali Na. 1

(Shilingi milioni)

| SEHEMU | 1976 | 1977 | 1978 | 1979 | 1980 | 1981 | 1982 | 1983 | 1984 | 1985 | 1986 | 1987 | Badiliko % 86/87 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Kilimo, Uwindaji, Misitu na Uvuvi | 9.046 | 11.131 | 12.506 | 14.728 | 16.636 | 20.338 | 26.449 | 32.737 | 41.295 | 61.231 | 84.153 | 120.941 | 43.70 |
| 2. Madini | 214 | 243 | 228 | 284 | 329 | 299 | 266 | 249 | 337 | 251 | 474 | 563 | 18.80 |
| 3. Viwanda | 2.811 | 3.287 | 3.859 | 3.868 | 4.097 | 4.501 | 4.361 | 4.869 | 5.932 | 6.665 | 7.417 | 9.044 | 21.90 |
| 4. Umeme na Maji | 219 | 254 | 261 | 275 | 424 | 423 | 421 | 514 | 551 | 1.071 | 2.096 | 2.259 | 7.80 |
| 5. Ujenzi | 884 | 1.111 | 1.052 | 1.229 | 1.498 | 1.614 | 1863 | 1.252 | 1.661 | 2.061 | 3.257 | 3.658 | 12.30 |
| 6. Uuzaji na Mahoteli | 2.839 | 3.407 | 3.889 | 4.344 | 4.713 | 5.479 | 6.814 | 8.148 | 10.447 | 14.195 | 18.851 | 27.453 | 5.60 |
| 7. Uchukuzi na Mawasiliano | 1.685 | 1.793 | 1.917 | 2.113 | 3.019 | 3.133 | 3.395 | 3.507 | 4.789 | 7.021 | 9.863 | 16.794 | 70.30 |
| 8. Fedha na Huduma za Biashara | 2.036 | 2.419 | 2.686 | 2978 | 3.744 | 4.507 | 4.891 | 5.252 | 6.028 | 6.659 | 8.127 | 11.062 | 36.10 |
| 9. Serikali na Huduma Nyingine | 2.342 | 2.596 | 2873 | 3342 | 3959 | 4732 | 5.446 | 7.372 | 8.614 | 10.735 | 11.340 | 12.771 | 12.60 |
| 10. Toa Ushuru wa Huduma za Mabenki | 424 | 543 | 689 | 844 | 965 | 1.120 | 1.360 | 1.292 | 1.511 | 1.806 | 2.544 | 6.444 | 153.30 |
| 11. Pato la Taifa | 21.652 | 25.698 | 28.582 | 32.317 | 37.454 | 43.986 | 52.546 | 62.608 | 78.143 | 108.083 | 143.034 | 198.101 | 42.20 |

*Chanzo:*—Idara ya Takwimu.

## JUMLA YA PATO LA TAIFA (GDP) KISEKTA KWA GHARAMA ZAKE

(Bei za miaka inayohusika)

Jedwali Na. 2 (Asilimia)

| SEHEMU | 1976 | 1977 | 1978 | 1979 | 1980 | 1981 | 1982 | 1983 | 1984 | 1985 | 1986 | 1987 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kilimo, Uwindaji, Misitu na Uvuvi ...... | 41·8 | 43·3 | 43·8 | 45·6 | 44·4 | 46·3 | 50·3 | 53·7 | 54·1 | 56·6 | 58·9 | 61·1 |
| Madini .......... | 1 | ·9 | ·8 | ·9 | ·9 | ·7 | ·5 | ·4 | ·4 | ·3 | ·4 | ·3 |
| Viwanda .......... | 13 | 12·8 | 13·5 | 12 | 10·9 | 10·2 | 8·3 | 8 | 7·7 | 6·9 | 6·2 | 4·6 |
| Umeme na Maji .......... | 1 | 1 | ·9 | ·9 | ·1 | 1 | ·8 | ·8 | ·7 | 1·1 | 1·6 | 1·1 |
| Ujenzi .......... | 4 | 4·3 | ·7 | ·8 | 4 | 3.7 | 3·5 | 2·1 | 2·2 | 2 | 1·7 | 1·9 |
| Uuzaji na Mahoteli .......... | 13·1 | 13·3 | 3·4 | 3·4 | 12·6 | 12·5 | 3 | 13·4 | 12·7 | 13·7 | 13·8 | 13·9 |
| Uchukuzi na Mawasiliano .......... | ·8 | 0 | 6·7 | 6·5 | 8·1 | 7·1 | ·5 | 5.7 | 6·3 | 7·1 | 6·5 | 8·5 |
| Fedha na Huduma za Biashara .......... | 9·4 | 9·4 | ·4 | 9·2 | 10 | 3 | 9·3 | 8·6 | 8·1 | 6·8 | 6·2 | 5·6 |
| Serikali na Huduma Nyingine .......... | 10·8 | ·1 | 10 | 10·3 | 10 | 10·8 | ·4 | 9·5 | 8·7 | 7·3 | 6·3 | 6·5 |
| Toa Ushuru wa Huduma za Mabenki ... | 1·9 | 2·1 | 2·4 | 2·6 | 2·6 | 2·6 | ·6 | 2·2 | 1·9 | 1·8 | 1·6 | 3·3 |
| Jumla ... | 100 | 100 | 100 | 100 | 100 | 100 | 100 | 100 | 100 | 100 | 100 | 100 |

*Chanzo:*—Idara ya Takwimu.

## JUMLA YA PATO LA TAIFA (GDP) KISEKTA KWA GHARAMA ZAKE

(Bei za mwaka 1976)

Jedwali Na. 3 (Shilingi milioni)

| SEHEMU | 1976 | 1977 | 1978 | 1979 | 1980 | 1981 | 1982 | 1983 | 1984 | 1985 | 1986 | 1987 | Badiliko %86/87 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kilimo, Uwindaji, Misitu na Uvuvi | 9,046 | 9,150 | 8,998 | 9,066 | 9,418 | 9,511 | 9,639 | 9,914 | 10,312 | 10,931 | 11,557 | 12,066 | 4.4 |
| Madini | 214 | 231 | 189 | 200 | 189 | 193 | 193 | 174 | 186 | 174 | 167 | 165 | −1.2 |
| Viwanda | 2,811 | 2,641 | 2,730 | 2,821 | 2,683 | 2,382 | 2,304 | 2,103 | 2,159 | 2,075 | 1,991 | 2,075 | 4.2 |
| Umeme na Maji | 220 | 244 | 286 | 318 | 400 | 417 | 420 | 413 | 439 | 461 | 544 | 585 | 7.5 |
| Ujenzi | 884 | 915 | 783 | 879 | 932 | 890 | 930 | 549 | 660 | 601 | 752 | 774 | 2.9 |
| Uuzaji na Mahoteli | 2,839 | 2,782 | 2,797 | 2,839 | 2,839 | 2,725 | 2,668 | 2,612 | 2,640 | 2,662 | 2,953 | 3,086 | 4.8 |
| Uchukuzi na Mawasiliano | 1,685 | 1,652 | 1,699 | 1,634 | 1,818 | 1,652 | 1,694 | 1,473 | 1,482 | 1,509 | 1,514 | 1,582 | 4.5 |
| Fedha na Huduma za Biashara | 2,036 | 2,089 | 2,208 | 2,338 | 2,483 | 2,529 | 2,702 | 2,817 | 2,984 | 3,046 | 3,283 | 3,362 | 2.4 |
| Serikali na Huduma Nyingine | 2,342 | 2,497 | 2,997 | 3,255 | 3,188 | 3,551 | 3,556 | 3,543 | 3,549 | 3,616 | 3,283 | 3,309 | .8 |
| Toa Ushuru wa Huduma za Mabenki | 424 | 462 | 485 | 501 | 531 | 549 | 667 | 716 | 755 | 797 | 836 | 862 | |
| Jumla | 21,653 | 21,739 | 22,202 | 22,849 | 23,419 | 23,308 | 23,439 | 22,882 | 23,656 | 24,278 | 25,158 | 26,142 | 3.9 |

*Chanzo:*—Idara ya Takwimu.

Huduma za serikali zinafanyiwa marekebisho kwa kipindi chote cha 1976-87

# JUMLA YA PATO LA TAIFA (GDP) KISEKTA KWA GHARAMA ZAKE

(Bei za mwaka 1976)

Jedwali Na. 4

(Asilimia)

| SEHEMU | 1976 | 1977 | 1978 | 1979 | 1980 | 1981 | 1982 | 1983 | 1984 | 1985 | 1986 | 1987 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kilimo, Uwindaji, Misitu na Uvuvi ...... | 41·78 | 42·09 | 40·53 | 39·68 | 40·22 | 40·82 | 41·12 | 43·33 | 43·59 | 45·02 | 45·94 | 46·16 |
| Madini ...... | ·99 | 1·06 | ·85 | ·88 | ·81 | ·83 | ·82 | ·76 | ·79 | ·72 | ·66 | ·63 |
| Viwanda ...... | 12·98 | 12·15 | 12·30 | 12·35 | 11·46 | 10·22 | 9·83 | 9·19 | 9·13 | 8·55 | 7·91 | 7·94 |
| Umeme na Maji ...... | 1·02 | 1·12 | 1·29 | 1·39 | 1·71 | 1·79 | 1·79 | 1·80 | 1·86 | 1·90 | 2·16 | 2·24 |
| Ujenzi ...... | 4·08 | 4·21 | 3·53 | 3·85 | 3·98 | 3·82 | 3·97 | 2·40 | 2·79 | 2·48 | 2·99 | 2·96 |
| Uuzaji na Mahoteli ...... | 13·11 | 12·80 | 12·60 | 12·43 | 12·12 | 11·69 | 11·38 | 11·42 | 11·16 | 10·96 | 11·74 | 11·80 |
| Uchukuzi na Mahoteli ...... | 7·78 | 7·60 | 7·65 | 7·15 | 7·76 | 7·09 | 7·23 | 6·44 | 6·26 | 6·22 | 6·02 | 6·05 |
| Fedha na Huduma za Biashara ...... | 9·40 | 9·61 | 9·95 | 10·23 | 10·60 | 10·85 | 11·53 | 12·31 | 12·61 | 12·55 | 13·05 | 12·86 |
| Serikali na Huduma Nyingine ...... | 10·82 | 11·49 | 13·50 | 14·25 | 13·61 | 15·24 | 15·17 | 15·48 | 15·00 | 14·89 | 13·05 | 12·66 |
| Toa Ushuru wa Huduma za Mabenki ... | 1·96 | 2·13 | 2·18 | 2·19 | 2·27 | 2·36 | 2·86 | 3·13 | 3·19 | 3·28 | 3·52 | 3·30 |
| Jumla ... | 100·00 | 100·00 | 100·00 | 100·00 | 100·00 | 100·00 | 100·00 | 100·00 | 100·00 | 100·00 | 100·00 | 100·00 |

*Chanzo*:—Idara ya Takwimu.

## 2.—UKUZAJI WA RASILIMALI

1. Mwaka 1987 ukuzaji wa rasilimali ulikuwa Sh. 7,168 milioni (katika bei za mwaka 1976), huu ukiwa ni upungufu wa Sh. 400 milioni au asilimia 5.3 kwa kulinganisha na ukuzaji rasilimali wa Sh. 7,586 milioni mwaka 1986. Upungufu uliotokea mwaka 1987 ni mkubwa kuliko uliotokea mwaka 1986 wa Sh. 49 milioni au asilimia 0.6 na ulisababishwa na upungufu katika nyanja za vifaa vya usafiri na vifaa vinginevyo na pia shughuli nyingine za ujenzi mbali na majengo. Uwiano wa ukuzaji wa rasilimali na Pato la Taifa katika bei za mwaka 1976 ulikuwa asilimia 27.4 mwaka 1987 ambapo mwaka 1986 ulikuwa asilimia 30.2.

2. Uwekezaji katika majengo kwa jumla ulikuwa Sh. 1,304 milioni mwaka 1987 ikiwa ni ongezeko la Sh. 278 milioni kwa kulinganisha na mwaka 1986 ambapo rasilimali ya majengo ilikuwa Sh. 1,026 milioni. Ongezeko la uwekezaji katika majengo lilitokana hasa na majengo yasiyo ya kuishi. Uwekezaji katika ujenzi vijijini uliongezeka kwa Sh. 9 milioni mwaka 1987 kufikia Sh. 367 milioni. Kama ilivyokuwa mwaka 1986, ujenzi wa maghala ulichangia kwa kiasi kikubwa katika ongezeko la rasilimali ya majengo yasiyo ya kuishi katika mwaka 1987.

3. Rasilimali iliyotokana na shughuli nyingine za ujenzi ilikuwa na thamani ya Sh. 791 milioni, ukiwa ni upungufu wa Sh. 278 milioni au asilimia 26 kwa kulinganisha na mwaka 1986. Kwa jumla, kumekuwepo matatizo ya upatikanaji wa zana na vifaa vya ujenzi huo kutokana na uhaba wa fedha za kigeni. Matokeo yake ni kupungua kwa ukuaji wa rasilimali ya nyanja hizo yaani barabara, madaraja, mifereji na uendelezaji ardhi. Aidha, imekuwa vigumu kufanya matengenezo kwa rasilimali zilizojengwa miaka ya nyuma kwa sababu hiyo.

4. Ununuzi wa vifaa ulikuwa Sh. 4,650 milioni mwaka 1987 ukiwa ni upungufu wa Sh. 451 milioni au asilimia 8.8 kwa kulinganisha na ununuzi uliofanywa mwaka 1986. Upungufu huu ni zaidi kidogo ya upungufu wa Sh. 416 uliotokea mwaka 1986. Sehemu kubwa ya upungufu uliotokea mwaka 1987 kwa upande wa vifaa ilihusu vifaa vya usafiri. Utaratibu wa kuruhusu watu binafsi wenye fedha zao za kigeni kununua magari madogo ya mizigo ulipoanzishwa mwaka 1984, kulikuwepo ongezeko kubwa la uingizaji wa magari nchini mwaka huo (1984) na pia mwaka uliofuata (1985). Kuanzia mwaka 1986 kumekuwepo upungufu ambao, pamoja na mambo mengine, ni matokeo ya upunguzaji wa thamani ya fedha wa mara kwa mara ambao unaongeza gharama za kuingiza bidhaa nchini. Hata hivyo uingizaji wa magari uliofanywa mwaka 1987, japo pungufu ya uingizaji uliofanywa miaka ya 1986 na 1985, ni mkubwa kuliko uingizaji uliofanywa katika kipindi cha 1977—1984. Kumekuwepo juhudi za makusudi kwa upande wa serikali kuimarisha sekta ya mawasiliano na uchukuzi chini ya Mpango wa Kufufua Uchumi. Serikali imeweza kupata vifaa vya usafiri kama misaada na vingine imenunua

yenyewe, licha ya uhaba wa fedha za kigeni ambao umelikabili Taifa kwa muda mrefu. Ununuzi wa vifaa vinginevyo ulipungua pia, ingawa upungufu uliotokea mwaka 1987 wa Sh. 141 milioni ni mdogo ukilinganishwa na upungufu wa Sh. 330 uliotokea mwaka 1986.

5. Ingawa kiwango cha ukuzaji wa rasilimali cha mwaka 1987 ni pungufu na viwango vilivyofikiwa miaka miwili iliyotangulia yaani 1986 na 1985, ukuzaji huo ni mkubwa kuliko uliofikiwa katika miaka ya 1977—1984. Kwa jumla, baada ya upungufu mkubwa wa ukuzaji wa rasilimali uliotokea mwaka 1983, miaka iliyofuatia imeshuhudia nafuu katika ukuzaji wa rasilimali. Uchumi utaweza kutengamaa zaidi ikiwa rasilimali hiyo itatumika vizuri. Lakini itabidi vile vile zifanywe juhudi kuimarisha rasilimali za barabara, madaraja, uendelezaji ardhi na mifereji, ambazo ukuaji wake umeshuka mno. Ukuaji wa rasilimali hizo mwaka 1987 ulikuwa nusu ya ukuaji uliowahi kufikiwa mwaka 1980 wa Sh. 1,569 milioni.

## UKUZAJI WA RASILIMALI

(Bei za miaka inayohusika)

Jedwali 5: (Sh. Milioni)

| Aina | 1977 | 1978 | 1979 | 1980 | 1981 | 1982 | 1983 | 1984 | 1985 | 1986 | 1987 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| *Majengo:* | | | | | | | | | | | |
| Ya kuishi ............... | 160 | 183 | 202 | 213 | 427 | 386 | 185 | 359 | 592 | 500 | 516 |
| Ujenzi Vijiji ............ | 315 | 363 | 420 | 496 | 574 | 657 | 764 | 932 | 1,116 | 1,337 | 1,569 |
| Yasiyo ya kuishi ....... | 846 | 749 | 943 | 1,126 | 1,446 | 1,373 | 898 | 1,219 | 1,388 | 2,595 | 4,338 |
| Jumla ... | 1,321 | 1,295 | 1,565 | 1,835 | 2,447 | 2,416 | 1,847 | 2,510 | 3,096 | 4,432 | 6,423 |
| *Shughuli Nyingine:* | | | | | | | | | | | |
| Uendelezaji Ardhi .... | 168 | 112 | 167 | 165 | 358 | 293 | 158 | 270 | 539 | 790 | 358 |
| Barabara, Madaraja .. | 208 | 190 | 450 | 664 | 444 | 323 | 581 | 513 | 557 | 631 | 1,019 |
| Maji ....................... | 207 | 198 | 212 | 213 | 287 | 332 | 239 | 315 | 347 | 473 | 1,076 |
| Mengineyo .............. | 1,340 | 1,255 | 1,172 | 1,482 | 1,141 | 2,037 | 709 | 1,105 | 1,319 | 3,058 | 1,641 |
| Jumla ... | 1,923 | 1,755 | 2,001 | 2,524 | 2,230 | 2,985 | 1,687 | 2,203 | 2,762 | 4,952 | 4,094 |
| *Vifaa:* | | | | | | | | | | | |
| Usafiri ..................... | 978 | 1,140 | 2,591 | 1,150 | 1,516 | 1,278 | 975 | 4,986 | 7,566 | 13,492 | 13,745 |
| Vingineyo ................ | 2,441 | 3,140 | 2,435 | 3,121 | 2,439 | 4,146 | 3,243 | 2,274 | 3,448 | 6,457 | 22,698 |
| Jumla ... | 3,419 | 4,280 | 5,026 | 4,271 | 3,955 | 5,424 | 4,218 | 7,260 | 11,014 | 19,949 | 36,443 |
| Rasilimali ya Kudumu .. | 6,663 | 7,330 | 8,592 | 8,630 | 8,632 | 10,825 | 7,752 | 11,973 | 16,872 | 29,333 | 46,960 |
| Ongezeko la Limbikizo . | 861 | 764 | 866 | 1,055 | 1,498 | 1,410 | 1,836 | 1,645 | 2,091 | 2,487 | 3,685 |
| Uzalishaji rasilimali— | | | | | | | | | | | |
| Jumla ... | 7,524 | 8,094 | 9,458 | 9,685 | 10,130 | 12,235 | 9,588 | 13,618 | 18,963 | 31,820 | 50,645 |

*Chanzo:*—Idara ya Twakimu.

## UKUZAJI WA RASILIMALI

Jedwali Na. 6:

(Bei za Mwaka 1976)

(Sh. Milioni).

| Aina | 1977 | 1978 | 1979 | 1980 | 1981 | 1982 | 1983 | 1984 | 1985 | 1986 | 1987 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| *Majengo:* | | | | | | | | | | | |
| Ya Kuishi ............... | 130 | 134 | 144 | 132 | 236 | 192 | 81 | 138 | 169 | 108 | 100 |
| Ujenzi Vijiji ............ | 284 | 291 | 299 | 307 | 315 | 323 | 331 | 340 | 349 | 358 | 367 |
| Yasiyo ya Kuishi ...... | 688 | 550 | 676 | 700 | 799 | 683 | 394 | 467 | 397 | 560 | 837 |
| Jumla... | 1,102 | 975 | 1,119 | 1,139 | 1,350 | 1,198 | 806 | 945 | 915 | 1,026 | 1,304 |
| *Shughuli Nyingine:* | | | | | | | | | | | |
| Ardhi ........................ | 136 | 82 | 119 | 103 | 198 | 146 | 69 | 103 | 154 | 171 | 69 |
| Barabara, Madaraja Maji na Kazi Nyingine ... | 1,427 | 1,207 | 1,312 | 1,466 | 1,034 | 1,339 | 671 | 741 | 635 | 898 | 722 |
| Jumla... | 1,563 | 1,289 | 1,431 | 1,569 | 1,232 | 1,485 | 740 | 844 | 789 | 1,069 | 791 |
| *Vifaa:* | | | | | | | | | | | |
| Usafiri ...................... | 874 | 918 | 1985 | 783 | 986 | 794 | 577 | 2,817 | 3,789 | 3,503 | 3,193 |
| Vinginevyo .............. | 2,181 | 2,528 | 1,865 | 2,124 | 2,238 | 2,575 | 1,919 | 1,285 | 1,728 | 1,598 | 1,457 |
| Jumla... | 3,055 | 3,446 | 3,850 | 2,907 | 3,224 | 3,369 | 2,496 | 4,102 | 5,517 | 5,101 | 4,650 |
| Rasilimali ya Kudumu .. | 5,720 | 5,710 | 6,400 | 5,615 | 5,806 | 6,052 | 4,042 | 5,891 | 7,221 | 7,196 | 6,745 |
| Ongezeko la Limbikizo . | 734 | 513 | 425 | 488 | 562 | 511 | 590 | 442 | 414 | 390 | 423 |
| Uzalishaji rasilimali —Jumla... | 6,454 | 6,223 | 6,825 | 6,103 | 6,368 | 6,563 | 4,632 | 6,333 | 7,635 | 7,586 | 7,168 |

*Chanzo:*—Idara ya Twakimu.

Jedwali 7:

## UZALISHAJI WA RASILIMALI: SEKTA YA BINAFSI NA YA UMMA

(Sh. Milion)

| Sekta | 1978 | 1979 | 1980 | 1981 | 1982 | 1983 | 1984 | 1985 | 1986 | 1987 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| *Sekta ya Umma:* | | | | | | | | | | |
| Serikali | 1.426 | 2.032 | 2.330 | 2.485 | 2.369 | 1.639 | 1.815 | 2.210 | 3.520 | 6.024 |
| Mashirika | 2.517 | 2.353 | 2.525 | 2.174 | 3.533 | 2.017 | 2.637 | 4.428 | 8.346 | 7.565 |
| Taasisi + | 11 | 19 | 18 | 88 | 72 | 85 | 145 | 152 | 173 | 248 |
| Jumla... | 3.954 | 4.404 | 4.873 | 4.747 | 5.974 | 3.741 | 4.597 | 6.790 | 12.039 | 13.837 |
| Sekta ya binafsi* | 3.376 | 4.188 | 3.757 | 4.885 | 4.851 | 4.011 | 7.376 | 10.082 | 17.294 | 33.123 |
| Jumla — Rasilimali ya kudumu | 7.330 | 8.592 | 8.630 | 8.632 | 10.825 | 7.752 | 11.973 | 16.872 | 29.333 | 46.960 |
| Ongezeko la Limbikizo | 764 | 866 | 1.055 | 1.498 | 1.410 | 1.836 | 1.645 | 2.091 | 2.487 | 3.685 |
| Jumla Ongezeko la Limbikizo | 8.094 | 9.458 | 9.685 | 10.130 | 12.235 | 9.588 | 13.618 | 18.963 | 31.820 | 50.645 |

*Chanzo:* Idara ya Takwimu

+Non-profit making bodies.

*Includes Rural Own-account Construction.

## 3.—BIASHARA NA HALI YA MALIPO NA NCHI ZA NJE

### I. BIASHARA YA BIDHAA

1. Bidhaa zilizouzwa nchi za nje katika mwaka 1987, zilikuwa na thamani ya Sh. 17,629.0 milioni ikilinganishwa na Sh. 11.068.0 milioni zilizopatikana katika mwaka 1986. Thamani ya bidhaa zilizonunuliwa kutoka nchi za nje katika mwaka 1987 ilifikia Sh. 57,418 milioni, kutoka Sh. 30.270 milioni mwaka 1986. Maongezeko hayo makubwa katika thamani ya uuzaji na ununuzi kutoka nchi za nje yamesababishwa na urekebishaji wa thamani ya shilingi kwani kwa kutumia dola za Kimarekani, thamani ya uuzaji wa bidhaa nchi za nje ilibakia kwenye kiwango cha mwaka 1986 cha dola 347 milioni. wakati uagizaji wa bidhaa uliongezeka kidogo kutoka dola 1.047 milioni mwaka 1986 hadi dola 1,092.0 milioni katika mwaka 1987. Inakadiriwa kuwa uagiziaji bidhaa kwa fedha zisizopitia Benki Kuu ulifikia dola 300 milioni mwaka 1987, karibu asilimia 27.5 ya uagizaji wote.

**Bidhaa zilizouzwa nchi za nje:**

2. Katika mwaka 1987 kahawa iliingiza nchini kiasi cha Sh. 5,255 milioni ikilinganishwa na Sh. 5.348 milioni zilizopatikana mwaka 1986; ambao ni upungufu wa Sh. 93 milioni. Upungufu huu ulitokana na kushuka kwa bei ya kahawa katika soko la dunia kwa asilimia 38.7 kutoka dola 3.2 kwa kilo mwaka 1986 mpaka dola 1.9 kwa kilo katika mwaka 1987. Upungufu wa asilimia 20.0 katika kiasi cha kahawa iliyouzwa nje (kutoka tani 49,510 mwaka 1986 hadi 39,578 katika mwaka 1987) ulichangia pia katika upungufu wa mapato yatokanayo na mauzo.

3. Thamani ya pamba iliyouzwa nchi za nje katika mwaka 1987 ilikuwa Sh. 2,830.0 milioni ikilinganishwa na Sh. 1,033.0 milioni zilizopatikana mwaka 1986. Ongezeko hili lilitokana na kuongezeka kwa kiasi cha pamba iliyouzwa nchi za nje kutoka tani 31,938 mwaka 1986 hadi tani 43,843 katika mwaka 1987, ongezeko la asilimia 37.3. Bei ya pamba katika soko la dunia iliongezeka pia.

4. Katika mwaka 1987, thamani ya mauzo ya nyuzi za katani nchi za nje iliongezeka kutoka Sh. 159 milioni mwaka 1986 hadi kufikia Sh. 293 milioni. Ongezeko hili lilitokana hasa na ongezeko la kiasi cha katani iliyouzwa nje kwa asilimia 49.8 kutoka tani 11,776 mwaka 1986 hadi kufikia tani 17,648 mwaka 1987. Ongezeko katika kiasi lilisaidia pia kufidia upungufu wa mapato kwa zao hili ambalo lingeweza kutokea kutokana na kushuka kwa bei kwa asilimia 38.7 kutoka dola 394.85 kwa tani mwaka 1986 hadi dola 241.95 kwa tani katika mwaka 1987.

5. Kiasi cha chai iliyouzwa nchi za nje katika mwaka 1987 kiliongezeka kwa asilimia 4.0 kutoka tani 11,418 mwaka 1986 hadi kufikia tani 11,872. Thamani ya chai iliyouzwa nje ilipungua, kutoka dola 13.6 milioni zilizopatikana mwaka 1986 hadi kufikia dola 11.9 milioni katika mwaka

1987. Upungufu katika mapato yatokanayo na uuzaji wa chai nchi za nje ulisababishwa na kushuka kwa bei ya chai kwa asilimia 16.7 kutoka dola 1.2 kwa kilo mwaka 1986 hadi kufikia dola 1.0 kwa kilo katika mwaka 1987.

6. Thamani ya tumbaku iliyouzwa nje mwaka 1987 ilipungua kwa dola 2.9 milioni kutoka dola 13.1 milioni mwaka 1986 hadi kufikia dola 10.2 milioni. Hali hii ilisababishwa na upungufu katika kiasi cha tumbaku iliyouzwa nje kutoka tani 7,699 mwaka 1986 hadi kufikia tani 6,094 mwaka 1987 pamoja na kushuka kwa bei kwa asilimia 1.6.

7. Kulikuwa na ongezeko kubwa la bei ya korosho zisizobanguliwa la asilimia 295.3 katika mwaka 1987 kulinganisha na mwaka 1986 ambalo lilifidia upungufu wa kiasi kilichouzwa kwa asilimia 71.8. Kutokana na kuongezeka kwa bei, thamani ya korosho iliyouzwa nje iliongezeka kutoka dola 15.3 milioni mwaka 1986 hadi kufikia dola 17.0 milioni katika mwaka 1987.

8. Kwa mwaka wa pili mfululizo, mapato kutokana na mauzo ya karafuu nchi za nje yaliendelea kushuka zaidi. Thamani ya mauzo ya karafuu nchi za nje ilipungua kutoka dola 14.9 milioni zilizopatikana mwaka 1986 hadi kufikia kiasi cha dola 3.9 milioni katika mwaka 1987. Upungufu huu mkubwa ulisababishwa na kupungua kwa kiasi kilichouzwa nje kwa asilimia 57.7 kutoka tani 3.122 mwaka 1986 hadi kufikia tani 1,322 katika mwaka 1987 pamoja na kushuka kwa bei kwa asilimia 38.9 katika soko la dunia.

9. Bidhaa nyingine muhimu iliyouzwa nchi za nje ni almasi ambayo thamani ya mauzo yake ilishuka toka dola 5.9 milioni mwaka 1986 hadi kufikia dola 4.7 milioni mwaka 1987. Upungufu ulisababishwa na kushuka kwa bei ya almasi kwa asilimia 8.13 pamoja na kilichouzwa toka gramu 38,926 mwaka 1986 hadi kufikia gramu 17,036 katika mwaka 1987.

10. Bidhaa nyingi zilizouzwa nchi za nje zilinunuliwa na Nchi za Jumuiya ya Soko la Ulaya (EEC) pasipo Uingereza, ambazo zilichukua asilimia 36.4 ya mauzo yote. Wanunuzi wakubwa katika kundi hili ni Ujerumani Magharibi, Uholanzi, Italia na Ubelgiji. Nchi za Jumuia ya Madola zilinunua asilimia 24.5 ya bidhaa zilizouzwa nje na nchi za wanachama wa Nchi huru za Afrika zilinunua asilimia 10.0. Soko la Jumuia ya Nchi za Kijamaa (CMEA) zilinunua asilimia 2.4. Nchi nyingine ambazo ni pamoja na Marekani, Japani, Hongkong, China, Sweden na nyinginezo zilinunua asilimia 26.8 ya bidhaa zote zilizouzwa nchi za nje.

## II.—HALI YA MALIPO NA NCHI ZA NJE

11. Katika mwaka 1987, nakisi katika urari wa malipo na nchi za nje (Tanzania Bara) iliongezeka kwa dola 52.93 milioni toka dola 288.6 milioni mwaka 1986 kufikia nakisi ya dola 341.53 milioni. Nakisi hii kubwa imesababishwa na pengo kubwa katika biashara ya bidhaa pamoja na nakisi kubwa katika urari wa huduma kutokana na ongezeko kubwa la malipo ya riba.

12. Urari wa biashara ya bidhaa ulikuwa na nakisi ya dola 745.0 milioni sawa na ongezeko la asilimia 6.45 ikilinganishwa na mwaka 1986 uliokuwa na nakisi ya dola 699.89 milioni. Hapakuwepo ongezeko katika thamani ya bidhaa zilizouzwa nje, thamani yake ilikuwa dola 347 milioni sawa na ilivyokuwa mwaka 1986. Thamani ya bidhaa zilizoagizwa kutoka nje iliongezeka kutoka dola 1,047.46 milioni mwaka 1986 hadi dola 1,092.0 milioni katika mwaka 1987. Ongezeko la nakisi katika urari wa biashara ya bidhaa lilitokana na kuongezeka kwa thamani za bidhaa zilizoagizwa kutoka nje hasa bidhaa za rasilimali na za kati ambazo kwa pamoja ziligharimu dola 907.75 milioni.

13. Urari wa huduma kwa mwaka 1987 ulionyesha nakisi ya dola 124.0 milioni ikilinganishwa na nakisi ya dola 85.1 milioni mwaka 1986. Ongezeko kubwa katika nakisi lilitokana na kuongezeka katika malipo ya riba ambayo yalifikia dola 169.43 milioni pamoja na kupungua kwa mapato kutokana na huduma kutoka dola 110.0 milioni katika mwaka 1986 hadi kufikia dola 100.0 milioni mwaka 1987.

14. Katika mwaka 1987, urari wa uhamisho wa mali uliongezeka kwa dola 110.0 milioni kutoka dola 473.0 milioni mwaka 1986 hadi kufikia dola 583.0 milioni. Ongezeko katika ziada linatokana na kuongezeka kwa mapato ya uhamisho wa mali toka nchi rafiki na mashirika ya kimataifa kama ruzuku na vile vile uagizaji bidhaa uliofanywa na vyombo au watu binafsi bila kutumia fedha za Benki Kuu

15. Kutokana na mwenendo wa biashara na nchi za nje unavyoonyesha, urari wa biashara ya bidhaa, huduma pamoja na uhamisho wa mali, urari wa malipo ya kawaida (current account balance) kwa mwaka 1987 ulikuwa na nakisi ya dola 286.0 milioni ikilinganishwa na nakisi ya dola 312.0 milioni iliyotokea katika mwaka 1986. Unafuu huu katika urari wa malipo ya kawaida ulitokana na ziada kubwa katika urari wa uhamisho wa mali.

16. Kwa mwaka 1987 mapato kutokana na mikopo ya muda mrefu na wa kati kwa Serikali, mashirika na makampuni binafsi kuhusiana na rasilimali yaliongezeka kwa kiasi cha dola 48.0 milioni kutoka dola 165.0 milioni zilizoingia mwaka 1986 hadi kufikia dola 213.0 milioni. Ongezeko

hili lilitokana na kuongezeka kwa kiasi cha mikopo na misaada toka kwa wafadhili kuunga mkono juhudi za Taifa za kufufua uchumi. Malipo ya rasilimali yaliongezeka kutoka dola 186.0 milioni mwaka 1986 hadi kufikia dola 219.62 milioni.

17. Kwa upande mwingine, karadha za bidhaa zilikuwa na urari wa dola 4.78 milioni ukilinganisha na mapato ya dola 27.9 milioni kwa upande mmoja; na malipo ya dola 23.22 milioni kwa upande mwingine.

## THAMANI YA BIASHARA BAINA YA TANZANIA NA NCHI NYINGINE

Jedwali Na. 8

| Aina ya Biashara | (Sh. Milioni) 1983 | 1984 | 1985 | 1986 | 1987 | (US$ milioni) 1985 | 1986 | 1987 | Badiliko (%) 1986/87 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Zilizouzwa Nje (Exports) | 4,319 | 5,866 | 5,937 | 11,068 | 17,629 | 339·55 | 323·12 | 256·79 | -[illegible] |
| Bidhaa Halisi (Domestic Exports) | 4,187 | 5,761 | 5,832 | 10,905 | 17,036 | 333·54 | 318·37 | 248·15 | -22·05 |
| Zilizouzwa Tena (Re-Exports) | 132 | 1,105 | 105 | 163 | 593 | 6·01 | 4·76 | 8·64 | 81·52 |
| Zilizoagizwa (Imports) | 9,018 | 12,961 | 17,962 | 30,017 | 57,416 | 1,027·27 | 876·33 | 836·34 | -4·56 |
| Jumla (Exports + Imports) | 13,337 | 188,277 | 23,899 | 41,085 | 75,045 | 1,366·82 | 1,199·45 | 1,093·13 | -[illegible] |
| Urari (Exports Less Imports) | -4,699 | -7,095 | -12,025 | -18,949 | -39,787 | -687·73 | -553·21 | -570·55 | 4·76 |
| Thamani ya Fedha (Sh/US $) | 11·2626 | 15·5065 | 17·4851 | 34·2531 | 68·6313 | | | | |

## AINA ZA BIDHAA ZILIZOAGIZWA KUTOKA NCHI ZA NJE

Jedwali Na. 9

(Sh. Milioni)

| Mwaka | Bidhaa za Matumizi ya Kawaida | Bidhaa za Kati | | Bidhaa za Viwanda | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Vifaa vya Ujenzi | Nyinginezo | Vyombo vya Uchukuzi na Mashine | Vifaa Vingine | |
| 1980 | 1.430 | 676 | 3.435 | 1.128 | 3.560 | 10.229 |
| 1981 | 1.044 | 665 | 3.175 | 1.153 | 3702 | 9.739 |
| 1982 | 992 | 659 | 3.777 | 3746 | 1.325 | 10.499 |
| 1983 | 918 | 553 | 3.166 | 2.918 | 1.463 | 9.018 |
| 1984 | 1.225 | 829 | 4.981 | 4.070 | 1.856 | 12.961 |
| 1985 | 1.570 | 1.225 | 6.325 | 6.176 | 2.815 | 17.962 |
| 1986 | 2.145 | 2.103 | 9.737 | 11.014 | 5.271 | 30.270 |
| 1987* | 9.889 | 9.111 | 10.556 | 25.107 | 2.755 | 57.418 |

*Chanzo:* Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango.
*Takwimu za muda.

## MIZANIA YA MALIPO NA NCHI ZA NJE

Jedwali Na. 10 (US $ milioni)

| | 1985 Halisi | 1986 Halisi | 1987 Matarajio |
|---|---|---|---|
| A. *Urari wa Biashara* | −713·99 | −699·89 | −745·00 |
| Ziuzwazo nje (f.o.b.) | 285·60 | 347·57 | 347·00 |
| Zinunuliwazo nje (f.o.b.) | 999·19 | 1,047·10 | 1,092·00 |
| B. *Urari wa Huduma* | −68·10 | −85·10 | −124·00 |
| Mapato | 108·10 | 110·00 | 100·00 |
| Malipo | 176·20 | 195·10 | 224·00 |
| C. *Urari wa Uhamisho wa Mali* | 366·70 | 473.00 | 583·00 |
| Mapato | 394·30 | 501·00 | 610·00 |
| Malipo | 27·60 | 28·00 | 27·00 |
| Urari wa Biashara ya Bidhaa Huduma na Uhamisho wa Mali | −414·99 | −311·99 | −286·00 |
| D. Mikopo ya muda mrefu na wakati (Urari) | −18·50 | −21·00 | −6·62 |
| Iliyoingia | 200·00 | 165.00 | 213·00 |
| Iliyotoka | 218·50 | 186·00 | 219·62 |
| E. Misaada ya Bidhaa (Urari) | 28·00 | 122·60 | 4·78 |
| F. Makosa na Masahihisho | 10·99 | −78·21 | −53·69 |
| H. Urari wa Malipo yote | −394·60 | −288·60 | −341·53 |
| I. Mabadiliko katika akiba ya fedha za Kigeni ((−) = ongezeko) | +394·60 | +288·60 | +341·53 |

*Chanzo*:—Benki Kuu ya Tanzania.

Jedwali Na. 11

## AINA NA THAMANI YA BIDHAA ZILIZOAGIZWA KUTOKA NJE

| Aina | (Shs. Milioni) 1982 | 1983 | 1984 | 1985 | 1986 | 1987 | (US$ Milioni) 1985 | 1986 | 1987 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 0. Chakula | 986 | 911 | 1.223 | 1.533 | 2.124 | 3.312 | 87·67 | 62·01 | 48·24 |
| 1. Viburudisho na Tumbaku | 6 | 7 | 12 | 37 | 53 | 80 | 2·12 | 1·55 | 1·17 |
| 2. Bidhaa zisizosindikwa | 248 | 235 | 293 | 515 | 719 | 1.937 | 29·45 | 20·99 | 28·22 |
| 3. Mafuta ya petroli | 2.352 | 2.016 | 2.749 | 3.800 | 5.559 | 7.174 | 217·33 | 162·29 | 104·50 |
| 4. Mafuta ya mimea/wanyama | 149 | 67 | 229 | 233 | 446 | 581 | 13·33 | 13·02 | 8·46 |
| 5. Madawa | 1.028 | 848 | 1.710 | 1.777 | 3.362 | 5.916 | 101·63 | 98·15 | 86·17 |
| 6. Bidhaa za Viwanda | 1698 | 1.600 | 2228 | 3.189 | 5.470 | 10.556 | 182·38 | 159·69 | 153·76 |
| 61 & 62 Ngozi na mpira | 106 | 120 | 180 | 353 | 810 | 1286 | 20·19 | 23·65 | 18·73 |
| 63 & 64 Mbao na karatasi | 243 | 170 | 236 | 850 | 409 | 713 | 20·02 | 11·94 | 10·39 |
| 65 Nguo | 300 | 208 | 297 | 519 | 944 | 1092 | 29·68 | 27·56 | 15·91 |
| 66 Madini yasiyochuma | 122 | 158 | 152 | 204 | 357 | 832 | 11·67 | 10·42 | 12·12 |
| 67 Chuma na chuma pua | 401 | 436 | 636 | 652 | 1.132 | 3.436 | 37·29 | 33·05 | 50·05 |
| 68 Madini ya Vyuma aina nyingine | 111 | 125 | 134 | 197 | 278 | 571 | 11·27 | 8·12 | 8·32 |
| 69 Bidhaa za Chuma | 416 | 383 | 593 | 875 | 1.541 | 2.625 | 60·04 | 41·99 | 38·24 |
| 7. Mashine na vyombo vya uchukuzi | 3.746 | 2.918 | 4.070 | 6.176 | 10.784 | 25.107 | 353·22 | 314·83 | 365·72 |
| Magari madogo ya abiria | 99 | 62 | 73 | 133 | 330 | 847 | 7·61 | 9·63 | 12·34 |
| Magari mengine ya uchukuzi | 786 | 771 | 1.357 | 1.985 | 4088 | 9.185 | 113·53 | 119·35 | 133·79 |
| Mashine | 2.901 | 2.085 | 2.640 | 4.058 | 6.366 | 15075 | 232·08 | 185·85 | 219·59 |
| 8. Bidhaa nyingine za viwanda | 271 | 276 | 382 | 714 | 1.473 | 2.751 | 40·83 | 43·00 | 40·07 |
| 9. Bidhaa nyingine mbalimbali | 16 | 17 | 9 | 29 | 27 | 4 | 1·66 | ·79 | ·06 |
| Thamani ya Fedha (Sh./US $) | 9·3243 | 11·2626 | 15·5065 | 17·4851 | 34·2531 | 68·6513 | | | |

*Chanzo:*—Idara ya Forodha.

## THAMANI YA BIDHAA ZILIZOAGIZWA KUTOKA NCHI ZILIZOTAJWA

Jedwali Na. 12

| Nchi | (Sh. milioni) | | | | | (US$ milioni) | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1983 | 1984 | 1985 | 1986 | 1987 | 1985 | 1986 | 1987 |
| Nchi za OAU | 1.041 | 958 | 1,164 | 2 060 | 3,129 | 66·57 | 60·14 | 45·58 |
| Kenya | 97 | 117 | 361 | 1,254 | 1,785 | 20·65 | 36·61 | 26·00 |
| Uganda | 67 | 187 | 48 | 57 | 10 | 2·75 | 1·66 | ·15 |
| Jumuiya ya Madola | 2096 | 2,651 | 3,938 | 6,971 | 14,118 | 225·22 | 203·51 | 205·65 |
| Uingereza | 1204 | 1.502 | 2 278 | 3626 | 8.479 | 130·28 | 105·86 | 123·51 |
| Singapore | 60 | 124 | 123 | 308 | 444 | 7·03 | 8·99 | 6·47 |
| Canada | 144 | 103 | 341 | 346 | 737 | 19·50 | 10·10 | 10·74 |
| India | 175 | 200 | 233 | 451 | 1,181 | 13·33 | 13·17 | 17·20 |
| Australia | 31 | 85 | 71 | 113 | 328 | 4·06 | 3·30 | 4·78 |
| Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EEC)* | 3 900 | 5,593 | 7222 | 12 720 | 28,280 | 413·04 | 371·35 | 411·74 |
| Ubelgiji | 379 | 543 | 485 | 885 | 1.055 | 27·74 | 25·84 | 15·37 |
| Denmark | 150 | 281 | 365 | 1.039 | 2,813 | 20·87 | 30·33 | 40·98 |
| Ujerumani Magharibi | 1.099 | 1.399 | 1.461 | 3 203 | 7085 | 83·56 | 93·51 | 103·20 |
| Italia | 417 | 1.041 | 1,371 | 2011 | 5079 | 78·41 | 58·71 | 73·98 |
| Uholanzi | 440 | 624 | 642 | 1.186 | 2803 | 36·72 | 34·62 | 40·83 |
| Jumuiya ya Nchi za Kijamaa (CMEA) | 218 | 237 | 425 | 977 | 582 | 24·31 | 28·52 | 8·48 |
| U.S.S.R. | 64 | 50 | 130 | 235 | 95 | 7·43 | 6·86 | 1·38 |
| Yugoslavia | 65 | 81 | 234 | 674 | 391 | 13·38 | 19·68 | 5.70 |
| Nchi Nyingine | 3.362 | 5.365 | 7.833 | 12,672 | 22348 | 447·98 | 369·95 | 325·53 |
| Marekani | 311 | 472 | 656 | 951 | 1985 | 37·52 | 27·76 | 28·91 |
| Sweden | 246 | 447 | 551 | 954 | 1,757 | 31·51 | 27·85 | 25·59 |
| Japan | 961 | 1 264 | 1,607 | 3.470 | 6,526 | 91·91 | 101·30 | 95·06 |
| China | 127 | 240 | 285 | 470 | 557 | 16·30 | 13·72 | 8·11 |
| Hong Kong | 45 | 54 | 100 | 247 | 396 | 5.72 | 7·21 | 5·77 |
| Thamani ya Fedha (Shs/US $) | 11·2626 | 15·5065 | 17·4851 | 34.2531 | 68·6513 | | | |

*Chanzo*.—Idara ya Forodha.

*Spain na Portugal zimejiunga toka 1985.

## THAMANI YA BIDHAA ZILIZOPELEKEWA KWA NCHI ZILIZOTAJWA

Jedwali Na. 13

| Nchi | (Sh. milioni) 1983 | 1984 | 1985 | 1986 | 1987 | (US$ milioni) 1985 | 1986 | 1987 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Nchi za OAU | 470 | 632 | 324 | 697 | 1,956 | 18·53 | 20·35 | 28·49 |
| Kenya | 8 | 77 | 19 | 104 | 503 | 1·09 | 3·04 | 7·33 |
| Uganda | 29 | 48 | 35 | 190 | 180 | 2·00 | 5·55 | 2·62 |
| Jumuiya ya Madola | 885 | 1,538 | 1,402 | 2,790 | 4,854 | 80·18 | 81·45 | 70·71 |
| Uingereza | 18 | 821 | 852 | 1,367 | 1,879 | 48·73 | 39·91 | 27·37 |
| Singapore | 104 | 122 | 418 | 439 | 50 | 23·91 | 12·82 | ·73 |
| Canada | 18 | 43 | 19 | 34 | 30 | 1·09 | ·99 | ·44 |
| India | 83 | 327 | 91 | 503 | 1,120 | 5·20 | 14·68 | 16·31 |
| Australia | 13 | 26 | 15 | 20 | 91 | ·86 | ·58 | 1·33 |
| Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EEC)* | 2,050 | 3,241 | 2,957 | 6,398 | 7,215 | 169·12 | 186·79 | 105·10 |
| Ubelgiji | 85 | 82 | 130 | 249 | 316 | 7·43 | 7·27 | 4·60 |
| Denmark | 15 | 63 | 18 | 93 | 15 | 1·03 | 2·72 | ·22 |
| Ujerumani Magharibi | 708 | 1,261 | 1,196 | 2,678 | 2,071 | 68·40 | 78·18 | 30·17 |
| Italia | 231 | 369 | 258 | 540 | 586 | 14·76 | 15·76 | 8·54 |
| Uholanzi | 308 | 418 | 347 | 774 | 1,397 | 19·85 | 22·60 | 20·35 |
| Jumuiya ya Nchi za Kijamaa (CMEA) | 189 | 216 | 84 | 61 | 470 | 4·80 | 1·78 | 6·85 |
| U.S.S.R. | 49 | 51 | 24 | 23 | 102 | 1·37 | ·67 | 1·49 |
| Yugoslavia | 189 | 37 | 21 | 20 | 139 | 1·20 | ·58 | 2·02 |
| Nchi Nyingine | 1,080 | 1,470 | 1,557 | 2,714 | 5,323 | 89·05 | 79·23 | 77·54 |
| Marekani | 102 | 173 | 115 | 221 | 407 | 6·58 | 6·45 | 5·93 |
| Sweden | 17 | 13 | 12 | 27 | 63 | ·69 | ·79 | ·92 |
| Japan | 175 | 263 | 209 | 489 | 674 | 11·61 | 14·28 | 9·82 |
| China | 1 | 40 | 60 | 63 | 19 | 3·43 | 1·84 | ·28 |
| Hong Kong | 137 | 132 | 41 | 176 | 517 | 2·34 | 5·14 | 7·53 |
| Thamani ya Fedha (Shs/US $) | 11·2626 | 15·3065 | 17·4851 | 34·2531 | 68·6513 | | | |

*Chanzo*—Idara ya Forodha.

*Spain na Portugal zimejiunga toka 1985.

## BIASHARA KATI YA TANZANIA NA NCHI ZA SOKO NAFUU ZA MASHARIKI NA KUSINI MWA AFRIKA

Jedwali Na. 14 (Shs. milioni)

| | Bidhaa zilizouzwa | | Bidhaa zilizoagizwa | | Urari | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1986 | 1987 | 1986 | 1987 | 1986 | 1987 |
| Burundi ........................ | 56 | 57 | 12 | 256 | 44 | 99 |
| Ethiopia ........................ | 1 | 60 | 14 | 1 | −13 | 56 |
| Kenya ........................ | 105 | 503 | 1,254 | 1,785 | −1,149 | −1,282 |
| Lesotho ........................ | — | — | — | — | — | — |
| Malawi ........................ | 9 | 24 | 40 | 15 | −31 | 9 |
| Mauritius ........................ | 10 | 6 | 9 | 2 | 1 | 4 |
| Rwanda ........................ | 10 | 15 | 5 | 2 | 5 | 13 |
| Somalia ........................ | 33 | 15 | 7 | 4 | 26 | 11 |
| Swaziland ........................ | 1 | 2 | 6 | 50 | −5 | −48 |
| Uganda ........................ | 190 | 180 | 57 | 10 | 133 | 170 |
| Zambia ........................ | 31 | 106 | 294 | 463 | −263 | −357 |
| Zimbabwe ........................ | 14 | 33 | 94 | 193 | −80 | −160 |
| Thamani ya Fedha (Shs/US $) ... | 34·2531 | 68·6513 | 34·2431 | 68·6513 | 34·2531 | 68·6513 |

*Chanzo:*—Idara ya Takwimu.

## KIASI NA THAMANI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE

(Tani)

Jedwali Na. 15

(Shs. Milioni)

| Bidhaa | 1983 | 1984 | 1985 | 1986 | 1987 | Badiliko % (1986/87) | 1983 | 1984 | 1985 | 1986 | 1987 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kahawa | 50,250 | 54,634 | 43,054 | 49,510 | 39,578 | −20·00 | 1,427 | 2,293 | 2,031 | 5,348 | 5,255 |
| Pamba | 39,[illegible]70 | 28,760 | 22,107 | 31,938 | 43,843 | 37·30 | 689 | 754 | 514 | 1,033 | 2,830 |
| Katani* | 26,590 | 20,789 | 15,195 | 11,776 | 17,648 | 49·80 | 145 | 157 | 100 | 159 | 293 |
| Karafuu | 982 | 2,308 | 12,265 | 3,122 | 1,321 | −57·70 | 87 | 148 | 843 | 511 | 265 |
| Korosho | 10,514 | 33,497 | 21,608 | 60,963 | 17,184 | −71·80 | 72 | 335 | 193 | 523 | 1,169 |
| Chai | 16,601 | 11,110 | 11,654 | 11,418 | 11,872 | 4·00 | 243 | 359 | 279 | 455 | 822 |
| Tumbaku | 5,284 | 4,707 | 7,744 | 7,699 | 6,094 | −20·00 | 127 | 138 | 232 | 449 | 700 |
| Almasi† | 50,454 | 58,149 | 57,141 | 38,926 | 17,036 | −56·20 | 222 | 271 | 347 | 399 | 322 |

*Chanzo:*—Idara ya Forodha.

*Sisal Fibre.

†Kipimo ni gramu.

## BEI YA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE

Jedwali Na. 16

| Bidhaa | (Shs./tani) | | | | | | | (US $/tani) | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1976 | 1982 | 1983 | 1984 | 1985 | 1986 | 1987 | 1976 | 1985 | 1986 | 1987 | Badiliko% (1986/87) |
| Kahawa | 22.150 | 23.184 | 28.398 | 41.970 | 47.173 | 108.016 | 13.770 | 2,607·90 | 2,697·90 | 3,153.47 | 1,933·98 | −38·67 |
| Pamba | 11.040 | 13.491 | 17.325 | 26.217 | 23.251 | 32.333 | 64.546 | 1,299·77 | 1,329·70 | 943·94 | 940·20 | −·40 |
| Katani* | 2,830 | 4.420 | 5.453 | 7.552 | 6.581 | 13.523 | 16.610 | 333·18 | 376·38 | 394·85 | 241·96 | −38·72 |
| Karafuu | 35.980 | 81.578 | 88.595 | 64.125 | 68.732 | 163.686 | 200.235 | 4,236·03 | 3,930·89 | 4,778·72 | 2,916·70 | −38·96 |
| Korosho | 1.976 | 7.751 | 6.848 | 10.000 | 8.932 | 8.580 | 68.018 | 232·64 | 510·83 | 250·66 | 990·78 | 295·26 |
| Chai | 11.210 | 14.408 | 14.638 | 32.313 | 23.940 | 39.867 | 69.217 | 1,319·79 | 1,369·17 | 1,163·89 | 1,008·24 | −13·37 |
| Tumbaku | 22.260 | 17.687 | 24.025 | 29.318 | 29.959 | 58.261 | 114.898 | 2,610·74 | 1,713·41 | 1,700·90 | 1,673·65 | −1·60 |
| Almasi | 1.790 | 3.690 | 4.400 | 4.600 | 6.073 | 10.261 | 18.904 | 210·74 | 347·32 | 299·56 | 275·22 | −8·13 |
| Thamani ya Fedha (Shs./US $) | 8·4938 | 9·3243 | 11·2626 | 15·5065 | 17·4851 | 32·2531 | 68·6513 | | | | | |

*Sisal fibre.

*Chanzo*: Idara ya Takwimu.

# FAHIRISI YA BEI ZA BIDHAA MUHIMU ZILIZOUZWA NCHI ZA NJE

Jedwali Na. 17

| Bidhaa | (Fahirisi ya bei kwa kutumia US$) 1982 | 1983 | 1984 | 1985 | 1986 | 1987 | Badiliko Asilimia 1986/87 | (Fahirisi ya bei kwa kutumia T.Sh.) 1985 | 1986 | 1987 | Badiliko Asilimia 1986/87 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kahawa | 95 | 97 | 104 | 103 | 121 | 74 | −38·67 | 213 | 488 | 599 | 22·92 |
| Pamba | 111 | 118 | 130 | 102 | 73 | 72 | −·40 | 211 | 293 | 585 | 99·63 |
| Katani* | 142 | 145 | 146 | 113 | 119 | 73 | −38·72 | 233 | 478 | 587 | 22·81 |
| Karafuu | 207 | 186 | 98 | 93 | 113 | 69 | −38·96 | 191 | 455 | 557 | 22·33 |
| Korosho | 357 | 261 | 277 | 220 | 108 | 426 | 295·26 | 452 | 435 | 3.442 | 692·20 |
| Chai | 117 | 98 | 158 | 104 | 88 | 76 | −13·37 | 214 | 356 | 617 | 73·62 |
| Tumbaku | 72 | 81 | 72 | 65 | 65 | 64 | −1·60 | 135 | 262 | 516 | 97·21 |
| Almasi | 188 | 185 | 143 | 165 | 142 | 131 | −8·13 | 339 | 573 | 1056 | 84·13 |

*Sisal fibre.

*Chanzo:* Idara ya Takwimu.

## 4.—MAELEKEO YA FEDHA ZA SERIKALI

1. Bajeti ya Serikali ya mwaka 1987/88 ilikisiwa kuwa na jumla ya matumizi ya kiasi cha Sh. 77,326 milioni, ambazo zinajumlisha Sh. 60,071.0 milioni za matumizi ya kawaida, na Sh. 17,255.0 milioni za matumizi ya maendeleo. Makisio haya yana ongezeko la karibu Sh. 21,631·0 milioni au asilimia 39 toka makadirio ya Sh. 55,595·0 milioni ya kipindi cha mwaka uliopita wa 1986/87. Kwa upande mwingine, mapato ya kawaida yalikadiriwa kufikia Sh. 55,450.0 milioni ambazo zinajumlisha Sh. 8,850.0 milioni za misaada ya uagizaji bidhaa. Katika jumla ya Sh. 7,875.0 za mapato ya maendeleo toka humu nchini. Sh. 2,000.0 milioni zilikadiriwa kuwa mikopo isiyo ya mabenki kwa serikali; na mikopo ya serikali kutoka mabenki ilikadiriwa kuwa Sh. 236.0 milioni; mapato mengine yalikisiwa kufikia Sh. 10,258.0 milioni na pengo kutoka bajeti ya kawaida lilikadiriwa kufikia Sh. 4,621.0 milioni. Kiasi cha Sh. 9,382 milioni kilikisiwa kuwa mikopo na ruzuku kutoka nje hivyo kufanya jumla ya Sh. 17,255.0 milioni za mapato ya maendeleo.

2. Makadirio ya mwaka 1987/88 yalikuwa ni makubwa ikilinganishwa na mwaka uliopita (1986/87) ambapo mapato ya kawaida yalitegemewa kufikia Sh. 34,498.0 milioni na mapato ya maendeleo Sh. 15,859.0 milioni. Haya ni maongezeko ya karibu asilimia 60.7 kwa upande wa mapato ya kawaida na asilimia 8.8 kwa upande wa mapato ya maendeleo. Hadi kufikia mwisho wa mwezi Machi, 1988 matumizi yalifikia Sh. 43,405.1 milioni, matumizi ya kawaida yakiwa ni Sh. 37,310.3 milioni na matumizi ya maendeleo Sh. 6,094.8 milioni. Matokeo haya yalikuwa sawa na asilimia 62 ya makadirio ya matumizi ya kawaida na asilimia 35 ya makadirio ya matumizi ya maendeleo. Kuhusu mapato, matokeo hadi mwisho wa Machi 1988, yalifikia jumla ya Sh. 39,968.2 milioni za mapato ya kawaida ambazo ni sawa na asilimia 72 ya makadirio. Ufanisi mzuri ulipatikana katika ukusanyaji kodi ya mapato ambapo matokeo hadi Machi 1988 yalikuwa kiasi cha Sh. 8,386.3 milioni au asilimia 95.4 ya makadirio ya Sh. 8,792.0 milioni.

3. Kwa kuzingatia mwenendo halisi wa bajeti baada ya kutafakari matokeo hadi robo ya tatu ya mwaka 1987/88, mategemeo hadi Juni, 1988 ni kama ifuatavyo:—

(i) Mapato ya kawaida yanategemewa kuongezeka kwa kiasi cha Sh. 1,079.5 milioni na hivyo kufikia Sh. 56,529.5 milioni. Ongezeko hili linatokana na ufanisi katika mapato yaliyotokana na kodi; na hasa misaada ya uagizaji na gawio za mashirika.

(ii) Matumizi ya kawaida yanatarajiwa kuvuka kiwango kilichokadiriwa cha Sh. 60,071.0 milioni kwa kiasi cha Sh. 1,693.7 milioni na kufikia Sh. 61,764.7 milioni. Kuongezeka kwa matumizi ya kawaida kunatazamiwa kusababisha kuongezeka kwa pengo

(nakisi) la bajeti ya kawaida kwa kiasi cha Sh. 614.5 milioni. Hata hivyo maongezeko katika matumizi ya kawaida yatarekebishwa kidogo na upungufu katika matumizi ya maendeleo ambayo yanatarajiwa kufikia Sh. 15,091.0 milioni au asilimia 12.0 chini ya makisio ya Sh. 17,255.0 milioni. Wizara na mashirika ya umma zinategemewa kutumia kiasi cha Sh. 13,900.2 milioni tu badala ya Sh. 14,808.0 milioni zilizokisiwa na mikoa inategemewa kutumia Sh. 1.190.7 milioni ambazo ni chini ya nusu ya makisio ya Sh. 2,447.0 milioni.

(iii) Mapato kutoka nje yanategemewa kufikia Sh. 6,624.0 milioni. Kiasi hiki kinajumlisha mikopo na ruzuku. Mikopo isiyo ya mabenki inategemewa kuvuka malengo ya Sh. 2,000 milioni kwa Sh. 500 milioni; ambapo mikopo ya mabenki inatarajiwa kufikia Sh. 613.4 milioni.

4. Kuhusu mgawanyo wa huduma za Serikali, huduma za kawaida, ambazo ni pamoja na shughuli za kawaida (utawala, mambo ya nje na usalama); Ulinzi, Elimu, Afya, Nyumba na Jamii, zilipangiwa kutumia Sh. 34,201.6 milioni, sawa na asilimia 44.04 ya fedha zote zilizokuwa zimekisiwa kutumika katika mwaka 1987/88. Katika miaka ya nyuma, sekta hizi zilikuwa zinatumia zaidi ya asilimia 50 ya fedha zote. Katika makisio hayo ya mwaka 1987/88, Deni la Taifa lilipangiwa kutumia asilimia 33.78 ya fedha zote; ikilinganishwa na asilimia 25.25 katika mwaka 1986/87. Ongezeko katika matumizi ya Deni la Taifa yametokana na kupevuka kwa mikopo mingi ya ndani; lakini hasa kutokana na kupanda kwa matumizi ya madeni ya nje kufuatia kupungua thamani ya shilingi. Kwa upande mwingine, matumizi kwa ajili ya Huduma za Maendeleo, (hasa Kilimo, Uvuvi na Misitu; Madini, Viwanda na Ujenzi; Mabarabara na Madaraja) yameendelea mwaka 1987/88 kuwa katika kiwango cha asilimia 22 hadi 23 ya fedha zote za Serikali Kuu.

## MWENENDO WA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI

Jedwali Na. 18

| | 1983/84 Halisi | 1984/85 Halisi | 1985/86 Halisi | 1986/87 | | 1987/88 | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Makadirio | Mategemeo Halisi. | Makisio | Mategemeo |
| 1. BAJETI YA KAWAIDA | | | | | | | |
| 1. *Mapato ya Kawaida* | *15,490·1* | *19,143·0* | *22,321·0* | *34,498·0* | *34,499·5* | *55,450·0* | *56,529·5* |
| 1.1 *Mapato yatokanayo na Kodi* | *13,564·5* | *17,254·3* | *19,662·1* | *31,813·0* | *29,526·8* | *44,865·0* | *45,081·9* |
| 1.1.1 Ushuru wa Forodha | | 1,531·0 | 1,468·4 | 4,935·0 | 4,067·3 | 6,483·0 | 5,527·5 |
| 1.1.2 Kodi ya Mauzo (Ndani) | 9,593·2 | 8,878·3 | 9,289·0 | 14,711·0 | 12,425·0 | 21,312·0 | 20,358·2 |
| 1.1.3 Kodi ya Mauzo (Nje) | | 1,275·6 | 1,344·7 | 3,943·0 | 3,671·3 | 5,566·0 | 4,885·1 |
| 1.1.4 Kodi ya Mapato | 4,067·3 | 4,678·2 | 6,175·6 | 6,781·0 | 7,351·4 | 8,792·0 | 9,307·3 |
| 1.1.5 Kodi Nyingine | | 891·4 | 1,384·4 | 1,473·0 | 2,011·8 | 2,712·0 | 3,003·8 |
| 1.2 *Mapato yasiyotokana na Kodi* | *1,901·1* | *1,888·1* | *2,658·9* | *2,653·0* | *4,972·7* | *10,775·0* | *13,497·6* |
| 1.2.1 Kasma Na. 50 | 70·7 | 170·5 | 193·6 | 300·0 | 337·6 | 185·0 | 587·6 |
| 1.2.2 Misaada ya Uagizaji bidhaa | — | 1,185·0 | 1,489·1 | 1,189·0 | 3,112·2 | 8,850·0 | 9,700·0 |
| 1.2.3 Gawio za Mashirika ya Umma | 454·6 | 408·6 | 441·2 | 600·0 | 956·9 | 790·0 | 2,400·0 |
| 1.2.4 Mapato mengine (Wizara na Mikoa) | 1,284·1 | 75·0 | 474·0 | 501·0 | 501·0 | 685·0 | 685·0 |
| 1.2.5 Mapato mengine (Appropriation in Aid) | 91·7 | 49·0 | 61·0 | 65·0 | 65·0 | 75·0 | 75·0 |
| 2. *Matumizi ya Kawaida* | *16,626·6* | *21,336·5* | *27,402·3* | *39,736·0* | *39,309·8* | *60,071·0* | *61,765·0* |
| 2.1 Mfuko Mkuu wa Taifa | 2,711·6 | 4,192·2 | 6,510·0 | 11,468·6 | 11,660·4 | 21,405·8 | 20,405·8 |
| 2.2 Wizara | 10,789·4 | 11,807·7 | 14,323·9 | 18,646·4 | 20,624·0 | 25,562·9 | 29,871·4 |
| 2.3 Matumizi Maalum | | 1,049·3 | 999·99 | 3,282·0 | | 5,586·0 | |
| 2.4 Serikali za Mitaa | | 2,445·8 | 3,609·1 | 3,932·1 | 4,618·8 | 5,965·0 | 6,931·7 |
| 2.4.1 Halmashauri za Miji | | 429·0 | 633·0 | 682·4 | | 916·0 | |
| 2.4.2 Halmashauri za Wilaya | | 2,016·8 | 2,975·9 | 3,249·7 | 4,618·8 | 4,749·0 | 6,931·7 |
| 2.5 Tawala za Mikoa | 3,125·6 | 1,841·7 | 1,958·8 | 2,239·0 | 2,406·5 | 2,851·3 | 3,039·3 |
| 3. *Salio/Nakisi ya Bajeti ya Kawaida* | *−1,136·5* | *−2,193·5* | *−5,081·3* | *−7,305·0* | *−4,810·3* | *−4,621·3* | *−5,235·5* |
| 4. BAJETI YA MAENDELEO | | | | | | | |
| 4. *Mapato Kutoka Nchini* | *4,213·1* | *3,901·4* | *4,595·0* | *6,917·0* | *6,377·2* | *7,875·0* | *8,166·9* |
| 4.1.1 Salio/Nakisi ya Bajeti ya Kawaida | −1,136·5 | −2,193·5 | −5,081·3 | −7,305·0 | −4,810·3 | −4,621·3 | −5,235·5 |
| 4.1.2 Mikopo isiyo ya Mabenki | 675·2 | 1,125·0 | 1,308·0 | 2,143·0 | 2,556·7 | 2,000·0 | 2,500·0 |
| 4.1.3 Mikopo ya Mabenki | 3,374·0 | 3,310·4 | 4,925·0 | 2,500·0 | 1,656·3 | 226·0 | 613·4 |
| 4.1.4 Mapato mengine | 1,300·4 | 1,629·5 | 4,243·7 | 9,579·0 | 6,974·5 | 10,258·0 | 10,589·0 |
| 4.2 *Mapato Kutoka Nje* | *1,134·4* | *1,489·7* | *1,422·0* | *8,942·0* | *5,455·1* | *9,382·0* | *6,624* |
| 4.2.1 Mikopo | 679·2 | 853·5 | 594·0 | | | | |
| 4.2.2 Ruzuku | 455·2 | 685·2 | 828·0 | 8,942·0 | 5,455·1 | 9,382·0 | 6,624 |
| *Mapato ya Maendeleo* | *4,834·3* | *5,391·1* | *5,817·0* | *15,859·0* | *11,832·3* | *17,255·0* | *15,090·9* |
| 5. *Matumizi ya Maendeleo* | | | | | | | |
| 5.1 Wizara na Mashirika ya Umma | 4,197·2 | 4,467·1 | 4,964·0 | 14,482·0 | 11,832·3 | 14,808·0 | 13,900·2 |
| 5.2 Mikoa | 637·1 | 924·0 | 833·0 | 1,377·0 | | 2,447·0 | 1,190·9 |
| 5.3 Matumizi ya Maendeleo | 4,834·3 | 5,391·1 | 5,817·0 | 15,859·0 | 11,832·3 | 17,255·0 | 15,090·9 |

*Chanzo:*—Wizara ya Fedha, Mipango na Uchumi.

*Tanbihi:* (Takwimu katika Jedwali Na. 18 na 19 hazilingani kutokana na njia tofauti za utayarishaji wake)

## MGAWANYO WA HUDUMA ZA SERIKALI

Jedwali Na. 19 (Sh. milioni)

| Aina ya Huduma | 1983/84 Matumizi Kawaida | 1983/84 Matumizi Maendeleo | 1983/84 Jumla Halisi | 1984/85 Matumizi Kawaida | 1984/85 Matumizi Maendeleo | 1984/85 Jumla Halisi | 1985/86 Matumizi Kawaida | 1985/86 Matumizi Maendeleo | 1985/86 Jumla Halisi | 1986/87** Matumizi Kawaida | 1986/87** Matumizi Maendeleo | 1986/87** Jumla Halisi | 1987/88* Matumizi Kawaida | 1987/88* Matumizi Maendeleo | 1987/88* Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. HUDUMA ZA KAWAIDA | 4,373·2 | 354·7 | 4,727·9 | 7,125·3 | 877·3 | 8,002·6 | 13,902·9 | 809·9 | 14,712·8 | 11,335·6 | 1,447·4 | 12,783·0 | 14,850·4 | 2,184·9 | 17,035·3 |
| 1.1 Utawala | 2,908·7 | 253·6 | 3,162·3 | 4,877·7 | 639·0 | 5,516·7 | 8,381·7 | 620·8 | 9,002·3 | 7,579·3 | 1,175·2 | 8,754·7 | 9,225·0 | 1,830·5 | 11,055·5 |
| 1.2 Mambo ya Nje | 199·7 | 4·1 | 203·8 | 351·5 | 4·7 | 356·2 | 1,432·3 | 1·0 | 1,433·3 | 1,099·7 | 48·7 | 1,148·4 | 1,432·3 | 48·7 | 1481·0 |
| 1.3 Usalama | 1,264·8 | [illegible] | 1,264·8 | 1,896·1 | 233·6 | 2,129·7 | 4,088·9 | 188·1 | 4,277·0 | 2,656·6 | 223·5 | 2,880·1 | 4,193·1 | 305·7 | 4,498·8 |
| 2. ULINZI | 2,319·3 | 424·4 | 2,743·7 | 3,201·7 | 457·1 | 3,658·8 | 4,398·0 | 551·2 | 4,949·2 | 5,802·3 | 858·3 | 6,660·6 | 6,323·4 | 943·5 | 7,266·9 |
| 3. ELIMU | 2,203·4 | 299·2 | 2,502·6 | 1,481·9 | 313·2 | 1,795·1 | 1,900·7 | 420·5 | 2,321·2 | 3,109·2 | 1,117·9 | 4,227·1 | 3,283·0 | 885·2 | 4,168·2 |
| 4. AFYA | 1,092·5 | 78·3 | 1,170·8 | 1,270·4 | 58·3 | 1,328·7 | 2,381·5 | 64·8 | 2,446·3 | 2,063·3 | 149·3 | 2,212·6 | 2,764·1 | 309·9 | 3,074·0 |
| 5. HUDUMA ZA JAMII | 42·7 | 19·4 | 62·1 | 106·2 | 18·3 | 125·0 | 96·7 | 26·2 | 122·9 | 118·1 | 32·3 | 150·4 | 194·2 | 133·4 | 327·6 |
| 6. NYUMBA NA MASLAHI YA JAMII | 125·1 | 86·6 | 211·7 | 123·9 | 132·9 | 256·8 | 172·5 | 161·2 | 333·7 | 255·7 | 197·6 | 453·3 | 219·3 | 339·6 | 558·9 |
| 6.1 Nyumba | 33·8 | 30·7 | 64·5 | 3·5 | 76·8 | 80·3 | 14·8 | 34·1 | 48·9 | 4·8 | 56·6 | 61·4 | 14·8 | 141·4 | 156·2 |
| 6.2 Ustawi wa Jamii | 91·3 | 23·4 | 114·7 | 80·2 | 9·1 | 89·3 | 153·8 | 10·1 | 163·9 | 249·2 | 74·7 | 323·9 | 200·6 | 67·7 | 263·3 |
| 6.3 Usafi wa Mazingira | 0·0 | 32·5 | 32·5 | 40·2 | 47·0 | 87·2 | 3·9 | 117·0 | 120·9 | 1·7 | 66·3 | 68·0 | 3·9 | 135·5 | 139·4 |
| 7. HUDUMA NYINGINE ZA JAMII | 396·2 | 43·7 | 439·9 | 563·1 | 26·0 | 589·1 | 731·3 | 39·6 | 770·9 | 856·2 | 93·6 | 949·8 | 1,358·7 | 412·0 | 1,770·7 |
| 8. HUDUMA ZA MAENDELEO | 2,045·3 | 3,528·0 | 5,573·3 | 2,434·6 | 4,028·7 | 6,463·3 | 2,987·0 | 3,917·3 | 6,904·3 | 4,260·5 | 8,145·8 | 12,406·3 | 5,185·0 | 12,046·5 | 17,231·5 |
| 8.1 Utawala | 223·5 | 261·0 | 484·5 | 363·5 | 405·7 | 769·2 | 335·1 | 552·4 | 887·5 | 420·4 | 540·0 | 960·4 | 513·1 | 923·1 | 1,436·2 |
| 8.2 Kilimo, Uvuvi na Misitu | 698·2 | 881·7 | 1579·9 | 883·4 | 770·7 | 1,654·1 | 1,096·0 | 896·0 | 1,992·0 | 1,341·7 | 3,008·5 | 4350·2 | 1,796·9 | 3,915·5 | 5,712·4 |
| 8.3 Madini Viwanda na Ujenzi | 201·4 | 1,290·3 | 1,491·7 | 225·6 | 1,448·9 | 1,674·5 | 169·1 | 1,003·5 | 1,172·6 | 201·6 | 2,395·5 | 2,597·1 | 249·0 | 3,212·4 | 3,461·4 |
| 8.4 Maji na Umeme | 325·4 | 386·7 | 712·1 | 299·9 | 379·7 | 679·6 | 413·4 | 467·0 | 880·4 | 549·6 | 909·0 | 1,458·6 | 588·8 | 1,317·8 | 1,906·6 |
| 8.5 Mahsaraburu na Madaraja | 426·5 | 468·3 | 895·3 | 414·6 | 562·1 | 976·7 | 361·6 | 558·7 | 920·3 | 560·1 | 685·3 | 1,245·4 | 688·8 | 1,311·9 | 2,000·7 |
| 8.6 Usafiri Majini | 0·0 | 0·7 | 0·7 | 6·8 | 6·9 | 13·7 | 10·2 | 19·2 | 29·4 | 88·3 | 20·2 | 108·5 | 56·5 | 52·0 | 108·5 |
| 8.7 Usafiri Mwingine na Mawasiliano | 174·2 | 225·6 | 399·8 | 235·2 | 452·8 | 688·0 | 595·9 | 420·0 | 1,015·9 | 1089·9 | 559·1 | 1697·0 | 1,277·6 | 1,284·8 | 2,562·4 |
| 8.8 Huduma Nyingine (Utalii) | 6·1 | 3·2 | 9·3 | 5·6 | 1·9 | 7·5 | 5·7 | 0·5 | 6·2 | 8·9 | 28·2 | 37·1 | 14·3 | 29·0 | 43·3 |
| 9. MENGINEYO | 4,028·9 | 0·0 | 4,028·9 | 5,219·0 | 0·0 | 5,219·0 | 7,203·1 | 0·0 | 7,203·1 | 13,457·5 | 0·0 | 13,457·5 | 26,234·8 | 0·0 | 26,234·8 |
| 9.1 Deni la Taifa | 3,881·6 | 0·0 | 3,881·6 | 5,031·8 | 0·0 | 5,031·8 | 6,851·8 | 0·0 | 6,851·8 | 13,141·9 | 0·0 | 13,141·9 | 25,806·9 | 0·0 | 25,806·9 |
| 9.2 Huduma za Fedha | 11·9 | 0·0 | 11·9 | 8·3 | 0·0 | 1·3 | 16·8 | 0·0 | 16·8 | 24·5 | 0·0 | 24·5 | 111·5 | 0·0 | 111·5 |
| 9.3 Malipo ya Uzeeni | 135·4 | 0·0 | 135·4 | 178·9 | 0·0 | 178·9 | 334·5 | 0·0 | 334·5 | 291·1 | 0·0 | 291·1 | 316·4 | 0·0 | 316·4 |
| Jumla ... | 16,626·6 | 4,834·3 | 21,460·9 | 21,526·1 | 5,912·3 | 27,438·4 | 33,773·7 | 5,990·7 | 39,764·4 | 41,258·4 | 12,012·2 | 53,300·6 | 60,412·9 | 17,255·0 | 77,667·9 |

Chanzo: Idara ya Takwimu.
** Makadirio Yaliyoidhinishwa
* Makadirio.

## 5.—FEDHA. MABENKI NA MASHIRIKA MENGINE YA FEDHA UKUAJI WA KARADHA NA UJAZI WA FEDHA

**Ukuaji wa Karadha:**

1. Maendeleo katika ukuaji wa karadha na kupanuka kwa ujazi wa fedha yamekuwa kinyume cha malengo. Japokuwa karadha kwa bodi za mazao na Shirika la Taifa la Usagishaji ilipangwa kupunguzwa kwa kiasi cha Sh. 1,400 milioni katika mwaka 1987/88, matarajio ni kwamba badala yake kutakuwepo na ongezeko la kiasi cha Sh. 7,290 milioni la karadha. Lengo limevukwa kupita kiasi kwa kuwa hisia zilizotumiwa katika kuliweka hazikutekelezwa. Hisia kubwa zilikuwa kwamba Shirika la Usagishaji lingerekebishwa kimuundo na ki-utekelezaji kusudi liwe mnunuzi wa mwisho wa nafaka na mdhibiti wa akiba ya dharura ya nafaka. Hatua zinazotakiwa kutekeleza hayo hazikuchukuliwa. Hii ilisababisha karadha kwa bodi za mazao na Shirika la Usagishaji kuongezeka zaidi ya mara sita katika nusu ya kwanza ya 1987/88 kutoka makadirio ya Sh. 1,600 milioni hadi Sh. 9,760·9 milioni. Katika jumla ya nyongeza hii, Shirika la Usagishaji lilitumia asilimia 52·0; ambapo Bodi ya Pamba ilitumia asilimia 24 na Bodi ya Tumbaku asilimia 12·4.

2. Karadha kwa vyombo vingine, mbali ya bodi za mazao, Shirika la Usagishaji na Vyama vya Ushirika, ilipangwa kuongezeka kwa Sh. 13,023.4 milioni au kwa asilimia 90. Madhumuni ya nyongeza hii kubwa yalikuwa kukidhi mahitaji ya viwanda na sekta ya biashara hasa kutokana na kupungua kwa thamani ya fedha. Matokeo kwa kipindi cha Julai—Desemba 1987/88 yanaonyesha kwamba karadha kwa vyombo hivi iliongezeka kwa kiasi cha Sh. 4,376 milioni tu; ikidhihirisha wazi kwamba sekta hizi muhimu zimebinywa kupatiwa karadha katika mazingira ya hali ngumu ya ukwasi. Karadha kwa Vyama vya Ushirika iliongezeka kwa zaidi ya asilimia 100 au Sh. 7,526·7 milioni. Na kwa pamoja, Vyama vya Ushirika, bodi za mazao na Shirika la Taifa la Usagishaji, vilitumia kiasi cha asilimia 80 ya karadha yote ya kibiashara katika mwaka 1987/88. Maendeleo yaliyoelezwa hapo juu katika kipindi cha Julai—Desemba, 1987/88 yalisababisha ongezeko la jumla la karadha la asilimia 32·8 au Sh. 21,455·5 milioni, na ongezeko la asilimia 36·7 katika ujazi wa fedha, tafsiri pana.

3. Hadi mwisho wa mwaka 1987/88 matarajio ni kwamba karadha kwa ujumla itakuwa na ongezeko la Sh. 22,655·8 milioni, sawa na asilimia 34·6 ikilinganishwa na makadirio ya ongezeko la Sh. 11,326·8 milioni au asilimia 17. Katika jumla hiyo, mikopo ya serikali kutoka mabenki inategemewa kuongezeka kwa sh. 1,900 milioni au asilimia 5·6. Karadha

kwa sekta nyingine inatarajiwa kuongezeka ifuatavyo: Bodi za Mazao Sh. 7,299 milioni au asilimia 67·8; Vyama vya Ushirika Sh. 4,728·8 milioni au asilimia 69·8; na Sekta nyingine za Uzalishaji na Biashara— sh. 8,728 milioni, sawa na asilimia 62·5 ikilinganishwa na makisio ya ongezeko la Sh. 13,023·4 milioni au asilimia 90.

**Hali ya Fedha za Kigeni:**

4. Akiba halisi ya fedha za kigeni ilikisiwa kuonyesha nafuu ya dola 20 milioni kutoka nakisi ya sh. 13,264·1 milioni hadi nakisi ya Sh. 12,355·5 milioni. Dalili zinaonyesha malengo hayo yatafikiwa hadi mwisho wa 1987/88.

**Ujazi wa Fedha:**

5. Kwa jumla maendeleo haya yanatarajiwa kusababisha ongezeko la Sh. 9,750 milioni au asilimia 20·1 la Ujazi wa Fedha, ambapo makadirio yalikuwa ongezeko la Sh. 4,928·6 milioni (asilimia 10·7). Athari zake zitaweza kuvuruga lengo la kupunguza ukuaji wa haraka wa bei na kuleta uwiano unaostahili kati ya fedha na sekta halisi katika uchumi.

## MABENKI NA MASHIRIKA MENGINE YA FEDHA

**Benki Kuu ya Tanzania:**

6. Mpaka mwisho wa Desemba 1987, mapato ya Benki Kuu yalifikia kiasi cha Sh. 5,427·5 milioni. Hili ni ongezeko la kiasi cha Sh. 3,563·1 milioni au asilimia 191·0 ikilinganishwa na Sh. 1,864·5 milioni zilizoidhinishwa mwishoni mwa Desemba 1986. Katika kipindi cha mwaka huu Benki Kuu imetumia jumla ya Sh. 2,330·6 milioni ambalo ni ongezeko la kiasi cha Sh. 1,025·0 milioni au asilimia 92 ikilinganishwa na sh. 1,305·6 milioni zilizotumika mwaka uliopita.

7. Mpaka mwisho wa mwezi Desemba, nusu ya kipindi cha mwaka 1987/88, jumla ya amana zote katika Benki Kuu zilikuwa kiasi cha Sh. 17,251·7 milioni, ambazo zinajumlisha Sh. 12,111·9 milioni za malimbikizo ya fedha za kigeni za Benki ya Taifa ya Biashara (NBC).

Hili ni ongezeko la Sh. 7,231·5 milioni au asilimia 72·0 ikilinganishwa na Sh. 10,020·2 milioni zilizokuwepo mwisho wa Desemba mwaka uliopita. Fedba zilizokuwa mikononi mwa watu zilifikia kiasi cha Sh. 26,328·5 milioni ikilinganishwa na Sh. 19,451·6 milioni zilizokuwa mikononi mwa watu mwaka uliopita.

8. Jumla ya mikopo yote kwa Serikali na Mabenki ilifikia kiasi cha Sh. 20,283·0 milioni hadi Desemba 1987, kati ya hizo Sh. 19,782·0 milioni ni mikopo iliyotolewa kwa mabenki na Sh. 501·0 milioni kwa Serikali. Mwaka uliopita wa 1986, Mabenki yalikopeshwa Sh. 1,726·0 milioni tu.

9. Dhamana ya Taifa (Government Securities) inayoshikiliwa na Benki Kuu ilifikia Sh. 33,190·0 milioni ikilinganishwa na kiasi cha Sh. 31,191·8 milioni kilichoshikiliwa mwishoni mwa 1986.

**Benki ya Taifa ya Biashara:**

10. Katika kipindi cha mwaka 1987, amana za Benki zimeongezeka kwa kiasi cha Sh. 8,014·5 milioni, toka kiasi cha Sh. 30,693·1 milioni zilizokusanywa hadi Desemba 1986, hadi Desemba 87 kilifikia Sh. 38,707·6 milioni. Ongezeko hili kubwa la amana limetokana na jitihada za Benki kukusanya amana kutoka kwa wateja wake.

11. Mikopo ya Benki kwa sekta mbali mbali katika kipindi cha mwaka 1987 ililikia kiasi cha Sh. 47,261·6 milioni ikilinganishwa na kiasi cha Sh. 23,496·6 milioni cha mkopo kilichotolewa hadi Desemba mwaka uliotangulia wa 1986. Hili ni sawa na ongezeko la kiasi cha Sh. 23,765·0 milioni au zaidi ya asilimia 100. Sehemu kubwa ya ongezeko hilo ilikwenda kwenye ununuzi wa mazao ya kilimo, ambapo hadi Desemba 1987 kiasi cha 33,561·1 milioni kilikopwa ililinganishwa na kiasi cha Sh. 17,003·7 milioni kilichokopwa hadi Septemba 1986. Sekta nyingine, hasa viwanda na biashara zilipata kiasi cha Sh. 9,371·6 milioni.

12. Matumizi ya Benki kwa kipindi cha mwaka 1986/87 yalifikia kiasi cha Sh. 7,761·0 milioni ikilinganishwa na Sh. 1,915·8 milioni zilizotumika katika kipindi cha mwaka 1985/86. Matumizi haya makubwa yametokana na kuongezeka kwa matumizi ya malipo ya riba kwa wateja ambayo yalifikia kiasi cha Sh. 6,568·0 milioni ililinganishwa na kiasi cha Sh. 1,066·8 kilichotumika mwaka wa 1985/86 halikadhalika malipo kwa shughuli za nje yalikuwa kiasi cha Sh. 10,344·4 milioni amba o katika mwaka 1985/86 hakukuwa na malipo yoyote.

13. Katika kipindi cha 1986/87 Benki imeweza kupata mapato makubwa yaliyofikia kiasi cha Sh. 10,744·7 milioni ikilinganishwa na Sh. 2,769·2 zilizopatikana katika kipindi cha mwaka uliopita. Hili ni ongezeko la kiasi cha Sh. 8,005·5 milioni. Ongezeko kubwa la mapato limetokana na kuongezeka kwa mapato yanayotokana na riba inayolipwa kwenye mikopo ambayo ilifikia kiasi cha Sh. 9,435·7 milioni ililinganishwa na Sh. 1,995·2 zilizopatikana mwaka wa 1985/86. Mapato kutokana na Commission pia yaliongezeka na kufikia Sh. 1,037·5 milioni toka Sh. 412·3 milioni katika kipindi cha mwaka 1985/86. Kutokana na kuongezeka kwa mapato kwa kiasi kikubwa, faida halisi imeongezeka na kufikia Sh. 1,499·2 milioni katika mwaka 1986/87 ikilinganishwa na faida halisi ya Sh. 376·6 milioni iliyopatikana mwaka 1985/86.

14. Benki imekuwa ikiendesha na kupanua shughuli zake kutokana na jinsi mahitaji ya wateja wake yanavyozidi kuongezeka. Hata hivyo, baadhi ya matatizo yaliendelea kuikabili Benki na kt ahabisha upungufu katika utoaji huduma katika baadhi ya sehemu. Matatizo hayo ni pamoja

na ukosefu au upungufu wa fedha za kigeni kwa ajili ya kununulia mashine na magari kwa ajili ya shughuli za Benki; upungufu wa wafanyakazi wenye ujuzi; ukosefu wa sehemu zinazofaa kujenga na kuongeza matawi yake pamoja na nyumba za wafanyakazi; ukosefu wa vituo vya Polisi katika baadhi ya maeneo huko vijijini ambayo yangefaa kufunguliwa matawi ya Benki; kukosekana au kupungua vifaa vya ujenzi; na hali ya kupanda haraka kwa bei ambayo inaendelea katika uchumi wetu ambayo inasababisha bei zote za malighafi au bidhaa zinazosaidia kuongeza ufanisi katika shughuli za Benki kuwa juu.

15. Licha ya kuendelea matatizo haya, Benki iliendelea kujitahidi kuongeza ufanisi na kutoa huduma nzuri kwa wateja wake. Kwa hiyo basi Benki inaelekeza mkazo mkubwa katika:—

(i) Kuongeza ufanisi katika huduma kwa wateja wake.
(ii) Kuongeza na kupanua shughuli zake hadi vijijini ili kuongeza mapato.
(iii) Kuongeza na kuelekeza karadha katika sekta ya kilimo na vijijini.
(iv) Kutoa mikopo ya kati na muda mrefu katika sekta zote muhimu katika uchumi.
(v) Kuwianisha na kuimarisha shughuli za benki za kimataifa na biashara ya nje.

Benki ya Ushirika na Maendeleo Vijini:

16. Katika kipindi cha mwaka 1986/87, Benki iliidhinisha jumla ya mikopo 516 yenye thamani ya sh. 1.967·5 milioni ikilinganishwa na mikopo 449 yenye thamani ya Sh. 1,234·9 milioni ya mwaka 1985/86.

17. Ki—mkopaji, kiasi kikubwa cha fedha kilitolewa kwa Vyama Vikuu vya Ushirika vilivyopata Sh. 1,507·8 milioni, ikifuatiwa na Wakopaji Binafsi waliopata Sh. 260·1 milioni; na Makampuni na Mashirika yaliyopata Sh. 132·1 milioni. Mfumo huu wa wakopaji ulikuwa hivyo pia katika mwaka 1985/86. Mwenendo huu wa ukopeshaji unaonyesha kwamba kumekuwa na mabadiliko makubwa katika mfumo wa wakopaji kutoka Benki ya Ushirika na Maendeleo Vijijini. Japokuwa hadi mwaka 1984/85 vilikuwa vijiji 801 vilivyokopa Sh. 244·5 milioni, vikifuatiwa na Wakopaji Binafsi 591 waliokopa Sh. 83·1 milioni; na Vyama vya Msingi 54 vilivyokopa Sh. 68·9 milioni; na wakopaji wengine wadogo wadogo; hadi kufikia mwaka 1986/87 mambo yalikuwa yamebadilika. Vijiji vya msingi havikopi tena. Badala yake Vyama Vikuu vya Ushirika 26 vilikuwa ndiyo wateja wakubwa wa Benki. Vijiji 36 tu ndiyo vilikuwa vimesalia vikakopa Sh. 25 milioni tu; na kwa jumla, idadi ya wakopaji wa mwanzoni mwa miaka ya themanini wamepungua sana. Kurejeshwa kwa Vyama vya Ushirika katika mwaka 1984 yayumkinika kumesababisha kubinywa kwa wakopaji wengine wengi kutoka Benki hii kwani katika miaka ya 1985/86 na 1986/87 Vyama Vikuu vya Ushirika

vilitumia wastani wa asilimia 82 ya mikopo yote kwa mwaka. Ki-mradi pembejeo za majira zimeendelea kupatiwa asilimia kubwa ya mikopo hiyo ikifuatiwa na usafiri vijijini—asilimia 28·09 (1986/'87) kutoka asilimia 6·2 katika mwaka 1985/86.

Mapato ya Benki katika kipindi cha 1986/87 yalifikia Sh. 405·0 milioni, ambapo mwaka uliotangulia wa 1985/86 Benki ilipata Sh. 181·9 milioni, hili ni ongezeko la kiasi cha Sh. 223·1 milioni. Ongezeko hili kubwa limetokana na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na shughuli mpya za kibiashara za Benki (Commercial banking).

18. Matumizi yaliongezeka kutoka Sh. 178·7 milioni mwaka 1985/86 hadi kufikia Sh. 365·0 milioni katika kipindi cha mwaka 1986/'87. Sehemu kubwa ya matumizi yalikuwa ni riba kwa mikopo inayopokelewa na Benki ambapo kiasi cha sh. 137·2 kililipwa.

19. Faida taslimu iliongezeka kutoka Sh. 3·3 milioni katika mwaka 1985/86 hadi kufikia Sh. 39·9 milioni, hili ni sawa na ongezeko la kiasi cha Sh. 36·6 milioni. Ongezeko hili kubwa limetokana na kuongezeka kwa mapato kwa kiasi kikubwa cha Sh. 223·1 milioni. Katika jumla ya kiasi cha Sh. 405 milioni kilichopatikana sehemu kubwa imetokana na inayotozwa kwenye mikopo ambayo imeongezeka sana toka Sh. 162·5 zilizopatikana mwaka 1985/86 mpaka kiasi cha Sh. 364·6 katika kipindi cha 1986/'87. Hili ni ongezeko la kiasi cha Sh. 202·1 milioni.

20. Tatizo kubwa linaloendelea kuikabili Benki hivi sasa ni wakopaji wengi, hasa Vyama vya ushirika kushindwa kulipa madeni; hivyo kuifanya Benki kukabiliwa na hali ngumu ya ukwasi. Hata hivyo, ili kutafuta ufumbuzi wa haraka wa suala hili la upungufu wa fedha, Benki iliamua kufungua matawi ambayo yangefanya shughuli za kibiashara. Mpaka sasa Benki hii ina matawi hayo ya shughuli za kibiashara yapatayo tisa ambayo ni Lumumba, Morogoro, Shinyanga, Mwanza, Singida, Moshi, Arusha, Tanga na Iringa. Lengo ni kufungua matawi kama haya katika mikoa yote ifikapo mwaka 1992. Pia Benki inatarajia kuchukua shughuli za ununuzi wa mazao ambazo awali zilikuwa zikifanywa na Benki ya Taifa ya Biashara.

**Shirika la Bima la Taifa:**

21. Mapato yatokanayo na bima za maisha yanatarajiwa kupungua kwa Sh. 3·4 milioni kutoka Sh. 293·0 milioni mwaka 1987. Upungufu huo wa mapato katika bima za maisha unatokana na hali mbaya ya uchumi ambayo imeathiri mapato ya wateja., Kutokana na hali hiyo wateja wengi wameiona bima ya maisha kama ni anasa na wengi waliokuwa na bima hiyo hawaoni umuhimu wa kuendelea nayo. Vile vile shirika linaendelea kuwa na tatizo la idadi ya wateja wapya wa bima za maisha kuendelea kushuka. Pia kupungua kwa ajira katika mashirika

na serikali kumepunguza watu ambao wangekuwa na uwezo wa kuchukua bima za maisha na hii imesababisha kuongeza idadi ya wateja wanaokatiza mikataba yao na shirika. Mapato kutokana na bima nyinginezo yaani bima za magari, moto, anga, maji na nyinginezo yalitarajiwa kuongezeka kwa Sh. 569·7 milioni kutoka Sh. 1,145·3 milioni zilizopatikana mwaka 1986 hadi kufikia Sh. 1,715·0 milioni katika mwaka 1987. Ongezeko kubwa katika mapato ya bima nyinginezo linatokana na kuongezeka kwa bima za magari kufuatia kuongezeka kwa idadi ya magari nchini pamoja na wateja kuongeza viwango vyao vya bima (comprehensive covers) za vifaa walivyoviwekea bima baada ya kuona umuhimu wa kufanya hivyo. Vile vile kumekuwa na ongezeko katika viwango vya bima za magari. Mfuko wa Akiba wa Mashirika ya Umma unatarajiwa kupungua kwa Sh. 42·7 milioni kutoka Sh. 322·7 milioni za mwaka 1986 hadi kufikia Sh. 280·0 milioni mwaka 1987. Sababu kubwa ya upungufu inatokana na mashirika mengi kushindwa kutoa michango kama inavyotakiwa na hii imesababishwa na hali mbaya ya ukwasi (adverse liquidity position) ya mashirika mengi. Vile vile mashirika mengi bado hayajatekeleza ongezeko la mishahara ambayo ingeanza kutumika mwezi Julai 1987.

22. Matumizi yanayotokana na shughuli za kawaida yalitarajiwa kufikia Sh. 372·2 milioni katika mwaka 1987 ikilinganishwa na Sh. 298·6 milioni za mwaka 1986. Katika kipindi cha mwaka 1987, Shirika la Bima lilitarajia kuwekeza Sh. 3,046·22 milioni katika sekta mbalimbali ikilinganishwa na Sh. 2,514·5 milioni zilizowekezwa mwaka 1986. Kati ya kiasi hicho, Sh. 1,603 milioni zilitarajiwa kuwekezwa katika dhamana za serikali ikilinganishwa na Sh. 1,211·7 milioni katika mwaka 1986.

**Benki ya Nyumba Tanzania:**

23. Katika mwaka 1986/87 kulikuwa na ongezeko la mapato ya benki kwa kiasi cha Sh. 204·6 milioni kutoka Sh. 207·7 milioni mwaka uliopita hadi kufikia Sh. 412·3 Sh milioni. Kuongezeka kwa mapato kunatokana na kurudisha mikopo na kupanda kwa riba inayotozwa kwenye mikopo. Kwa upande wa matumizi, yalifikia Sh. 236·1 milioni kutoka Sh. 162·7 milioni mwaka 1985/86. Maongezeko katika matumizi yametokana na kuongezeka kwa faida itolewayo na Benki kwa amana za wateja. Aidha gharama za uendeshaji na uwekezaji zimepanda kutokana na kuongezeka haraka kwa bei katika mazingira ya uchumi unaozorota.

24. Mwaka 1986/87, benki iliidhinisha mikopo yenye thamani ya Sh. 178·0 milioni ikilinganishwa na mikopo yenye thamani ya Sh. 155·6 milioni mwaka uliotangulia. Mikopo ya kibiashara iliyoidhinishwa ilifikia Sh. 21·3 milioni. Kwa jumla fedha iliyotolewa (disbursement) na benki kama mikopo ilifikia Sh. 169·8 milioni mwaka 1986/87 kutoka Sh. 129·0 milioni mwaka 1985/86.

25. Katika mwaka 1986/87, watu binafsi walipatiwa mikopo yenye thamani ya Sh. 21·9 milioni ikilinganishwa na mwaka uliotangulia ambapo walipatiwa Sh. 4·8 milioni. Hii ni kwa sababu wakopaji wengi walioomba mikopo hawakutimiza masharti yaliyowekwa na benki kwa ajili ya mikopo hiyo.

26. Kwa miaka michache ya nyuma hadi kufikia mwaka 1984/85, wakopaji wakubwa walikuwa watu binafsi. Lakini kutokea hapo hali imebadilika na wakopaji wakubwa kwa sasa wamekuwa ni wafanyabiashara kwa miradi ya kibiashara. Hivi sasa wateja wengi wa Benki ya Nyumba wanafika kuomba mikopo ya ujenzi wa majengo ya kibiashara kama vile maghala na mahoteli. Hali hii imesababishwa hasa na riba inayotozwa kwenye mikopo kuongezeka kwa kiasi kikubwa katika muda mfupi; wakati viwango vya mikopo ambavyo wateja wangeweza kulipa havitoshi kugharimia ujenzi wa nyumba kutokana na kupanda kwa gharama za ujenzi.

**Benki ya Rasilimali Tanzania:**

27. Mapato ya Benki ya Rasilimani yalifikia kiasi cha Sh. 754·6 milioni katika mwaka 1986/87 ikilinganishwa na Sh. 310·5 milioni katika mwaka uliotangulia. Matumizi hayo yaliongezeka kutoka Sh. 301·1 milioni hadi kufikia kiasi cha Sh. 727·3 milioni mwaka 1986/87. Faida baada ya kutoa kodi iliongezeka kutoka Sh. 1·4 milioni mwaka uliopita hadi kufikia Sh. 8·7 milioni mwaka 1986/87. Mapato ya ziada yalitokana kwa sehemu kubwa, na riba za mikopo na ada kwa miradi. Matumizi ya benki yaliongezeka kutokana na kuongezeka kwa gharama za mkopo toka kwa wafadhili kulikotokana na kuongezeka kwa riba na pia kufanya malipo ya mikopo mingi iliyopevuka.

Sababu nyingine ni kuweka kiasi kikubwa cha kutosha cha fedha ambacho ilibidi kutenga kwa ajili ya madeni ambayo hayategemewi kulipwa na wadeni (doubtful debts).

28. Wateja wakubwa wa Benki ya Rasilimali ni Mashirika ya Umma na Makampuni ya watu binafsi. Matatizo ambayo yamekuwa yanawapata wateja wa Benki ni yale ya:

(i) Ukosefu wa fedha za kigeni ambao huwafanya wasiweze kuagiza malighafi spea n.k.

(ii) Uchakavu wa mashine ambao unahitaji marengenezo ambayo hayawezi kufanyika kutokana na ukosefu wa spea zinazoagizwa toke nje.

(iii) Uzalishaji mdogo wa mitambo unaotokana na ukosefu wa malighafi na spea, kukatika kwa mara kwa mara kwa maji na umeme; kukosa soko la bidhaa zao kutokana na gharama kubwa za uzalishaji ikilinganishwa na bidhaa zinazotoka nje.

(iv) Miradi inayoendelea kukosa vifaa vya ujenzi ambavyo huagizwa toka'nje na pia ukosefu wa fedha za hapa hasa baada ya kupunguza thamani ya fedha yetu.

29. Matatizo hayo yanayowapata wateja wa benki ndiyo chanzo kikubwa kwa wengi wao kushindwa kurudisha mikopo wakati muda wake wa kurudishwa ukiwadia. Hata hivyo, Benki imeshachukua hatua za kuimarisha usimamizi wa miradi inayoihudumia na kuona namna gani inaweza kuwasaidia wateja wake.

30. Katika miaka ya karibuni, wafadhili wakubwa wa benki walipunguza utoaji wa mikopo kwa Benki ya Rasilimali kutokana na mikopo ya nyuma kutolipwa katika muda uliopangwa kulikosababishwa na hali ngumu ya uchumi wa Taifa. Mikopo inayopitia Hazina toka kwa wafadhili nayo haikupatikana kwa sababu ilibidi kupelekwa kwenye miradi mingine ya kitaifa. Aidha wadeni walikuwa hawarudishi fedha/ kwa sababu zilizokwishakuelezwa. Sababu zote hizi zimefanya fedha ambazo benki inahitaji kwa shughuli zake kuwa kidogo. Hivyo, kutokana na uhaba wa fedha, Benki imetazama upya masharti ya kutoa mikopo. Miradi ambayo itapewa mikopo ni ile inayokubaliana na Mpango wa Kufufua Uchumi (ERP) na inatimiza masharti yafuatayo:—

(i) Kuongeza upatikanaji wa bidhaa muhimu ambazo zimeadimika kama vile sabuni, viatu, chakula na vinywaji
(ii) Kuongeza upatikanaji wa bidhaa za kati na malighafi zitakazosukuma maendeleo ya kilimo, usafirishaji au utengenezaji wa bidhaa muhimu
(iii) Kuongeza bidhaa za kuuza nchi za nje.
(iv) Kuongeza mapato ya serikali.

31. Kwa sasa upatikanaji wa mapato kutoka kwa wafadhili wa nje pamoja na ulipaji wake wa madeni umekuwa mgumu sana. Mpaka sasa hakuna mafanikio yoyote yaliyokwishapatikana kwenye mazungumzo yanayoendelea ya kutafuta njia nyingine za mapato. Mapato ya kutoka nje yamepungua sana wakati sehemu za uwekaji wa rasilimali zinaendelea kuongezeka.

**Shirika la Taifa la Akiba ya Wafanyakazi:**

32. Mapato yalitarajiwa kufikia Sh. 865 milioni katika mwaka 1987/88 ikilinganishwa na Sh. 724 milioni zilizopatikana mwaka 1986/87. Ongezeko kubwa la mapato linatokana na kuongezeka kwa mapato toka riba ya vitega uchumi hasa hupevuka kwa dhamana za Taifa ambazo Shirika lilinunua miaka ya nyuma. Vile vile kumekuwa na ongezeko la michango ya wanachama baada ya kima cha chini cha mishahara kuongezwa kutoka Sh. 810 hadi Sh. 1,260 kwa mwezi, na mishahara yote kwa jumla kupandishwa. Kutokana na hatua zinazoendelea kuchukuliwa kurekebisha baadhi ya vigezo muhimu katika uchumi na

kuchepua uwekezaji wa Shirika. riba za vitega uchumi zinazidi kuwa kianzio muhimu cha mapato ya Shirika. kwani mchango wake umekuwa ukiongezeka haraka katika miaka hii ya karibuni kutoka Sh. 260 milioni mwaka 1985/86. Sh. 324 milioni mwaka 1986/87 na hatimaye kufikia Sh. 425 milioni mwaka 1987/88. Michango ya wanachama imeendelea kuwa na ongezeko la kadri isipokuwa pale vima vya mishahara viiipopandishwa.

33. Kwa upande wa matumizi, katika kipindi cha 1987/88 Shirika lilitarajia kuwekeza kiasi cha Sh. 1,031·0 milioni katika vitega uchumi mbali mbali vya mfuko wa Akiba na Bodi ya Wadhamini; ununuzi wa dhamana za Taifa ukiwa Sh. 550·0milioni. Mwaka 1986/87 Sh. 870 milioni zitumika katika vitega uchumi na ununuzi wa dhamana za Taifa ulifikia kiasi cha Sh. 500 milioni. Gharama za uendeshaji wa shirika zinatarajiwa kufikia Sh. 148 milioni mwaka 1987/88 ikilinganishwa na kiasi cha Sh. 132 milioni zilizotumika mwaka 1986/87. Malipo ya mafao ya uanachama yanatarajiwa kufikia kiasi cha Sh. 115 milioni wakati Sh. 162·0 milioni zililipwa mwaka 1986/87. Kuongezeka kwa malipo hayo katika mwaka 1986/87 kutoka mafipo ya Sh. 150·0 milioni ya mwaka 1985/86, kulitokana na wateja wengi kuchelewa kuleta madai yao ya kuachishwa kazi kufuatia agizo la Serkali la kupunguza ajira serikalini na katika mashirika ya Umma.

34. Katika mwaka 1987/88, wanachama walio hai walikisiwa kuwa 666,000 wakati mwaka 1986/87 walikuwa 591,000. Waajiri hai mwaka 1986/87 walikuwa 11.333.

**Benki ya Posta:**

34. Katika mwaka 1987, Benki ya Posta ilitarajiwa kuwa na jumla ya mapato ya Sh. 96·2 milioni, ikilinganishwa na Sh. 59·6 milioni zilizopatikana mwaka uliopita wa 1986. Katika jumla hiyo, mapato yanayotoka na na riba inayotozwa kwenye vitega uchumi vyake ilitarajiwa kufikia kiasi cha Sh. 96·1 milioni na mapato kutoka vyanzo vingine matarajio yalikuwa ni kupata Sh. 0·06 milioni. Mapato yameongezeka kwa kuwa riba za vitega uchumi (za dhamana za Taifa) zimeongezwa; na yangeongezeka zaidi kama Benki ingekuwa na michepuo katika uwekezaji rasilimali zake.

35. Matumizi ya Benki katika mwaka 1987, yalitarajiwa kufikia kiasi cha Sh. 193·8 milioni ikilinganishwa na Sh. 89·5 milioni zilizotumika mwaka uliopita. Matumizi yaliyoongezeka ni yale ya kutokana na kurekebisha viwango vya riba za vitega uchumi, ambapo faida ya amana za wateja iliongezeka zaidi ya mara dufu kutoka Sh. 80·7 milioni mwaka 1986 hadi Sh. 185·2 milioni.

36. Amana zote za wateja kwa ujumla ziliongezeka toka Sh. 628·1 milioni mwaka 1986 hadi Sh. 1,160·1 milioni katika mwaka 1987. Hili ni ongezeko la kiasi cha Sh. 178 milioni. Amana za Akiba ziliongezeka kutoka Sh. 468·8 milioni mwaka 1986 mpaka kufikia Sh. 846·5 milioni mwaka 1987, wakati Amana za Wadu ziliongezeka kutoka Sh. 142·7 milioni hadi Sh. 272·9 milioni, na Amana za muda maalum kutoka Sh. 15·6 milioni hadi Sh. 40·6 milioni. Kuongezeka kwa amana zote kwa kiasi kikubwa kunatokana na kuongezeka kwa riba ambazo zimewavutia wateja wengi.

37. Wateja wameongezeka kutoka 711,407 mwaka uliotangulia wa 1986 hadi kufikia 738,223 katika mwaka 1987. Kati ya hao, wateja wa amana za akiba wameongezeka kutoka 661,747 hadi kufikia 685,657; wateja wa amana za Wadu kutoka 49,350 hadi 52,510 ingawaje wale wa amana za muda maalum wamepungua kutoka 310 hadi 56.

38. Kwa upande wa ununuzi wa dhamana za Serikali katika mwaka 1987/88, Benki ilidhamiria kutumia kiasi cha Sh. 160 milioni. Lakini mpaka ilipofikia mwishoni mwa mwezi Aprili 1988, Benki ilikuwa imenunua dhamana za Serikali za jumla ya Sh. 200 milioni.

39. Matatizo yanayoendelea kuikabili Benki ni Usafiri ambao ungewezesha kuwafikia wateja wanaoishi schemu za vijijini; riba inayotolewa kwa ajili ya amana ni kubwa ikilinganishwa na riba inayopatikana katika vianzio vyake vya fedha. Lakini licha ya matatizo haya, Benki inatarajia kutoa huduma bora zaidi na kwa ufanisi unaoridhisha.

**Shirika la Fedha la Maendeleo la Tanganyika:**

40. Mwaka 1987, Kampuni iliidhinisha mikopo yenye thamani ya Sh. 78,268 milioni ikilinganishwa na kiasi cha Sh. 49,032·0 milioni kilichoidhinishwa mwaka uliotangulia. Kati ya kiasi hicho cha Sh. 78,268 milioni, Sh. 72·3 milioni zilikuwa katika fedha za kigeni na kiasi kilichobakia cha Sh. 78,195·7 milioni ni fedha za hapa nchini. Kwa sasa hivi Benki inakabiliwa na upungufu wa fedha za hapa nchini hivyo haitayakubali maombi ya miradi yanayohitaji fedha za hapa nchini. Hata hivyo, Kampuni imepatiwa mkopo kutoka European Investment Bank (EIB) wa kiasi cha Sh. 500 milioni ambazo zitatolewa kwa miradi yenye matarajio mazuri na yenye uwezo wa kuzalisha fedha za kigeni.

41. Mapato ya Kampuni mwaka 1987 yalikuwa Sh. 187·9 milioni ikilinganishwa na Sh. 74·5 milioni kwa mwaka uliotangulia wa 1986. Ongezeko hili kubwa lilisababishwa hasa na mapato ya Sh. 86·2 milioni yaliyotokana na kubadilisha thamani ya fedha, "exchange gain" ambayo haikuwepo katika miaka ya nyuma. Vivyo hivyo, mapato yatokanayo na riba yalipanda kutoka Sh. 50·9 milioni za mwaka 1986 hadi kufikia Sh. 76·6 milioni; ongezeko likiwa la Sh. 25·7 milioni, sawa na asilimia 50·5. Mapato mengine yalikuwa na jumla ya ongezeko la Sh. 1·5 milioni.

42. Matumizi ya Kampuni katika mwaka 1987, yalifikia kiasi cha Sh. 07·4 milioni ikilinganishwa na Sh. 73·6 milioni zilizotumika mwaka 1986. Hili ni sawa na ongezeko la kiasi cha Sh. 33,745·0 milioni. Kutokana na shughuli hizo, faida baada ya kodi ilipanda hadi kufikia Sh. 100·5 milioni mwaka 1987 kutoka Sh. 3·6 milioni mwaka 1986.

43. Kampuni imekuwa ikikabiliwa na matatizo mbali mbali ambayo yamesababisha upungufu katika ufanisi wa kazi. Matatizo hayo ni pamoja na kuendelea kushuka kwa thamani ya shilingi ambako kumesababisha madeni ya nje kuwa aghali sana; na pia kumesababisha upungufu wa fedha za hapa nchini. Hali kadhalika, wakopaji wa fedha za kigeni kupitia Kampuni, pia wanakabiliwa na tatizo la ulipaji madeni yao kwa sababu ya kubadilika badilika kwa thamani ya shilingi. Matokeo yake ni kuongezeka kwa wanaoshindwa kulipa madeni. Matatizo mengine ni mapato madogo kutokana na kupungua kwa matumizi ya uwezo wa rasilimali zilizowekezwa; Kutolipwa kwa madeni ni kwa sababu ya matatizo ya ukwasi na riba ndogo inayokusanywa kutokana na utekelezaji hafifu wa miradi. Kuhusu miradi mipya, ni michache sana inayoanzishwa kwa sababu gharama kubwa ya mikopo inayotolewa; pia, kwa kuendelea kushuka kwa thamani ya shilingi, wateja wengi wanasita kuanzisha miradi mipya.

## HALI YA FEDHA KWA JUMLA KATIKA MWAKA 1984—1988
## TANZANIA BARA

Jedwali Na. 20 (Sh. milioni)

| | Juni 1984 | Juni 1985 | Juni 1986 | Juni 1987 | Juni 1988 | Juni 1988 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Halisi | Halisi | Halisi | Halisi | Makisio | Malegemeo |
| 1. Akiba halisi ya Fedha za Kigeni | −7,517·3 | −8,861·9 | −14,464·1 | −17,458·3 | −24,394·1 | −24,700·0 |
| 2. Karadha ..................... | 33,100·0 | 39,601·5 | 50,410·4 | 65,431·9 | 76,758·7 | 88,087·7 |
| (a) Mikopo ya Serikali Kutoka Mabenki ..................... | 23,927·5 | 27,073·8 | 32,271·4 | 33,927·7 | 31,927·7 | 35,827·7 |
| (b) Karadha kwa Sekta Nyinginezo Uchumi ..................... | 9,172·5 | 12,527·7 | 18,139·0 | 31,504·2 | 44,831·0 | 52,260·0 |
| Katika ya ke: Kwa bodi za Mazao: ........... | 5,492·7 | 5,246·4 | 7,061·9 | 10,771·0 | 9,371·0 | 18,070·0 |
| 3. Nyinginezo ..................... | 881·7 | 1,239·4 | 8,057·7 | 13,962·0 | 26,985·4 | 22,690·0 |
| 4. Ujazi wa Fedha kwa Tafsiri Pana . | 26,490·6 | 32,615·9 | 39,368·9 | 48,408·0 | 53,248·8 | 58,138·0 |
| 5. Valuation Account ..................... | −26·2 | −636·9 | 3,292·7 | 4,836·0 | 13,820·2 | 9,250·3 |

*Chanzo:* Benki Kuu.

## BENKI YA TAIFA YA BIASHARA: AMANA NA KARADHA

Jedwali Na. 21 (Sh. milioni)

| | | Amana | Karadha | Dhamana | Lingamsho kati ya Karadha na Amana (asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1984 | Machi | 17,514·00 | 9,136·00 | 12,749·80 | 52 |
| | Juni | 18,499·30 | 9,095·00 | 11,399·90 | 49 |
| | Septemba | 20,084·10 | 9,995·00 | 11,399·80 | 50 |
| | Desemba | 24,258·80 | 11,543·30 | 13,617·30 | 48 |
| 1985 | Machi | 26,212·70 | 13,541·90 | 14,578·00 | 52 |
| | Juni | 27,312·80 | 13,096·40 | 14,737·30 | 48 |
| | Septemba | 27,540·70 | 19,148·40 | 15,297·30 | 70 |
| | Desemba | 27,651·70 | 17,809·00 | 15,857·30 | 64 |
| 1986 | Machi | 26,023·1 | 16,881·6 | 8,233·3 | 65·0 |
| | Juni | 25,759·6 | 17,321·1 | 6,610·8 | 67·2 |
| | Septemba | 28,899·0 | 19,924·7 | 3,601·9 | 69·0 |
| | Desemba | 30,693·1 | 23,496·6 | 3,601·9 | 77·0 |
| 1987 | Machi | 31,586·5 | 26,126·9 | 3,600·8 | 82·7 |
| | Juni | 30,209·2 | 29,343·6 | 3,601·8 | 97·1 |
| | Septemba | 37,085·2 | 39,187·1 | 3,491·3 | 105·7 |
| | Desemba | 38,707·6 | 47,261·6 | 3,489·2 | 122·1 |

*Chanzo:* Benki ya Taifa ya Biashara.

## BENKI YA TAIFA YA BIASHARA: MIKOPO KUFUATANA NA SEKTA ZA UCHUMI

Jedwali Na. 22 (Shilingi milioni)

| Kipindi | | Kilimo | Viwanda | Ujenzi | Biashara | Ununuziwa Bidhaaza Kilimo | Usafirishaji | Sekta Nyinginezo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1981 | Machi | 221·3 | 866·2 | 224·7 | 1,429·5 | 8,149·2 | 201·0 | 44·4 | 9,136·3 |
| | Juni | 289·3 | 1,053·6 | 215·5 | 1,887·5 | 5,420·5 | 172·2 | 56·4 | 9,095·0 |
| | Septemba | 354·1 | 1,177·3 | 245·9 | 1,874·2 | 6,090·4 | 428·0 | 24·8 | 9,952·2 |
| | Desemba | 650·5 | 1,331·5 | 289·1 | 1,600·4 | 7,434·9 | 420·5 | 16·5 | 11,543·4 |
| 1985 | Machi | 445·2 | 1,424·1 | 227·4 | 2,759·9 | 6,875·3 | 294·3 | 1,575·7 | 13,541·9 |
| | Juni | 889·9 | 846·3 | 302·2 | 1,905·4 | 6,873·2 | 323·8 | 1,955·6 | 13,096·4 |
| | Septemba | 2,015·9 | 1,261·3 | 247·5 | 5,707·2 | 8,234·6 | 344·2 | 1,337·7 | 19,148·4 |
| | Desemba | 645·2 | 1,443·2 | 270·9 | 4,860·7 | 9,388·9 | 338·6 | 861·5 | 17,809·0 |
| 1986 | Machi | 1,411·3 | 1,681·2 | 299·6 | 1,508·1 | 11,868·6 | 370·9 | 230·6 | 16,881·6 |
| | Juni | 591·8 | 2,622·3 | 310·4 | 1,744·7 | 11,307·0 | 310·4 | 257·0 | 17,321·1 |
| | Septemba | 954·4 | 2,886·0 | 252·7 | 1,428·6 | 13,578·9 | 491·2 | 332·8 | 19,924·7 |
| | Desemba | 890·0 | 2,705·2 | 285·9 | 1,845·7 | 17,003·7 | 471·9 | 294·2 | 23,496·6 |
| 1987 | Machi | 1,123·1 | 4,307·8 | 301·2 | 3,435·3 | 16,024·7 | 510·6 | 424·2 | 26,126·9 |
| | Juni | 640·0 | 4,730·0 | 291·0 | 2,656·0 | 18,871·0 | 649·0 | 1,506·6 | 29,313·6 |
| | Septemba | 1,913·5 | 5,288·3 | 540·2 | 3,177·0 | 26,839·6 | 938·2 | 526·3 | 39,187·1 |
| | Desemba | 1,662·7 | 5,331·7 | 440·2 | 4,039·9 | 33,561·1 | 965·4 | 1,260·1 | 47,261·6 |

*Chanzo:*—Benki ya Taifa ya Biashara.

## BENKI YA USHIRIKA NA MAENDELEO VIJIJINI
## MGAWANYO WA MIKOPO

Jedwali Na. 23

(Sh. Milioni)

| Ki-Mkopaji | 1983/84 | | 1984/85 | | 1985/86 | | 1986/87 | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Idadi | Thamani | Idadi | Thamani | Idadi | Thamani | Idadi | Thamani |
| 1. Vyama vya Msingi vya Ushirika | 2 | 0·2 | 54 | 68·9 | 41 | 1,075·0 | 26 | 1,507·8 |
| 2. Vijiji | 913 | 84·1 | 801 | 244·5 | 75 | 33.8 | 36 | 25·0 |
| 3. Mashirika ya Wilaya ya Maendeleo | — | — | 1 | 0·5 | — | — | — | — |
| 4. Mashirika ya Umma/Makampuni | 12 | 11·3 | 45 | 63·1 | 18 | 125·10 | 37 | 132·10 |
| 5. Muungano (Associations) | 2 | 29·9 | 3 | 0·5 | — | — | 1 | 18·9 |
| 6. Wabia (Partnership) | 2 | 0·6 | — | — | — | — | — | — |
| 7. Watu binafsi | 119 | 21·4 | 591 | 83·1 | 315 | 91·8 | 406 | 266·1 |
| 8. Wengine | — | — | — | — | — | — | 10 | 25·3 |
| Jumla ya Mikopo muda mrefu na kati ... | 1,045 | 147·5 | 1,495 | 460.2 | 449 | 1,325·7 | 516 | 1,969·2 |
| **Ki-Mradi** | | | | | | | | |
| 1. Pembejeo za Majira | 636 | 87·5 | 688 | 213·1 | 36 | 1,042·7 | 31 | 1,209·1 |
| 2. Ukuzaji na Ustawishaji Mazao | 3 | 0·5 | 5 | 1·5 | 8 | 22·1 | 26 | 44·0 |
| 3. Mifugo | 23 | 5·4 | 147 | 14·1 | 70 | 24·8 | 88 | 27·1 |
| 4. Usafirishaji Vijijini | 25 | 13·7 | 156 | 119·2 | 74 | 76·6 | 164 | 552·7 |
| 5. Viwanda Vidogo vidogo | 295 | 23·5 | 216 | 16·6 | 41 | 3·9 | 111 | 42·1 |
| 6. Maghala | 1 | 0·1 | 6 | 0·9 | 2 | 0·1 | — | — |
| 7. Zana za Kilimo | 58 | 15·0 | 271 | 85·1 | 184 | 60·6 | 80 | 79·5 |
| 8. Uvuvi | 4 | 1·6 | 6 | 10·3 | 34 | 5·1 | 16 | 12·7 |
| | 1,045 | 147·5 | 1,495 | 460·2 | 449 | 1,325·7 | 516 | 1,969·2 |

*Chanzo*—Benki ya Ushirika na Maendeleo Vijijini.

## SHIRIKA LA AKIBA YA TAIFA YA WAFANYAKAZI

Jedwali 24

| Mwaka (1) | Waajiri (Namba) | | Wanachama (000) | | Mapato (Sh. Milioni) | | | Matumizi (Sh. Milioni) | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Jumla (2) | Walio hai | Jumla (2) | Walio hai | Michango (3) | Riba ya Vitega Uchumi | Jumla | Vitega Uchumi (4) | Uendeshaji | Malipo kwa Wanachama | Jumla |
| 1976/77 | 10,670 | — | 947 | — | 149 | 62 | 211 | 141 | 16 | 70 | 227 |
| 1977/78 | 11,283 | — | 1,018 | — | 199 | 75 | 234 | 180 | 17 | 55 | 252 |
| 1978/79 | 12,098 | — | 1,084 | — | 145 | 77 | 222 | 177 | 20 | 59 | 256 |
| 1979/80 | 12,739 | — | 1,151 | — | 165 | 89 | 254 | 217 | 21 | 56 | 294 |
| 1980/81 | 13,436 | 6,634 | 1,223 | 293 | 204 | 104 | 308 | 245 | 33 | 60 | 338 |
| 1981/82 | 14,227 | 8,382 | 1,301 | 380 | 238 | 124 | 362 | 281 | 37 | 73 | 391 |
| 1982/83 | 15,841 | 9,100 | 1,359 | 423 | 254 | 144 | 398 | 289 | 45 | 65 | 399 |
| 1983/84 | 15,999 | 9,832 | 1,421 | 488 | 278 | 190 | 468 | 334 | 55 | 79 | 468 |
| 1984/85 | 17,130 | 10,885 | 1,493 | 553 | 342 | 237 | 579 | 464 | 78 | 123 | 665 |
| 1985/86 | 18,059 | 11,102 | 1,563 | 572 | 402 | 260 | 662 | 431 | 92 | 150 | 673 |
| 1986/87 | 18,945 | 11,333 | 1,636 | 591 | 400 | 324 | 724 | 576 | 132 | 162 | 870 |
| 1987/88(5) | 19,823 | 1,221 | 1,711 | 666 | 440 | 425 | 865 | 768 | 148 | 115 | 1031 |

*Chanzo*:—Shirika la Akiba ya Taifa ya Wafanyakazi

(1): Unaishia tarehe 30 Juni.

(2): Cumulative membership on register since inception.

(3): Statutory Contribution.

(4): Matumizi halisi ya fedha.

(5): Takwimu za muda.

## 6.—UAJIRI, MISHAHARA NA BEI

**Uajiri na Mishahara:**

1. Katika mwaka 1987 palikuwepo ongezeko dogo la uajiri nchini. Idadi ya waajiriwa iliongezeka kutoka 692,745 mwaka 1986 hadi 700,037 mwaka 1987, sawa na ongezeko la asilimia 1·05. Ongezeko hilo ni dogo ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 4·6 mwaka 1986 na asilimia 4·5 mwaka 1985.

2. Kupungua kwa ongezeko la ajira karibu kila mwaka na hasa kuanzia mwaka 1984 kunatokana na sababu mbili muhimu. Sababu ya kwanza ni usimamishaji wa ajira mpya katika serikali na baadhi ya vyombo vyake kwa kada fulani za wafanyakazi, isipokuwa waalimu na wafanyakazi katika vyombo vya afya. Aidha, serikali imefanya jitihada za makusudi kuanzia mwaka 1984 kudhibiti uajiri nchini ili kudumisha uwiano kati ya ajira na mahitaji yake katika uchumi na kuleta ufanisi na tija. Hata hivyo, kutokana na lengo la CHAMA na Serikali la kumtaka kila mwenye uwezo wa kufanya kazi kufanya hivyo, ni wazi kuwa pamoja na jitihada za kuongeza tija mashambani na sehemu nyingine za kazi, sekta isiyo ya serikali hasa ushirika na sekta ya binafsi zitakuwa na jukumu kubwa zaidi la kupanua shughuli zake na kuongeza ajira.

3. Kwa jumla, sekta zote ziliongeza uajiri ingawa kwa viwango tofauti. Sekta za huduma za kiuchumi kwa pamoja ziliongeza uajiri kwa asilimia 2·7 zikilinganishwa na sekta ya utawala na huduma za kijamii zilizoongeza ajira kwa asimilia 0·6 tu. Sekta za uzalishaji mali ambazo ziliajiri asilimia 35·28 ya watumishi wote kwa mwaka 1987, ziliongeza ajira kwa asilimia 0·42.

4. Ingawa uajiri kwa jumla uliongezeka kwa kasi ndogo ya asilimia 1·05, mishahara kwa upande mwingine iliongezeka kwa zaidi ya asilimia 9·0. Ongezeko hilo lilitokana na kupandishwa kwa mishahara ya watumishi iliyotangazwa na serikali hapo Julai 1987.

**Bei:**

5. Mwaka 1987, bei kama zinavyopimwa na Fahirisi ya Bei kwa Wakazi wa Mijini Tanzania Bara (CPI) ziliendelea kupanda kwa kasi. Ongezeko la bei la wastani katika mwaka 1987 lilikuwa asilimia 29·9 ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 32·4 mwaka 1986. Katika kipindi hiki, kasi ya ongezeko la bei ilikuwa kubwa zaidi katika robo ya nne ya mwaka kwani kati ya Januari na Septemba, ongezeko lilikuwa la asilimia 14·7 tu. Sehemu kubwa ya ongezeko hilo la asilimia 29·9 ilitokea katika robo ya nne kutokana hasa na ongezeko la bei la asilimia 17 kwa chakula peke yake. Ongezeko hili kubwa lilitokana na matatizo ya usambazaji japokuwa chakula kilikuwapo cha kutosha. Kwa jumla, kasi ya ongezeko la bei iliyoanza kupungua mwaka 1985 imeendelea japokuwa kwa kiwango kidogo kwa miaka mitatu sasa.

6. Hali hii ya bei katika mwaka 1987 ilitokana kwa kiasi kikubwa na kupungua kwa kasi ya ongezeko la bei za bidhaa zinazotumiwa na wananchi wenye kipato cha chini na cha kati. Kulikuwepo unafuu katika ongezeko la bei za vyakula ambazo kwa jumla zilipanda kwa asilimia 30·7 ikilinganishwa na kupanda kwa asimilia 34·8 mwaka 1986 na bei za mavazi ambazo zilipanda kwa asilimia 17·5 ikilinganishwa na asilimia 23·2 mwaka 1986.

7. Pamoja na unafuu kidogo ulioelezwa, bei ziliendelea kupanda kutokana na kuendelea kushuka thamani ya fedha ya Tanzania, uzalishaji mdogo viwandani na kutodhibiti bei za bidhaa zinazoagizwa kutoka nje na watu binafsi.

## UAJIRI NA MISHAHARA KATIKA SEKTA MBALIMBALI ZA UCHUMI 1984–87: TANZANIA BARA

Jedwali Na. 25

| Sekta | Uajiri (Idadi) | | | | Badiliko (%) | Mishahara kwa mwaka (Sh. milioni) | | | | Badiliko (%) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1984+ | 1985++ | 1986++ | 1987* | 1986/87 | 1984+ | 1985++ | 1986++ | 1987* | 1986/87 |
| Kilimo ........ | 108,114 | 109,230 | 116,475 | 117,209 | ·63 | 639·04 | 985·2 | 1,156·82 | 1,328·64 | 14·85 |
| Madini ........ | 5,360 | 6,009 | 6,207 | 5,620 | −16·22 | 97·68 | 106·89 | 116·6 | 116·98 | ·33 |
| Viwanda ........ | 115,908 | 121,101 | 123,334 | 124,210 | ·71 | 1,430·00 | 1,539·81 | 1,658·1 | 1,785·36 | 7·67 |
| Maji na Umeme .... | 27,091 | 26,645 | 27,539 | 28,705 | 4·23 | 325·55 | 256·6 | 276·4 | 277·51 | ·4 |
| Ujenzi ........ | 34,365 | 30,227 | 26,411 | 27,008 | 2·26 | 400·68 | 450·48 | 506·47 | 565·00 | 11·57 |
| Blashara ........ | 46,707 | 47,162 | 47,210 | 48,489 | 2·71 | 618·25 | 675·56 | 738·18 | 801·45 | 8·57 |
| Mawasiliano na Uchukuzi ........ | 61,279 | 64,241 | 69,287 | 70,742 | 2·1 | 928·82 | 1,046·03 | 1,178·04 | 1,320·00 | 12·05 |
| Fedha ........ | 16,646 | 17,585 | 19,579 | 19,794 | 1·11 | 424·7 | 473·75 | 528·47 | 587·38 | 11·15 |
| Huduma ........ | 217,910 | 279,907 | 256,745 | 258,260 | ·59 | 3,043·13 | 3,267·71 | 3,508·87 | 3,762·2 | 7·21 |
| Jumla ... | 633,380 | 662,107 | 692,745 | 700,037 | 1·05 | 8,107·87 | 8,802·06 | 9,667·95 | 10,544·52 | 9·07 |

*Chanzo:* Idara ya Takwimu.

\+ Tarakimu halisi (Actual figures).

* Tarakimu zilizokisiwa (Estimated/Projected figures).

++ Makisio yaliyorekebishwa (Revised estimates).

Jedwali Na. 26

## UAJIRI NA MISHAHARA KATIKA MIKOA 1983–1987: TANZANIA BARA

| Mkoa | Uajiri (Idadi) 1984+ | 1985++ | 1986++ | 1987* | Badiliko (%) 1986/87 | Mishahara kwa Mwaka (Sh. milioni) 1984+ | 1985++ | 1986++ | 1987* | Badiliko (%) 1986/87 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Arusha | 41,804 | 43,620 | 44,794 | 45,410 | 1·37 | 479·6 | 549·69 | 609·7 | 661 | 8·41 |
| Pwani | 7,175 | 9,427 | 12,293 | 13,185 | 7·26 | 80·46 | 139·68 | 149·7 | 156·6 | 4·61 |
| D Salaam | 188,810 | 196,305 | 202,025 | 204,002 | ·98 | 3,038·49 | 3,153·37 | 3,454·88 | 3,759·9 | 8·83 |
| Dodoma | 24,257 | 26,886 | 29,498 | 31,594 | 7·11 | 296·86 | 250·9 | 275·09 | 331·77 | 20·6 |
| Iringa | 47,372 | 39,985 | 40,822 | 39,529 | −4·17 | 431·36 | 363·45 | 401·73 | 455·62 | 13·59 |
| Kagera | 12,891 | 15,448 | 8,324 | 17,965 | −1·96 | 221·94 | 259·62 | 291·9 | 326·46 | 11·84 |
| Kigoma | 13,668 | 14,358 | 14,918 | 1,515 | 1·56 | 150·3 | 195·78 | 218·92 | 245·98 | 12·36 |
| Kilimanjaro | 35,512 | 37,820 | 39,867 | 39,571 | −·74 | 421·76 | 480·2 | 258·[illegible] | 563·45 | 6·71 |
| Lindi | 12,891 | 13,537 | 14,073 | 14,221 | 1·05 | 155·6 | 184·08 | 206·53 | 214·8 | ·4 |
| Mara | 13,578 | 13,633 | 13,549 | 12,954 | −4·4 | 181·95 | 196·06 | 277.3 | 279·8 | ·9 |
| Mbeya | 26,654 | 26,468 | 26,016 | 25,100 | −3·52 | 277·5 | 268·12 | 273·74 | 306·23 | 11·87 |
| Morogoro | 42,784 | 45,192 | 47,250 | 47,263 | ·03 | 448·12 | 572·7 | 588·4 | 672·72 | 14·33 |
| Mtwara | 17,154 | 17,139 | 16,949 | 16,486 | −2·23 | 166·32 | 196·81 | 217·1 | 241·1 | 11·05 |
| Mwanza | 30,340 | 32,952 | 35,425 | 35,089 | −·95 | 388·3 | 466·06 | 515·13 | 531·4 | 3·16 |
| Rukwa | 7,752 | 8,554 | 9,344 | 9,768 | 4·54 | 96·3 | 132·23 | 148·74 | 158·3 | 6·43 |
| Ruvuma | 12,406 | 13,193 | 11,911 | 11,398 | −4·31 | 147·3 | 150·7 | 166·87 | 177·6 | 6·43 |
| Shinyanga | 19,466 | 20,518 | 21,406 | 21,900 | 2·31 | 275·41 | 240·76 | 266·15 | 291·9 | 9·67 |
| Singida | 10,712 | 11,639 | 12,517 | 13,054 | 4·29 | 119·15 | 147·88 | 163·42 | 176·2 | 7·82 |
| Tabora | 17,900 | 18,040 | 16,925 | 16,329 | −3·52 | 166·74 | 166·18 | 177·05 | 201·38 | 13·74 |
| Tanga | 50,254 | 57,393 | 64,881 | 70,068 | 7·99 | 573·41 | 678·79 | 737·6 | 792·31 | 7·42 |
| Jumla | 633,380 | 662,107 | 692,787 | 700,037 | 1·05 | 8,107·87 | 8,802·06 | 9,667·95 | 10,544·42 | 9·07 |

*Chanzo:* Idara ya Takwimu.

\+ Tarakimu halisi (Actual figures).

* Tarakimu za Makisio (Estimated/Projected figures).

\+ + Makisio yaliyorekebishwa (Revised estimates).

## FAHIRISI YA BEI ZA REJAREJA YA BIDHAA ZITUMIWAZO NA WATU WA KIPATO CHA CHINI—DAR ES SALAAM (1977=100)

Jedwali Na. 27

| Mwaka | Bidhaa zote | | Chakula | |
|---|---|---|---|---|
| | Fahirisi | Badiliko (Asilimia) | Fahirisi | Badiliko (Asilimia) |
| 1966 | 30·00 | — | 29·50 | — |
| 1967 | 30·80 | 2·67 | 30·00 | 1·69 |
| 1968 | 31·90 | 3·57 | 30·40 | 1·33 |
| 1969 | 32·30 | 1·25 | 29·90 | −1·64 |
| 1970 | 33·40 | 3·41 | 31·00 | 3·68 |
| 1971 | 34·60 | 3·59 | 32·50 | 4.84 |
| 1972 | 38·20 | 10·40 | 36·00 | 10·77 |
| 1973 | 41·70 | 9·16 | 40·50 | 12·50 |
| 1974 | 54·50 | 30·70 | 53·10 | 31·11 |
| 1975 | 80·10 | 46·97 | 79·70 | 50·09 |
| 1976 | 98·90 | 23·47 | 98·40 | 23·46 |
| 1977 | 115·60 | 16·89 | 115·90 | 17·78 |
| 1978 | 135·00 | 16·78 | 138·90 | 19·84 |
| 1979 | 141·00 | 4·44 | 141·90 | 2·16 |
| 1980 | 165·20 | 17·16 | 168·00 | 18·39 |
| 1981 | 215·00 | 30·15 | 215·70 | 28·39 |
| 1982 | 262·90 | 22·28 | 266·50 | 23·55 |
| 1983 | 325.00 | 23·62 | 318·30 | 19·44 |
| 1984 | 381·80 | 17·48 | 348·40 | 9·46 |
| 1985 | 559·70 | 46·60 | 508·00 | 45·81 |
| 1986 | 787·90 | 40·77 | 759·10 | 49·43 |
| 1987 | 997·80 | 26·64 | 954.52 | 25·74 |

*Chanzo:* Idara ya Takwimu.

## FAHARISI YA BEI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WAFANYAKAZI WA KIMA CHA KATI—DAR ES SALAAM (1977=100)

Jedwali Na. 28

| Mwaka | Miezi: Machi | Juni | Septemba | Desemba | Fahirisi (Wastani) | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1967 | 38·90 | 40·50 | 40·10 | 40·80 | 40·08 | — |
| 1968 | 41·40 | 41·50 | 41·70 | 42·00 | 41·65 | 3·93 |
| 1969 | 41·70 | 41·70 | 41·70 | 41·70 | 41·70 | ·12 |
| 1970 | 42·00 | 42·20 | 42·50 | 42·50 | 42·30 | 1·44 |
| 1971 | 42·60 | 42·70 | 43·20 | 43·10 | 42·90 | 1·42 |
| 1972 | 43·40 | 43·50 | 44·80 | 45·20 | 44·23 | 3·09 |
| 1973 | 49·60 | 49·70 | 50·70 | 52·60 | 50·65 | 14·53 |
| 1974 | 53·90 | 60·80 | 62·90 | 76·00 | 63·40 | 25·17 |
| 1975 | 81·40 | 82·90 | 88·10 | 88·40 | 85·20 | 34·38 |
| 1976 | 92·90 | 93·30 | 95·10 | 95·90 | 94·30 | 10·68 |
| 1977 | 101·70 | 100·70 | 102·60 | 115·90 | 105·23 | 11·59 |
| 1978 | 122·70 | 122·10 | 122·10 | 137·90 | 126·20 | 19·93 |
| 1979 | 145·30 | 144·70 | 146·90 | 151·50 | 147·10 | 16·56 |
| 1980 | 160·80 | 166·60 | 174·40 | 204·70 | 176·63 | 20·07 |
| 1981 | 214·60 | 228·60 | 238·30 | 249·40 | 232·73 | 31·76 |
| 1982 | 258·20 | 271·60 | 300·20 | 340·00 | 292·50 | 25·68 |
| 1983 | 348·20 | 350·10 | 367·20 | 389·20 | 363·68 | 24·33 |
| 1984 | 405·70 | 413·50 | 486·20 | 544·90 | 462·58 | 27·19 |
| 1985 | 577·70 | 580·40 | 707·40 | 780·30 | 661·45 | 42·99 |
| 1986 | 852·30 | 865·90 | 903·30 | 1,024·10 | 911·40 | 37·79 |
| 1987 | 1,135·70 | 1,115·10 | 1,191·60 | 1,336·70 | 1,194·78 | 31·10 |

*Chanzo:* Idara ya Takwimu.

FAHIRISI YA BIDHAA NA HUDUM

Jedwali Na. 28A

| Mwezi | Chakula |
|---|---|
| 1975—Machi | 98·10 |
| Juni | 90·60 |
| Septemba | 88·90 |
| Desemba | 96·10 |
| 1976—Machi | 100·30 |
| Juni | 97·60 |
| Septemba | 102·40 |
| Desemba | 104·00 |
| 1977—Machi | 114·00 |
| Juni | 108·30 |
| Septemba | 109·80 |
| Desemba | 115·60 |
| 1978—Machi | 127·50 |
| Juni | 126·30 |
| Septemba | 120·40 |
| Desemba | 150·40 |
| 1979—Machi | 155·40 |
| Juni | 149·80 |
| Septemba | 151·90 |
| Desemba | 153·00 |
| 1980—Machi | 168·50 |
| Juni | 178·80 |
| Septemba | 188·30 |
| Desemba | 213·40 |
| 1981—Machi | 224·00 |
| Juni | 245·70 |
| Septemba | 255·10 |
| Desemba | 273·00 |
| 1982—Machi | 276·30 |
| Juni | 299·20 |
| Septemba | 352·20 |
| Desemba | 404·90 |
| 1983—Machi | 392·00 |
| Juni | 394·40 |
| Septemba | 408·20 |
| Desemba | 440·90 |
| 1984—Machi | 406·40 |
| Juni | 309·90 |
| Septemba | 483·20 |
| Desemba | 548·90 |
| 1985—Machi | 582·00 |
| Juni | 575·50 |
| Septemba | 734·80 |
| Desemba | 827·70 |
| 1986—Machi | 916·00 |
| Juni | 898·10 |
| Septemba | 928·80 |
| Desemba | 1,065·10 |
| 1987—Machi | 1,213·30 |
| Juni | 1,165·40 |
| Septemba | 1,262·30 |
| Desemba | 1,314·00 |

*Chanzo:*—Idara ya Takwimu

## FAHIRISI YA GHARAMA YA MAISHA YA WENYE KIPATO CHA JUU—DAR ES SALAAM

(1977—100)

Jedwali Na. 29

| | Mwezi | Vyakula Vinywaji na Tumbaku | Nguona Vialu | Vifaa vya Nyumbani | Mishahara ya Watumishi wa Nyumbani | Uchukuzi | Huduma za Afya | Michezona Starehe | Mengineyo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1974 | Juni ........................ | 62·2 | 65·5 | 56·5 | 83·9 | 52·4 | 107·70 | 81·3 | 100·90 |
| | Desemba ................ | 79·7 | 69·5 | 57·1 | 83·9 | 57·00 | 122·10 | 81·3 | 121·60 |
| 1975 | Juni ........................ | 82·00 | 74·5 | 65·1 | 112·8 | 94·30 | 122·10 | 84·00 | 128·20 |
| | Desemba ................ | 82·30 | 79·4 | 66·6 | 114·6 | 113·60 | 124·00 | 89·40 | 139·90 |
| 1976 | Juni ........................ | 85·90 | 81·5 | 67·4 | 114·9 | 147·20 | 136·70 | 85·10 | 156·00 |
| | Desemba ................ | 86·70 | 84·5 | 79·9 | 115·2 | 150·70 | 148·40 | 85·80 | 175·50 |
| 1977 | Juni ........................ | 94·30 | 88·6 | 87·5 | 116·4 | 176·70 | 150·50 | 98·20 | 179·7 |
| | Desemba ................ | 109·30 | 108·1 | 86.6 | 121·1 | 179·70 | 158·80 | 100·40 | 186·5 |
| 1978 | Juni ........................ | 113·70 | 133·9 | 88·4 | 124·8 | 179·70 | 163·10 | 100·60 | 187·4 |
| | Desemba ................ | 116·10 | 134·6 | 94·1 | 127·2 | 184·10 | 199·30 | 110·80 | 189·1 |
| 1979 | Juni ........................ | 128·90 | 151·5 | 97·8 | 127·2 | 188·50 | 205·00 | 120·90 | 233·1 |
| | Desemba ................ | 136·80 | 162·3 | 115·7 | 131·4 | 190·70 | 213·70 | 134·40 | 239·5 |
| 1980 | Juni ........................ | 157·70 | 176·4 | 141·2 | 137·5 | 205·70 | 224·00 | 144·10 | 254·8 |
| | Desemba ................ | 182·80 | 181·9 | 161·7 | 148·00 | 215·60 | 279·30 | 164·70 | 263·9 |
| 1981 | Juni ........................ | 225·40 | 186·9 | 166·2 | 149·4 | 242·90 | 318·60 | 205·80 | 329·9 |
| | Desemba ................ | 241·60 | 188·6 | 168·5 | 149·5 | 260·80 | 341·20 | 206·20 | 372·8 |
| 1982 | Juni ........................ | 289·10 | 221·6 | 209·9 | 211·7 | 296·90 | 380·50 | 236·50 | 380·5 |
| | Desemba ................ | 337·10 | 243·8 | 221·5 | 211·9 | 313·40 | 336·00 | 281·70 | 410·9 |
| 1983 | Juni ........................ | 379·80 | 262·6 | 293·2 | 211·9 | 342·60 | 492·20 | 288·00 | 417·1 |
| | Desemba ................ | 425·80 | 272.4 | 307·9 | 211·9 | 359.70 | 516·80 | 289·30 | 424·4 |
| 1984 | Juni ........................ | 414·90 | 390·1 | 286·1 | 211·5 | 385·60 | 625·30 | 334·40 | 400·6 |
| | Desemba ................ | 497·80 | 537·6 | 424·2 | 212·8 | 451·10 | 664·20 | 391·50 | 456·8 |
| 1985 | Juni ........................ | 504·10 | 594·1 | 432·6 | 213·5 | 451·10 | 664·20 | 391·50 | 491·3 |
| | Desemba ................ | 620·50 | 687·9 | 507.7 | 213·5 | 496·50 | 702·40 | 391·50 | 520·4 |
| 1986 | Juni ........................ | 733·90 | 725·1 | 598·9 | 253·8 | 702·50 | 1,013·50 | 534·30 | 599·3 |
| | Desemba ................ | 885·40 | 869·9 | 605·2 | 253·8 | 815·40 | 1,061·40 | 535.70 | 793·5 |
| 1987 | Juni ........................ | 1,012·20 | 1,017·0 | 785·8 | 253·8 | 1,174·30 | 1,090·20 | 596·40 | 992·6 |
| | Desemba ................ | 1,364·20 | 1,208·6 | 1,080·9 | 355·30 | 1,457·80 | 1,345·10 | 713·90 | 1,443·8 |

*Chanzo*:—Idara ya Takwimu.

## FAHIRISI YA GHARAMA YA MAISHA YA WENYE KIPATO CHA JUU DAR ES SALAAM

(1977 = 100).

Jedwali Na. 30

| Mwaka | Miezi | | Fahirisi (Wastani) | (Badiliko) (%) (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|
| | Juni | Desemba | | |
| 1966 | 38·00 | 39·3 | 39·05 | — |
| 1967 | 40·50 | 41·20 | 40·85 | 4·61 |
| 1968 | 41·80 | 42·70 | 42·25 | 3·43 |
| 1969 | 42·40 | 43·60 | 43·00 | 1·78 |
| 1970 | 45·60 | 46·40 | 46·00 | 6·98 |
| 1971 | 48·10 | 49·70 | 48·90 | 6·30 |
| 1972 | 50·40 | 52·80 | 51·60 | 5·52 |
| 1973 | 54·00 | 60·40 | 57·20 | 10·85 |
| 1974 | 64·20 | 75·40 | 69·80 | 22·03 |
| 1975 | 85·20 | 90·00 | 87·60 | 25·50 |
| 1976 | 98·70 | 102·10 | 100·40 | 14·61 |
| 1977 | 111·60 | 122·30 | 116·95 | 16·48 |
| 1978 | 128·00 | 131·70 | 129·85 | 11·03 |
| 1979 | 143·70 | 151·70 | 147·70 | 13·75 |
| 1980 | 169·60 | 188·40 | 179·00 | 21·19 |
| 1981 | 219·60 | 233·70 | 226·65 | 26·62 |
| 1982 | 268·80 | 307·90 | 288·35 | 27·22 |
| 1983 | 343·80 | 371·80 | 357·80 | 24·09 |
| 1984 | 383·00 | 470·40 | 426·70 | 19·26 |
| 1985 | 480·40 | 569·90 | 525·15 | 23·07 |
| 1986 | 684·60 | 799·80 | 742·20 | 41·33 |
| 1987 | 955·80 | 1,261·60 | 1,108·70 | 49·38 |

*Chanzo*: Idara ya Takwimu.

## FAHIRISI YA BEI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIKAZO NA WAKAZI WA MIJINI TANZANIA BARA

(1977=100)

Jedwali Na. 31

| Robo Mwaka | Chakula | Vinywaji na Tumbaku | Kodi ya Nyumba | Umeme, Mafuta ya yaTaa, Maji | Nguo na Viatu | Fenicha na Vyombo vya Chakula | Huduma na Mahitaji ya Nyumbani | Huduma za Afya | Michezo na Starehe | Usafiri |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1974—1 | 50·40 | 58·10 | 183·80 | 47·50 | 53·50 | 92·90 | 67·60 | 146·60 | 65·00 | 61·00 |
| 2 | 61·70 | 63·10 | 103·80 | 45·30 | 66·30 | 50·00 | 73·50 | 98·60 | 66·20 | 63·10 |
| 3 | 62·80 | 68·70 | 95·80 | 48·10 | 60·50 | 64·30 | 73·50 | 85·00 | 55·00 | 69·60 |
| 4 | 87·40 | 72·80 | 95·80 | 47·00 | 63·80 | 64·30 | 73·50 | 104·80 | 57·50 | 80·30 |
| 1975—1 | 89·50 | 73·40 | 98·80 | 59·30 | 68·20 | 64·30 | 73·50 | 88·00 | 60·00 | 76·00 |
| 2 | 87·80 | 86·30 | 103·30 | 69·90 | 67·10 | 85·70 | 79·40 | 102·60 | 57·50 | 85·70 |
| 3 | 81·60 | 84·10 | 103·30 | 61·00 | 77·00 | 85·70 | 79·40 | 105·60 | 85·00 | 81·90 |
| 4 | 83·70 | 84·10 | 103·20 | 64·30 | 78·50 | 85·70 | 100·00 | 105·60 | 100·00 | 84·60 |
| 3 | 498·90 | 452·00 | 187·40 | 510·50 | 412·10 | 771·40 | 291·20 | 623·10 | 357·10 | 358·50 |
| 4 | 547·70 | 472·00 | 193·00 | 526·30 | 497·00 | 857·10 | 379·40 | 623·10 | 385.70 | 424·40 |
| 1985—1 | 565·30 | 476·00 | 217·00 | 565·80 | 546·50 | 942·90 | 470·60 | 753·80 | 400·00 | 446·30 |
| 2 | 563·90 | 523·00 | 217·00 | 717·10 | 564.60 | 985·70 | 488·20 | 753·80 | 400·00 | 456·10 |
| 3 | 572·60 | 528·00 | 217·00 | 717·10 | 698·00 | 1,114·30 | 555·90 | 750·80 | 400·00 | 456·10 |
| 4 | 682·20 | 540·00 | 217·00 | 717·10 | 745·50 | 1,171·40 | 638·20 | 792·30 | 400·00 | 456·10 |
| 1986—1 | 761·20 | 588·00 | 217·00 | 717·10 | 745·50 | 1,228·60 | 697·10 | 938·50 | 428·60 | 461·00 |
| 2 | 730·10 | 824·00 | 217·00 | 789·50 | 755·60 | 1,342·90 | 714·70 | 953·80 | 428·60 | 551·20 |
| 3 | 811·40 | 876·00 | 217·00 | 772·40 | 777·80 | 1,378·60 | 1,085·30 | 1,269·20 | 428·60 | 565·90 |
| 4 | 911·40 | 996·00 | 217·00 | 892·10 | 867·70 | 1,428·60 | 1,085·30 | 1,446·20 | 514·30 | 639·00 |
| 1987—1 | 987·90 | 996·00 | 217·00 | 892·10 | 898·00 | 1,535·70 | 1,097·10 | 1,484·60 | 514·30 | 739·00 |
| 2 | 969·60 | 1,304·00 | 217·00 | 936·80 | 916·20 | 1,557·10 | 1,097·10 | 1,484·60 | 514·30 | 929·90 |
| 3 | 1,031·30 | 1,336·00 | 217·00 | 1,128·90 | 939·40 | 1,564·30 | 1,120·60 | 1,500·00 | 728·60 | 975·60 |
| 4 | 1,207·00 | 1,424·00 | 217·00 | 1,142·10 | 944·40 | 1,650·00 | 1,244·10 | 1,500·00 | 1071·40 | 980·50 |

*Chanzo:*—Idara ya Takwimu.

## FAHIRISI YA BEI YA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WAKAZI WA MJINI—TANZANIA BARA (1977 = 100)

Jedwali Na. 32

| Mwaka | Robo ya Mwaka | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Robo ya Kwanza | Robo ya Pili | Robo ya Tatu | Robo ya Nne | Fahirisi (Wastani) | Badiliko (Asilimia) |
| 1969 | 40·60 | 40·70 | 41·40 | 41·30 | 41·00 | — |
| 1970 | 42·10 | 42·51 | 42·40 | 42·70 | 42·43 | 3·48 |
| 1971 | 43·50 | 44·20 | 44·20 | 45·30 | 44·05 | 3·83 |
| 1972 | 45·50 | 46·70 | 48·90 | 50·30 | 47·85 | 8·63 |
| 1973 | 51·70 | 52·90 | 52·90 | 53·80 | 52·83 | 10·40 |
| 1974 | 54·70 | 60·70 | 61·60 | 75·60 | 63·15 | 19·55 |
| 1975 | 78·30 | 80·40 | 78·70 | 81·00 | 79·60 | 26·05 |
| 1976 | 82·00 | 85·40 | 86·50 | 86·40 | 85·10 | 6·91 |
| 1977 | 96·00 | 94·00 | 92·60 | 97·40 | 95·00 | 11·63 |
| 1978 | 103·00 | 104·00 | 105·50 | 113·80 | 106·58 | 12·18 |
| 1979 | 114·90 | 116·60 | 121·10 | 128·90 | 120·35 | 12·93 |
| 1980 | 139·20 | 149·10 | 163·40 | 175·20 | 156·73 | 30·22 |
| 1981 | 181·20 | 188·30 | 203·20 | 215·00 | 196·93 | 25·65 |
| 1982 | 224·60 | 234·10 | 271·90 | 285·00 | 253·90 | 28·93 |
| 1983 | 291·70 | 314·00 | 324·30 | 360·50 | 322·63 | 27·07 |
| 1984 | 374·20 | 401·00 | 466·40 | 515·20 | 439·20 | 36·13 |
| 1985 | 542·60 | 557·80 | 580·80 | 660·30 | 585·38 | 33·28 |
| 1986 | 717·30 | 715·80 | 788·00 | 879·80 | 775·23 | 32·43 |
| 1987 | 938·40 | 947·70 | 1,009·50 | 1,134·00 | 1,007·40 | 29·95 |

Chanzo:—Idara ya Takwimu.

## FAHIRISI MBALIMBALI ZA BIDHAA NA HUDUMA ZITUMIWAZO NA WAKAZI WA MIJINI—TANZANIA BARA (1977 = 100)

Jedwali Na. 33

| Mwaka | Fahirisi: Dar es Salaam—Kipato cha Chini | Fahirisi: Dar es Salaam—Kipato cha Kati | Fahirisi: Dar es Salaam—Kipato cha Juu | Fahirisi: Wakazi wa Mijini Tanzania Bara | Badiliko (Asilimia): Dar es Salaam Kipato cha Chini | Badiliko (Asilimia): Dar es Salaam Kipato cha Kati | Badiliko (Asilimia): Dar es Salaam Kipato cha Juu | Badiliko (Asilimia): Wakazi wa Mijini Tanzania Bara |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1970 | 33·40 | 42·30 | 46·00 | 42·40 | 3·40 | 1·40 | 7·00 | 3,40 |
| 1971 | 34·60 | 42·90 | 48·90 | 44·10 | 3·59 | 1·42 | 6·30 | 4·01 |
| 1972 | 38·20 | 44·20 | 51·60 | 47,90 | 10·40 | 3·03 | 5·52 | 8·62 |
| 1973 | 41·70 | 50·70 | 57·20 | 52·80 | 9·16 | 14·71 | 10·85 | 10·23 |
| 1974 | 54·50 | 63·40 | 69·80 | 63·20 | 30·70 | 25·05 | 22·03 | 19·70 |
| 1975 | 80·10 | 85·20 | 87·60 | 79·60 | 46·97 | 34·38 | 25·50 | 25·95 |
| 1976 | 98·90 | 94·10 | 100·40 | 85·10 | 23·47 | 10·45 | 14·61 | 6·91 |
| 1977 | 115·60 | 105·20 | 117·00 | 95·00 | 16·89 | 11·80 | 16·53 | 11·63 |
| 1978 | 135·00 | 126·20 | 129·90 | 106·60 | 16·78 | 19·96 | 11·03 | 12·21 |
| 1979 | 141·00 | 147·10 | 147·70 | 120·40 | 4·44 | 16·56 | 13·70 | 12·95 |
| 1980 | 165·20 | 176·60 | 179·00 | 156·70 | 17·16 | 20·05 | 21·19 | 30·15 |
| 1981 | 215·90 | 232·70 | 226·70 | 196·90 | 30·69 | 31·77 | 26·65 | 25·65 |
| 1982 | 262·90 | 292·50 | 288·40 | 253·90 | 21·77 | 25·70 | 27·22 | 28·95 |
| 1983 | 325·00 | 363·70 | 357·60 | 322·60 | 23·62 | 24·34 | 23·99 | 27·06 |
| 1984 | 381·80 | 462·60 | 426·70 | 439·20 | 17·48 | 27·19 | 19·32 | 36·14 |
| 1985 | 559·70 | 661·50 | 525·2 | 585·4 | 46·60 | 43·00 | 23·08 | 33·29 |
| 1986 | 787·9 | 931·4 | 742·2 | 775·2 | 40·77 | 37·78 | 41·32 | 32·42 |
| 1987 | 997·80 | 1,194·78 | 1.108·70 | 1.007·40 | 26·64 | 31·10 | 49·38 | 29·95 |

*Chanzo*.—Idara ya Takwimu.

## 7.—MASHIRIKA YA UMMA

1. Kwa jumla, utendaji wa Mashirika ya Umma mwaka 1986 uliendelea kuathiriwa na hali ngumu ya uchumi kama ilivyokuwa kwa nyanja nyingine. Mchango wa Mashirika ya Umma katika Pato la Taifa mwaka 1986 ulikuwa Sh. 13,243 milioni likiwa ni ongezeko la Sh. 899 milioni au asilimia 7.3 kwa mchango katika mwaka 1985 uliokuwa Sh. 12,344 milioni. Ongezeko lilitokana na Mashirika ya Sekta za Kilimo, Viwanda, Biashara, Umeme na Maji, Usafirishaji, Fedha na Huduma za biashara. Tofauti na mwaka 1985 ambapo faida halisi ya Mashirika ilipungua, kulikuwepo ongezeko la faida la Sh. 344 milioni mwaka 1987. Ongezeko hilo lilichangia katika Pato la Taifa lililotokana na Mashirika ya Umma. Mambo mengine yaliyochangia ni nyongeza ya jumla ya mishahara kutoka Sh. 3,962 milioni mwaka 1985 kufikia Sh. 4,318 milioni mwaka 1986 (licha ya kupunguza ajira kwa asilimia 10.8 kutoka idadi ya waajiriwa 191,751 mwaka 1985 kufikia 171,031 mwaka 1986) na ongezeko la karibu mara mbili la utengaji kwa ajili ya uchakavu (depreciation reserve).

**Mapato na Matumizi:**

2. Matumizi ya Mashirika ya Umma kwa jumla mwaka 1986 yalipungua kwa asilimia 3.5 kutoka Sh. 51,849 milioni mwaka 1985 kufikia Sh. 50,033 milioni mwaka 1986. Mashirika ambayo matumizi yake yalipungua ni ya sekta ya ujenzi na ya biashara. Jumla ya matumizi ya mashirika ya sekta ya ujenzi yalipungua kutoka Sh. 315 milioni mwaka 1985 hadi kufikia Sh. 141 milioni mwaka 1986 na ya biashara kutoka Sh. 22,079 milioni kufikia Sh. 16,944 milioni. Matumizi ya mashirika ya sekta ya kilimo hayakutofautiana sana na ya mwaka 1985. Mashirika ya sekta nyingine yalikuwa na ongezeko la matumizi.

3. Kwa jumla, kuyumbayumba kwa uchumi kumefanya mashirika yaanze kuangalia suala la gharama kwa makini zaidi. Kwa upande wa mashirika ya ujenzi, mapato yalipungua kutoka Sh.313 milioni mwaka 1985 kufikia Sh. 119 milioni mwaka 1986. Kwa upande wa mashirika ya biashara, mapato yalishuka toka Sh. 23,991 milioni mwaka 1985 kufikia Sh. 17,608 milioni mwaka 1986. Mapato ya mashirika ya sekta nyingine yaliongezeka kwa viwango mbali mbali. Hata hivyo, kutokana na upungufu wa mapato ya sekta za biashara na ujenzi, mapato ya mashirika yote kwa jumla yalipungua kwa asilimia 2.6 kutoka Sh. 56,063 mwaka 1985 hadi Sh. 54,591 mwaka 1986.

4. Faida halisi ya mashirika kwa jumla mwaka 1986 iliongezeka kwa asilimia 8.2 kutoka Sh. 4,214 milioni mwaka 1985 kufikia Sh. 4,558 milioni mwaka 1986. Ongezeko hili lilijitokeza katika Mashirika ya sekta za Viwanda, Umeme na Maji, fedha na huduma za biashara. Mashirika yaliyokuwa na upungufu wa faida ni ya sekta za ujenzi, biashara na usafirishaji.

5. Mashirika ya sekta ya biashara yaliendelea kukabiliwa na ushindani mkubwa uliosababishwa na kulegeza masharti ya biashara hapo mwaka 1984 kwa kuwaruhusu watu binafsi kuingiza nchini bidhaa fulani fulani. Faida ya mashirika haya ilipungua kutoka Sh. 1,912 milioni mwaka 1985 kufikia Sh. 664 milioni mwaka 1986. Pamoja na ushindani huu, sababu nyingine ya kushuka kwa mapato na hivyo faida ni uzalishaji mdogo wa bidhaa.

6. Mashirika ya sekta ya usafirishaji yalikumbwa na ongezeko kubwa la gharama mbali mbali zikiwemo gharama za spea, matairi na mipira ya ndani. Hii ilisababisha mashirika yapate hasara ya Sh. 514 milioni kwa kulinganisha na faida iliyopatikana mwaka 1985 ya Sh. 458 milioni. Mashirika ya sekta ya ujenzi yaliendelea kukabiliwa na upungufu wa nyenzo za kazi hivyo yaliendelea kuendesha shughuli zake kwa hasara kutoka jumla ya hasara ya Sh. milioni 2 mwaka 1985 kufikia hasara ya Sh. 22 milioni mwaka 1986.

7. Jitihada za kuyafanya mashirika yaliyo katika misingi ya kibiashara kupunguza kuitegemea Serikali ziliendelea. Ruzuku na misaada kutoka Serikalini kwenda katika mashirika ya umma iliendelea kupungua mwaka 1986 na kuwa Sh. 2,018.6 milioni ikilinganishwa na Sh. 2,467.2 milioni mwaka 1985.

**Uwekezaji Rasilimali:**

8. Uwekezaji rasilimali katika mashirika ya umma mwaka 1986 uliongezeka kwa asilimia 58.6 kutoka Sh. 4,428 milioni mwaka 1985 kufikia Sh. 7,024 milioni mwaka 1986. Mashirika yaliyokuwa na ongezeko la uwekezaji ni ya sekta za viwanda (kutoka Sh. 1,461 milioni mwaka 1985 kufikia Sh. 2,037 milioni mwaka 1986); ujenzi (kutoka Sh. 455 milioni kufikia Sh. 692 milioni); usafirishaji (kutoka Sh. 415 milioni kufikia Sh. 684 milioni); umeme na maji (kutoka Sh. 1,068 milioni kufikia Sh. 2111 milioni) na Fedha na Hudutna za biashara (kutoka Sh. 475 milioni kufikia Sh. 1,156 milioni). Ongezeko la uwekezaji lilitokana hasa na hatua za kuimarisha mashirika kwa kuzingatia maelekezo ya Mpango wa Kufufua Uchumi hasa mashirika ya sekta za viwanda, ujenzi na usafirishaji. Katika sekta ya umeme na maji mchango mkubwa ulitokana na Shirika la Ugavi wa Umeme (TANESCO). Shirika liliendelea kupanua huduma zake hasa gridi inayoelekea kaskazini/magharibi yaani Dodoma/Singida/Shinyanga/Tabora/Mwanza/Musoma.

## VIPIMO MBALI MBALI VYA MAFANIKIO YA MASHIRIKA YA UMMA

Jedwali Na. 34

| Sekta | Ualhi (Idadi) | | | Faida halisi (Sh. milioni) | | | Mchango kwa Pato la Taifa (Sh. milioni) | | | Patolili lozalishwa na kila Mfanyakazi (Sh.) | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1984 | 1985 | 1986 | 1984 | 1985 | 1986 | 1984 | 1985 | 1986 | 1984 | 1985 | 1986 |
| Kilimo | 21,013 | 23,652 | 22,438 | 72 | 110 | 128 | 413 | 437 | 459 | 19,669 | 18,161 | 20,456 |
| Uchimbaji Madini | 4,124 | 4,594 | 3,814 | −29 | −64 | −7 | 74 | 65 | 119 | 17,919 | 14,124 | 31,201 |
| Viwanda | 57,842 | 65,037 | 53,153 | 771 | 827 | 2533 | 2,499 | 3553 | 5696 | 43,199 | 54,630 | 107,162 |
| Ujenzi | 3,308 | 3,715 | 1,452 | 40 | −2 | −22 | 117 | 90 | 18 | 35,248 | 24,226 | 12,397 |
| Umeme na maji | 8,374 | 9,319 | 9,490 | 90 | 162 | 754 | 488 | 920 | 2,510 | 58,264 | 98,723 | 264,489 |
| Biashara | 21,503 | 22,571 | 21,387 | 2,156 | 1,912 | 664 | 2887 | 3,208 | 1,463 | 134,241 | 142,129 | 68,406 |
| Usafirishaji | 42,130 | 44,922 | 39,110 | 233 | 458 | −514 | 1,778 | 2,770 | 2,164 | 42,191 | 61,662 | 55,331 |
| Fedha, huduma za Biashara | 15,796 | 15,999 | 18,406 | 1,706 | 831 | 1,063 | 1,246 | 1,293 | 807 | 78,881 | 80,818 | 43,844 |
| Huduma Nyinginezo | 1,863 | 1,942 | 1,781 | −12 | −20 | −41 | 12 | 8 | 7 | 6,549 | 4,119 | 3930 |
| Jumla | 175,953 | 191,751 | 171,031 | 5,027 | 4,214 | 4,558 | 9,514 | 12,344 | 13,243 | 54,071 | 64,375 | 77,430 |

*Chanzo:* Idara ya Takwimu.

## MUHTASARI WA TAKWIMU ZA MASHIRIKA YA UMMA

Jedwali Na. 35

(Sh. milioni)

| Sekta | Mishahara | | | Matumizi | | | Mapato | | | Uwekaji wa rasilimali | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1984 | 1985 | 1986 | 1984 | 1985 | 1986 | 1984 | 1985 | 1986 | 1984 | 1985 | 1986 |
| Kilimo ..................... | 229 | 257 | 241 | 718 | 814 | 816 | 790 | 924 | 944 | 26 | 42 | 24 |
| Uchimbaji Madini ...... | 60 | 76 | 83 | 364 | 369 | 611 | 334 | 305 | 604 | 50 | 80 | 46 |
| Viwanda ..................... | 878 | 1,054 | 1.294 | 13,611 | 17,097 | 17,679 | 14,382 | 17.924 | 20,212 | 908 | 1.461 | 2.037 |
| Ujenzi ..................... | 70 | 85 | 39 | 351 | 315 | 141 | 391 | 313 | 119 | 283 | 455 | 692 |
| Umeme na maji ......... | 145 | 180 | 256 | 955 | 1,601 | 2,786 | 1,045 | 1.763 | 3,540 | 664 | 1.068 | 2,111 |
| Biashara ..................... | 410 | 474 | 465 | 16,712 | 22,079 | 16,944 | 18,868 | 23,991 | 17,608 | 268 | 431 | 273 |
| Usafirishaji ............... | 1,094 | 1.239 | 1.512 | 4,110 | 5.551 | 6,604 | 4,343 | 6,009 | 6,090 | 258 | 415 | 684 |
| Fedha, huduma za Biashara ............... | 447 | 578 | 399 | 2,351 | 3,925 | 4,249 | 4,057 | 4,756 | 5,312 | 295 | 475 | 1,156 |
| Huduma Nyinginezo .. | 17 | 19 | 29 | 91 | 98 | 203 | 79 | 78 | 162 | 0 | 1 | 1 |
| Jumla ... | 3,350 | 3,962 | 4,318 | 39,263 | 51,849 | 50,033 | 44,289 | 56,063 | 54,591 | 2,752 | 4,428 | 7,024 |

*Chanzo*: Idara ya Takwimu.

# 8—MAENDELEO YA SAYANSI NA TEKINOLOJIA

1. Katika kipindi cha 1987/88 jitihada zilielekezwa katika kuendeleza shughuli za utafiti, utundu mpya pamoja na kuhakikisha kuwa tekinolojia ambazo zipo zinafanya kazi kikamilifu. Kwa hiyo hatua mbali mbali zilichukuliwa katika kujenga uwezo wa Taifa wa kuhudumia (service) tekinolojia hizo. Hali kadhalika katika juhudi za kusambaza matokeo ya utafiti wakisayansi kwa wananchi kwa jumla, vyombo vya Utafiti na Maendeleo (R & D) viliwajibika kubuni mfumo mzuri wa kusambaza matokeo ya utafiti na uvumbuzi ili yaweze kutumika katika kuendeleza sekta mbalimbali za uchumi. Wananchi wengi hivi sasa wameanza kuelewa umuhimu wa tekinolojia katika kuongeza tija na ubora wa maisha yao.

2. Ili kutanikisha shabaha na malengo ya kuendeleza sayansi na tekinolojia ni muhimu kuelekeza rasilimali inayotengwa kuendeleza shughuli za utafiti na maendeleo (R & D) kulingana au kufuata misingi iliyopendekezwa na Sera ya Taifa ya Sayansi na Tekinolojia. Sera hiyo inatoa umuhimu wa juu katika kuendeleza sekta za Kilimo, Viwanda na Maliasili.

3. Katika jitihada za kuendeleza sayansi na tekinolojia nchini, vyombo au Mashirika yanayohusika yalitekeleza shughuli mbali mbali kama inavyoelezwa katika aya zifuatazo:

**Baraza la Utafiti wa Kisayansi:**

4. Katika kipindi cha mwaka 1987/88 Baraza la Utafiti wa Kisayansi (UTAFITI) liliendelea na shughuli zake muhimu ikiwa ni pamoja na kuratibu maendeleo ya sayansi na tekinolojia nchini. Shirika lilitoa kiasi cha Sh. 1.5 milioni kwa watafiti mbalimbali ili kuwawezesha kufanya utafiti katika sekta za kilimo, afya na maliasili. Kiasi hiki ni kama asilimia 38.0 ya fedha zote ambazo zilitengwa kwa shughuli za kuendeleza utafiti.

5. Baraza liliendelea na mradi wake wa kuendeleza matumizi ya Nishati itokanayo na samadi/mabaki ya mimea (Dodoma Rural Energy Project) huko Dodoma na kuendeleza utafiti kuhusu kuongeza ubora wa majiko yanayotumia mkaa.

6. Kitengo cha Usambazaji wa habari cha Baraza la Utafiti (TANRIS) kwa kushirikiana na NTIS (National Technical Information Service) kiliendelea kutoa habari za maendeleo ya Sayansi na Tekinolojia kwa Wanasayansi na Wanatekinolojia pamoja na watumiaji wengine nchini.

7. Shughuli za uendelezaji utundu (innovation) mbalimbali ziliendelea kutiliwa mkazo zaidi katika mwaka 1987/88. na Baraza liliweza kuwatunukia Tuzo ya Sayansi na Tekinolojia Watanzania mbali mbali kati ya mwaka 1982—1988, ambao wameendeleza tekinolojia katika sekta mbalimbali za uchumi hasa Viwanda, Kilimo, Nishati na Maliasili. Ni madhumuni ya Baraza kuendelea kutoa motisha kwa Watanzania ili kufanikisha uendelezaji na matumizi ya tekinolojia nchini.

**Tume ya Mionzi (National Radiation Commission):**

8. Tume ya Mionzi ilianzisha utaratibu wa kutoa huduma kwa wafanyakazi wapato 355 ambao wanatumia au kufanya kazi katika sehemu zinazotumia vifaa vya nguvu za mionzi (kama X-ray, Isotopes na vifaa vingine vya nguvu za nuklia/atomiki). Huduma hizo ni pamoja na kuchunguza kiasi cha nguvu za mionzi (Radiation) ambacho wafanyakazi hao wanapata katika miili yao kutokana na matumizi ya vifaa hivyo. Madhumuni ya utafiti huo ni kutoa tahadhari juu ya matumizi mabaya ya vyombo hivyo, na vile vile kuwakinga wafanyakazi au watumiaji wa vifaa hivyo ili wasipate madhara yoyote yale.

9. Katika kuimarisha huduma ya kinga, Tume imeanzisha ukaguzi wa vituo vinavyohusika na matumizi ya nguvu za mionzi na kutoa ushauri na miongozo kuhusu usalama wa wafanyakazi na watumishi wengine, ubora wa mitambo, na ubora wa sehemu zenyewe za kufanyia kazi hizo. Hali kadhalika Tume imekwisha anzisha huduma ya kupima mazingira (environmental monitoring) ili kutoa tahadhari mapema endapo sehemu hizo zitaonekana kuwa na kiasi kikubwa cha nguvu za mionzi (radio-active sources).

**National Institute for Medical Research (NIMR):**

10. Katika kipindi cha 1987/88 Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) iliendelea na utafiti kuhusu magonjwa ya tumbo, zinaa, na malaria ili kubuni mbinu na namna ya kutibu au kuzuia magonjwa hayo. Hali kadhalika, Kitengo cha Utafiti wa Dawa za Asili kilichopo Muhimbili Medical Centre kiliendelea na utafiti wake kuhusu madawa ya asili ambayo yangeweza kutumika katika matibabu ya magonjwa mbalimbali.

**Tanzania Food and Nutrition Centre (TFNC):**

11. Taasisi ya lishe ilijishughulisha na utafiti wa aina mbali mbali hasa kuhusuana na lishe iliyoko katika vyakula vinavyotumiwa na wananchi. Utafiti huu ulihusiana na jinsi ya kuhifadhi ubora wa vyakula na ukosekanaji wa aina fulani ya Vitamini hasa Vitamini A, madini ya joto na chuma. Katika kufanikisha utafiti huo Shirika lilisaidiwa na Mashirika kama UNICEF na WFP.

**Tanzania Agricultural Research Organisation (TARO):**

12. TARO pamoja na vituo vyake vya utafiti wa mazao mbalimbali. iliendelea na utafiti wake wa kupata miche na mbegu bora ambazo huvumilia mazingira na hazishambuliwi ovyo na wadudu waharibifu. Matokeo ya baadhi ya utafiti huo yamekwisha sambazwa kwa wakulima kwa matumizi yao. Mazao yanayohusika ni pamoja na Mahindi. Korosho, Pamba. Miwa, Mtama na Katani.

**Uyole Agricultural Centre (UAC):**

13. Kituo cha Utafiti wa Kilimo cha Uyole. Mbeya licha ya kuendeleza utafiti wa mazao ya pareto, mahindi, viazi mviringo, matunda mboga na maendeleo ya mifugo, kituo kilianza programu ya zao la kakao ambalo linaonyesha dalili za kustawi katika mikoa ya Mbeya na Tanga. Baadhi ya matokeo ya utafiti huo umekwisha sambazwa kwa wakulima (kwa mfano: mbegu bora za mboga. viazi mviringo. matunda na mahindi).

**Tanzania Livestock Research Organisation (TALIRO):**

14. Katika kipindi cha mwaka 1987/88. Taasisi ya Utafiti wa Mifugo pamoja na vituo vilivyoko chini ya Taasisi hiyo, viliendelea kufanya utafiti juu ya magonjwa ya mifugo. malisho bora ya mifugo. uzalishaji wa mifugo bora pamoja na njia bora za kuongeza mazao ya mifugo hasa maziwa na nyama.

**Makutupora Viticulture Research:**

15. Kituo hiki. kiliendelea na kufanya utafiti wa mizabibu, na mvinyo kwa manufaa ya wakulima. Aidha, kituo kilitoa huduma za ushauri kwa wakulima na watengenezaji wa mvinyo. kuwafundisha wataalam na wakulima jinsi ya kilimo bora, cha mizabibu na usindikaji mbegu kwa ajili ya mafuta (oenology).

**Dakawa Agro-Scientific Research Centre:**

16. Katika kipindi cha mwaka 1987 kituo kiliendelea kufanya utafiti wa mazao, hasa mpunga. mahindi na mboga kwa umwagiliaji ili kuongeza uzalishaji wa mazao hayo. Shughuli nyingine zilizofanyika zilihusiana na utengenezaji wa mashine ya kupukuchulia mahindi.

**Tropical Pesticides Research Institute (TPRI):**

17. Taasisi hii iliendelea na udhibiti wa aina ya mimea inayoingizwa nchini toka nchi za nje (Plant quarantine). na vile vile kuendeleza programu ya kukabili au kuzuia wadudu wanaoshambulia mazao mbali mbali ikiwa ni pamoja na mahindi na miwa.

**Utafiti na Maendeleo katika Sekta ya Maliasili:**

18. Taasisi muhimu za utafiti na maendeleo (R & D) zinazoshughulikia sekta ya maliasili ni pamoja na Tanzania Fisheries Research Institute (TAFIRI). Tanzania Forestry Research Institute (TAFORI) na Serengeti Wildlife Research Institute (SWRI). Pamoja

na matatizo ya vifaa na fedha za kuendeleza utafiti. Taasisi hizi zimejitahidi kuelekeza utafiti katika maeneo machache muhimu. TAFIRI ilijishughulisha zaidi na utafiti wa zana na mbinu mbali mbali za kuvulia samaki hasa kwa ajili ya wavuvi wadogo wadogo, pamoja na kukadiria kiasi cha samaki ambacho kinaweza kuvuliwa pasipo kuathiri mazingira ya maeneo yenyewe. TAFORI iliendeleza utafiti kuhusu matumizi bora ya misitu/miti, hifadhi ya mazingira, kilimo cha mseto, pamoja na kuzalisha miche inayovumilia hali ya hewa ya sehemu mbali mbali nchini. SWRI ilikuwa na jukumu la kuoanisha shughuli za utafiti wa wanyamapori unaofanywa na vituo vya Gombe, Mahale, Serengeti, Kingupira pamoja na Njiro. Utafiti ulihusika zaidi na maendeleo ya wanyamapori, mazingira yao na jinsi ya kuvuna wanyama hao kwa matumizi ya wananchi kwa jumla. Uwezekano wa kujaribu kuwafuga baadhi ya wanyama pori ulianza kuchunguzwa. Utafiti mwingine ulihusu ubora wa mazao ya nyuki ili kufanikisha shabaha ya kuzalisha asali na nta ambayo masoko yake yameongezeka hapa nchini na nchi za nje.

19. Kituo cha Utafiti wa Nyumba na Vifaa vya Ujenzi (BRU) kiliendelea na shughuli yake hiyo muhimu. Utafiti ulihusika zaidi na majaribio ya aina ya bati ya kuezekea nyumba ambayo hutengenezwa kutokana na katani na saruji (Sisal reinforced sheets), ujenzi wa nyumba nafuu kulingana na mazingira au hali ya hewa ya sehemu mbalimbali za nchi, matumizi ya mchanga, chokaa, silica, na udongo wa mfinyanzi katika kutengeneza vifaa mbalimbali vya ujenzi.

**Utafiti na Maendeleo katika Sekta ya Viwanda:**
**Tanzania Engineering Manufacturing and Design Organisation (TEMDO):**

20. TEMDO iliendelea na kubuni michoro inayoweza kutumika katika utengenezaji wa mashine na vipuri mbali mbali; na kutoa ushauri wa kihandisi kwa Makampuni na watu mbali mbali. Katika jitihada za kuendeleza teknolojia nchini TEMDO ilijishughulisha na kubuni michoro na kusimamia utengenezaji wa mashine zifuatazo: pump za kusukuma maji, mashine za kupukuchua mahindi na mpunga, mashine za kutengeneza matofali pamoja na foroma (moulds) za kutengeneza vipuri mbali mbali. Hali kadhalika TEMDO ilisimamia ukamilishaji wa ujenzi wa ofisi zao mpya pamoja na karakana ya kufanyia kazi. Ukamilishaji na ujenzi wa karakana utaipa TEMDO uwezo wa kubuni na kutengeneza mashine na vifaa mbali mbali kwa ajili ya matumizi katika sekta mbali mbali.

**Centre for Agricultural Mechanisation and Rural Technology (CAMARTEC):**

21. Katika juhudi za kusaidia maendeleo ya kilimo nchini, CAMARTEC iliendelea na juhudi zake za kutawanya habari na kutoa majaribio kuhusu zana rahisi mbali mbali za kilimo ambazo zimetengenezwa na Shirika hilo. Zana hizo ni pamoja na majembe (plau) ya kukokotwa na ng'ombe, nyenzo za usafirishaji vijijini, na hifadhi ya mazao. Hali kadhalika CAMARTEC ilijishughulisha pia na uendelezaji wa teknolojia ya biogas, nguvu za upepo na jua (wind and solar energy) na utengenezaji wa vifaa mbali mbali kwa matumizi ya wananchi vijijini.

22. Ili kuhakikisha kuwa wananchi wanaelewa vizuri matumizi ya zana hizo CAMARTEC iliendesha mafunzo mbali mbali kituoni hapo, na kutoa ushauri wa jinsi ya kuhudumia vifaa hivyo. Muhimu pia ni kazi ya kujaribu uwezo na ufanisi (efficiency) wa zana za kilimo kama matrekta, plau, n.k., ambazo huagizwa toka nchi za nje au ambazo hutengenezwa na baadhi ya makampuni hapa nchini. Shughuli hii inamwezesha mtengenezaji kujua dosari zilizopo na hatimaye kurekebisha mambo fulani katika zana hizo.

**Tanzania Industrial Research Development Organisation (TIRDO):**

23. TIRDO iliendelea na utengenezaji wa majaribio ya vifaa vya kufundishia mashuleni, na vile vile kukamilisha uchunguzi kuhusu "process technology" ifaayo katika kutengeneza "caustic soda" kutokana na magadi ya Ziwa Natron. Mitambo ya majaribio ya "process" hiyo ilizinduliwa rasmi mapema mwaka 1988, na caustic soda itokanayo na mitambo hiyo imeonekana kuwa bora kwa matumizi katika viwanda vya sabuni, nguo na vinginevyo.

**Tanzania Bureau of Standards (TBS):**

24. Shirika la kudhibiti Viwango (TBS) liliimarisha zaidi shughuli zake za kutayarisha na kuweka viwango vya ubora wa bidhaa mbali mbali zinazotengenezwa na baadhi ya viwanda hapa nchini. Huduma hiyo ni muhimu hasa katika kuelewa, kutumia na kuendeleza teknolojia kwa jumla kwani TBS huwa ni kiungo kati ya watengenezaji wa bidhaa na watumiaji wa bidhaa hizo. Hadi Mei, 1988 TBS ilikuwa imekwisha tayarisha na kuweka viwango vya bidhaa mbali mbali kama ifuatavyo: nguo (vitenge, khanga, vitambaa vya kushona nguo); vyakula mbali mbali ikiwa ni pamoja na mafuta ya kupikia, vyakula vya mifugo, sukari, vinywaji baridi, nyama ya makopo, mikate, maziwa ya watoto n.k.; bidhaa za umeme kama "bulbs na cables"; radieta, betri na namba (plates) za magari, dawa za mbu na bidhaa kadhaa za chuma.

**MEIDA (Metal Engineering Development Association):**

25. Katika kipindi cha 1987/88, Shirika la Uendelezaji Uhandisi Vyuma (MEIDA) lilishughulikia uroaji wa mafunzo kwa wahandisi na mafundi stadi katika nyanja zifuatazo:

- Uchoraji na urengenezaji wa vifaa (design and manufacture of press loos)
- Njia mbali mbali za ukataji vyuma na mabati (metal cutting techniques);
- Uendeshajina uhakiki waubora(Management Assurance of Quality).

Hali kadhalika, MEIDA ilielekeza juhudi zake za mradi wa "MEIDA—TAMCO ANCILLARY" wenye lengo la kusaidia kampuni zenye uwezo wa kutengeneza vikorombwezo (components) vya magari aina ya SCANIA, ikiwa ni pamoja na kuzipatia kampuni hizo michoro na vielelezo mbali mbali vya urengenezaji wa vikorombwezo hivyo. Vikorombwezo vinavyolengenezwa kwa wakati huu ni vya radiators, silencers, paints, thinners, bumpers, inner cross members, brackets, tyres na tubes.

**Utafiti Mwingine:**

26. Katika jitihada za kuendeleza sayansi na tekinolojia baadhi ya vyombo vingine na watu binafsi waliendeleza utafiti katika sekta mbali mbali. Vyuo Vikuu vya Dar es Salaam na Sokoine, Morogoro pamoja na taasisi nyingine za mafunzo zilihusika zaidi na utafiti huo. IPI (Institute of Production Innovation) iliyoko katika Kitivo cha Uhandisi cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kiliweza kubuni na kutengeneza mashine na vipuri mbali mbali kwa ajili ya matumizi ya sekta za kilimo na viwanda. Hali kadhalika, IPI iliendelea kutoa ushauri katika masuala ya uhandisi hasa viwandani.

## 9.—IDADI YA WATU NCHINI

1. Idadi ya watu nchini Tanzania katika mwaka 1987 ilikadiriwa kuwa 23·2 milioni—Tanzania Bara ikiwa na watu 22·6 milioni na Zanzibar ikiwa na watu 0·61 milioni. Ilikadiriwa pia kuwa kati ya idadi hii asilimia 78·6 walikuwa wanaishi vijiini Tanzania Bara, na asilimia 64 ya watu wote Zanzibar walikuwa wanaishi vijijini. Kwa hiyo Zanzibar ina asilimia kubwa zaidi ya watu wanaoishi mijini kuliko Tanzania Bara.

2. Hali ya vizazi na vifo nchini haitegemewi kuwa ilibadilika mwaka 1987 kutoka hali ilivyokuwa mwaka 1986 ya watoto 48 kuzaliwa kwa kila Watanzania 1,000 kwa mwaka na vifo 15 kutokea kwa kila Watanzania 1,000 kila mwaka. Kwa hali hii inategemewa kuwa katika mwaka 1987 idadi ya watu nchini iliongezeka kwa asilimia 3·3, kama

ilivyokuwa miaka iliyotangulia. Uchambuzi wa sensa ya mwaka 1978 umeonyesha kuwa pamoja na hali hii ya jumla kwa nchi nzima, vizazi, vifo na ongezeko la idadi ya watu inatofautiana kutoka mkoa hadi mkoa. Hali ya vizazi kimkoa ni watoto 35 hadi 62 wanaozaliwa kwa kila watu 1,000 kwa mwaka, ambapo vifo kwa kila watu 1,000 kwa mwaka hutofautiana kimkoa kutoka mikoa yenye idadi ya vifo 10 hadi mikoa yenye vifo 23. Kutokana na tofauti hii ya vizazi na vifo kimkoa kasi ya ongezeko la idadi ya watu pia hutofautiana kati ya mikoa. Sensa ya mwaka 1978 ilionyesha kuwa kati ya mwaka 1967—1978 ongezeko la idadi ya watu kimkoa ilikuwa kati ya asilimia 1·7 na asilimia 7·8 kwa mwaka.

3. Katika kitabu hiki toleo la mwaka jana vilitajwa vyombo mbali mbali vinavyoshughulikia masuala ya idadi ya watu. Vyombo hivi ni pamoja na kitengo cha Sensa kilicho chini ya Idara ya Takwimu. Kitengo hiki kina jukumu la kukusanywa takwimu zote zinazohusiana na idadi ya watu nchini. Hivi sasa Taifa linajiandaa kufanya sensa ya tatu tangu Tanzania ijitawale. Sensa hii itafanyika tarehe 28 Agosti mwaka 1988.

4. Ofisi ya Msajili Mkuu wa Serikali iliyoko Wizara ya Sheria ni chombo kingine muhimu cha Serikali katika masuala ya idadi ya watu. Ofisi hii pamoja na mambo mengine ina jukumu la kuandikisha vizazi na vifo nchini. Tangu mwaka 1981 ofisi hii imekuwa na kazi kubwa ya kuimarisha na kupanua huduma za uandikishaji wa vizazi na vifo ili zienee nchi nzima. Hadi mwaka 1987 uimarishaji na upanuzi wa huduma hizo ulikuwa umeenea katika wilaya 12 Tanzania Bara na wilaya zote 10 za Zanzibar. Lengo ni kuandikisha vizazi na vifo vijijini kwa kutumia makatibu wa vijiji, na pia hospitalini. Uzoefu wa miaka saba iliyopita umeonyesha kuwa uandikishaji wa vizazi na vifo hospitalini una mafanikio makubwa. Uandikishaji wa vizazi na vifo uliokamili unaiwezesha nchi kujua kwa usahihi kasi ya ongezeko la idadi ya watu wake.

5. Vyombo vingine vya Serikali vinavyojishughulisha na idadi ya watu ni Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais kupitia Mradi na Elimu ya Familia (Family Life Education Programme—FLEP) na Wizara ya Elimu kupitia Mradi wa Elimu ya Familia Mashuleni. Jukumu la FLEP ni kuwaelimisha wananchi juu ya mahusiano kati ya uzazi na maendeleo ya familia. Lengo la Elimu ya Familia mashuleni ni kuwaandaa vijana kuwa wazazi bora. Hadi mwaka 1987 shughuli za FLEP zilikuwa zimeenea katika Mikoa 5.

6. Wizara za Afya Tanzania Bara na Zanzibar zina miradi mikubwa ya kuendeleza afya ya mama na mtoto na uzazi wa mpango. Miradi hii ina lengo la kupunguza vifo vya akina mama na watoto kwa kusambaza huduma za kinga ya maradhi kama vile huduma za chanjo na uzazi wa majira.

7. Chama cha Uzazi na Malezi Bora Tanzania (UMATI) kimeshughulikia uzazi wa majira na malezi bora ya watoto tangu mwaka 1959. Hivi sasa chama hiki kinashirikiana na Wizara za Afya katika kutoa huduma za uzazi wa mpango. Kazi muhimu ya UMATI imekuwa kufundisha wafanyakazi wa Wizara ya Afya katika kutoa huduma za uzazi wa mpango, na pia kuelemisha wanachama wake na wananchi kwa jumla umuhimu wa uzazi wa mpango katika maendeleo ya familia na nchi kwa jumla.

8. Chama cha Mapinduzi kimekuwa mstari wa mbele katika kuwaelimisha viongozi wake mahusiano kati ya ongezeko la idadi ya watu na maendeleo ya nchi. Jumuia ya Wazazi Tanzania (WAZAZI) imeanzisha Elimu ya Familia na Malezi kwa viongozi na wanachama wake.

9. Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ikishirikiana na Taasisi nyingine imepiga hatua kubwa katika kuandaa Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu. Matarajio ni kwamba Sera hiyo itakuwa tayari ifikapo Desemba 1988. Kati ya mwezi Mei na Agosti mwaka 1988 zitaendeshwa warsha za kujadili mapendekezo ya awali ili kupata maoni kutoka jumuia mbali mbali kabla mapendekezo ya mwisho ya sera hayajaandikwa.

## 10.—HALI YA UCHUMI DUNIANI NA USHIRIKIANO WA KIUCHUMI KIMATAIFA

Hali ya uchumi duniani ilikuwa ya mchanganyiko katika mwaka 1987. Kukua kwa uchumi wa nchi chache zilizoendelea kuliambatana na kulegalega ama kuzorota kwa uchumi wa nchi nyingine zilizoendelea. Vile vile, hali ya uchumi wa nchi zinazoendelea ilitofautiana ambapo ukuaji wa uchumi wa nchi za Kiafrika (Sub-Sahara) na zile zinazouza nje mafuta ya petroli ulikuwa mdogo mno au ulishuka. Papo hapo, uchumi wa nchi kadhaa zinazoendelea uliweza kukua kwa viwango vizuri. Kwa jumla, hali ya uchumi duniani iliendelea kuwa ngumu na kuathiri nchi zinazoendelea hasa za Kiafrika kutokana na kuwepo kwa matatizo sugu hususan kuongezeka kwa malimbikizo ya madeni, bei duni kwa bidhaa zinazouzwa nje na nchi zinazoendelea na kuyumba kwa viwango vya ubadilishanaji fedha (exchange rate instability). Ingawaje nchi nyingi hasa zinazoendelea ziliandaa na kutekeleza mipango ya kurekebisha na kufufua uchumi wao na pia azma ya kushirikiana kimataifa ilizidi kudhihirika kuwa ni muhimu, hapakuwepo na hatua thabiti zilizochukuliwa kimataifa kutatua matatizo yaliyopo ya kiuchumi duniani.

**Uzalishaji, Biashara na Bei:**

2. Pato la Taifa (GDP) duniani liliongezeka kwa asilimia 3·2 katika mwaka 1987 ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 3·5 katika mwaka 1986. Pato la Taifa la nchi zilizoendelea za Magharibi lilikuwa kwa asimilia 2·7 katika mwaka 1987 kama ilivyokuwa katika mwaka 1986. Ongezeko halisi la kukua kwa uchumi wa nchi za kijamaa lilishuka kutoka asilimia 4·6 katika mwaka 1986 hadi asilimia 3·2 katika mwaka 1987. Pato la Taifa la nchi zinazoendelea liliongezeka kwa asilimia 2·1 katika mwaka 1987 ikilinganishwa na asimilia 3·2 mwaka 1986. Ongezeko la Pato la Taifa la nchi za Kiafrika kwa jumla lilikuwa asilimia 0·8 katika 1987 ikilinganishwa na asilimia 0·5 katika mwaka 1986 ambapo Pato la Taifa la nchi za Kiafrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara liliongezeka kwa asilimia 2·5 katika mwaka 1987 ikilinganishwa na asilimia 3·7 mwaka 1986.

**Ongezeko la Pato la Taifa (GDP) Duniani:**

(Katika asilimia)

| | *1986* | *1987* |
|---|---|---|
| Dunia | 3·5 | 3·2 |
| Nchi zilizoendelea za Magharibi | 2·7 | 2·7 |
| Marekani | (2·9) | (2·7) |
| Japan | (2·5) | (3·5) |
| Ulaya Magharibi | (2·5) | (2·3) |
| Nchi zilizoendelea za Kijamaa | 4·6 | 3·2 |
| China | 7·4 | 10·0 |
| Nchi zinazoendelea | 3·2 | 2·1 |
| Bangladesh | 4·4 | 2·5 |
| Brazil | 8·2 | 3·5 |
| Nigeria | −6·0 | 1·0 |
| Nchi za Kiafrika (Kusini mwa Jangwa la Sahara) | 3·7 | 2·5 |

*Chanzo:* Makadirio ya Umoja wa Mataifa.

3. Wingi wa biashara duniani (World Trade Volume) uliongezeka kwa asilimia 4 katika mwaka 1987, ikiwa ni mara ya pili ya kupatikana kwa kiwango cha juu kama hiki katika miaka ya 1980. Ongezeko hili lilitokana hasa na ongezeko katika biashara ya bidhaa za viwanda (asilimia 5) na kilimo (asilimia 4). Thamani ya mauzo ya bidhaa nje (merchandise exports) iliongezeka kwa asilimia 15·5 katika mwaka 1987 na kufikia Dola za Kimarekani bilioni 2,450. Kiwango hiki kilifikiwa kutokana na kuongezeka kwa wingi wa biashara, kushuka kwa thamani ya dola ya Kimarekani pamoja na kutoyumbayumba kwa bei (katika dola za Kimarekani) za mafuta ya petroli na bidhaa nyingine za asilia.

4. Katika mwaka 1987 bei (kwa dola za kimarekani) za bidhaa zisizo za mafuta ya petroli (non-oil commodities) ziliongezeka kwa asilimia 8·6 kuliko zile za mwaka 1986. Hata hivyo, wastani wa fahirisi ya bei katika fedha za SDR ulishuka kwa asilimia 1·8. Kuongezeka kwa bei za bidhaa katika dola za Kimarekani kunatokana hasa na bei za juu za bidhaa za vyuma na malighafi za kilimo. Bei za malighafi ya kilimo ziliongezeka kwa wastani wa asilimia 33·5 katika mwaka 1987 kutokana na mahitaji makubwa na upungufu wa utoaji wa baadhi ya bidhaa, kama vile pamba ya kati (medium-staple cotton), na magogo. Kwa upande mwingine, bei za bidhaa za vinywaji zilianguka kwa asilimia 28 ambapo bei ya kahawa ilianguka kwa asilimia 37·4 kutokana na kuzinduka kwa uzalishaji huko Brazil na malimbikizo (stocks) katika nchi walaji. Katika mwaka 1987, bei za bidhaa katika dola za Kimarekani zilizouzwa na nchi zilizoendelea zilipanda kwa asilimia 13·4 kutoka kiwango cha mwaka 1986. Lakini kwa upande wa nchi zinazoendelea bei za bidhaa zake zilipanda kwa asilimia 3·3 tu.

5. Ongezeko la bei kwa wastani katika nchi zilizoendelea lilikuwa asilimia 2·9 katika mwaka 1987, ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 2·4 katika mwaka 1986, kiwango ambacho kilikuwa ndicho cha chini sana katika miaka 22. Ongezeko la bei kwa wastani katika nchi zinazoendelea lilikuwa kubwa sana hasa katika robo ya tatu ya mwaka 1987 ambapo ongezeko la bei lilikuwa asilimia 47·2 ikilinganishwa na asilimia 29·4 katika robo ya tatu ya mwaka 1986. Ongezeko hili lilitokana hasa na ongezeko kubwa la bei katika nchi za Marekani ya Kusini ambako ongezeko la bei kwa wastani kwa mwaka lilikuwa asilimia 130·1.

**Hali ya Fedha na Misaada Duniani:**

6. Katika mwaka 1987 uchumi duniani ulikabiliwa na matatizo makubwa hasa yahusuyo mizania ya malipo (external imbalances), malimbikizo ya madeni ya nchi zinazoendelea, na kuyumba kwa viwango vya ulipanaji (exchange rate instability).

7. Kulikuwepo ongezeko la asilimia 20 katika akiba ya fedha za kigeni duniani (global reserves) na kufikia kiwango cha SDR bilioni 503 katika mwaka 1987. Ongezeko hilo lilitokana na nchi chache zilizoendelea hasa Japani na Ujerumani Magharibi na pia China na Taiwan. Papo hapo, akiba ya fedha za kigeni ya nchi zinazoendelea ilipungua kwa asilimia 0·2 na kufikia SDR bilioni 132; kiwango ambacho ndicho cha chini sana katika miaka ya 80. Mabadiliko haya katika akiba ya fedha za kigeni yalitokana hasa na kuingilia kati kwa Serikali katika masoko ya fedha za kigeni (foreign exchange intervention), marekebisho katika biashara ya kawaida (current account adjustments) na kukopa katika masoko ya fedha duniani. Kutokana na mabadiliko hayo, Japani ilichukua nafasi ya Ujerumani Magharibi, kuwa nchi yenye malimbikizo ya akiba isiyo ya dhahabu makubwa kuliko nchi yoyote duniani.

8. Mnamo Oktoba 19, 1987, soko la dunia la hisa, malimbikizo ya bidhaa na ubadilishanaji fedha lilitikiswa vibaya (stock market crash) na kusababisha kuyumba kwa biashara ya soko hilo. Thamani ya dola ya Kimarekani ilishuka kwa wastani wa asilimia 16 katika mwaka 1987 ikilinganishwa na asilimia 13 katika mwaka 1986. Fedha za Kijapani (Yen) ilijitokeza kuwa na thamani kubwa sana kuliko aina ya fedha zingine.

9. Malimbikizo ya madeni ya nchi zinazoendelea yaliongezeka kwa asilimia 6¼ na kufikia dola za Kimarekani bilioni 1,190 katika mwaka 1987. Ongezeko hili linatokana basa na kuthamini upya (revaluation) mikopo katika fedha zisizo katika dola za Kimarekani. Malimbikizo ya Madeni ya nchi za Kiafrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara yaliongezeka kutoka dola za Kimarekani bilioni 101 katika mwaka 1986 hadi bilioni 218 katika mwaka 1987. Kiwango hiki cha madeni ni sawa na asilimia 70 ya Pato la Taifa (GDP) na pia ni mara tatu ya mapato ya mauzo nchi za nje ya nchi za Kiafrika. Hali duni ya nchi za Kiafrika katika madeni ilianza kutambulika na Jumuiya ya Kimataifa.

10. Katika kutambua hali duni na ugumu wa kutekeleza juhudi za kurekebisha uchumi wa nchi zinazoendelea hasa nchi za Kiafrika zilizo kusini mwa jangwa la Sahara, Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) lilianzisha Mfuko wa Nyongeza wa Kurekebisha Uchumi (Enhanced Structural Adjustment Facility—ESAF) mnamo Desemba 1987. Mfuko huo unaongezea SDR bilioni 6 (dola za Kimarekani bilioni 8·4) kwenye Mfuko wa Kurekebisha Uchumi (Structural Adjustment Facility—SAF) ulioanzishwa mnamo Machi 1986 wenye SDR bilioni 2·7. Katika kutumia Mfuko huo, nchi mwanachama itaweza kukopa hadi asilimia 250 ya hisa yake na masharti yatalingana na yale yatolewayo na SAF, ikiwa pamoja na riba yenye ruzuku (Subsidized interest rate) ya asilimia 0·5 na malipo yatafanywa katika mikupuo 10 ya kila nusu mwaka itakayoanza miaka 5½ baada ya kutolewa fedha. Ili kukopa kutoka mfuko huo, nchi mwanachama inahitajika kuwa na makubaliano na Shirika la Fedha la Kimataifa na Benki ya Dunia kuhusu urekebishaji wa uchumi wake.

11. Mnamo Novemba, 1987 maafikiano yalifikiwa na Wafadhili huko The Hague, Uholanzi, kuupatia Mfuko wa Maendeleo wa Afrika (African Development Fund) Mkupuo wa Tano wa fedha za kiasi cha dola za Kimarekani bilioni 2,700 kwa miaka mitatu (1988—1990). Kiwango hicho cha fedha ni ongezeko la dola za Kimarekani bilioni 1,200 ikilinganishwa na mkupuo wa nne na kililingana na lengo lililowekwa na Uongozi wa Benki ya Afrika. Vile vile, mnamo Februari, 1988, kikundi cha Wataalamu kilichoteuliwa na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kilitoa ripoti yake yenye mapendekezo kuhusu mpango mahsusi uliohitajika kuzisaidia nchi za Kiafrika katika matatizo ya fedha na rasilimali. Mapendekezo hayo yanahusu hasa kupunguza mzigo wa

madeni na kuongezeka kwa misaada. Imekadiriwa katika ripoti hiyo, kwamba nchi za Kiafrika zinahitaji misaada ya kiasi cha dola za Kimarekani bilioni 5 kila mwaka katika miaka mitano ijayo ili kuleta mafanikio katika utekelezaji wa mipango ya kufufua na kurekebisha uchumi wao.

12. Mnamo Februari, 1988, Bodi ya Utendaji ya Benki ya Dunia ilikubaliana na uamuzi wa kuongeza rasilimali ya Benki (capital increase) kwa kiasi cha dola za Kimarekani bilioni 74·8 kutokana hasa na michango na hisa mpya. Ongezeko hilo litaongeza uwezo wa Benki wa kuzisaidia nchi zinazoendelea kwa kuongeza mikopo kwa kiwango cha zaidi ya dola za Kimarekani bilioni 20 kwa mwaka katika miaka ya 1990. Ongezeko hili litakuwa la tatu. Ongezeko la pili lilifanywa mwaka 1980.

**Mfumo Mpya wa Uchumi Duniani (NIEO):**

13. Kikao cha Saba cha Mkutano wa Umoja wa Mataifa kuhusu Biashara na Maendeleo (UNCTAD VII) kilichofanyika Geneva, mnamo Julai, 1987 hakukuleta matumaini ya msukumo mpya katika kutatua matatizo makubwa yanayoukabili uchumi duniani wala ishara thabiti ya kuleta Mfumo Mpya wa Uchumi Duniani. Kikao hicho kiliweza tu kutoa Hatua za Vitendo (Final Act of UNCTAD VII) katika masuala makubwa yanayohusu Misaada na Rasilimali kwa maendeleo, biashara ya bidhaa, biashara ya kimataifa na Matatizo ya nchi masikini sana duniani (LDCs).

14. Awamu Mpya ya majadiliano ya biashara baina ya mataifa (Uruguay Round of Multilateral Trade Negotiations) iliendelea kwa vikao mbali mbali vya kamati zake. Kamati ya Biashara na Maendeleo iliunda kamati ndogo inayohusu masuala ya maslahi ya nchi masikini sana duniani (LDCs) ambayo ilikutana mnamo Februari, 1988. Katika kikao cha kamati ndogo hiyo, nchi masikini sana duniani zilitoa mapendekezo yao ya awali ya kuomba upendeleo wa kufikiriwa ipasavyo (preferential and favourable treatment) katika Awamu Mpya ya Majadiliano ya biashara baina ya nchi wanachama wa Mkataba wa Kimataifa wa Biashara na Ushuru (GATT).

15. Tume Teule ya Ushirikiano wa nchi zinazoendelea (South Commission) chini ya mwenyekiti wake, Mwalimu J. Nyerere ilifanya vikao viwili, kimoja kilifanyika Geneva, Uswisi, mnamo Oktoba, 1987 na kingine, Kuala Lumpur, mnamo Machi, 1988. Vikao hivo viliweza kutafakari malengo na misingi ya kazi ya Tume (objectives and terms of reference). Vile vile, Tume ilitoa uchambuzi wa tatizo la madeni duniani na mkakati unaohitajika kukubaliana na tatizo hili ikiwa pamoja na haja na kuwepo kwa vikao (forum) vya nchi zenye madeni.

**Ushirikiano Kati ya Nchi za Kiafrika, Caribbean na Pacific (ACP) na Nchi za Jumuiya ya Uchumi ya Ulaya (EEC):**

16. Nchi za ACP ziliendelea kutekeleza mipango yao kufuatana na mkataba wa Lome III. Masuala mbali mbali ya ushirikiano baina ya nchi za ACP na EEC yalijadiliwa katika vikao mbali mbali vilivyofanyika. Vikao viwili vya Bunge la Pamoja (ACP/EEC Joint Assembly) vilivyofanyika Lisbon, Portugal, mnamo Septemba, 1987 na kingine kilifanyika Lome, Togo, mnamo Machi, 1988. Kikao cha 43 cha Baraza la Mawaziri wa nchi za ACP kilifanyika Brussels, Ubelgiji, na kujadili bajeti ya Sekretariati ya ACP kwa mwaka 1988. Mwishoni mwa mwaka 1987 EEC ilitoa ECU milioni 100 kuzisaidia nchi za Kiafrika masikini sana na zenye madeni katika kuimarisha na kurekebisha uchumi wao. Kikao cha Mawaziri wa ACP na EEC kilifanyika mnamo Mei 1988 kujadili utekelezaji wa Lome III na matayarisho ya mkataba mpya utakaobadili Lome III. Tanzania imeanza kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mikataba yote ya Lome katika mipango yake kitaifa.

**Ushirikiano wa Kiuchumi Baina ya Nchi Zinazoendelea (ECDC) na Ushirikiano wa Kiufundi Baina ya Nchi Zinazoendelea (TCDC):**

17. Juhudi za kukuza ushirikiano wa kiuchumi baina ya nchi zinazoendelea (Economic Co-operation among Developing Countries—ECDC) ziliendelea ingawaje bila kuwa na msukumo mkubwa. Mkutano wa sita wa kamati ya ufuatiliaji na utaratibu wa ECDC (Intergovernmental Follow-up Co-ordination and Committee—IFCC VI) ulifanyika mnamo Septemba 1987 huko Havana, Cuba. Mkutano huo ulitafakari na kujadili maendeleo ya ushirikiano katika sekta mbali mbali za uchumi; Mfuko wa Perez-Guerrero kusaidia ECDC na TCDC (Perez—Guerrero Trust Fund for Economic and Technical Cooperation among Developing Countries); na Mbinu za uimarishaji na uainishaji wa utaratibu na ufuatiliaji wa shughuli za ECDC na TCDC. Mnamo Machi 1988, Mawaziri wa Nchi zinazoendelea walitia saini uanzishaji wa Mkataba wa Mfumo wa biashara baina ya nchi zinazoendelea (GSTP) katika mkutano uliofanyika Belgrade, Yugoslavia.

18. Katika kuleta msukumo mpya katika kuendeleza ushirikiano wa kiufundi baina ya nchi zinazoendelea (Technical Co-operation among Developing Countries—TCDC) Peru ilifanya mkutano wake pamoja na nchi kadhaa zinazoendelea zilizoalikwa ikiwa pamoja na Tanzania huko Lima mnamo Oktoba, 1987. Madhumuni ya mkutano huo ilikuwa kubadilishana uwezo na mahitaji baina ya nchi zilizoshiriki (Programming Exercise).

**Tume ya Uchumi ya Bara la Afrika (ECA) na Hali ya Uchumi wa Bara la Afrika:**

19. Hatua za kutekeleza Mpango Maalumu wa Utekelezaji wa Umoja wa Mataifa juu ya Ufufuaji na Maendeleo ya Uchumi wa Afrika (United Nations Programme of Action for African Recovery and Development (UN-PAAERD) (1986—1990) ziliendelea kuchukuliwa na nchi mbali mbali kwa viwango tofauti. Kwa mfano, baadhi ya malengo ya mpango huo uliopitishwa na kikao maalum cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa mnamo Julai 1986 yamefikiwa kama ifuatavyo—nchi 28 za Afrika zimekwishachukua hatua madhubuti za kurekebisha hali ya uchumi na usimamizi katika vyombo vinavyohusika; 2/3 ya nchi za Afrika zimekwisha fikisha lengo la kuongeza rasilimali katika kilimo kwa asilimia 25; zaidi ya 4/5 ya nchi za Kiafrika zimekwisha anzisha mpango maalum wa kutoa motisha (incentive prices) kwa wakulima na kiasi cha 2/3 ya nchi za Afrika zimeanza mikakati mipya ya usambazaji bidhaa na kupunguza ruzuku (subsidies). Tatizo kubwa na la msingi katika utekelezaji wa mpango huu ni upungufu wa fedha za kigeni kutokana na sababu kubwa tatu:—Kwanza kuendelea kushuka kwa kiasi kikubwa kwa bei ya bidhaa za kilimo (commodities), pili kiwango kidogo cha misaada kutoka nje kwa ajili ya kusaidia mpango huu ikilinganishwa na kiasi kinachohitajika, na mwisho, ongezeko kubwa na sugu la malipo ya madeni ya nje ambalo huchukua sehemu kubwa ya mapato ya fedha za kigeni.

20. Ili kufuatilia kikamilifu utekelezaji wa mpango huo, Tume ya Uchumi ya Bara la Afrika sasa inaendelea na maandalizi ya kutathmini utekelezaji wake kwa nusu ya kwanza ya kipindi cha utekelezaji. Hatua zingine za ufuatiliaji wa utekelezaji zilizokwisha chukuliwa ni pamoja na kufanyika kwa mkutano wa kimataifa juu ya changa moto ya Ufufuaji na kuongeza kasi ya Maendeleo ya Uchumi wa Bara la Afrika (International Conference: The Challenge of African Economic Recovery and Accelerated Development) uliofanyika Abuja, Nigeria, mnamo Juni 1987 na mkutano wa Kimataifa juu ya Binadamu kama rasilimali muhimu na lengo la Ufufuaji na Maendeleo ya Uchumi wa Bara la Afrika (International Conference on Human Aimension of Africa Economic Recovery and Development) uliofanyika Khartoum, Sudan, mnamo Machi, 1988.

21. Ongezeko la Uchumi wa Afrika mwaka 1987 lilikuwa hafifu tena. Pato la Taifa (GDP) la nchi za Bara la Afrika kwa pamoja liliongezeka kidogo tu kiasi cha asilimia 0·8 ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 0·5 mwaka 1986. Kwa upande mwingine ongezeko la pato la nchi zisizouza mafuta nje lilikuwa asilimia 1·6 ikilinganishwa na ongezeko kubwa la asilimia 3·7 mwaka 1986, lililozidi ongezeko la idadi ya watu na la kwanza la aina yake katika kipindi cha miaka kumi. Ufanisi wa

mwaka 1986 ulitokana na hali nzuri ya hewa iliyoambatana na sera bora za kusaidia kilimo. Kuwepo kwa hali ya ukame katika baadhi ya nchi pamoja na kushuka bei ya bidhaa za kilimo hasa kahawa kulisababisha Pato la Taifa kushuka mwaka 1987. Pato la nchi zinazotoa mafuta liliongezeka kwa asilimia ndogo 0·3 ikilinganishwa na kushuka kwa pato kwa kiasi cha asilimia 1·2 mwaka 1986. Ongezeko hili duni lilitokana hasa na kuendelea kushuka kwa bei ya mafuta na upunguzaji wa uzalishaji mafuta uliokuwa unapendekezwa na OPEC.

**Ushirikiano wa Kiuchumi Baina ya Nchi Zilizo Kusini mwa Bara la Afrika (SADCC):**

22. Nchi za ushirikiano wa kiuchumi zilizoko kusini mwa Bara la Afrika (SADCC) ziliendelea vizuri katika kuimarisha na kuendeleza ushirikiano katika nyanja mbali mbali za uchumi. Mikutano na vikao vya taasisi na vyombo mbali mbali vya SADCC ilifanyika ili kuleta msukumo zaidi. Mkutano wa kila mwaka wa nchi za SADCC na Wafadhili ulifanyika Arusha, mnamo Februari, 1988. Majadiliano na ahadi za misaada katika mkutano huo vililenga kwenye maendeleo ya huduma za kiuchumi na shughuli za biashara na uzalishaji (Development of Infrastructure and Enterprise). Hivyo, wafadhili walitoa ahadi za kusaidia miradi na programu za sekta hizo kama vile mabarabara, reli, bandari na vyombo vya usafiri.

**Soko Nafuu la Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika (PTA):**

23. Mkataba wa Soko la nafuu la Nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika uliendelea kutekelezwa katika nyanja zake zote. Kwa kuzingatia uzito wa tatizo la ukatili na unyama wa Makaburu wa Afrika Kusini, kwa wananchi wake walio wengi na athari kwa nchi zinazopakana na nchi hiyo, mkutano maalum wa Mawaziri wa nchi za PTA ulifanyika mnamo Aprili, 1988 huko Kampala, Uganda. Mkutano huo ulijadili na kupendekeza hatua kadhaa za kuutenga utawala wa Makaburu na kuzisaidia nchi zinazopakana na Afrika Kusini ili kukabili vikwazo vya kiuchumi vitakavyotokea katika kuutokomeza utawala huo hasa katika nyanja za biashara na fedha, mawasiliano, usafirishaji na nishati.

**Tume za Ushirikiano kati ya Tanzania na Nchi Rafiki pamoja na Mashirika ya Kimataifa (Joint Commissions):**

24. Katika mwaka wa 1987, Tanzania imeendelea kudumisha na ushirikiano wa Tume za pamoja. Juhudi katika kuimarisha na kustawisha maendeleo ya biashara, kilimo, usafirishaji, viwanda na nishati zimeendelea. Hata hivyo, vikwazo mbali mbali vimeendelea kuathiri mafanikio ya Tume hizi. Kitu kilichojitokeza zaidi katika mwaka 1987 ni tatizo la kutoweza kutimiza makubaliano hasa kwa upande wa Tanzania kutokana na hali duni ya biashara yetu. Juhudi zinafanywa

kuweza kuzishirikisha nchi rafiki katika uzalishaji mazao zaidi kusudi ziada iweze kutumika katika biasbara. Pia ufumbuzi unatafutwa wa kuweza kuimarisha na kufufua miradi iliyoko katika Tume ya pamoja. Hata hivyo tatizo kubwa bado ni uhaba wa vipuri na malighafi. Kwa jumla, nia ya ushirikiano ipo na maeneo ya usbirkiano yapo ila hali ngumu ya uchumi bado inakwamisha utekelezaji.

**Ushirikiano wa Nchi za Afrika Masharki:**

25. Ingawaje hapakuwepo na Kikao cha Tume ya pamoja ya Ushirikiano wa Nchi Tatu (Tripartite Joint Commission of Co-operation) ambacho kingechambua na kupendekeza maendeleo ya ushirikiano katika nyanja mbali mbali, kulikuwepo na vikao vya Wataalamu vilivyotayarisha mikakati mbali mbali ya kukuza na kuimarisha ushirikiano katika sekta ya mawasiliano na uchukuzi na uendelezaji wa utafiti wa kisayansi.

# SURA YA III

# MAENDELEO KATIKA SEKTA MBALI MBALI

## 1.—KILIMO NA MIFUGO

Hali ya uzalishaji katika sekta ya kilimo kwa kipindi cha mwaka 1987/88 iliendelea kuwa nzuri hasa kutokana na hali nzuri ya bewa pamoja na:

(a) Kuendelea kuongezeka kwa rasilimali inayotengwa kwa ajili ya sekta hii ambayo kwa upande wa serikali, rasilimali inayotengwa ni sawa na karibu asilimia 30 ikilinganishwa na asilimia 11 iliyokuwa ikitengwa mwaka 1982/83.

(b) Upangaji wa bei kila mwaka na utangazaji wake kabla ya msimu. Mwenendo wa bei kwa nafaka muhimu umekuwa kama ifuatavyo:—

| | 1985/86 | 1986/87 | 1987/88 |
|---|---|---|---|
| (i) Mahindi Sh./Kg. ............... | 5·80 | 6·30 | 8·20 |
| (ii) Mpunga Sh./Kg. ............... | 8·30 | 9·50 | 14·40 |
| (iii) Ngano Sh./Kg. .................. | 6·60 | 7·30 | 9·00 |
| (iv) Maharage Sh./Kg. ............. | 13·20 | 14·40 | 26·60 |
| (v) Sorghum Sh./Kg. ............... | 4·40 | 4·80 | 6·[illegible] |

(c) Uongezekaji wa bidhaa muhimu hadi vijijini.

(d) Matumizi yanayoongezeka ya pembejeo inayopatikana hasa mbolea, ingawa bado matatizo ya usambazaji.

(e) Uanzishaji upya wa Vyama vya Ushirika ambao umesaidia kurahisisha usambazaji wa pembejeo na ununuzi wa mazao vijijini ingawa nao kwa upande mwingine umekabiliwa na matatizo ya maghala, usafirishaji na fedha za kununulia mazao.

**Mazao ya Chakula:**

2. Kwa ujumla hali ya uzalishaji wa mazao ya chakula kwa msimu wa mwaka 1987/88 inategemewa kuwa nzuri kama ile ya mwaka 1986/87. Uzalishaji wa mahindi umeongezeka kutoka tani 2·7 milioni mwaka 1986/87 hadi tani 2·8 milioni, mpunga kutoka tani 567,589 hadi tani 567,600 na ngano kutoka tani 56,0[illegible] hadi tani 58,000. Kama inavyoonyeshwa katika Jedwali lifuatalo jumla ya ununuzi wa mazao ya chakula uliofanywa na Shirika la Taifa la Usagishaji kwa mwaka 1987/88 ulikuwa tani 357,450 ikilinganishwa na tani 254,518 zilizonunuliwa mwaka 1986/87 sawa na ongezeko la asilimia 40·4. Mazao yote yanaonyesha ongezeko kubwa isipokuwa kwa ununuzi wa mtama ambao ulipungua kwa asilimia 3·5. Kwa jumla ununuzi kwa mwaka 1987/88 umefikia asilimia 91·6 ya lengo la tani 390,100.

## UNUNUZI WA MAZAO YA CHAKULA ULIOFANYWA NA SHIRIKA LA TAIFA LA USAGISHAJI

| Zao | 1986/87 | 1987/88 | Asilimia Ongezeko | Lengo 1987/88 |
|---|---|---|---|---|
| Mahindi ..................... | 167,793 | 218,208 | 30·1 | 237,682 |
| Mpunga ..................... | 9,750 | 38,851 | 98·5 | 31,851 |
| Ngano ..................... | 33,672 | 42,759 | 26·9 | 47,810 |
| Uwele ..................... | 6,056 | 5,845 | −3·5 | 18,063 |
| Muhogo ..................... | 11,857 | 18,577 | 56·7 | 15,529 |
| Maharage ..................... | 25,390 | 33,127 | 30·5 | 39,175 |
| Jumla ... | 254,518 | 357,450 | 40·4 | 390,110 |

*Chanzo:* Wizara ya Kilimo na Maendeleo ya Mifugo.

**Sukari:**

3. Uzalishaji wa sukari kwa mwaka 1987/88 ulikuwa mzuri zaidi ikilinganishwa na mwaka 1986/87. Jumla ya tani 103,530 za sukari zilizalishwa ikiwa ni ongezeko la asilimia 9·2. Tatizo kubwa lilikuwa hasa kwa kiwanda cha Kagera ambacho kilizalisha tani 943 tu sawa na asilimia 2 ya uwezo wake. Matatizo mengine yalikuwa ni pamoja na uhaba wa fedha za kutosheleza mahitaji ya viwanda ya ukarabati, ununuzi wa spea na magari ya kusombea miwa.

**Mazao ya Biashara:**

4. Katika kipindi cha 1987/88, ununuzi wa mazao ya biashara kwa ujumla uliendelea vizuri, hasa kwa mazao ya pamba, katani na korosho. Ununuzi wa mazao ya chai na pareto ulikuwa na ongezeko dogo na ununuzi wa mazao ya kahawa na tumbaku ulipungua kidogo ikilinganishwa na msimu uliopita wa mwaka 1986/87.

**Korosho:**

5. Ununuzi wa zao la korosho katika msimu wa 1987/88 umeongezeka na kufikia tani 25,000 ikilinganishwa na tani 16,548 zilizonunuliwa mwaka 1986/87. Pamoja na ongezeko hilo, uzalishaji wa korosho unakabiliwa na matatizo ya magonjwa, uzee wa miti ya mikorosho pamoja na uhaba wa vifaa vya usafirishaji.

**Mkonge:**

6. Uzalishaji wa mkonge umeongezeka katika kipindi cha mwaka 1987/88 na kufikia tani 33,170 ikilinganishwa na tani 30,151 zilizozalishwa mwaka 1986/87. Ongezeko hili linatokana na kuzingatia kanuni za ukuzaji na utunzaji bora wa mkonge, kuongezeka kwa uwezo wa

usafirishaji, ukarabati wa vifaa vya mashambani na viwandani pamoja na kuendeleza juhudi za upandaji wa marudio (replanting). Hata hivyo uzalishaji wa mkonge uliendelea kukabiliwa na uchakavu wa mitambo pamoja na uhaba wa wakataji.

**Kahawa:**

7. Katika kipindi cha mwaka 1987/88 ununuzi wa kahawa umeendelea vizuri. Hadi kufikia Machi 1988, kiasi cha tani 50,000 zimenunuliwa ikilinganishwa na tani 42,000 zilizonunuliwa mwaka 1986/87. Hata hivyo uzalishaji wa kahawa unakabiliwa na matatizo ya magonjwa (CBD) pamoja na uhaba wa pembejeo basa madawa na vifaa vya usafirishaji. Jitihada zinafanywa ili kuhakikisha pembejeo zinapatikana kwa wakati unaofaa, pamoja na kuongeza vifaa vya usafirishaji na kutengeneza barabara.

**Pamba:**

8. Katika mwaka 1987/88, Bodi ya Pamba iliendelea na majukumu ya kusimamia na kuratibu uuzaji wa nyuzi za pamba hapa nchini na ng'ambo, ununuzi wa pamba (lint) kutoka kwa wachambuaji (ginners) ambao ni Vyama vya Ushirika vya mikoa. Aidha Bodi ilihusika kikamilifu katika kuishauri serikali katika masuala ya uzalishaji na uuzaji pamba.

9. Uzalishaji pamba katika mwaka 1987/88 kama ulivyokuwa katika mwaka 1986/87 umeendelea kuwa wenye mafanikio makubwa. Hadi kufikia Machi 1988 jumla ya marobota 450,000 yalikwishanunuliwa na inakisiwa kuwa marobota 470,000 yatanunuliwa hadi Juni. Hili ni ongezeko la asilimia 17·5 ikilinganishwa na marobota 400,000 yaliyozalishwa mwaka 1986/87. Mafanikio haya ya uzalishaji wa pamba yametokana na sababu nyingi, ikiwa ni pamoja na hali nzuri ya hewa, bei nzuri ya pamba kwa mkulima na upatikanaji wa bidhaa muhimu na za motisha kwa wakulima.

10. Pamoja na mafanikio haya kilimo cha pamba kimeendelea kuathiriwa na uhaba wa maghala ya kuhifadhia pamba, uhaba wa vyombo vya kusafirishia pamba (malori na mabehewa ya treni) pamoja na uwezo mdogo wa vinu vya kuchambulia pamba (ginneries) kutokana na uzee na ukosefu wa vipuri.

**Tumbaku:**

11. Ununuzi wa tumbaku katika msimu wa mwaka 1987/88 ulipungua kutoka tani 16,465 za mwaka 1986/87 hadi kufikia tani 12,921. Huu ni upungufu wa tani 3,544 sawa na asilimia 21·5. Kushuka kwa uzalishaji wa tumbaku kumesababishwa hasa na ukosefu wa pembejeo kama mbolea, ukosefu wa huduma kwa wakulima (extension services), ukosefu wa mabani na majengo ya kugredi tumbaku na uhaba wa miti ya kukaushia tumbaku.

**Pareto:**

12. Ununuzi wa maua ya pareto kwa mwaka 1987/88 umeongezeka hadi kufikia tani 1,300 (Machi) kutoka tani 1,231 ambazo zilinunuliwa mwaka 1986/87. Hili ni ongezeko la tani 69 sawa na asilimia 5·3. Hata hivyo ongezeko hili ni dogo ikilinganishwa na tani 1,600 zilizonunuliwa mwaka 1985/86. Ongezeko la ununuzi wa maua ya pareto katika mwaka 1987/88 limetokana na kuongezeka kwa uzalishaji katika maeneo mapya katika mikoa ya Iringa na Mbeya. Aidha, ugumu wa uuzaji wa mahindi, bei nzuri ya pareto, kutekelezwa kwa sheria ndogo ndogo (by laws) katika wilaya mbali mbali na kadhalika kwa vituo vya kuhudumia wakulima wa pareto nako kumechangia katika ongezeko hili. Hata hivyo pamoja na juhudi nyingi uhaba wa mbegu na miche ya pareto umeendelea kuwa kikwazo cha uendelezaji wa zao hili japokuwa juhudi za kuzalisha miche zaidi zimeendelea.

**Chai:**

13. Utengenezaji wa chai katika mwaka 1987/88 ulikuwa na ongezeko dogo sana kwani hadi Machi 1988 ni tani 13,400 za chai ndizo zilikwishatengenezwa ikilinganishwa na tani 13,397 zilizotengenezwa mwaka 1986/87. Sababu za mwenendo huu ni pamoja na uhaba wa vyombo vya usafiri hasa kwa wakulima wadogo, ubovu wa barabara katika mashamba ya chai, uhaba wa wachumaji chai hasa katika mashamba makubwa ya watu binafsi na ya Mamlaka ya Chai na uchakavu wa viwanda vya kusindika majani mabichi ya chai. Juhudi za kutatua matatizo haya ikiwa ni pamoja na kutekeleza mradi wa kuimarisha kilimo cha wakulima wadogo "The Small Holder Tea Consolidation Project" na kuinua hali ya maisha ya wachumaji chai zimeendelea.

**Zana na Pembejeo:**

14. **Mbolea:** Makadirio ya mahitaji ya mbolea kwa msimu wa mwaka 1987/88 yalikuwa ni tani 180,000. Kiasi halisi kilichotegemewa kupatikana kilikuwa tani 200,000; kati ya hizo tani 25,000 zilitarajiwa kuzalishwa nchini na tani 125,000 zilitarajiwa kupatikana kutoka nchi za nje kwa njia ya msaada. Kiasi cha tani 50,000 ni bakaa ya mwaka 1986/87. Upatikanaji halisi ulikuwa tani 164,392 sawa na asilimia 94 ya mahitaji. Hata hivyo usambazaji wake bado ulikuwa na matatizo hasa ya usafirishaji na ukosefu wa maghala. Kwa jumla matumizi ya mbolea nchini bado ni madogo ambapo matumizi ni wastani wa kilo 8·4 kwa hekta ikilinganishwa na wastani wa kilo 12 kwa Bara la Afrika.

**Mbegu Bora:**

15. Matumizi ya mbegu bora nchini nayo bado ni madogo sana na ni kiasi cha asilimia 10 tu ya eneo lote linalolimwa mazao ya chakula kupandwa mbegu bora. Katika msimu wa mwaka 1987/88, mahitaji ya mbegu bora yalikadiriwa kuwa ni tani 11,000; upatikanaji ulitegemewa

kuwa tani 9,000 ikiwa ni pamoja na bakaa kutokana na msimu wa mwaka 1986/87. Kiasi cha tani 2,000 kilitarajiwa kuagizwa kutoka nje. Upatikanaji halisi ulikuwa ni tani 7,430 sawa na asilimia 67·5 ya makadirio ya mahitaji.

**Zana za Kilimo:**

16. Matumizi ya zana bora na mashine za kilimo ni njia mojawapo ya kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo. Hata hivyo upatikanaji wake unategemea sana fedha za kigeni kwa ajili ya kununua zana zenyewe au malighafi za kutengeneza zana hizo nchini. Upatikanaji wa matrekta kwa mwaka 1987/88 unatarajiwa kufikia matrekta 428 tu ikilinganishwa na makadirio ya mahitaji ya trekta 1,800; majembe ya mkono 417,800 ikilinganisbwa na mahitaji ya majembe 2,500,000 upatikanaji wa plau, ndimi na minyororo ulifikia wastani wa asilimia 33·3 ya makadirio ya mahitaji.

MAHITAJI NA UPATIKANAJI WA ZANA NA PEMBEJEO MSIMU WA MWAKA 1987/88

| Pembejeo/Zana | Mahitaji | Upatikanaji hadi 15/2/1988 |
|---|---|---|
| Mbolea tani '000' | 180 | 164·4 |
| Mbegu bora tani | 11,000 | 7,430 |
| Madawa ya Wadudu Lita '000' | 3,554 | 2,116 |
| Tani | 714 | 9,002 |
| Madawa ya Magonjwa Lita '000' | 258 | — |
| Tani | 6,209 | 5·0 |
| Madawa ya Magugu Lita '000' | 1,380 | 266 |
| Tani | 252 | 32 |
| Matrekta | 1,800 | 428 |
| Majembe ya Mkono '000' | 2,500 | 418 |
| Plau '000' | 40 | 11 |
| Ndimi za Plau '000' | 400 | 105 |
| Minyororo | 400 | 22 |
| Mashoka '000' | 300 | 54 |
| Mapanga '000' | 1,200 | 118 |
| Tupa '000' | 240 | 144 |
| Magunia (Jute) '000' | 17,700 | 14,354 |
| Magunia (Sisal) '000' | 5,500 | 3,459 |
| Polysacks '000' | 6,000 | 4,000 |

*Chanzo:* Wizara ya Kilimo na Maendeleo ya Mifugo.

## MIFUGO

17. Idadi ya mifugo ya asili hapa nchini iliendelea kuchukua nafasi kubwa zaidi ikilinganishwa na mifugo ya kisasa. Mifugo hii ilichukukua karibu asilimia 98 ya mifugo yote. Vile vile hali na mbinu za ufugaji bazi kubadilika sana na hivyo kufanya uzalishaji wa mazao mbali mbali ya mifugo kutobadilika sana ikilinganishwa na uzalishaji wa mwaka 1986.

**Uzalishaji:**

18. Mwenendo wa uzalishaji wa mazao mbali mbali ya mifugo (nyama, maziwa, mayai, ngozi n.k.) ulionyesha sura ifuatayo:—

Uzalishaji wa nyama ya ng'ombe ulishuka kwa asilimia 21·5, kutoka tani 135,000 mwaka 1986 kufikia tani 106,000 mwaka 1987. Hali hii ilitokana na ongezeko dogo la ng'ombe karibu asilimia 0·8 kulingana na sensa ya 1984 na kwamba vuno la mifugo hii ilikuwa chini pia. Ulaji wa nyama kwa ujumla ulishuka kufikia wastani wa kilo 5·9 kwa mtu kwa mwaka. Uzalishaji wa maziwa kutokana na ng'ombe wa asili ulishuka kidogo kutoka lita 357 milioni mwaka 1986 kufikia 352 milioni mwaka 1987. Kwa upande mwingine sekta ya ng'ombe wa kisasa iliongeza uzalishaji maziwa kutoka lita 113 milioni mwaka 1986, kufikia lita 120 milioni mwaka 1987 sawa na ongezeko la asilimia 6·2. Kwa jumla uzalishaji wa maziwa kwa makundi yote mawili (asili na la kisasa) uliongezeka kidogo kutoka lita 470 milioni mwaka 1986 hadi kufikia 472 milioni mwaka 1987 sawa na ongezeko la asilimia 1·2. Hata hivyo ulaji wa maziwa kwa kila mtu ulishuka kutoka lita 21·5 mwaka 1986 kufikia 20·8 mwaka 1987. Hali hii ilisababishwa pamoja na mambo mengine na ongezeko la watu la asilimia 3·3 kila mwaka.

19. Kulikuwa na ongezeko kidogo la uzalishaji mayai. Kiasi cha mayai 318·0 milioni yalizalishwa mwaka 1987 ikilinganishwa na mayai 304·2 milioni mwaka 1986 sawa na ongezeko la asilimia 4·5. Hii ni sawa na wastani wa mayai 14·1 kwa kila mtu kwa mwaka. Kwa upande mwingine uzalishaji wa nyama ya kuku ulishuka kidogo kutoka tani 21,640 mwaka 1986 kufikia 21,000 mwaka 1987.

20. Kwa upande wa ukusanyaji ngozi, idadi ya ngozi za ng'ombe iliongezeka kutoka 405,755 mwaka 1986 kufikia 574,000 mwaka 1987, mbuzi kutoka ngozi 218,391 mwaka 1986 kufikia 326,000 mwaka 1987 na kondoo kutoka ngozi 85,467 mwaka 1986 hadi kufikia 116,600 mwaka 1987. Ongezeko hili la ngozi lilisababishwa na mbinu bora zilizotumiwa katika kukusanya zao bili, bei nzuri waliyopata wafugaji na wauzaji nchi za nje.

21. Mauzo ya ngozi (ng'ombe, mbuzi na kondoo) nchi za nje yaliongezeka kutoka jumla ya ngozi 371,221 mwaka 1986 hadi kufikia 880,040 mwaka 1987 sawa na ongezeko la asilimia 137·06. Mauzo ya ngozi hizi katika fedha za kigeni yaliongezeka kutoka Sh. 46,859 milioni mwaka

1986 hadi kufikia Sh. 161·3 milioni mwaka 1987. Ongezeko kubwa kama hili lilisababishwa na usafirishaji wa ngozi nyingi pamoja na bei nzuri za ngozi. Karibu ngozi zote za mbuzi na kondoo zilizokusanywa hapa nchini ziliuzwa nje.

22. Kuhusu utengenezaji vyakula vya mifugo, kiwango cha tani 75,000 kilifikiwa mwaka 1987 ikilinganishwa na tani 35,000 zilizotengenezwa mwaka 1986. Kiwango hiki kilifikiwa kutokana na viwanda vingi vya watu binafsi kujihusisha kikamilifu na utengenezaji wa vyakula vya mifugo viliagizwa kutoka nje.

23. Kuhusu maendeleo ya uzalishaji kwa chupa (uhamilishaji) kiasi cha ng'ombe 15,000 walihamilishwa mwaka 1987 ikilinganishwa na ng'ombe 12,000 mwaka 1986. Shughuli hii ilizingatia zaidi uzalishaji wa ng'ombe wa maziwa.

24. Uzalishaji wa mitamba chotara wa maziwa uliendelea kufanyika katika vituo (LMUs) 18. Kiasi cha mitamba chotara 1,200 ilizalishwa 1987 ikilinganishwa na mitamba chotara 518 iliyozalishwa 1986. Ongezeko hili kubwa lilitokana na kuimarisha baadhi ya mashamba haya hasa Mabuki, Sao Hill, Mivumoni na kuongeza huduma muhimu katika mashamba yaliyobaki.

25. Kuhusu huduma za afya kwa mifugo, kampeni ya kuzuia sotoka iliendelea. Kiasi cha ng'ombe 8·8 milioni walidungwa sindano kuwakinga na ugonjwa wa sotoka. Vile vile shughuli za kupambana na ugonjwa wa ndorobo (nagana), kupe pamoja na magonjwa mengine ziliendelea.

**Kampuni ya Ranchi za Taifa (NAPCO):**

26. Idadi ya ng'ombe katika kampuni hii ilianza kuongezeka kidogo kutoka ng'ombe 81,611 mwaka 1986 kufikia ng'ombe 82,563 mwaka 1987 sawa na ongezeko la asilimia 1·2. Ongezeko hili lilisababishwa na kuimarisha huduma muhimu katika huria hizi kama vile maji, malisho, matunzo bora na usafiri. Vile vile kiasi cha ng'ombe 14,559 waliuzwa au kuchinjwa mwaka 1987 ikilinganishwa na ng'ombe 11,424 waliouzwa au kuchinjwa mwaka 1986.

**Kampuni ya ng'ombe wa maziwa (DAFCO):**

| 331 | Mbao, Bidhaa za Mbao | 63 | 60 | 60 | 285 | 316 | 375 | 210 | 216 | 261 | 75 | 100 | 114 | 21 | 23 | [illegible] |
| 332 | Fanicha za Mbao | 57 | 55 | 55 | 147 | 173 | 205 | 110 | 122 | 148 | 37 | 51 | 57 | 4 | 5 | [illegible] |
| 341.2 | Karatasi, Uchapishaji | 56 | 52 | 52 | 882 | 1,167 | 1,385 | 543 | 821 | 993 | 339 | 346 | 392 | 80 | 49 | [illegible] |
| 351.2.3 | Usafishaji Mafuta, Chemicals | 43 | 46 | 46 | 1,969 | 2,133 | 2,532 | 1,398 | 1,588 | 1,921 | 71 | 545 | 611 | 76 | 82 | [illegible] |
| 355 | Bidhaa za mpira | 6 | 8 | 8 | 354 | 674 | 800 | 262 | 476 | 576 | 92 | 198 | 224 | 8 | 9 | [illegible] |
| 356 | Bidhaa za Plastic | 5 | 5 | 5 | 123 | 129 | 153 | 7 | 98 | 119 | 46 | 31 | 34 | 8 | 13 | [illegible] |
| 361.2.9 | Bidhaa za madini yasiyo chuma | 12 | 14 | 14 | 806 | 1,056 | 1,253 | 733 | 981 | 1,187 | 73 | 75 | 66 | 123 | 118 | [illegible] |
| 371.72.81 | Chuma na bidhaa zake | 45 | 49 | 49 | 1,983 | 1,974 | 2,343 | 1,595 | 1,522 | 1,842 | 388 | 452 | 501 | 85 | 46 | [illegible] |
| 382.3 | Utengenezaji Mitambo | 21 | 23 | 23 | 575 | 702 | 833 | 412 | 531 | 642 | 163 | 171 | 191 | 32 | 36 | [illegible] |
| 384 | Vyombo vya Usafiri | 16 | 20 | 20 | 619 | 1,293 | 1,535 | 640 | 965 | 1,166 | 179 | 328 | 367 | 8 | 20 | [illegible] |
| 385.390 | Mengineyo | 12 | 14 | 14 | 129 | 144 | 171 | 107 | 116 | 140 | 22 | 28 | 31 | 1 | 3 | [illegible] |
| | Jumla | 657 | 665 | 665 | 16,944 | 20,141 | 23,870 | 12,527 | 15,174 | 18,339 | 4,417 | 4,967 | 5,531 | 899 | 976 | [illegible] |

Chanzo: Idara ya Takwimu
Takwimu za mwaka 1986 ni za muda.

## 5. BIASHARA YA NDANI NA UTALII

**Biashara ya Ndani:**

1. Biashara ya ndani iliendelea kuimarishwa chini ya vyombo vya umma katika kipindi cha 1987. Biashara muhimu ya jumla ilifanywa na makampuni ya biashara ya Taifa na Mikoa. Hatua kadhaa zilizochukuliwa na Serikali za kulegeza masharti ya biashara kuwaruhusu watu binafsi kuingiza bidhaa kadhaa nchini kwa kutumia fedha zao za kigeni ziliendelea kutekelezwa. Bidhaa za aina nyingi zinapatikana ingawa bei zake ni za juu.

2. Thamani ya bidhaa mbali mbali zilizouzwa na makampuni ya Biashara ya Taifa (NTC) na ya Mikoa (RTC) katika mwaka 1987 ilifikia Sh. 10,641 milioni kulinganishwa na Sh. 9,139·33 milioni zilizofikiwa mwaka 1986. Kati ya fedha hizo Sh. 3,252 milioni zilitokana na mauzo ya kampuni za Biashara za Taifa na Sh. 7,389 milioni zilitokana na mauzo ya kampuni za Biashara ya Mikoa. Faida baada ya kodi kwa mauzo haya ilikuwa Sh. 150 milioni kwa NTC's na Sh. 101·0 milioni kwa RTC's. Hata hivyo mauzo halisi yaliyofikiwa yalikuwa ya chini sana kuliko yalivyokadiriwa. Hali hii ilitokana na uzalishaji mdogo wa uagizaji bidhaa kutokana na matatizo ya fedha za kigeni. Biashara ya ndani inatarajiwa kuonyesha mwelekeo wa kuridhisha hasa baada ya Serikali kuchukua hatua za kurekebisha uchumi (ERP).

**Utalii:**

3. Kulikuwa na maendeleo mazuri ya kukua kwa sekta hii katika kipindi cha 1987 ukilinganisha na miaka ya nyuma. Sababu kubwa ni kutokana na ufumbuzi wa mpaka baina yetu na Kenya, kupungua kwa gharama za huduma kwa watalii katika mahoteli na sehemu za vivutio. Kwa mfano, bei za vyakula zimepunguzwa ukilinganisha na viwango vinavyotozwa mahali pengine duniani. Kutokana na hali hiyo, idadi ya watalii iliongezeka kutoka 67,000 mwaka 1986 hadi 94,000 mwaka 1987, sawa na ongezeko la asilimia 40. Lakini hakukuwa na ongezeko kubwa katika siku za kulala wageni ambazo ziliongezeka kwa asilimia 10·3 au kutoka siku 426000 mwaka 1986 hadi 470,000 mwaka 1987. Kati ya jumla ya siku 1,477,000 za kulala, 1,007,000 zilikuwa za Watanzania ambapo mwaka 1986 idadi ilikuwa siku 105,000 tu. Safari za wageni katika mbuga za wanyama ziliongezeka kutoka 62,000 mwaka 1986 hadi 87,000 mwaka 1987, ikiwa ni ongezeko la asilimia 40. Safari za malipo ziliongezeka kwa kiasi cha asilimia 22·48 au kutoka safari 138,556 mwaka 1986 hadi 169,710 mwaka 1987.

4. Ongezeko la watalii liliambatana na ongezeko la hoteli ambazo ziliongezeka kutoka 165 mwaka 1986 hadi 174 mwaka 1987 lakini vyumba vya kulala vilipungua kutoka 5,264 hadi 5,141 mwaka 1987.

5. Kwa upande wa miradi ya maendeleo, uimarishaji wa Chuo cha Mafunzo ya Hoteli na Utalii ulifanyika kwa kununua majiko, kufunga mabomba ya maji katika jengo la chuo, kupaka rangi majengo na ujenzi wa jengo la kufulia nguo. Ujenzi wa awamu ya tatu ya hoteli ya New-Africa ulisimama kutokana na mvutano baina ya kondrata na Shirika la Utalii.

## IDADI YA WATALII, SIKU ZAO HOTELINI, NA MAKADIRIO YA FEDHA ZA KIGENI ZILIZOPATIKANA

Jedwali Na. 55 (000)

| Maelezo | 1981 | 1982 | 1983 | 1984 | 1985 | 1986 | 1987 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Watalii ............ | 83 | 70 | 52 | +64 | +63 | +67 | +94 |
| Siku hotelini, Jumla ........ | 1,182 | 1,226 | 1,240 | 1,362 | 1,410 | 1,477 | 1,477 |
| Watanzania .................. | 645 | 768 | 840 | 964 | 998 | 1,051 | 1,007 |
| Wageni ...................... | 537 | 458 | 400 | 398 | 412 | 426 | 470 |
| Safari za Wageni katika Mbunga za Wanyama ... | 48 | 55 | 48 | 59 | 58 | 62 | 87 |
| Mapato, Fedha za Kigeni (Sh. Mil.) .......... | 180·2 | 122·9 | 159·6 | 176·6 | 345·3 | 812·8 | ... |

*Chanzo.* Idara ya Takwimu/Benki Kuu.
+ : Makisio.

## SAFARI KATIKA MBUGA ZA WANYAMA

Jedwali Na. 54

(Namba)

| Mbunga | Safari zote | | | | | Safari za Malipo | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1984 | 1985 | 1986 | 1987 | Badiliko % 1986/87 | 1984 | 1985 | 1986 | 1987 | Badiliko % 1986/87 |
| Serengeti | 23,554 | 22,001 | 27,966 | 35,657 | 27·50 | 22,897 | 2) ,382 | 27,183 | 34,659 | 27·50 |
| Manyara | 35.418 | 35,454 | 35,381 | 46.519 | 31·48 | 29,372 | 30,596 | 29.331 | 38.564 | 31·48 |
| Ngorongoro | 47.142 | 38,910 | 42,918 | 54,720 | 27·50 | 45,190 | 37,315 | 41,158 | 52,476 | 27·50 |
| Arusha | 8,673 | 7,993 | 5 847 | 8,685 | 48·54 | 7,705 | 7.201 | 5,268 | 7,825 | 48.54 |
| Mikumi | 24,375 | 21,699 | 22,622 | 10,180 | 55·00 | 20,871 | 18,311 | 19,093 | 15,344 | −19·64 |
| Ruaha | 4,092 | 4,629 | 2,964 | 5928 | 100·00 | 3,844 | 4,079 | 2,611 | 5.223 | 100·04 |
| Tarangire | 7,169 | 6,114 | 7,284 | 7874 | 8·10 | 5,023 | 4,286 | 5,104 | 5.520 | 8·15 |
| Kilimanjaro | 9,391 | 8,559 | 8933 | 10.059 | 12·60 | 9,336 | 7,934 | 8,281 | 9,325 | 12·61 |
| Gombe | 677 | 933 | 573 | 841 | 46·77 | 658 | 858 | 527 | 774 | 46·87 |
| Jumla ... | 160,491 | 146,292 | 154.488 | 180,463 | 16·81 | 144,896 | 131,962 | 138,556 | 169,710 | 22·48 |

*Chanzo:* Idara ya Takwimu.
*: Makisio.

## NAFASI KATIKA HOTELI NA MATUMIZI YAKE

Jedwali Na. 55

| Maelezo | Dar es Salaam | | | Arusha - Moshi | | | Mbuga za Wanyama†† | | | Zanzibar | | | Sehemu nyingine | | | Jumla | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1985 | 1986 | 1987 | 1985 | 1986 | 1987 | 1985 | 1986 | 1987 | 1985 | 1986 | 1987 | 1985 | 1986 | 1987 | 1985 | 1986 | 1987 |
| Idadi ya Hoteli | 38 | 39 | 41 | 28 | 28 | 30 | 10 | 10 | 10 | 12 | 13 | 14 | 74 | 75 | 79 | 162 | 163 | 174 |
| Vyumba vilivyokuwepo (namba)† | 1,694 | 1,733 | 1,633 | 1,197 | 1234 | 1,056 | 508 | 584 | 336 | 235 | 253 | 255 | 1,442 | 1,513 | 1,009 | 5,076 | 5,264 | 5,141 |
| Siku za Kulala Hotelini (000) | 609·2 | 666·8 | 640·4 | 315·4 | 292·5 | 263·9 | 76 | 81·8 | 145 | 58·2 | 61·2 | 58·7 | 330·7 | 372·3 | 368·5 | 1,410·5 | 1,476·7 | 1,476·5 |
| Watanzania | 397·1 | 421·5 | 428·5 | 240·4 | 228 | 176·6 | 30·3 | 28 | 30·6 | 37·9 | 38·6 | 31·5 | 292·6 | 344·8 | 340·2 | 998·3 | 1,060·9 | 1,007·3 |
| Nchi Nyingine za Afrika | 43·7 | 49·4 | 44·8 | 22·1 | 16·8 | 24·5 | 3 | 2·3 | 3·9 | 2·5 | 2·2 | 4·3 | 5·8 | 8·8 | 7·4 | 77·3 | 79·6 | 85 |
| Ulaya | 130·2 | 136·7 | 115·3 | 32·6 | 30·1 | 41·7 | 21·2 | 24·6 | 50·3 | 12·7 | 14·2 | 15·6 | 23·2 | 21·3 | 17·3 | 219·7 | 226·9 | 240·2 |
| Amerika | 18·4 | 21·5 | 16·4 | 13·4 | 12·9 | 15·3 | 19·9 | 26·9 | 56 | 1·9 | 2·4 | 2·8·2 | 3·2 | 2·9 | 1·8 | 56·7 | 66·9 | 93·8 |
| Asia na Australia | 39·8 | 37·7 | 35·2 | 6·9 | 4·7 | 5·2 | 1·7 | 2 | 3·3 | 4·2 | 3·6 | 4·1 | 5·9 | 4·5 | 1·8 | 98·5 | 52·4 | 50·3 |
| Siku za Kulala Hotelini % | 100 | 100 | 100 | 100 | 100 | 100 | 100 | 100 | 100 | 100 | 100 | 100 | 100 | 100 | 100 | 100 | 100 | 100 |
| Watanzania | 63·1 | 63·2 | 66·9 | 76·2 | 77·9 | 66·9 | 39·9 | 33·4 | 21·1 | 64 | 63·2 | 53·7 | 88·5 | 89·9 | 92·3 | 70·8 | 71·2 | 70·1 |
| Nchi Nyingine za Afrika | 7 | 7·4 | 7 | 7 | 5·8 | 9·3 | 3·9 | 2·8 | 2·7 | 4·3 | 3·5 | 7·3 | 1·8 | 2·4 | 2 | 5·5 | 5·4 | 6 |
| Ulaya | 21·7 | 20·5 | 18 | 10·3 | 18·3 | 15·1 | 27·7 | 29·1 | 34·7 | 21·5 | 23·2 | 26·6 | 7 | 5·7 | 4·7 | 15·6 | 15·4 | 15·5 |
| Amerika | 2·9 | 3·2 | 2·6 | 4·3 | 4·4 | 5·8 | 26·2 | 32·1 | 39·2 | 3·1 | 4·3 | 5·4 | 9 | 8 | ·5 | 4 | 4·5 | 3 |
| Asia na Australia | 6·3 | 5·7 | 5·5 | 2·2 | 1·6 | 2·2 | 2·3 | 2·4 | 2·3 | 7·1 | 5·9 | 7 | 1·8 | 1·2 | ·5 | 4·1 | 3·5 | 3·4 |

††: Kanda ya Kaskazini.
†: Kama ilivyokuwa tarehe 31 Desemba.

## IDADI YA WATALII NA SIKU ZA KULALA WAGENI

Jedwali Na. 56

| Mwaka | Wageni | | Siku Hotelini | | Wastani |
|---|---|---|---|---|---|
| | (000) | Badiliko % | (000) | Badiliko % | Siku Hotelini |
| 1980 | 73 | — | 557 | 19·3 | 7·6 |
| 1981 | 83 | −13·7 | 537 | −3·6 | 6·5 |
| 1982 | 70 | −15·7 | 458 | −14·7 | 6·5 |
| 1983 | 52 | −25·7 | 400 | −12·7 | 7·7 |
| 1984 | 64 | 0 | 398 | −·5 | 6·2 |
| 1985 | 63 | 3·8 | 412 | 3·5 | 6·5 |
| 1986 | 67 | −3·7 | 426 | +3·4 | 6·4 |
| 1987 | *94 | 40·3 | 469 | +10·1 | *5.0 |

*Chanzo:*—Idara ya Takwimu.
*: Makisio.

## 6.—UJENZI, ARDHI NA MAENDELEO YA NYUMBA

**Ujenzi:**

1. Mwaka 1987 umeshuhudia kuongezeka kwa shughuli za ujenzi kama ambavyo vigezo mbali mbali vya kiuchumi vimeonyesha vikiwemo, mchango wa sekta ya ujenzi katika Pato la Taifa, na matumizi ya vitaa vya ujenzi. Mchango wa ujenzi katika Pato la Taifa uliongezeka kutoka Sh. 752.0 milioni mwaka 1986 hadi Sh. 774.0 milioni mwaka 1987 (kwa bei za mwaka 1976) au ongezeko la asilimia 2.9. Ongezeko hili linatokana na kuongezeka kwa shughuli za ujenzi nchini ambazo zimewezekana kutokana na nafuu ya upatikanaji wa vitaa vya ujenzi nchini, vikiwamo saruji, mabati, mbao, nondo na misumari, n.k.

2. Upatikanaji wa baadhi ya vifaa vya ujenzi uliongezeka kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji katika viwanda vya hapa nchini na ulegezaji masharti ya biashara na nchi za nje. Baadhi ya bidhaa zinazozalishwa hapa nchini ambazo uzalishaji wake umeongezeka ni mbao, saruji na mabati. Ongezeko la uzalishaji katika viwanda umetokana na kupatiwa misaada ya uagizaji bidhaa (import support) chini ya Mpango wa Kufufua Uchumi.

Pamoja na unafuu katika upatikanaji wa vitaa vya ujenzi uliotokea mwaka 1987, bei zake ziliendelea kupanda, kama inavyoonyeshwa hapa chini:—

### FAHIRISI ZA BEI ZA BAADHI YA VIFAA VYA UJENZI
(Kwa Bei za Mwaka 1980)

| Mwaka<br>Bidhaa | 1980 | 1981 | 1982 | 1983 | 1984 | 1985 | 1986 | 1987 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Saruji .......... | 100 | 101 | 105 | 113 | 176 | 201 | 266 | 342 | 28.57 |
| Chuma ........ | 100 | 138 | 138 | 196 | 234 | 348 | 583 | 864 | 48·19 |
| Mabati ........ | 100 | 100 | 100 | 157 | 251 | 251 | 512 | 512 | 0·0 |
| Plaiwudi ...... | 100 | 105 | — | 170 | — | — | 635 | 865 | 36·22 |
| Misumari ya Bati ........... | 100 | 127 | 127 | 170 | 169 | 314 | 775 | 775 | 0·0 |
| Misumari mingine ....... | 100 | 126 | — | 245 | 362 | 402 | 614 | 801 | 30·45 |
| Chipuboli .... | 100 | 175 | — | 192 | — | — | 630 | 850 | 34·92 |

*Chanzo*—Baraza la Taifa la Ujenzi (National Construction Council).

3. Uwezo wa kutekeleza miradi ya ujenzi nchini haukuwa na ongezeko kubwa kama unavyothibitishwa na kuendelea kuwapo kwa idadi kubwa ya makondrata wa madaraja ya chini ambao uwezo wao wa ujenzi ni mdogo—kutokana na uwezo mdogo kimtaji, utaalam na uzoefu. Hadi Desemba, 1987, Bodi ya Wasanifu, Wakadiria Majengo na Makondrata ilikuwa na Wasanifu 138, Wakadiria majengo 46 na Makondrata 871 waliosajiliwa ikilinganishwa na makondrata 861 waliokuwapo mwaka 1986. Makondrata wa daraja la kwanza hadi la nne wamepungua kutoka 225 mwaka 1986 hadi 188 mwaka 1987, wakati ambapo makondrata wa daraja la tano hadi la saba waliongezeka kutoka 636 mwaka 1986 hadi 683 mwaka 1987. Mgawanyo wa makondrata katika madaraja na miaka mbali mbali umeonyeshwa katika jedwali hapa chini.

KAMPUNI ZA MAKONDRATA ZILIZOSAJILIWA NCHINI

| Daraja<br>Mwaka | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1977 | 19 | 13 | 21 | 45 | 32 | 22 | 16 | 168 |
| 1978 | 24 | 15 | 29 | 62 | 55 | 38 | 43 | 266 |
| 1979 | 29 | 16 | 37 | 72 | 86 | 58 | 66 | 264 |
| 1980 | 33 | 18 | 44 | 77 | 122 | 86 | 98 | 479 |
| 1981 | 40 | 15 | 68 | 102 | 116 | 84 | 117 | 542 |
| 1982 | 40 | 16 | 70 | 106 | 119 | 94 | 146 | 591 |
| 1985 | 39 | 22 | 61 | 97 | 118 | 133 | 284 | 754 |
| 1986 | 39 | 23 | 63 | 100 | 124 | 150 | 362 | 861 |
| 1987 | 36 | 21 | 39 | 92 | 130 | 147 | 406 | 871 |

*Chanzo*—Bodi ya Wasanifu, Wakadiriaji Majengo na Makondrata.

4. Idadi kubwa ya makondrata nchini imewezesha kuwepo kwa hali ya ushindani katika sekta, hali ambayo inatoa changamoto kwa wajenzi kuelekeza juhudi katika kupunguza gharama za uendeshaji ili kutoa bei za kiushindani na kuinua ubora wa kazi. Hata hivyo mgawanyo wa makondrata katika miji mbali mbali unaonyesha kuwa wengi wao wako Dar es Salaam hali ambayo inaongeza gharama za ujenzi kutokana na gharama za kusafirisha mitambo na zana za ujenzi hadi kwenye maeneo ya ujenzi katika mikoa yenye uhaba wa makondrata. Urekebishaji wa hali hii unahitaji juhudi mahsusi za kuinua uwezo wa wajenzi walioko katika madaraja ya chini na hasa katika mikoa yenye upungufu kwa kuwapatia kazi ili wajipatie mitaji na uzoefu pamoja na kuimarisha utaratibu wa kutoa mafunzo unaoendelea chini ya mradi wa "Sixth Highway".

5. Licha ya kuwepo miradi mingi ya kutekeleza makondrata waliendelea kukabiliwa na matatizo ya ucheleweshaji wa malipo kutoka kwa wateja wakuu wa huduma za ujenzi wakiwemo Serikali na Mashirika ya Umma. Aidha, uchakavu wa zana na mitambo ya ujenzi uliwakabili makondrata hasa wale ambao hawakuwa na uwezo wa kuagiza zana kutoka nje. Hali hii iliwafanya makondrata wa hapa nchini kutokuwa na uwezo wa kutekeleza miradi ya ubandisi (Civil engineering works) kama ya barabara ambayo hutumia kiasi kikubwa cha zana zinazoagizwa kutoka nje ya nchi ikilinganishwa na kazi za majengo.

**Ardhi:**

6. Katika kipindi cha 1987/88 nyanja hii ilikabiliwa na matatizo kadhaa hasa ya ujenzi holela na msongamano wa majumba mijini kutokana na kukua kwa miji na ongezeko la haraka la idadi ya watu. Vile vile ukosefu wa matumizi bora ya ardhi mijini na vijijini pamoja na ukosefu wa huduma muhimu za kiuchumi na kijamii katika sehemu wanazoishi wananchi na pia ukosefu wa viwanja vilivyopimwa na ukosefu wa ramani za uwiano mbali mbali yaliathiri ukuaji wa sekta ya ardhi uwekezaji wa rasilimali kutokana na uendelezaji wa ardhi ulikuwa Sh. 358 milioni mwaka 1987 ukilinganishwa na Sh. 790 milioni za mwaka 1986, katika bei za miaka hiyo. Hata hivyo miradi mbali mbali ilitekelezwa katika nyanja za upimaji na ramani, uthamini wa ardhi, huduma za makazi, mipango miji na matumizi bora ya ardhi.

7. Katika kutekeleza sera ya Kilimo na Mifugo, upimaji mipaka ya vijiji uliendelea katika mikoa ya Mtwara, Tanga, Mbeya na Dododma. Uchoraji wa ramani za vijiji na utayarishaji wa ramani za hati za kumiliki ardhi uliendelea katika vijiji vya mikoa ya Mtwara, Mara na Mbeya. Mzabuni wa kupiga picha Mkoa wa Shinyanga kutoka angani alichaguliwa na kazi hiyo itaendelea mwaka 1988/89.

8. Shughuli za upimaji na ramani ziliendelea kwenye kanda ya Kaskazini Mashariki ya Tanzania ambapo jumla ya "map sheets" 53 za utayarishaji wa ramani za uwiano 1:50,000 zilikamilika na marekebisho ya alama za upimaji kati ya jiji la Dar es Salaam na mji wa Kibaha uliendelea.

9. Utathmini wa ardhi uliendelea katika miji ya mikoa ya Ruvuma, Rukwa, Mtwara na jiji la Dar es Salaam. Ununuzi wa baadhi ya vifaa vya upimaji kama darubini na distomat ulifanyika.

10. Shughuli za kutayarisha mipango kabambe ya miji ziliendelea na kukamilika katika miji ya Mwanza, Arusha na Hai. Maandalizi ya utayarishaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi vijijini yalifanyika kwa kukusanya na kuchambua takwimu katika vijiji vichache vya mikoa

ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Morogoro, Dodoma, Iringa na Mbeya. Utayarishaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika mikoa ya kanda ya Reli ya Uhuru na kanda ya Ziwa ilikamilika. Mipango kabambe ya Wilaya ilitayarishwa kwa Wilaya za Loliondo, Tabora na Mbinga.

11. Utekelezaji wa mradi wa huduma za makazi jijini Dar es Salaam uliendelea ambapo viwanja 2,000 vimepimwa katika eneo la Tegeta. Michoro ya kihandisi ya ujenzi wa huduma mbali mbali za kiuchumi na kijamii kwa ajili ya maeneo ya Tegeta, Tabata, Kinondoni Shamba, Hananasif na Mwananyamala Kisiwani pamoja na ripoti za kihandisi kuhusu ujenzi wa huduma hizo kwa maeneo yote zimetayarishwa.

**Nyumba:**

12. Kipindi cha mwaka 1987 kilishuhudiwa ongezeko la uwekezaji rasilimali katika majengo la Sh. 278 milioni hadi Sh. 1304 milioni kwa kulinganisha na Sh. 1,026 mwaka 1986. Ongezeko hili ni kubwa zaidi ongezeko la Sh. 111·0 milioni mwaka 1987 la uwekezaji rasilimali katika majengo umetokana na majengo yasiyo ya kuishi na hasa maghala.

13. Utafiti juu ya nyumba bora na vifaa bora vya ujenzi uliendelea kufanywa na kituo cha Utafiti wa Nyumba na Vifaa vya Ujenzi (BRU) kwa madhumuni ya kugundua (identify) vifaa nafuu vipatikanavyo hapa nchini na hatimaye kusambaza matokeo ya utafiti huo. Hata hivyo juhudi za kituo hicho zimekuwa zikiathiriwa na upungufu wa watafiti, uchakavu wa vifaa vya maabara na uhaba wa vyombo vya usafiri.

14. Upatikanaji wa mikopo ya nyumba za kuishi kwa watu binafsi umeendelea kuwa mdogo kutokana na wakopaji kushindwa kutimiza masharti ya ukopaji na riba kubwa inayotozwa na Benki ya Nyumba Tanzania (THB). Utaratibu wa kutoa mikopo ya nyumba kwa watumishi Serikalini pamoja na kusimamishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Nyumba kwa wakulima na wafanyakazi (Farmers and Workers Housing Development Fund) vilifutwa mwaka 1987.

15. Katika mwaka 1987, Mashirika ya Umma ya nyumba yakiwemo Shirika la Msajili wa Majumba, Shirika la Nyumba la Taifa na Kampuni ya Miliki ya Benki ya Nyumba Tanzania (TECO) pamoja na waajiri wakiwemo serikali, mashirika na taasisi mbali mbali wameendelea kujenga nyumba za kupangisha na za kuuza. Hata hivyo uwezo wa mashirika ya nyumba kujenga nyumba umeendelea kupungua kutokana na kupanda kwa gharama za ujenzi na riba kuwa za mikopo wakati ambapo mapato yanayotokana na kodi yamekuwa madogo kukidhi gharama za ujenzi au hata matengenezo. Katika mwaka 1986/87, Shirika la Nyumba la Taifa lilikamilisha nyumba 30 ikilinganishwa na nyumba

36 zilizokamilishwa mwaka 1985/86. Hii ni idadi ndogo ya nyumba zilizowahi kukamilishwa kuliko zote kutoka nyumba 2,350 mwaka 1968/69. Aidha, juhudi zimeendelea kufanyika za kuanzisha na kuimarisha vyama vya ushirika vya ujenzi wa nyumba ili kuwawezesha wakazi wa mijini na vijijini kujijengea nyumba zao wenyewe.

16. Aidha, kipindi cha mwaka 1987 kimeendelea kushuhudia ukuaji wa miji kiholela kwa ujenzi wa nyumba katika maeneo yasiyopimwa na yasiyokuwa ya huduma za makazi.

## 7.—USAFIRISHAJI NA MAWASILIANO

**Utangulizi:**

1. Sekta ya mawasiliano na uchukuzi ilikuwa kwa asilimia 4·5 kutoka Sh. 1,514.0 milioni mwaka 1986 hadi kufikia Sh. 1,582.0 milioni mwaka 1987 kwa bei za mwaka 1976. Ongezeko hili ni kubwa sana ikilinganishwa na ongezeko la Sh. 5.0 milioni au asilimia 0.3 kutoka Sh. 1,509.0 milioni mwaka 1985 hadi Sh. 1,514.0 milioni mwaka 1986. Hata hivyo sekta hii iliendelea kuathiriwa na upungufu wa vifaa, mitambo na vyombo mbalimbali vya uchukuzi pamoja na ubovu wa njia za uchukuzi hasa reli na barabara. Uwezo wa uchukuzi kwa njia ya barabara haukukidhi mahitaji ya uchumi na jamii kutokana na uhaba wa magari, matairi na mipira, ubovu wa barabara na uhaba wa baadhi ya vipuri. Huduma za usafiri na uchukuzi kwa njia ya reli zilionyesha dalili ya kuimarika ingawa bado yalikuwapo matatizo ya upungufu wa magari ya moshi na mabehewa, uhaba wa spea na uchakavu wa reli yenyewe na madaraja. Ingawa kulikuwa na maendeleo katika uimarishaji na upanuzi wa huduma za mawasiliano, matatizo ya uhaba wa fedha za kigeni, ukosefu wa mikonga na uchakavu wa mitambo na nyuzi za simu, ukosefu wa spea, uhaba wa magari ya kufanyia kazi na upungufu wa wataalam yaliendelea kuathiri utoaji wa huduma za simu nchini. Aidha huduma za posta, utabiri wa hali ya hewa, usafiri wa ndege na usalama wa usafiri wa anga ziliendelea kuathiriwa na uhaba wa huduma za msingi (basic facilities) na uchakavu wa vyombo na mitambo ya kufanyia kazi (operating equipments)

**Usafiri wa Barabara:**

2. Katika kipindi cha mwaka 1987 uchukuzi kwa njia ya barabara uliendelea kuathiriwa na uhaba wa magari ya mizigo na abiria, uhaba wa spea, matairi na mipira ya ndani; bei kubwa za malori na mabasi. Hata hivyo, kampuni za uchukuzi za mikoa ya Dodoma (KAUDO) Ruvuma (KAURU) Mtwara (KAUMU), Mwanza (KAUMA) na Tabora (KAUTA) ziliendelea kuimarishwa kwa kupatiwa malori mapya 71. Ingawa katika kipindi hiki kampuni zote zilikuwa na jumla ya malori na trela 346 na mabasi 40, ni malori 270 na mabasi 25 tu ndiyo yalikuwa yakifanya kazi.

3. Kampuni za uchukuzi za mikoa (RETCOs) zilisafirisha kiasi cha tani 178,576 za mazao na bidhaa mbalimbali ikilinganishwa na tani 153,221 katika kipindi cha 1986. Aidha makampuni ya KAUDO, KAUMU, KAURU na Kagera RETCO yaliendelea kutoa huduma ya usafiri kwa abiria katika kipindi hiki.

4. Mapato ya Kampuni za Uchukuzi za Mikoa (RETCOs) yaliongezeka kwa asilimia 62.7 kutoka Sh. 291.0 milioni mwaka 1986 hadi kufikia Sh. 473.5 milioni mwaka 1987. Ongezeko hili lilitokana na kuimarishwa kwa RETCOs, ongezeko la viwango vya ushuru, upatikanaji wa matairi na mipira ya ndani dizeli na jitihada za manejimenti katika kuongeza tija na kudhibiti gharama za uendeshaji. Aidha ufanisi huu uliyawezesha makampuni haya kuingiza faida ya Sh. 50.0 milioni ikilinganishwa na Sh. 17.0 milioni katika kipindi cha 1986. Hata hivyo uhaba wa vipuri vya magari ya aina ya Mitsubishi uliendelea kuwepo.

5. Mradi wa Matengenezo ya Magari nchini ya mradi maalum wa Sixth Highway Rehabilitation (Trucking Component) uliendelea kutekelezwa na unatarajia kuongeza uwezo wa malori hasa kwa ajili ya usombaji wa mazao vijijini mara utakapokamilika mwezi Desemba, 1988. Aidha utekelezaji wa Mradi wa "Agricultural Transportation Reinforcement" kwa kuimarisha RETCO uliendelea vizuri na malori 71 yalinunuliwa na kugawiwa kwa makampuni ya uchukuzi ya mikoa.

**Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA):**

6. Katika kipindi cha 1987, hali ya usafiri katika Jiji la Dar es Salaam iliendelea kuwa na pengo kubwa kati ya uwezo uliopo wa mabasi 201 na mahitaji halisi yanayokisiwa kuwa zaidi ya mabasi 700. Aidha Shirika la UDA liliendelea kushirikiana na mabasi ya watu binafsi (Dala Dala) yapatayo 180 katika kutoa huduma ya usafiri wa abiria Jijini Dar es Salaam.

7. Juhudi za kuinua uwezo wa shirika wa kuhudumia abiria hazikuleta matunda mazuri kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na ongezeko la haraka haraka la bei ya mabasi mapya, vipuri, matairi, n.k. lililotokana na kushuka kwa thamani ya sarafu ya Tanzania na nauli ndogo umbayo haiwiani na ongezeko la gharama za uendeshaji. Hivyo, katika kipindi hiki, shirika lilimudu kununua mabasi 12 tu kati ya mabasi 40 yaliyotengwa, na pia kuweza kufufua mabasi mengine 12 ya aina ya Ikarus. Hata hivyo idadi ya mabasi ya Shirika la UDA ilipungua kutoka 211 (makubwa 186 na madogo 25) mwaka 1986 na kufikia mabasi 201 (makubwa 177 na madogo 24) mwaka 1987. Kwa upande wa mabasi ya watu binafsi, idadi ya mabasi ilipungua kutoka 365 mwaka 1986 hadi 180 mwaka 1987 sawa na asilimia 51. Hata hivyo kutokana na kudhibiti gharama za uendeshaji na kuongeza ufanisi kiutendaji, idadi ya abiria

waliohudumiwa na shirika iliongezeka kwa asilimia 14 kutoka abiria 71.7 milioni mwaka 1986 hadi 81.8 milioni mwaka 1987. Aidha umbali wa kilometa—abiria uliongezeka kwa asilimia 3.5 kutoka 6,915,000 mwaka 1986 hadi 7,157,000 mwaka 1987.

**Kampuni ya Mabasi ya Taifa (KAMATA):**

8. KAMATA iliendelea kutoa huduma za usafiri wa abiria mikoani na Jijini Dar es Salaam kwa kiwango kidogo kwani ni mabasi 12 tu kati ya jumla ya mabasi 43 yaliyokuwa yakifanya kazi. Jambo ambalo liliathiri sana uwezo wa shirika ni matatizo ya ukwasi. Kampuni ilimudu kununua mabasi mawili (bado kuwekwa barabarani) tu kati ya 18 yaliyotengewa na Shirika la Magari la Taifa (SMC). Jitihada za kufufua mabasi 11 ziliendelea kufanywa katika kipindi hiki. Hivyo uwezo wa kampuni katika kutoa huduma zake uliendelea kufifia na idadi ya abiria ilipungua kwa asilimia 94·7 kutoka abiria 1,165,000 mwaka 1986 hadi 62,000 mwaka 1987. Aidha umbali wa kilometa abiria ulipungua kwa asilimia 66·7 kutoka 2,893,000 mwaka 1986 hadi 963,000 mwaka 1987. Kutokana na matatizo haya KAMATA ilijitoa katika njia zinazoingiza hasara na pia ililazimika kuuza karakana zake za Mwanza na Tanga, kufunga baadhi ya ofisi zake mikoani na kupunguza idadi ya wafanyakazi.

**Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT):**

9. Katika kipindi cha 1987 Chuo kiliendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi ili kuipatia sekta ya uchukuzi wataalam wa kuendesha shughuli zake kwa ufanisi. Idadi ya wanafunzi wa kozi ndefu wa mwaka wa kwanza waliosajiliwa ilikuwa 70 (20 uongozi wa usafirishaji na 50 wa ufundi wa magari) kama mwaka 1986. Aidha chuo kiliendesha jumla ya kozi fupi 16 zilizowashirikisha wafanyakazi 506 ikilinganishwa na kozi 10 zilizowashirikisha wafanyakazi 138 katika kipindi cha 1987. Chuo pia kiliendelea kufanya utafiti katika masuala yanayohusu uchukuzi na hivyo kutoa ushauri kwa makampuni na mashirika katika sekta hii. Matatizo ya ukosefu wa vyumba vya madarasa na ofisi pamoja na kutopatiwa kibali cha kununulia magari ya kufundishia na upungufu wa vifaa vya karakana yaliendelea kuathiri utoaji wa mafunzo chuoni.

**Usafiri wa Reli:**

(a) **Shirika la Reli Tanzania (TRC):**

10. Katika kipindi cha 1987 huduma ya uchukuzi kwa njia ya reli ziliendelea kuathiriwa na upungufu wa spea, matengenezo hafifu ya magari moshi na mabehewa ya abiria na mizigo, uchakavu wa reli na huduma duni ya mawasiliano kati ya stesheni mbalimbali. Magari ya moshi yalipungua kwa asilimia 17.2 kutoka 134 mwaka 1986 hadi 111 mwaka 1987, ingawa idadi ya mabehewa ya abiria na mizigo iliongezeka kwa asilimia 0.4 kutoka 7,295 mwaka 1986 hadi 7,324 mwaka 1987.

Kutokana na jitihada za shirika za kuongeza ufanisi na matumizi bora ya magari ya moshi na mabehewa yaliyopo, uchukuzi wa mizigo uliongezeka kwa asilimia 3.0 kutoka tani 877,000 mwaka 1986 hadi tani 903,000 mwaka 1987. Aidha uchukuzi wa abiria uliongezeka kwa asilimia 17 kutoka abiria 2.3 milioni mwaka 1986 na kufikia 2.7 milioni mwaka 1987.

**Mamlaka ya Reli ya Uhuru (TAZARA):**

11. Dalili za kuimarika kwa Mamlaka zilianza kujitokeza katika kipindi hiki. Idadi ya magari ya moshi iliongezeka kutoka 95 mwaka 1986 hadi 110 mwaka 1987 na msukumo mkubwa uliwekwa katika kuimarisha uchukuzi wa mizigo. Kutokana na azma hii, idadi ya mabehewa ya mizigo iliongezeka kutoka 1,796 mwaka 1986 hadi 1847 mwaka 1987. Mabehewa ya abiria yalibaki 95 kama ilivyokuwa katika kipindi cha 1986 na hivyo kutokuwa na mabadiliko ya idadi ya abiria waliosafirishwa.

12. Uchukuzi wa mizigo uliongezeka kutoka tani 1.16 milioni mwaka 1986 hadi 1.19 milioni mwaka 1987. ongezeko ambalo ni chini ya lengo lililowekwa la kusafirisha tani 1.27 mwaka 1987. Aidha kupungua kwa magari moshi DFH 2, uhaba wa mabehewa ya mizigo na upungufu wa wafanyakazi wenye ujuzi uliathiri ufanisi wa shughuli za Mamlaka.

**Usafiri katika Bahari na Maziwa:**

13. Kiasi cha bidhaa zilizopitia katika bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara kiliendelea kuongezeka kwa asilimia 7.8 kutoka tani 3.87 milioni mwaka 1986 hadi tani 4.17 milioni mwaka 1987. Ongezeko hili halikutokana tu na hali nzuri ya kilimo hapa nchini pamoja na nchi jirani kuongeza upitishaji wa bidhaa zao katika bandari za Tanzania, bali pia kwa nchi ya Zimbabwe kupitishia baadhi ya bidhaa zake katika bandari hizi.

14. Idadi ya abiria waliohudumiwa katika bandari hizi iliongezeka kwa asilimia 12.6 kutoka 94,500 mwaka 1986 hadi 106,400 mwaka 1987. Idadi ya meli zilizotia nanga katika bandari hizi ilipungua kwa asilimia 0.5 kutoka meli 1,247 zenye uwezo wa kubeba tani 4.76 milioni mwaka 1986 hadi 1 184 zenye uwezo wa kubeba tani 4.71 mwaka 1987. Upungufu wa idadi ya meli ulitokana na kuongezeka kwa matumizi ya meli kubwa hasa zinazobeba makontena.

15. Ili kuweza kuyamudu majukumu yake kikamilifu, mamlaka ya Bandari Tanzania (T.H.A.) iliendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo katika bandari za Dar es Salaam Tanga na Mtwara pamoja na bandari ndogo za Kilwa, Lindi na Mafia. Aidha ulifanyika uchunguzi wa utendaji kazi wa bandari ya Dar es Salaam ili kutoa ufumbuzi wa kuongeza ufanisi hapo baadaye.

**Usafiri katika Sehemu za Mwambao:**

16. Huduma za usafiri sehemu za mwambao ziliendelea kutolewa na Kampuni ya Meli Mwambao Tanzania (TACOSHILI) ikisaidiana na meli za watu binafsi (kama vile MV. Mwenge na nyinginc ndogo "Schooners" ambazo hubeba mizigo chini ya uwakala wa TACOSHILI) na meli za Shirika la Meli Zanzibar. Jumla ya tani (pay-tonnes) zilizosafirishwa ziliongezeka kwa asilimia 2.5 kutoka 107.719 mwaka 1986 hadi 110.402 mwaka 1987 na idadi ya abiria iliendela kupungua kwa asilimia 1.2 kutoka 22,869 mwaka 1986 hadi kufikia 22.600 mwaka 1987. Kutokana na kuongezeka kwa mizigo iliyohudumiwa pamoja na ruzuku kutoka NORAD, mapato ya shirika yaliongezeka kwa asilimia 34.8 kutoka Sh. 188.1 milioni mwaka 1986 hadi Sh. 253.6 milioni mwaka 1987. Ongezeko hili ni kubwa ikilinganishwa na ongezeko la mwaka 1986 kwa kiasi cha asilimia 22.5 kutoka Sh. 174.4 milioni mwaka 1986 hadi kufikia Sh. 213·7 miliom mwaka 1987. Hivyo mapato ya ziada yaliongezcka kwa asilimia 191.2 kutoka Sh. milioni 13.7 mwaka 1986 hadi Sh. 39.9 milioni mwaka 1987.

17. Lakini pamoja na mafanikio hayo. TACOSHILI iliendelea kukabiliwa na matatizo mengi ikiwa ni pamoja na kuzeeka kwa meli za Mv. Lindi na MS Mtwara na ukosefu wa matengenezo; ushuru na nauli ndogo, ukosefu wa "Dry Docking Facility" nchini kufanyia matengenezo makubwa ya meli na pia uhaba wa fedha za kigeni kwa ajili ya kufanyia matengenezo nchi za nje; na uhaba wa watalaam wananchi hasa katika fani ya usafirishaji kwa njia ya meli na ufundi.

**Usafiri wa Anga:**

**Shirika la Ndege Tanzania (ATC):**

18. Katika kipindi cha 1987 ATC ilikuwa na ndege mbili aina ya Boeing 737, tatu aina ya Fokker Friendship 27 na tatu aina ya DHC—6. Aidha Shirika lilikodi ndege moja aina ya Boeing 707 kutoka Zambia Airways kwa kipindi ambacho ndege za Shirika (ATC) zilipokuwa nje ya nchi kwa matengenezo. Kutokana na matatizo mbalimbali ikiwa ni pamoja na ukosefu wa fedha za kigeni kwa ajili ya kununulia vipuri na spea Shirika halikuweza kukidhi mahitaji ya huduma ya usafiri wa ndege ndani na nje ya nchi.

19. Katika kipindi hiki tani-kilometa zilizokuwapo ziliongezeka kutoka 38,510 mwaka 1986 hadi 42,107 mwaka 1987 na tani-kilometa zilizotumika ziliongezeka kutoka 23,798 mwaka 1986 hadi 25,314 mwaka 1987. Hata hivyo kutokana na uhaba wa spea. matumizi ya tani-kilomita yalikuwa asilimia 60.1 ikilinganishwa na asilimia 61.8 mwaka 1986. Aidha viti-kilomita vilivyokuwepo viliongezeka kutoka 321,200 mwaka 1986 hadi 362,839 mwaka 1987 na vilivyotumika viliongezeka pia kutoka 238,917 mwaka 1986 hadi 249,462 mwaka 1987. Hivyo matumizi halisi ya viti-kilomita yalipungua kutoka asilimia 74.4 mwaka 1986 hadi 60.1 mwaka 1987.

20. Usafiri wa abiria ulionyesha dalili za kuimarika. Idadi ya abiria waliohudumiwa iliongezeka kwa asilimia 3.4 kutoka 441,000 mwaka 1986 hadi 456,000 mwaka 1987. Aidha shirika liliongeza mapato yake kwa asilimia 56 kutoka Sh. 850.4 milioni mwaka 1986 hadi Sh. 1,326.3 milioni mwaka 1987. Hata hivyo kutokana na "inflation" na kupungua kwa thamani ya sarafu ya Tanzania gharama za uendeshaji ziliongezeka kutoka Sh. 1,377.5 milioni mwaka 1986 hadi Sh. 1,742.7 milioni mwaka 1987. Hata hivyo shirika liliweza kupunguza hasara kwa asilimia 40.6 kutoka Sh. 512.3 milioni mwaka 1986 hadi kufikia Sh. 304.1 milioni mwaka 1987.

**Huduma za Posta na Simu:**

(a) **Huduma za Posta:**

21. Shughuli za kiuchumi na jamii ziliendelea kupanuka zaidi katika kipindi cha 1987 ikilinganishwa na kasi ya kupanuka kwa huduma za posta. Hata hivyo kiutekelezaji kipindi cha 1987 kilikuwa cha mafanikio zaidi kuliko ilivyokuwa mwaka 1986.

22. Idadi ya Posta iliongezeka kwa asilimia 2.3 kutoka 738 (Ofisi ndogo za posta 576 na Idara za posta 162) mwaka 1986 hadi 757 (ofisi ndogo za posta 589 na Idara za posta 168) mwaka 1987. Aidha masanduku ya binafsi yaliongezeka kwa asilimia 6.7 kutoka masanduku 85,508 mwaka 1986 hadi 91,258 mwaka 1987. Hata hivyo ongezeko hili ni dogo sana ikilinganishwa na ongezeko la mahitaji la asilimia 28.2 kutoka masanduku 37,329 mwaka 1986 hadi 47,855 mwaka 1987.

23. Utoaji wa huduma hafifu uliendelea kutokana na matatizo mbalimbali ikiwa ni pamoja na ukosefu wa vifaa muhimu vya posta kutokana na ukosefu wa fedha za kigeni, bei ndogo inayotozwa kulinganisha na gharama za uendeshaji, na uhaba wa magari ya kukusanya, kusambaza na kusafirisha barua/vifurushi.

(b) **Huduma za Simu:**

24. Katika jitihada ya kuongeza utoaji wa huduma za simu ndani na nje ya nchi, Shirika lilipanga kutekeleza miradi 208 katika kipindi cha 1987 na miradi 55 au asilimia 26.4 ilikamilishwa, ikiwa ni pamoja na mradi wa "Microwave" katika njia za Nyololo--Njombe--Songea na Mbeya-Tukuyu--Malawi na UHF link Mbeya--Sumbawanga—Mpanda. Miradi mingine ni "Automatic Exchanges" za Shinyanga (Line 1400), Kijitonyama jijini Dar es Salaam (Line 4000) na "Magnets Exchanges" za Mlandizi, Mtera na Kanyigo. Aidha, kutokana na kukamilisha utekelezaji wa miradi mbalimbali, Shirika limeweza kuongeza uwezo wa njia za simu (capacity of exchange) kwa asilimia 4.6 kutoka njia 73,942 mwaka 1986 hadi 77,347 mwaka 1987. Njia za simu zilizokuwa zikitumika katika kipindi hiki ziliongezeka kwa asilimia 8.2 kutoka njia 54,460 mwaka 1986 na kufikia 58,919 mwaka 1987. Kwa upande mwingine maombi yaliongezeka kwa asilimia 11.9 kutoka maombi 66,718 mwaka 1986 hadi 74,628 mwaka 1987.

25. Utoaji wa huduma za simu uliendelea kuathiriwa na matatizo mengi ikiwa ni pamoja na ukosefu wa mitambo, mikonga mipya (cables), viungo (joints) na vipuri.

**Usimamizi wa Usafiri** wa Anga:

26. Juhudi za kuimarisha na kupanua huduma za usalama wa anga ziliendelea kwa kutekeleza miradi kadhaa ikiwa ni pamoja na ufungaji wa mitambo ya Radio & Navigational Aids katika miji ya Zanzibar, Mwanza na Pemba, ununuzi wa mitambo ya "Aeronautical Fixed Telecommunication Network kwa ajili ya mawasiliano kati ya Dar es Salaam na nchi jirani; na uimarishaji wa Chuo cha Civil Aviation.

**Utabiri wa Hali ya Hewa:**

27. Jitihada za kuimarisha shughuli za kukusanya na kutawanya taarifa za hali ya hewa nchini ziliendelea katika kipindi cha 1987 kwa utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Hata hivyo mafanikio yakuridhisha hayakupatikana kutokana na matatizo mbalimbali hasa uhaba wa vifaa vya upimaji na utabiri wa hali ya hewa (met. instruments), vifaa vya anga za juu (Upper Air Equip.) na vifaa vya mawasiliano (Telecom. Equip). Lakini utekelezaji wa miradi mingine ulikuwa wa kuridhisha, hususan ujenzi wa kituo cha "Upper Air Station" cha Mtwara, ujenzi wa vituo vya "Snoptic Stations" vya Mahenge, Sumbawanga, Shinyanga na Kilwa Masoko pamoja na ujenzi wa Chuo cha Utabiri wa Hali ya Hewa cha Kigoma.

## HUDUMA ZA USAFIRI DAR ES SALAAM

Jedwali Na. 57

| Mwaka | Abiria (000) | Mabasi (Idadi)† | | Umbali (000 km) |
|---|---|---|---|---|
| | | Makubwa | Madogo | |
| 1976 | 86,235 | 280 | 50 | 9,974 |
| 1977 | 94,824 | 280 | 50 | 11,886 |
| 1978 | 99,535 | 230 | 66 | 10,126 |
| 1979 | 99,269 | 224 | 44 | 9,652 |
| 1980 | 105,876 | 186 | 40 | 9,579 |
| 1981 | 105,152 | 154 | 40 | 9,542 |
| 1982 | 119,686 | 190 | 40 | 9,517 |
| 1983 | 107,827 | 188 | 40 | 9,332 |
| 1984 | 98,779 | 186 | 30 | 9,063 |
| 1985 | 89,773 | 186 | 30 | 8,950 |
| 1986 | 71,705 | 186 | 25 | 6,915 |
| 1987 | 81,750 | 177 | 24 | 7,157 |

*Chanzo:*—Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA).
†: Kama ilivyokuwa 31 Desemba.

## KAMPUNI YA MABASI YA TAIFA (KAMATA)

Jedwali Na. 58

| Mwaka | Mabasi† (Idadi) | Abiria (000) | | Umbali (000km) | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Jumla | Badiliko % | Jumla | Badiliko % |
| 1977 | 94 | 920 | 13·2 | 4,792 | −19·1 |
| 1978 | 94 | 1,020 | 13·1 | 3,287 | −31·4 |
| 1979 | 83 | 1,006 | −1·4 | 5,243 | 59·5 |
| 1980 | 66 | 1,875 | 86·4 | 4,386 | −16·3 |
| 1981 | 72 | 2,168 | 15·6 | 4,859 | 10·8 |
| 1982 | 89 | 3,296 | 52·0 | 5,495 | 13·1 |
| 1983 | 91 | 1,849 | −43·9 | 5,440 | −1·0 |
| 1984 | 89 | 1,187 | −35·8 | 5,216 | −4·1 |
| 1985 | 80 | 1,717 | 44·7 | 4,496 | −13·8 |
| 1986 | 43 | 1,165 | −32·1 | 2,893 | −35·7 |
| 1987 | 43 | 62 | −94·7 | 963 | −66·7 |

*Chanzo.*—Kampuni ya Mabasi ya Taifa (KAMATA).
†: Kama ilivyokuwa 31 Desemba.

## SHIRIKA LA RELI TANZANIA

Jedwali Na. 59

| Maelezo | Kipimo | 1982 | 1983 | 1984 | 1985 | 1986+ | 1987 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Urefu wa Reli Kuu | Kms | 2.600 | 2.600 | 2.600 | 2.600 | 2.600 | 2.600 |
| Magari ya moshi (locomotives) | Namba | 194 | 202 | 153 | 155 | 134 | 111 |
| Mvuke | Namba | 86 | 86 | 46 | 43 | 22 | — |
| Dizeli | Namba | 108 | 116 | 107 | 112 | 112 | 111 |
| Jumla ya Mabehewa | Namba | 6,146 | 6,434 | 6.599 | 6,227 | 7,295 | 7.324 |
| Abiria | Namba | 212 | 232 | 215 | 231 | 172 | 172 |
| Mizigo ya kawaida+ | Namba | 4,916 | 4,939 | 4,928 | 4,831 | 5,890 | 5,642 |
| Mafuta+ | Namba | 364 | 672 | 600 | 632 | 750 | 750 |
| Mifugo+ | Namba | 222 | 221 | 220 | 227 | 130 | 360 |
| Mengineyo+ | Namba | 432 | 370 | 576 | 306 | 353 | 400 |
| Uchukuzi: Abiria | 000 | 2,443 | 3,104 | 2,977 | 3,040 | 2,291 | 2,672 |
| Mizigo | 000 Tani | 926 | 791 | 916 | 952 | 877 | 903 |

*Chanzo:* Shirika la Reli Tanzania.

+: Mabehewa makubwa (bogies) yamehesabiwa mara mbili.

## RELI YA UHURU-TAZARA

Jedwali Na. 59A

| Maelezo | Kipimo | 1982 | 1983 | 1984 | 1985 | 1986 | 1987 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Urefu wa reli+ | Kms | 1,860 | 1,860 | 1,860 | 1,860 | 1,860 | 1,860 |
| Magari ya Moshi | Namba | 96 | 105 | 110 | 109 | 95 | 110 |
| Reli kuu | Namba | 80 | 89 | 94 | 93 | 80 | 95 |
| Ya kujongeza | Namba | 16 | 16 | 16 | 16 | 15 | 15 |
| Mabehewa ya abiria | Namba | 97 | 97 | 97 | 95 | 95 | 95 |
| Abiria | Namba | 77 | 77 | 77 | 75 | 75 | 75 |
| Chakula | Namba | 10 | 10 | 10 | 10 | 10 | 10 |
| Vifurushi | Namba | 10 | 10 | 10 | 10 | 10 | 10 |
| Mabehewa ya mizigo | Namba | 1,962 | 1,962 | 1,962 | 1,847 | 1,796 | 1,847 |
| Mizigo ya kawaida | Namba | 1,787 | 1787 | 1,787 | 1,689 | 1,505 | 1,689 |
| Mifugo | Namba | 30 | 30 | 30 | 28 | 28 | 28 |
| Mafuta | Namba | 124 | 124 | 124 | 109 | 102 | 109 |
| Barafu | Namba | 21 | 21 | 21 | 21 | 20 | 21 |
| Menginेyo: | Namba | 147 | 147 | 147 | 138 | 128 | 138 |
| Breki | Namba | 78 | 78 | 78 | 71 | 66 | 71 |
| Ballast | Namba | 69 | 69 | 69 | 67 | 62 | 67 |
| Uchukuzi: Mizigo | 000Tani | 796 | 824 | 973 | 1,096 | 984 | 984* |
| Abiria | 000 | 987 | 564 | 1.198 | 1,065 | 1,161 | 1,161* |

*Chanzo:* Mamlaka ya Reli ya Uhuru.

+: Urefu halisi ni km 1,860·54, k. 974·914 zikiwa nchini Tanzania.

*: Takwimu za muda.

## USAFIRISHAJI KWA MELI: DAR ES SALAAM

Jedwali Na. 60

| Maelezo | Kipimo | 1982 | 1983 | 1984 | 1985 | 1986 | 1987 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Jumla ya meli | Namba | 884 | 808 | 795 | 866 | 887 | 846 |
| Uwezo wa kubeba mizigo | 000 | 3.738 | 3,579 | 3.445 | 3.286 | 3,667 | 3,631 |
| Jumla ya abiria | 000 | 82·3 | 134·7 | 57 | 71·9 | 72·5 | 79·4 |
| Jumla ya bidhaa zote | 000dwt | 3,286 | 3.184 | 3,578 | 3.150 | 3.526 | 3,811 |
| Bidhaa zilizopakuliwa | 000dwt | 2,482 | 2,441 | 2.580 | 2,312 | 2,633 | 2,768 |
| Za kawaida | 000dwt | 1,166 | 863 | 1,077 | 1,088 | 1,016 | 1,456 |
| Saruji | 000dwt | — | — | — | — | — | — |
| Mafuta | 000dwt | 1,306 | 1,561 | 1,491 | 1.209 | 1,603 | 1,312 |
| Mbolea | 000dwt | — | — | — | — | — | — |
| Mengineyo (1) | 000dwt | 10 | 17 | 12 | 15 | 14 | .. |
| Bidhaa zilizopakiwa | 000dwt | 803 | 738 | 993 | 837 | 889 | 1,036 |
| Za Kawaida | 000dwt | 670 | 615 | 756 | 708 | 667 | 918 |
| Mafuta | 000dwt | 112 | 111 | 209 | 122 | 216 | 118 |
| Mengineyo (1) | 000dwt | 21 | 12 | 28 | 7 | 6 | .. |
| Mabadilishano | 000dwt | 1 | 5 | 5 | 1 | 4 | 7 |

*Chanzo:* Mamlaka ya Bandari Tanzania.
(1): Kama vile molasses, talbw fats n.k.
.. Takwimu hazijapatikana.

## USAFIRISHAJI KWA MELI: TANGA

Jedwali Na. 60 (inaendelea)

| Maelezo | Kipimo | 1982 | 1983 | 1984 | 1985 | 1986 | 1987 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Jumla ya meli | Namba | 298 | 222 | 227 | 256 | 261 | 237 |
| Uwezo wa kubeba mizigo | 000 | 1.087 | 680 | 987 | 940 | 928 | 936 |
| Jumla ya abiria | 000 | 20 | 14 | 8 | 6 | 4 | 6 |
| Jumla ya bidhaa zote | 000dwt | 267 | 188 | 231 | 246 | 263 | 270 |
| Bidhaa zilizopakuliwa | 000dwt | 107 | 91 | 119 | 113 | 129 | 134 |
| Za kawaida | 000dwt | 81 | 53 | 80 | 81 | 94 | 82 |
| Saruji | 000dwt | — | — | — | — | — | — |
| Mbolea | 000dwt | 13 | 29 | 26 | 25 | 16 | 26 |
| Mafuta | 000dwt | 13 | 9 | 13 | 7 | 19 | 26 |
| Bidhaa zilizopakiwa | 000dwt | 160 | 97 | 112 | 133 | 134 | 136 |
| Za Kawaida | 000dwt | 160 | 97 | 112 | 133 | 134 | 136 |
| Mafuta | 000dwt | — | — | — | — | — | — |
| Matadilishano | 000dwt | — | — | — | — | — | — |

*Chanzo:* Mamlaka ya Bandari Tanzania

## USAFIRISHAJI KWA MELI: MTWARA

Jedwai Na. 60 *(inaendelea)*

| Maelezo | Kipimo | 1982 | 1983 | 1984 | 1985 | 1986 | 1987 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Jumla ya meli | Namba | 106 | 87 | 76 | 105 | 99 | 101 |
| Uwezo wa kubeba mizigo | 000 | 188 | 143 | 153 | 137 | 166 | 145 |
| Jumla ya abiria | 000 | 43 | 35 | 20 | 11 | 18 | 21 |
| Jumla ya bidhaa zote | 000dwt | 99 | 77 | 77 | 71 | 85 | 86 |
| Bidhaa zilizopakuliwa | 000dwt | 54 | 31 | 34 | 42 | 50 | 44 |
| Za kawaida | 000dwt | 42 | 20 | 22 | 32 | 31 | 32 |
| Mafuta | 000dwt | 12 | 11 | 12 | 10 | 19 | 12 |
| Bidhaa zilizopakiwa | 000dwt | 45 | 46 | 43 | 29 | 35 | 42 |
| Za Kawaida | 000dwt | 45 | 46 | 43 | 29 | 35 | 42 |
| Mafuta | 000dwt | | | | | | |
| Mabadil ishano | 000dwt | — | — | — | — | — | — |

*Chanzo:* Mamlaka ya Bandari Tanzania.

## USAFIRISHAJI KWA MELI: BANDARI ZOTE

Jedwali Na. 60 *(inaendelea)*

| Maelezo | Kipimo | 1982 | 1983 | 1984 | 1985 | 1986 | 1987 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Jumla ya meli | Namba | 1,285 | 1,117 | 1,098 | 1,227 | 1,247 | 1,184 |
| Uwezo wa kubeba mizigo | 000 | 5,013 | 4,402 | 4,585 | 4,363 | 4,761 | 4,712 |
| Jumla ya abiria | 000 | 145·3 | 183·7 | 85 | 88·9 | 94·5 | 106·2 |
| Jumla ya bidhaa zote | 000dwt | 3,69[illegible] | 3,449 | 3,88[illegible] | 3,467 | 3,874 | 4,167 |
| Bidhaa zilizopakuliwa | 000dwt | 2,643 | 2,563 | 2,733 | 2,467 | 2,812 | 2,946 |
| Za kawaida | 000dwt | 1,289 | 936 | 1,179 | 1,201 | 1,141 | 1,570 |
| Saruji | 000dwt | — | — | — | — | — | — |
| Mafuta | 000dwt | 1,331 | 1,581 | 1,516 | 1,226 | 1,641 | 1,350 |
| Mbolea | 000dwt | 13 | 29 | 26 | 25 | 16 | 26 |
| Mengineyo (1) | 000dwt | 10 | 17 | 12 | 15 | 14 | .. |
| Bidhaa zilizopakiwa | 000dwt | 1,[illegible]8 | 881 | 1,148 | [illegible] | 1,058 | 1,214 |
| Za Kawaida | 000dwt | 875 | 758 | 911 | 870 | 836 | 1,096 |
| Mafuta | 000dwt | 112 | 111 | 209 | 122 | 216 | 118 |
| Mengineyo (1) | 000dwt | 21 | 12 | 28 | 7 | 6 | .. |
| Mabadilishano | 000dwt | 1 | 5 | 5 | 1 | 4 | 7 |

(1): Kama vile molasses, tallow fats n.k.
.. Takwimu hazijapatikana.

## HUDUMA ZA POSTA

Jedwali Na. 61

| Maelezo | Kipimo | 1980 | 1981 | 1982 | 1983 | 1984 | 1985 | 1986 | 1987 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Ofisi ndogo za posta | Namba | 461 | 478 | 486 | 490 | 526 | 547 | 576 | 589 |
| Idara ya Posta | Namba | 145 | 148 | 151 | 153 | 158 | 160 | 162 | 168 |
| Masanduku binafsi | | | | | | | | | |
| Jumla | Namba | 61,244 | 67,309 | 67,811 | 73,034 | 76,933 | 81,558 | 85,508 | 91,258 |
| Yaliyokodishwa | Namba | 56,459 | 62,452 | 65,723 | 69,909 | 72,478 | 76,836 | 81,619 | 86,582 |
| Maombi yasiyotimizwa | Namba | 15,188 | 17 011 | 25,714 | 27,597 | 29,761 | 34,528 | 37,329 | 47,855 |
| Mifuko ya posta iliyokodishwa | Namba | 491 | 479 | 503 | 488 | 473 | 477 | +481 | 484 |
| Upelekaji barua nk. | | | | | | | | | |
| Barua | Mil. | 80 | 92 | 97 | 100 | 104 | 107 | 112 | 112 |
| Regista na barua za maana | 000 | 1,584 | 1,457 | 1,420 | 1,509 | 1,484 | 1,420 | 1,382 | 1,328 |
| Vifurushi nchini | 000 | 243 | 228 | 192 | 194 | 167 | 134 | 208 | 104 |
| Vifurushi vya nje | 000 | 8 | 9 | 15 | 15 | 17 | 18 | 17 | 14 |
| Leseni za kuuza stamp | Namba | 629 | 709 | 775 | 827 | 887 | 937 | 1,022 | 1,170 |

*Chanzo:* Shirika la Posta na Simu Tanzania.

Jedwali Na. 61A

## HUDUMA ZA SIMU

| Item | 1980 | 1981 | 1982 | 1983 | 1984 | 1985 | 1986 | 1987 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Telephones:** | | | | | | | | |
| Number of Exchanges | 154 | 156 | 159 | 160 | 161 | 167 | 173 | 180 |
| Manual | 123 | 125 | 126 | 127 | 127 | 132 | 138 | 143 |
| Automatic | 31 | 31 | 33 | 33 | 34 | 35 | 36 | 37 |
| Capacity (lines) | 50,027 | 51,845 | 53.637 | 59,120 | 66,550 | 71,202 | 73,942 | 77,347 |
| Manual | 12,027 | 13,345 | 13,437 | 14,120 | 14,650 | 15,302 | 15,842 | 16,447 |
| Automatic | 38,000 | 38,500 | 40,200 | 45,000 | 51,900 | 55,900 | 58,100 | 60,900 |
| Lines in use | 39,541 | 40,474 | 41,769 | 43.742 | 47,252 | 52,064 | 54,461 | 58,919 |
| Manual | 8,656 | 9,213 | 9,974 | 10,254 | 10,573 | 11,529 | 10,841 | 11,760 |
| Automatic | 30,885 | 31,261 | 31.795 | 33,488 | 36,679 | 40,535 | 43,619 | 47,159 |
| Telephone stations in use | 93,238 | 96,531 | 99,885 | 103,754 | 113,569 | 113,902 | 117,301 | 123,000 |
| **Telex:** | | | | | | | | |
| Number of exchanges | 3 | 3 | 3 | 3 | 3 | 3 | 3 | 3 |
| Capacity (lines) | 1,650 | 1,650 | 1,650 | 1,650 | 1,650 | 1,633 | 1,633 | 1,633 |
| Lines in use | 585 | 643 | 684 | 884 | 1,108 | 1,195 | 1,231 | 1,325 |
| **Radio—Call:** | | | | | | | | |
| Number of Stations | 3 | 3 | 3 | 3 | 3 | 3 | 3 | 3 |
| Subscribers | 229 | 230 | 238 | 245 | 257 | 256 | 256 | 258 |

*Chanzo:* Shirika la Posta na Simu Tanzania.

## HUDUMA ZA SIMU

Jedwali Na. 61B

| Item | Unit | 1980 | 1981 | 1982 | 1983 | 1984 | 1985 | 1986 | 1987 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Pending Application:** | | | | | | | | | |
| Telephone (Manual) | Number | 2,338 | 3,407 | 5,079 | 6,497 | 8,933 | 11,575 | 13,019 | 15,222 |
| Telephone (Automatic) | Number | 21,175 | 25,438 | 30,739 | 40,537 | 39,239 | 47,489 | 53,699 | 59,406 |
| Telex | Number | 448 | 523 | 600 | 613 | 717 | 1,105 | 1,283 | 2,137 |
| **Telephone Traffic:** | | | | | | | | | |
| Originating manually handled calls: | | | | | | | | | |
| Local | Million | 6·6 | 6·4 | 7·1 | 6·7 | 6·5 | 5·2 | 5·7 | 5·4 |
| Truck | Million | 2·9 | 3 | 3·1 | 3·1 | 3·1 | 2·9 | 3·9 | 4·4 |
| International | 000 | 239·4 | 297·5 | 410·4 | 496·1 | 538·1 | 561 | — | 500 |
| Metered units | Million | 275·9 | 230·5 | 278·1 | 259·9 | 416·8 | 449·7 | 486·1 | |
| **Telegragh Traffic:** | | | | | | | | | |
| Originating inland | Million | 96 | 81 | 63 | ·72 | ·61 | 1·10 | 1·2 | 1·3 |
| Originating external | 000 | 126·4 | 129·1 | 98 | 77·6 | 68·8 | 42·4 | 29·6 | 22·3 |
| **RADIO CALL—TRAFFIC** | | | | | | | | | |
| Originating telephone calls | 000 | 7·2 | 6·3 | 4·7 | 4.7 | 3·2 | 3·1 | 1·6 | |
| Originating telegrams | 000 | 7·3 | 4·6 | 3·7 | 4 | 2·8 | ·3 | ·044 | 0·0 |

*Chanzo:* Shirika la Posta na Simu Tanzania.

## SHIRIKA LA NDEGE TANZANIA+

Jedwali Na. 62

| Maelezo | Kipimo | 1980 | 1981 | 1982 | 1983 | 1984 | 1985 | 1986 | 1987 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Tani—Kilomita: | | | | | | | | | |
| Zilizokuwepo | 000 | 64,938 | 32,887 | 37,943 | 42,943 | 43.937 | 42945 | 38,510 | 42,107 |
| Zilizotumika | 000 | 27,857 | 17,676 | 20,337 | 22.118 | 26,376 | 27,121 | 23.798 | 25,314 |
| Matumizi | % | 42·9 | 53·7 | 53·6 | 52·6 | 60 | 63·1 | 61·8 | 60·1 |
| Viti—Kilomita: | | | | | | | | | |
| Vilivyokuwepo | 000 | 395,788 | 324,105 | 338,660 | 356,021 | 366,942 | 365,605 | 321,200 | 362,839 |
| Vilivyotumika | 000 | 284,027 | 180.264 | 210,628 | 227.121 | 262,314 | 256,584 | 238,917 | 249,462 |
| Matumizi | % | 47·7 | 55·6 | 62·2 | 63·8 | 71·5 | 70·2 | 74·4 | 68·8 |
| Abiria++ | 000 | 388 | 325 | 403 | 406 | 499 | 451 | 441 | 456 |
| Mizigo ya ziada | tani | 223 | 191 | 229 | 234 | 284 | 330 | 359 | 285 |
| Mizigo mingine | tani | 2.034 | 1,543 | 1,980 | 1,861 | 3.162 | 3,812 | 2,357 | 2,834 |
| Shehena za Posta | tani | 368 | 395 | 325 | 395 | 495 | 310 | 434 | 433 |
| Pato | Sh.mil. | 318·7 | 290·3 | 317·4 | 464·5 | 598·5 | 765.2 | 850·4 | 1,326·3 |

*Chanzo:* Shirika la Ndege Tanzania.

+: Takwimu zinahusu "scheduled traffic" tu.

++: Abiria waliolipa nauli kamili.

## 8.—MAJI NA NISHATI

**Maji:**

1. Katika mwaka 1987 Serikali iliendelea na juhudi za kusambaza huduma za maji vijijini na mijini. Jumla ya miradi 23 vijijini na miradi 25 mijini iliendelea kutekelezwa katika mwaka 1987. Shughuli muhimu katika miradi ya maji vijijini ziliendelea kuwa uchimbaji na ujenzi wa mabwawa na visima, uwekaji wa mabomba katika mitaro, ujenzi wa matangi na vituo vya maji na pia mafunzo ya wataalam. Mabwawa ya Bariadi, Kilimi (Nuga) na Mugumu yaliendelea kujengwa. Uchimbaji visima vifupi uliendelea katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma, Mbeya, Iringa, Morogoro, Shinyanga, Singida, Arusha na Tabora. Shughuli za kutandaza na kuunganisha bomba katika mitaro na ujenzi wa matangi na vituo vya maji ziliendelea katika miradi ya Wanging'ombe, Nyamaringo, Bagamoyo/Nzega/Bulenya/Nanga, na Handeni Trunk Main. Mafunzo ya wataalamu wa maji vijijini yaliendeshwa kupitia ofisi za wahandisi wa maji mikoani.

2. Kwa upande wa miradi ya maji mijini, shughuli muhimu zilikuwa ni ujenzi wa vyanzo vya maji, uimarishaji wa njia za kusambazia maji, ujenzi wa matangi na vituo vya kuchotea maji, uchunguzi na usanii. Uanzishaji, ujenzi na uimarishaji wa vyanzo vya maji uliendelea katika miji ya Mwanza, Arusha, Tanga, Dodoma, Shinyanga, Mugumu, Mtwara, Dar es Salaam na Bukoba. Njia za kusambazia maji katika miji ya Iringa, Musoma, Mwanza, Moshi, Kigoma na Maswa ziliimarishwa kwa kutandaza na kufunga bomba mpya au kukarabati zilizoharibika. Matangi ya kuhifadhi maji yalijengwa katika miji ya Mbeya, Iringa, Mwanza, Moshi, Kigoma na Musoma.

3. Pamoja na juhudi zilizofanywa katika kutekeleza miradi na shughuli mbali mbali zinazoambatana na utoaji huduma za maji, sehemu nyingi mijini na vijijini ziliendelea kukabiliwa na tatizo la upungufu wa maji. Hii ilitokana na uchakavu wa mitambo, upungufu wa umeme au mafuta ya kuendeshea mitambo ya maji, ukosefu wa vipuri, upungufu wa wataalamu wa maji na wakati mwingine, kukauka kwa baadhi ya vyanzo vya maji.

**Nishati:**

4. Sekta ya nishati iliendelea kuhudumia sekta mbali mbali za kiuchumi na kijamii. Vyanzo vikuu vya nishati viliendelea kuwa mafuta na umeme. Utafiti kuhusu vyanzo vipya vya nishati vinavyojadidika (new and renewable source of energy) uliendelezwa.

**Umeme:**

5. Tatizo la ukatikaji wa mara kwa mara wa umeme liliendelea kuwepo na lilisababishwa hasa na uchakavu wa mitambo ya umeme na nguvu ndogo ya umeme (low power/voltage) ikilinganishwa na matumizi.

6. Juhudi mbali mbali zilifanywa kupunguza tatizo hilo, zikiwa ni pamoja na kuendeleza ujenzi wa miradi mipya na ukarabati wa njia za kusambaza umeme. Kwa upande wa Dar es Salaam, maeneo yaliyohusishwa katika mpango huo ni Mikocheni, Kipawa Factory Zone III, Masaki na Sinza. Shughuli za ukarabati zilihusu pia mtambo wa umeme wa Kidatu ambao seti ya kwanza (set No. 1) ilikamilika na seti ya pili (set No. 2) inategemewa kufanyiwa matengenezo mara baada ya kuzinduliwa kwa jenereta la kwanza la mtambo wa Mtera. Ukarabati wa mtambo wa Hale ulikamilika na shughuli hizo zilianza kwa mtambo wa Nyumba ya Mungu.

7. Mradi wa utoaji umeme wa Mtera ambao unategemewa kuiongezea Gridi ya Taifa megawati 80 uliendelea kutekelezwa. Uwekaji wa jenereta ya kwanza yenye uwezo wa kutoa megawati 40 ulikamilika.

8. Utandazaji wa Gridi ya Taifa kuelekea kaskazini/magharibi ulifika Mwanza. Miji ya Singida na Shinyanga tayari inapata umeme wa gridi. Mji wa Mwanza utapatiwa umeme wa gridi pindi ujenzi wa kituo kidogo (substation) utakapokamilika. Ujenzi wa njia za umeme za Mwanza/Musoma na Shinyanga/Tabora za Kilovoti 132 uliendelea kutekelezwa na misingi ya kuwekea nguzo za umeme ilijengwa nusu ya njia hizo.

9. Mradi wa Uwemba/Mbinga wenye madhumuni ya kutoa umeme kwa ajili ya miji hiyo pamoja na mashamba ya karibu uliendelea kutekelezwa. Mashine ya kwanza ya kituo cha Uwemba ilifungwa.

10. Utekelezaji wa mradi wa upelekaji umeme mashambani na viwandani katika mikoa ya Shinyanga, Mwanza, Mbeya na Iringa haukuweza kuanza kutokana na kukosa wafadhili. Hata hivyo, serikali za Italia na Hispania na pia mashirika ya European Investment Bank na British Overseas Development Agency yalionyesha nia ya kusaidia utekelezaji.

**Mafuta na Gesi:**

11. Katika kipindi cha 1987/88, shughuli za utafutaji wa mafuta ziliendelea kufanywa na Shirika la Mafuta la Tanzania (Tanzania Petroleum Development Corporation) na pia Mashirika ya Nje. Mashirika ya TPDC na Petro Canada International Assistance Corporation yalifanya utafiti sehemu za Bigwa, Ras Winde na Kisiwa cha Pemba. AMOCO Tanzania Oil Company Ltd ilikamilisha tafsiri ya takwimu za aina ya miamba ya Bonde la Rukwa na Usangu na kugundua kuwa miamba hiyo ni myembamba na kwa hiyo haina mafuta yanayoweza kuchimbwa kibiashara (commercially).

12. Ujenzi wa kiwanda kidogo cha ndege Songo Songo ulikamilika na uligharimu Sh. 35 milioni.

# UWEZO WA MITAMBO YA UMEME

Jedwali Na. 63 (Megawati)

| Sehemu | 1982 | 1983 | 1984 | 1985 | 1986 | 1987 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| PWANI | 300·140 | 300·141 | 300·141 | 300·141 | 300·141 | 300·141 |
| Kidatu (Morogoro) | 200·000 | 200·000 | 200·000 | 200·000 | 200·000 | 200·000 |
| Pangani Falls (Tanga) | 17·500 | 17·500 | 17·500 | 17·500 | 17·500 | 17·500 |
| Hale (Tanga) | 21·000 | 21·000 | 21·000 | 21·000 | 21·000 | 21·000 |
| Dar es Salaam | 61·640 | 61·641 | 61·641 | 61·641 | 61·641 | 61·641 |
| ARUSHA/MOSHI | 13·660 | 13·384 | 13·385 | 13·385 | 13·385 | 13·385 |
| Arusha Thermal (Arusha) | 3·175 | 3·175 | 3·175 | 3·175 | 3·700 | 3·700 |
| Babati (Arusha) | 0·525 | 0·525 | 0·525 | 0·525 | 0·525 | 0·525 |
| Moshi Thermal (Moshi) | 0·800 | 0·524 | 0·525 | 0·525 | 0 | 0 |
| Kikuletwa (Moshi) | 1·160 | 1·160 | 1·160 | 1·160 | 1·160 | 1·160 |
| Nyumba ya Mungu (Moshi) | 8·000 | 8·000 | 8·000 | 8·000 | 8·000 | 8·000 |
| MATAWI MENGINE | 72·113 | 78·538 | 78·613 | 82·245 | 87·185 | 87·185 |
| Bukoba | 1·36 | 1·360 | 1·360 | 2·500 | 2·500 | 2·500 |
| Chamwino | 0 | 0·386 | 0·386 | 0·598 | ·668 | ·668 |
| Dodoma | 4·210 | 4·210 | 4·210 | 4·210 | 5·140 | 5·140 |
| Iringa/Tosamaganga | 1·970 | 1·970 | 1·970 | 1·970 | 1·220 | 1·220 |
| Kiabakari | 0 | 0·940 | 0·940 | 0·525 | 0·525 | 0·525 |
| Kigoma | 1·245 | 1·245 | 1·245 | 1·630 | 1·630 | 1·630 |
| Kilwa Masoko | 0 | 0·700 | 0·700 | 0·700 | 0·700 | 0·700 |
| Kondoa | 0 | 0·525 | 0·525 | 0·525 | 0·525 | 0·525 |
| Lindi | 0·360 | 0·360 | 0·360 | 0·180 | 0 | 0 |
| Mafia | 0·780 | 0·780 | 0·780 | 0·780 | 0·780 | 0·780 |
| Mbeya/Mbalizi/Iyunga | 13·040 | 13·040 | 13·040 | 13·040 | 13·900 | 13·900 |
| Mpwapwa | 0·415 | 0·415 | 0·415 | 0·330 | 1·120 | 1·120 |
| Mtwara | 5·415 | 5·415 | 5·415 | 4·338 | 4·400 | 4·400 |
| Musoma | 7·350 | 7·350 | 7·350 | 7·350 | 7·350 | 7·350 |
| Mwanza/Nyakato | 27·000 | 27·000 | 27·000 | 28·920 | 28·920 | 28·920 |
| Nachingwea | 0·850 | 0·950 | 0·950 | 0·950 | 0·960 | 0·960 |
| Njombe | 0 | 1·590 | 1·590 | 1·590 | 1·590 | 1·500 |
| Shinyanga | 1·660 | 1·660 | 1·660 | 1·660 | 1·660 | 2·100 |
| Singida | 0·690 | 1·985 | 1·985 | 1·280 | 1·790 | 1·790 |
| Songea | 1·235 | 1·160 | 1·235 | 1·235 | 2·563 | 2·563 |
| Sumbawanga | 0 | 0·580 | 0·580 | 1·350 | 1·520 | 1·520 |
| Tabora | 3·333 | 3·333 | 3·333 | 5·000 | 5·100 | 5·000 |
| Tukuyu/Mwakaleli | 1·200 | 1·200 | 1·200 | 1·200 | 1·200 | 1·200 |
| Tunduma | 0 | 0·384 | 0·384 | 0·384 | ·384 | ·384 |
| Jumla | 385·913 | 392·463 | 392·139 | 395·77 | 400·711 | 400·711 |

*Chanzo.*—Tanzania Electric Supply Company

## UUZAJI WA NGUVU ZA UMEME

Jedwali Na. 64

(Saa za kilowati milioni)

| Sehemu | 1982 | 1983 | 1984 | 1985 | 1986 | 1987[1] |
|---|---|---|---|---|---|---|
| PWANI | 557·50 | 495·90 | 504·17 | 582·89 | 608·28 | 663·96 |
| Dar es Salaam | 441·27 | 361·10 | 364·86 | 431·71 | 415·11 | 446·29 |
| Tanga | 76·71 | 69·75 | 70·23 | 69·34 | 86·88 | 100·50 |
| Morogoro | 40·42 | 35·67 | 39·18 | 42·57 | 65·79 | 73·92 |
| Zanzibar | 29·10 | 29·39 | 29·90 | 39·27 | 41·59 | 43·25 |
| ARUSHA—MOSHI | 79·43 | 91·06 | 94.34 | 95·55 | 107·82 | 121·83 |
| Arusha/Baboti | 57·35 | 57·42 | 57·89 | 56·14 | 64·03 | 71·65 |
| Moshi | 22·08 | 33·64 | 36·45 | 39·41 | 43·79 | 50·18 |
| MATAWI MENGINE | 100·37 | 106·24 | 125·43 | 144·69 | 193·03 | 219·58 |
| Bukoba | 3·65 | 2·66 | 3·13 | 4·83 | 3·61 | 3·86 |
| Dodoma/Chamwino | 10·01 | 10·18 | 10·19 | 14·38 | 13·38 | 14·82 |
| Iringa/Njombe | 6·29 | 5·49 | 8·79 | 19·14 | 63·56 | 66·23 |
| Kigoma | 4·15 | 2·50 | 3·82 | 4·02 | 4·86 | 5·22 |
| Kilwa/Masoko | ·00 | ·12 | ·20 | ·22 | 2.5 | 0·28 |
| Lindi | ·83 | 1·36 | 2·04 | 1·52 | 1·94 | 2·28 |
| Mafia | ·49 | ·74 | ·79 | ·61 | ·77 | 0·83 |
| Mbeya/Tunduma | 8·25 | 16·44 | 21·10 | 22·92 | 26·17 | 30·27 |
| Mpwapwa | ·53 | ·31 | ·77 | ·35 | ·33 | 1·62 |
| Mtwara | 3·73 | 3·34 | 4·26 | 4·40 | 5·22 | 5·75 |
| Musoma | 13·75 | 15·84 | 12·55 | 9·27 | 11·68 | 16·77 |
| Mwanza | 30·12 | 29·46 | 31·18 | 38·29 | 31·70 | 37·91 |
| Nachingwea | ·96 | ·49 | ·63 | ·77 | ·48 | 0·53 |
| Shinyanga | 5·07 | 4·87 | 6·30 | 6·02 | 7·14 | 8·19 |
| Singida | 1·14 | 1·33 | 2·16 | 1·57 | 3·08 | 3.40 |
| Songea | 1·87 | 1·84 | 2·18 | 1·79 | 1·65 | 1·79 |
| Sumbawanga | ·00 | 1·23 | 1·36 | 2·26 | 1·92 | 2·22 |
| Tabora | 4·14 | 5·25 | 9·21 | 8·98 | 11·39 | 13·23 |
| Tukuyu | 5·42 | 2·80 | 4·79 | 3·35 | 3·90 | 4·38 |
| Jumla | 737·30 | 693·20 | 723·93 | 823·13 | 909·13 | 1,005·37 |

*Chanzo*:—Tanzania Electric Supply Company.
([1]) Za Muda.

## UUZAJI WA UMEME KWA WATUMIAJI MBALI MBALI

Jedwali Na. 65 — Saa za Kilowati milioni

| Mwaka | Nyumba | Biashara | Viwanda | Mitoani | Zanzibar | Jumla | Matumizi ya Mitambo na nguvu zilizopotea | Jumla uliyotengenezwa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1971 | 64 | 49 | 255 | 4 | 0 | 372 | 54 | 426 |
| 1972 | 68 | 51 | 281 | 4 | 0 | 404 | 68 | 472 |
| 1973 | 74 | 53 | 300 | 4 | 0 | 431 | 85 | 516 |
| 1974 | 75 | 57 | 322 | 5 | 0 | 459 | 77 | 536 |
| 1975 | 86 | 56 | 339 | 5 | 0 | 486 | 72 | 558 |
| 1976 | 86 | 57 | 342 | 5 | 0 | 490 | 99 | 589 |
| 1977 | 93 | 60 | 358 | 5 | 0 | 516 | 103 | 619 |
| 1978 | 112 | 64 | 406 | 6 | 0 | 528 | 95 | 683 |
| 1979 | 131 | 76 | 442 | 4 | 0 | 653 | 100 | 753 |
| 1980 | 157 | 156 | 419 | 6 | 0 | 738 | 59 | 797 |
| 1981 | 168 | 152 | 425 | 6 | 39 | 790 | 33 | 823 |
| 1982 | 178 | 140 | 386 | 4 | 29 | 737 | 93 | 830 |
| 1983 | 175 | 130 | 355 | 4 | 9 | 693 | 163 | 856 |
| 1984 | 187 | 141 | 362 | 4 | 30 | 724 | 200 | 924 |
| 1985 | 198 | 137 | 444 | 5 | 39 | 823 | 229 | 1,052 |
| 1986 | 234 | 227 | 402 | 4 | 42 | 909 | 237 | 1,146 |
| 1987 (1) | 258 | 251 | 448 | 5 | 43 | 1,005 | 262 | 1,267 |

*Chanzo:* Tanzania Electric Supply Company.

(1): Ya muda.

# 9. ELIMU

1. Kipindi cha 1987 kilishuhudia kupanuka kwa elimu katika ngazi zote kama Jedwali namba 68 linavyoonyesha. Hata hivyo, juhudi za kuimarisha elimu inayotolewa ziliendelea kupata mafanikio hafifu kwani ongezeko la wanafunzi liliendelea kuwa kubwa kuliko uwezo wa Taifa wa kuongeza mahitaji mbali mbali muhimu kwa elimu kama vile madarasa, vitabu na walimu wenye ujuzi.

**Elimu ya Msingi:**

2. Elimu ya msingi imeendelea kupanuliwa na kuongezeka ijapokuwa kwa kiwango kidogo ikilinganishwa na mwaka uliopita. Maongezeko ya idadi ya shule za msingi za serikali na idadi ya vijana walioandikishwa kuanza darasa la kwanza yalikuwa madogo ikilinganishwa na 1986. Idadi ya vijana waliomaliza darasa la saba na jumla ya wanafunzi wote waliokuwamo katika shule hizo iliendelea kushuka ikilinganishwa na miaka iliyopita japokuwa pia kwa kiwango kidogo. Hali hii inathibitisha tatizo linalozikabili haadhi ya shule la kushindwa kupata idadi ya kutosha ya wanafunzi katika madarasa mbali mbali.

3. Wakati gharama za elimu ya msingi zimeendelea kupanda wastani wa matumizi ya kawaida kwa kila mwanafunzi wa shule za msingi umeendelea kushuka na kuwa chini ya theluthi moja ya mahitaji halisi. Hii ina maana ya upungufu mkubwa zaidi wa vifaa vya elimu ambavyo mwanafunzi anahitaji. Kwa hali hii uimarishaji wa elimu ya msingi bado umeendelea kuwa suala muhimu na gumu.

**Elimu ya Sekondari:**

4. Elimu ya Sekondari imeendelea kupanuka na kuongezeka pia katika mwaka 1987 ikilinganishwa na mwaka uliopita. Idadi ya shule za serikali, wanafunzi walioingia kidato cha kwanza na wale waliomaliza kidato cha nne na cha sita vyote vinaonyesha vimeongezeka katika mwaka 1987 ikilinganishwa na mwaka uliopita. Ongezeko la nafasi za elimu ya sekondari katika shule za serikali limetokana hasa na mpango ulioanza kutekelezwa miaka michache iliyopita unaotilia mkazo uanzishaji wa shule na madarasa ya kutwa ambao umebainika kuwa ni wa gharama nafuu.

5. Ijapokuwa takwimu za mwaka 1987 kuhusu elimu ya sekondari inayotolewa na sekta ya watu binafsi hazikuweza kupatikana, hapana shaka kwamba idadi ya shule za sekondari za binafsi na idadi ya wanafunzi katika shule hizo imekuwa ikiongezeka. Kwa kuzingatia wastani wa ongezeko la wanafunzi la asilimia 7.34 katika shule za sekondari za binafsi kwa kipindi cha 1978—86, idadi ya wanafunzi katika shule hizo huenda ilifikia wanafunzi 13.552 katika mwaka 1987. Katika

kipindi hicho hicho, nafasi za kidato cha kwanza katika shule za serikali zilikuwa zikiongezeka kwa wastani wa asilimia 3.55. Kwa misingi hiyo, ni dhahiri kwamba sekta ya binafsi katika elimu ya sekondari iliendelea kuongezeka kwa haraka kuliko sekta ya umma.

**Elimu ya Ualimu:**

6. Idadi ya vyuo vya ualimu kwa ngazi zote iliongezeka toka vyuo 39 mwaka 1986 na kufikia 40 mwaka 1987. Hata hivyo idadi ya wanafunzi katika vyuo hivyo ilishuka kutoka wanafunzi 12,409 mwaka 1986 hadi kufikia wanafunzi 11,667 mwaka 1987. Hali hii ni dalili ya kuongezeka kwa tatizo la upungufu wa walimu.

**Elimu ya Ufundi:**

7. Idadi ya vyuo vya Ufundi imeendelea kubakia vitatu (Dar es Salaam, Arusha na Mbeya). Hata hivyo idadi ya wanafunzi katika vyuo hivyo imeongezeka kutoka wanafunzi 1,550 mwaka 1986 hadi kufikia 1,675 mwaka 1987 baada ya Chuo cha Mbeya kuanza kuchukua wanafunzi hapo mwezi Julai 1986. Aidha idadi ya shule za sekondari za Ufundi iliendelea kuwa ile ile (5), ikiwa ni pamoja na shule ya Mazengo ambayo ilikamilika kubadilishwa na kuwa shule ya ufundi hapo mwaka 1986.

**Elimu ya Juu:**

8. Idadi ya wanafunzi Watanzania walioko katika mwaka wa kwanza wa masomo iliongezeka kwa wanafunzi 21 tu yaani toka wanafunzi 1,093 (1986) hadi wanafunzi 1,114 (1987) katika vyuo vikuu vya Dar es Salaam na Sokoine. Aidha jumla ya wanafunzi wote waliomo katika vyuo hivyo iliongeza kidogo na kufikia 3,373 mwaka 1987 baada ya kushuka toka wanafunzi 3,412 (1985) hadi wanafunzi 3,342 mwaka 1986. Elimu ya juu pia iliendelea kutolewa kwa Watanzania katika vyuo vingine vikiwemo Chuo cha Uongozi wa Maendeleo Mzumbe na Chuo cha Usimamizi wa Fedha Dar es Salaam.

## SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI: IDADI YA WANAFUNZI KWA VIDATO

Jedwali Na. 66

(Namba)

| Mwaku | I | II | III | IV | V | VI | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1978 | 8,797 | 9,790 | 9,702 | 9,582 | 1,902 | 2,018 | 41,792 |
| 1979 | 8,772 | 8,813 | 9,493 | 9,758 | 1,741 | 1,723 | 40,298 |
| 1980 | 8,847 | 8,612 | 8,645 | 9,320 | 1,761 | 1,645 | 38,830 |
| 1981 | 8,886 | 8,840 | 8,541 | 8,481 | 1,804 | 1,740 | 38,292 |
| 1982 | 9,116 | 8,842 | 8,763 | 8,352 | 2,121 | 1,788 | 38,983 |
| 1983 | 9,285 | 9,045 | 8,712 | 8,513 | 2,068 | 2,114 | 39,737 |
| 1984 | 9,696 | 9,187 | 8,856 | 8,531 | 2,215 | 2,132 | 40,617 |
| 1985 | 10,06[illegible] | 9,785 | 9,133 | 8,755 | 2,134 | 2,116 | 41,963 |
| 1986 | 10,789 | 9,855 | 9,401 | 8,679 | 2,363 | 2,276 | 43,36[illegible] |
| 1987 | 11,626 | 10,870 | 9,528 | 9,162 | 2,313 | 2,322 | 45,821 |
| Ongezeko % 1978—87 | 3·55 | 1·32 | −·23 | −·56 | 2·48 | 1·77 | 1·16 |

*Chanzo:* Wizara ya Elimu.

## SHULE ZA SEKONDARI ZA BINAFSI: IDADI YA WANAFUNZI KWA VIDATO

Jedwali Na. 66A

| Mwaka | I | II | III | IV | V | VI | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1978 | 7.165 | 6,294 | 5,108 | 3,523 | 170 | 140 | 22,400 |
| 1979 | 8.467 | 7,952 | 6,285 | 4.882 | 213 | 204 | 28,003 |
| 1980 | 6,677 | 8.482 | 7,107 | 5,917 | 126 | 153 | 28,465 |
| 1981 | 7,095 | 6.903 | 8,055 | 7,025 | 99 | 133 | 29,330 |
| 1982 | 7,988 | 7.161 | 7,139 | 7,482 | 261 | 140 | 30,162 |
| 1983 | 8.469 | 8,214 | 7.476 | 6,850 | 268 | 205 | 31,482 |
| 1984 | 9,079 | 8,866 | 8,142 | 6,724 | 475 | 305 | 33,591 |
| 1985 | 10,997 | 10.560 | 9,665 | 8,445 | 629 | 479 | 40,775 |
| 1986 | 12,625 | 12,389+ | 11,895+ | 10,073 | 730 | 567 | 48,279 |
| Ongezeko % 1978--86 | 7·34 | 8·83 | 11·14 | 14·03 | 19·98 | 19·11 | 10·08 |

+ : Makisio

*Chanzo:* Wizara ya Elimu

## WANAFUNZI WA TANZANIA KATIKA VYUO VIKUU VYA D'SALAAM NA SOKOINE

Jedwali Na. 67 (Namba)

| Idara | Miaka Yote 1984/85 | Miaka Yote 1985/86 | Miaka Yote 1986/87 | Miaka Yote 1987/88 | Mwaka wa Kwanza 1984/85 | Mwaka wa Kwanza 1985/86 | Mwaka wa Kwanza 1986/87 | Mwaka wa Kwanza 1987/88 | Mwaka wa Mwisho 1984/85 | Mwaka wa Mwisho 1985/86 | Mwaka wa Mwisho 1986/87 | Mwaka wa Mwisho 1987/88 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kilimo+ | 247 | 280 | 305 | 311 | 96 | 106 | 115 | 139 | 65 | 87 | 88 | 111 |
| Uganga wa Mifugo+ | 70 | 70 | 71 | 72 | 18 | 19 | 22 | 28 | 15 | 17 | 18 | 13 |
| Misitu | 67 | 73 | 66 | 70 | 21 | 27 | 22 | 29 | 20 | 25 | 21 | |
| Sayansi | 382 | 445 | 440 | 356 | 176 | 200 | 132 | 98 | 97 | 105 | 138 | 119 |
| Uhandisi | 643 | 634 | 616 | 657 | 180 | 179 | 188 | 191 | 139 | 153 | 121 | 119 |
| Utabibu | 201 | 216 | 214 | 204 | 53 | 49 | 60 | 54 | 32 | 47 | 46 | 27 |
| Madini | 49 | 54 | 52 | 47 | 19 | 24 | 15 | 13 | 16 | 12 | 16 | 21 |
| Madawa | 60 | 56 | 54 | 63 | 22 | 21 | 16 | 22 | 24 | 14 | 18 | 19 |
| Uganga wa meno | 50 | 48 | 42 | 41 | 7 | 13 | 13 | 11 | 12 | 8 | 12 | 10 |
| Biashara | 376 | 403 | 376 | 397 | 138 | 143 | 125 | 125 | 100 | 131 | 106 | 126 |
| Sheria | 177 | 181 | 183 | 194 | 60 | 61 | 64 | 70 | 59 | 60 | 58 | 61 |
| Sayansi ya Jamii | 944 | 952 | 923 | 961 | 357 | 385 | 321 | 334 | 305 | 275 | 290 | 303 |
| Jumla | 3,266 | 3,412 | 3,342 | 3,373 | 1,147 | 1,227 | 1,093 | 1,114 | 884 | 934 | 932 | 952 |

*Chanzo.* Wizara ya Elimu/Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
+: Zipo Chuo Kikuu cha Sokoine tangu 1987/88.

## MUHTASARI WA TAKWIMU ZA ELIMU

(Numba)

| Maelezo | 1981 | 1982 | 1983 | 1984 | 1985 | 1986 | 1987 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **SHULE ZA MSINGI ZA SERIKALI:** | | | | | | | |
| Idadi ya Shule | 9,947 | 10,102 | 10,015 | 10,079 | 10,147 | 10,234 | 10,403 |
| Idadi ya Walimu (000) | 82 | 88 | 90 | 91 | 93 | 95 | — |
| Wanafunzi, Darasa la I (000) | 498 | 497 | 542 | 533 | 525 | 523 | 549 |
| Wanafunzi, Darasa la VII (000) | 356 | 420 | 641 | 628 | 423 | 391 | 389 |
| Wanafunzi, Wote (000) | 3,531 | 3,504 | 3,554 | 3,484 | 3,160 | 3,156 | 3,155 |
| **SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI:** | | | | | | | |
| Idadi ya Shule | 83 | 85 | 85 | 85 | 86 | 95 | 102 |
| Idadi ya Walimu | 2,105 | 2,208 | 2,213 | 2,478 | 2,766 | 2,972 | — |
| Wanafunzi, Kidato cha I | 8,886 | 9,116 | 9,285 | 9,696 | 10,060 | 10,789 | 11,626 |
| Wanafunzi, Kidato cha IV | 8,481 | 8,352 | 8,513 | 8,531 | 8,755 | 8,679 | 9,162 |
| Wanafunzi, Kidato cha V | 1,804 | 2,121 | 2,068 | 2,215 | 2,114 | 2,363 | 2,313 |
| Wanafunzi, Kidato cha VI | 1,740 | 1,788 | 2,114 | 2,132 | 2,116 | 2,276 | 2,322 |
| Wanafunzi, Vidato Vyote | 38,292 | 38,983 | 39,737 | 40,617 | 41,963 | 43,363 | 45,821 |
| **ELIMU UFUNDI:** | | | | | | | |
| Idadi ya Vyuo | 2 | 2 | 2 | 2 | 2 | 3 | 3 |
| Idadi ya Walimu | 163 | 119 | 169 | 195 | 197 | 229 | 244 |
| Idadi ya Wanafunzi | 1,366 | 1,398 | 1,428 | 1,470 | 1,454 | 1,550 | 1,675 |
| **ELIMU YA WALIMU:** | | | | | | | |
| Idadi ya Vyuo | 36 | 37 | 38 | 38 | 39 | 39 | 40 |
| Idadi ya Walimu | 581 | 627 | 645 | 951 | 934 | 1,048 | 1,023 |
| Idadi ya Wanafunzi | 7,449 | 8,281 | 9,404 | 9,255 | 12,311 | 12,419 | 11,667 |
| **VYUO VIKUU NCHINI:** | | | | | | | |
| Wanafunzi wa Tanzania | | | | | | | |
| Mwaka wa Kwanza | 427 | 1,057 | 1,051 | 1,147 | 1,227 | 1,093 | 1,114 |
| Mwaka wa Mwisho | 745 | 776 | 787 | 884 | 934 | 932 | 952 |
| Miaka yote, Jumla | 2,688 | 2,911 | 3,057 | 3,266 | 3,412 | 3,342 | 3,373 |

*Chanzo*.—Wizara ya Elimu.

—Hazikupatikana.

## 10.—AFYA

**Huduma za Kinga:**

1. Huduma za kinga ziliendelea kupewa umuhimu wa juu katika mwaka 1987. Juhudi zaidi zilielekezwa kwenye mbinu za kupambana na magonjwa ya kuambukiza kama vile malaria, maradhi ya kuhara na kuhara damu. Uzuiaji wa magonjwa mengine yakiwemo tauni, kichocho na malale ulipewa umuhimu pia. Aidha, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii iliendesha kampeni za kuwaelimisha wananchi juu ya kujikinga na ugonjwa unaoharibu kinga za mwili dhidi ya maradhi (UKIMWI).

2. Huduma za afya kwa akina mama na watoto chini ya miaka mitano ziliendelea kutolewa kwenye jumla ya kliniki 3,056. Kliniki 2,413 miongoni mwake ziliendesha pia huduma za mpango wa chanjo kwa akina mama wajawazito na watoto dhidi ya surua, dondakoo, polio, pepopunda, kifaduro na kifua kikuu. Asilimia 65 ya watoto wanaostahili kupata huduma hizi waliishazipata hadi mwisho wa mwaka 1987. Lengo lilikuwa ni kufikia asilimia 70. Mbinu mbali mbali zimetumika ili kufanikisha mpango wa chanjo zikiwa ni pamoja na kusisitiza miongozo ya utekelezaji, kusambaza vifaa na dawa za chanjo mikoani/wilayani na kufanya tathmini ya utekelezaji mara kwa mara. Hata hivyo, uhaba wa mafuta ya taa kwa ajili ya kuendeshea majokofu na vile vile uhaba wa vifaa vya usafiri vimeathiri utekelezaji wa mpango huo kwa kiasi fulani.

**Huduma za Tiba:**

3. Uimarishaji wa huduma za tiba uliendelea kupewa mkazo mkubwa zaidi badala ya upanuzi. Matengenezo yaliendelea kufanywa kwa hospitali za Muhimbili, Kibong'oto, Mirembe na Mbeya na kwa baadhi ya vituo vya afya. Mradi wa madawa muhimu (Essential Drugs Programme), uliendelezwa pia kwa msaada wa wafadhili kutoka nje.

4. Matumizi ya vyombo vya afya yaani hospitali, zahanati, na vituo vya afya yameendelea kukua katika mwaka 1987. Kwa wastani, kila hospitali ilihudumia wagonjwa 368,612 mwaka 1987 kwa kulinganisha na wagonjwa 349,230 mwaka 1986. Kwa upande wa zahanati na vituo vya afya, wastani wa huduma ilikuwa ni wagonjwa 25,544 (zahanati) na 84,150 (Vituo vya afya) kwa kulinganisha na mwaka 1986 ambapo zahanati zilihudumia wastani wa wagonjwa 24,752 na vituo vya afya wagonjwa 78,020. Ongezeko la idadi ya watu wanaofika kwenye hospitali, zahanati na vituo vya afya ni matokeo ya mambo mbali mbali yakiwemo kuongezeka na kuenea kwa magonjwa mbali mbali, mwamko wa wananchi kuhusu huduma za tiba zinazotolewa na vyombo vya afya na pia ongezeko la idadi ya watu ambalo linakadiriwa kuwa asilimia 3·3 kwa mwaka.

**Utafiti, Mafunzo na Wafanyakazi:**

5. Utafiti juu ya maradhiya binadamu, lishe na chakula bora ulifanywa na mashirika yaliyo chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, yaani Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binaadamu na Shirika la Chakula na Lishe. Mafunzo mafupi kuhusu nyanja mbali mbali za afya zikiwemo huduma za meno na pia huduma za magonjwa ya akili zilitolewa.

6. Wataalamu mbali mbali (madaktari, madaktari wasaidizi, matabibu n.k.) wapatao 2.409 walifuzu mafunzo yao mwaka 1987 kwa kulinganisha na wataalamu 2,187 waliofuzu mwaka 1986. Idadi ya wafanyakazi wa afya wazalendo ilifikia 32.496 mwaka 1987 kwa kulinganisha na 31.003 mwaka 1986. Uwiano wa idadi ya watu na wafanyakazi wa afya unaonyesha kuwa kwa wastani, mfanyakazi mmoja alihudumia watu 692 mwaka 1987 ambapo katika mwaka 1986, uwiano huo ulikuwa mfanyakazi mmoja kwa watu 706.

Takwimu kuhusu Afya zimetolewwa katika majedwali 69—72.

## VYOMBO VYA AFYA NCHINI

Jedwali Na. 69

| Mwaka | Hospitali | | Zahanati[3] | | Vituo vya Afya Vijijini | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Idadi[1] | Vitanda[2] | Idadi | Vitanda | Idadi | Vitanda |
| 1975 | 147 | 19,400 | 1,766 | 8,485 | 138 | 3,386 |
| 1976 | 147 | 19,680 | 1,847 | 8,546 | 162 | 3,788 |
| 1977 | 148 | 19,823 | 1,997 | 8,646 | 181 | 3,988 |
| 1978 | 148 | 20,847 | 2,205 | 8,900 | 202 | 4,230 |
| 1979 | 149 | 21,291 | 2,568 | 9,165 | 235 | 4,620 |
| 1980 | 149 | 21,201 | 2,600 | 9,329 | 239 | 4,676 |
| 1981 | 149 | 21,352 | 2,644 | 9,386 | 239 | 4,676 |
| 1982 | 149 | 22,350 | 2,644 | 9,395 | 239 | 4,689 |
| 1983 | 149 | 22,350 | 2,644 | 9,395 | 239 | 4,689 |
| 1984 | 152 | 22,800 | 2,644 | 9,395 | 239 | 4,689 |
| 1985 | 152 | 22,800 | 2,831 | 11,320 | 260 | 5,122 |
| 1986 | 152 | 22,800 | 2,831 | 11,320 | 260 | 5,122 |
| 1987 | 152 | 22,800 | 2,831 | 11,320 | 260 | 5,122 |

*Chanzo:*—Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

(1) Ni pamoja na Hospitali za Magonjwa Maalum.

(2) Ukiondoa Vitanda vya Hospitali za Magonjwa Maalum.

(3) Ukiondoa Zahanati za Mashirika ya Umma na Binafsi.

WALIOFAULU MAFUNZO

Jedwali Na. 70

(Namba)

| Aina ya Mafunzo | 1977/78 | 1978/79 | 1979/80 | 1980/81 | 1981/82 | 1982/83 | 1983/84 | 1984/85 | 1985/86 | 1986/87 | 1987/88 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Madaktari Watanzania (a) | 47 | 54 | 40 | 40 | 34 | 56 | 48 | 44 | 55 | 82 | 96 |
| Madaktari Wasaidizi ...... | 35 | 7 | 32 | 22 | 37 | 31 | 45 | 46 | 35 | — | 46 |
| Watabibu (Medical Assista-nts) ...................... | 171 | 136 | 250 | 190 | 210 | 243 | 323 | 252 | 250 | 281 | 276 |
| Watabibu Wasaidizi Vijijini | 301 | 294 | 290 | 400 | 423 | 443 | 500 | 410 | 420 | 370 | 393 |
| Wauguzi Daraja "A" ...... | 105 | 148 | 200 | 126 | 140 | 150 | 345 | 159 | 141 | 123 | 135 |
| Wauguzi Daraja "B" ...... | 383 | 410 | 520 | 439 | 429 | 410 | 418 | 498 | 493 | 581 | 610 |
| Wauguzi Wakunga (MCHA) .................... | 330 | 354 | 512 | 420 | 417 | 491 | 441 | 104 | 363 | 538 | 413 |
| Mabwana Afya ............ | 25 | 22 | 17 | 40 | 53 | 43 | 44 | 41 | 75 | 55 | 262 |
| Mabwana Afya Wasaidizi | 45 | 45 | 102 | 90 | 120 | 143 | 190 | 139 | 140 | 157 | 178 |

*Chanzo:*—Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

(a) Waliokuwa katika mwaka wa mwisho wa masomo katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ni pamoja na Waganga wa Meno.

## MATUMIZI YA VYOMBO VYA AFYA: IDADI YA WAGONJWA

Jedwali Na. 71 ('000)

| Mwaka | Wagonjwu wa Nje | | | Waliolazwa | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Hospital | Zahanati | Vituo vya afya Vijijini | Hospital | Zahanati | Vituo vya afya vijijini |
| 1975 .......... | 28.500 | 49.576 | 8.155 | 710 | 139 | 179 |
| 1976 .......... | 29.700 | 52.800 | 10.235 | 785 | 143 | 215 |
| 1977 .......... | 31.480 | 54.000 | 11.860 | 843 | 150 | 225 |
| 1978 .......... | 32.500 | 59.000 | 12.500 | 900 | 165 | 260 |
| 1979 .......... | 33.700 | 59.850 | 12.870 | 920 | 175 | 265 |
| 1980 .......... | 33.768 | 60.628 | 12.973 | 922 | 178 | 275 |
| 1981 .......... | 35.254 | 62.645 | 13.115 | 925 | 180 | 279 |
| 1982 .......... | 38.779 | 63.909 | 14.427 | 927 | 183 | 285 |
| 1983.......... | 42.304 | 65.173 | 15.739 | 929 | 186 | 289 |
| 1984 .......... | 45.829 | 66.437 | 17.051 | 931 | 189 | 295 |
| 1985 .......... | 49.357 | 67.706 | 18.376 | 936 | 193 | 310 |
| 1986+ .......... | 52.121 | 69.873 | 19.938 | 962 | 199 | 327 |
| 1987+ .......... | 55.040 | 72.109 | 21.633 | 989 | 206 | 346 |

*Chanzo:* Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.
+: Makisio.

## IDADI YA WAFANYAKAZI WA AFYA

Jedwali Na 72 | Nambo

| Aina ya Wafanyakazi | 1976 | 1977 | 1978 | 1979 | 1980 | 1981 | 1982 | 1983 | 1984 | 1985 | 1986 | 1987 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Madaktari (b) | 683 | 727 | 769 | 830 | 889 | 950 | 1,015 | 1,065 | 1,115 | 1,160 | 1,000 | 1,053 |
| --ambapo wananchi | 356 | 400 | 442 | 503 | 566 | 599 | 732 | 782 | 820 | 865 | 846 | 899 |
| Madaktari Wasaidizi | 193 | 223 | 223 | 258 | 258 | 291 | 391 | 4,336 | 436 | 517 | 250 | 283 |
| Watabibu (Medical Assistants) | 770 | 930 | 1,061 | 1,235 | 1,400 | 1,589 | 1,808 | 2,131 | 2,383 | 2,633 | 2,857 | 3,192 |
| Waganga Wasaidizi Vijijini (RMAs) | 1,049 | 1,393 | 1,690 | 2,100 | 2,310 | 2,691 | 3,691 | 4,191 | 4,601 | 9,021 | 9,391 | 9,780 |
| Mabwana Afya | 156 | 170 | 176 | 186 | 222 | 270 | 309 | 353 | 394 | 535 | 570 | 604 |
| Mabwana Afya Wasaidizi | 455 | 500 | 545 | 585 | 681 | 789 | 918 | 1,108 | 1,247 | 1,740 | 1,880 | 2,016 |
| Wakunga/Wauguzi Daraja "A" | 1,100 | 1,255 | 1,340 | 1,465 | 1,591 | 1,717 | 1,852 | 2,197 | 2,356 | 2,721 | 2,871 | 3,021 |
| Wakunga/Wauguzi Daraja "B" | 3,720 | 4,423 | 4,750 | 5,250 | 5,684 | 6,070 | 6,439 | 6,857 | 7,242 | 7,430 | 7,620 | 7,810 |
| Wakunga Vijijini | 960 | 1,400 | 1,190 | 1,650 | 2,070 | 2,070 | 2,887 | 3,328 | 3,432 | 3,572 | 3,872 | 3,992 |

*Chanzo:* Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.
(b): Ni pamoja na Waganga wa Meno.

## 11. KAZI NA USTAWI WA JAMII

**Idara ya Kazi:**

1. Katika mwaka 1987 Idara ya Kazi iliendelea na jukumu la kusimamia sheria mbali mbali za kazi ili kufanikisha ufanisi na tija kwa mujibu wa sera ya Taifa ya Tija. Mapato na Bei. Idara ilifanya ukaguzi sehemu mbali mbali nchini ili kudhibiti utekelezaji wa Kima cha Chini cha Mishahara, mikataba ya kazi, ulipaji wa bonasi hali ya nyumba na mazingira ya kazi kwa jumla. Migogoro ya kazi iliendelea kushughulikiwa na Mahakama ya Kazi, na jumla ya Sh. 12,650,700 zililipwa kama fidia kutokana na ajali kwa watumishi wakiwa kazini.

2. Ili kuhakikisha viwanda vinajengwa kufuata matakwa ya sheria, ramani 52 zilipelekwa na kuchunguzwa. Kati ya hizo, 40 zilikubaliwa na 12 zilikataliwa kwa kuwa zilihitaji marekebisho. Pia wakaguzi wa viwanda walitembelea sehemu za ujenzi (construction sites) zipatazo 225 ili kutoa ushauri.

3. Zaidi ya kaguzi hizo maalum katika sehemu za ujenzi, bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara zilitembelewa pia na zana za kunyanyulia mizigo (lifting devices) zilikaguliwa. Jumla ya zana 297 zilikaguliwa na serikali iliingiza kiasi cha Sh. 47,865 zikiwa ada za ukaguzi kwa mujibu wa Sheria ya Viwanda.

4. Kaguzi za zana (plant inspection) mbali mbali zitumikazo viwandani zilifanyika kama ifuatavyo:—

| | |
|---|---|
| Steam Boilers ........................................ | 355 |
| Air Receivers ........................................ | 1,006 |
| Steam Receivers ........................................ | 111 |
| Lifts, chain blocks, cranes and Other lifting equipment ........................................ | 316 |
| Jumla ... | 1,788 |

5. Kaguzi hizi ziliingiza kiasi cha Sh. 205,800 kutokana na ada kwa mujibu wa Sheria ya Viwanda.

6. Idara ilifanya uchunguzi wa magonjwa yatokanayo na kazi (occupational diseases) na upimaji wa athari zinazoletwa na mazingira ya kazi (environmental monitoring), k.m. madini ya risasi, mavumbi katika viwanda vya nguo, asbestos, pamba n.k. Katika kutekeleza zoezi hili viwanda 64 vilitembelewa.

**Ajira:**

7. Katika mwaka 1987 Sheria ya Matumizi ya Nguvu Kazi iliendelea kutekelezwa kwa namna mbali mbali nchini. Juhudi kubwa ziliendelea kuelekezwa katika kilimo ingawa shughuli za viwanda vidogo zilitiliwa mkazo pia. Matatizo ya uhaba wa wataalam, fedha na nyenzo za kufanyia kazi yaliendelea kukabili utekelezaji wa Nguvu Kazi.

8. Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Utumishi iliendelea kuratibu utekelezaji wa miradi iliyobuniwa kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (ILO) huko Mela—Morogoro, Kihuhwi—Tanga, Tanga Munispaa, Moshi, Arusha na Madale—Dar es Salaam. Miradi hii ilitengewa Sh. 15 milioni katika mwaka wa fedha 1987/88 na inaendelea vizuri.

9. Katika jitihada za kutatua tatizo la ukosefu wa ajira vijijini na mijini na pia ajira ya akina mama, Idara ya Kazi imetekeleza mradi wa utafiti na takwimu za ajira wenye lengo la kuandaa miradi ya ajira kwa ajili ya vijana wasio na kazi mijini na vijijini na vile vile akina mama ili waweze kujitegemea. Wataalam wa vyuo Vikuu wameajiriwa kuandika miradi ya wilaya 18 na TISCO wameajiriwa kuandika miradi ya wilaya 15. Aidha Wizara iliendelea kudhibiti ajira ya wageni nchini kwa kutoa vibali vya kazi kwa wataalam wale tu ambao hakuna wazalendo wenye ujuzi wa kufanya kazi hizo. Kwa msimamo huo, ni wageni 1986 ndio waliopewa vibali vya kazi katika mashirika ya umma na sekta binafsi.

**Uhusiano wa Kimataifa:**

10. Licha ya ushirikiano na Shirika la Kazi Duniani (ILO), ambao umeelezwa hapo juu, mkaguzi mmoja (1) alihudhuria mafunzo ya miezi 9 nchini Japani kuhusu mfumo wa mazingira (environmental physiology). Wanafunzi wengine 4 walihudhuria warsha mbali mbali Kenya, Mauritius, Sweden na Finland.

11. Katika mwaka 1986/87 Idara ya Mafunzo na Majaribio ya Ufundi iliendelea na jukumu lake la kusimamia vyuo vya mafunzo ya ufundi. Utoaji wa mitihani ya majaribio ya ufundi uliimarishwa; hii ikiwa ni pamoja na utayarishaji mitihani yenyewe, usimamizi na kuratibu uongozi wake.

12. Jumla ya watahiniwa waliojiandikisha ilikuwa 11,951 kwa fani 58 za mafunzo mbali mbali. Matokeo ya mitihani yalionyesha kuwa wastani wa kufaulu (average pass mark) kitaifa ni alama 39·8 kama ifuatavyo:—

## MUHTASARI WA MATOKEO YA MITIHANI

| Daraja | Idadiya Waliojiandikisha | Waliojitokeza kufanya mitihani | Walioachishwa | Waliofaulu | Kiwango Cha kufaulu |
|---|---|---|---|---|---|
| III ................ | 8,748 | 7,521 | 263 | 3,057 | 42·7% |
| II ................ | 3,584 | 3,061 | 102 | 994 | 33·6% |
| I ................ | 1,709 | 1,369 | 92 | 480 | 37·8% |
| Jumla ... | 14,041 | 11,951 | 557 | 4,531 | 39·8% |

Kufikia mwishoni mwa mwaka 1986/87 vyuo vya Mafunzo na Majaribio ya ufundi vilikuwa 12: Chang'ombe (Dar es Salaam), Tanga, Mwanza, Arusha, Moshi, Mara, Bukoba, Iringa, Dodoma, Songea, Lindi na Morogoro.

## HALI YA UTUMISHI NCHINI (UCHUNGUZI WA MWAKA 1985)

13. Uchunguzi wa hali ya utumishi nchini ulifanyika mara ya mwisho mwaka 1985. Uchunguzi huo mbali ya kuonyesha hali ya utumishi nchini kwa mwaka huo, matokeo yake vile vile yalitumika kutoa takwimu (data base) kwa ajili ya makadirio ya mahitaji ya wataalam katika kipindi cha 1988/89—1992/93).

14. Kama Jedwali A linavyoonyesha hadi kufikia mwaka 1987/88 lengo la kujitosheleza kwa wataalam wetu wenyewe lilifikia kiwango cha asilimia 91·2 ikilinganishwa na miaka ya nyuma. Nafasi zilizokuwa wazi kwa daraja A zilikuwa 3,644, daraja B, 20,398 na C, 20,749 ikilinganishwa na nafasi wazi 4,954, kwa daraja A, 12,114 daraja B na 35,502 daraja C kwa mwaka 1980. Pia, uajiri wa wataalam wananchi (localization) ulikuwa asilimia 99·68 mwaka 1987/88 kama inavyoonyeshwa katika Jedwali hiyo.

**Mchanganyo wa Wataalam (Skill mix):**

15. Hadi kufikia mwaka 1987 mchanganyo wa wastani wa utaalam (General skill mix) ulikuwa umefikia 1:6:11:15 kutoka 1:3:14:19 uliokuwepo mwaka 1980. Kwa kutafsiri na kuangalia Jedwali B ni wazi kwamba kwa jumla kumekuwa na ongezeko la ujuzi katika Taifa mwaka hadi mwaka. Kwa mfano, katika mwaka 1964 asilimia 9·6 ya watumishi walikuwa daraja la D, asilimia 6·0 walikuwa daraja C, asilimia 1·6 walikuwa daraja la B, na asilimia 0·8 tu walikuwa wa daraja A. Sura

ya mwaka 1987 inaonyesha mafanikio makubwa. Watumishi wa daraja A wameongezeka kufikia asilimia 3·05, wa daraja B wamefikia asilimia 17·29, wa daraja C wamefikia asilimia 33·4, na daraja D wamepungua hadi asilimia 46·2. Ongezeko kubwa kwa Daraja A, B, na C inaonyesha umuhimu na juhudi ambazo serikali imefanya katika azma ya kujitosheleza kwa wataalam wa kizalendo.

**Mahitaji ya Wataalam:**

16. Kama inavyoonekana katika jedwali C inakadiriwa kuwa ifikapo mwaka 1992/93 watahitajika wataalam wa daraja A (Sayansi) 13,495, wa daraja A (Sanaa) 17,202 wa daraja B 162,704 wa daraja C 294,714 na wa daraja D 403,504. Ili kukidhi mahitaji haya serikali inafanya juhudi za kufungua na kupanua mashule, vyuo, kupeleka wanafunzi nje ya nchi na pia kuhimiza mafunzo kazini (on the job training).

Jedwali A:

KIWANGO CHA KUJITOSHELEZA KIUTAALAM NA KUJITEGEMEA KIUTAALAM

| Mwaka | Daraja la | Ikama | Raia | Uajiri Wageni | Jumla | Nafasi wazi | % Raia katika Uajiri | % Raia katika Ikama |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | A | 3,236 | 503 | 2,298 | 2,801 | 435 | 18·0 | 15·5 |
| 1964 | B | 6.438 | 4.467 | 1,311 | 3,778 | 702 | 77·3 | 68·9 |
| | C | 23,788 | 12.595 | 8,315 | 20,910 | 2,878 | 60·2 | 52·4 |
| | A | 4,689 | 1,403 | 2,673 | 4,076 | 613 | 34·4 | 29·9 |
| 1968 | B | 11.611 | 8,797 | 2,146 | 10,943 | 668 | 80·4 | 78·8 |
| | C | 31,690 | 25,986 | 3,597 | 29,083 | 2,607 | 87·6 | 80·4 |
| | A | 11,356 | 5,888 | 1,918 | 7,806 | 3,550 | 75.4 | 51·8 |
| 1974 | B | 22.609 | 23,149 | 845 | 23,994 | 5.281 | 96·5 | 87·0 |
| | C | 106,837 | 90,036 | 3.329 | 93,365 | 10.806 | 96·4 | 84·3 |
| 1980 | A | 18,710 | 12,752 | 1,004 | 13,756 | 4.954 | 92·7 | 68·2 |
| | B | 55,697 | 43,298 | 290 | 43,583 | 12,114 | 99·3 | 77·7 |
| | C | 214,414 | 178,647 | 265 | 178,912 | 35,502 | 99.9 | 83·3 |
| | A | 27,075 | 22,087 | 1,344 | 23,431 | 3,644 | 94·3 | 81·1 |
| 1988 | B | 147,331 | 132,114 | 419 | 132,533 | 20,398 | 99·6 | 89·6 |
| | C | 282,375 | 255,726 | 300 | 256,026 | 20,749 | 99·8 | 90·5 |

*Chanzo:* Uchunguzi wa hali ya Utumishi 1964—1985.

Jedwali B:

## MCHANGANYO WA UTAALAM (SKILL MIX)

| Mwaka | A | B | C | D | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| 1964 ............... | 2.801 | 5,778 | 20,940 | 321.768 | 351,257 |
| | 0·8% | 1·6% | 6·0% | 91·6% | 100% |
| 1968 ............... | 4,076 | 10,943 | 29,083 | 307,608 | 351.710 |
| | 1·2% | 3·1% | 8·3% | 87·5% | 100% |
| 1974 ............... | 7.806 | 23.994 | 93,365 | 358,921 | 484,086 |
| | 1·6% | 5·0% | 19·3% | 74·1% | 100% |
| 1980 ............... | 13.759 | 43.583 | 178.912 | 366.939 | 603.193 |
| | 2·3% | 7·2% | 29.7% | 60·8% | 100% |
| 1988 ............... | 23.431 | 132,533 | 256026 | 354.349 | 766.339 |
| | 3·05% | 17·29% | 33·4% | 46·2% | 100% |

*Chanzo:* Idara ya Mipango. Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Watumishi

Jedwali C:

## MAKADIRIO YA MAHITAJI YA WATUMISHI 1987—1991

| Daraja la Kazi | Uajiri Mwaka 1987/1988 | | | | Ongezeko la Kazi* 1988–1993 | Jumla ya Mahitaji 1988–1993 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Raia | Wageni | Jumla | Nafasi wazi | | |
| A—Sayansi | 9,314 | 809 | 10.123 | 1.683 | 3.372 | 13.495 |
| A—Sanaa | 12,773 | 535 | 13.308 | 1,961 | 3.894 | 17,202 |
| Jumla—A | 22,987 | 1.344 | 23.431 | 3,644 | 7.266 | 30,697 |
| B | 132,114 | 419 | 132.533 | 20.398 | 31.171 | 163.704 |
| C | 255.726 | 300 | 256.026 | 20,749 | 39.164 | 294,714 |
| D | 354.035 | 314 | 354.349 | 26.231 | 49.469 | 403.504 |
| **Jumla** ... | 763,962 | 2.377 | 766.339 | 71.022 | 127.070 | 892.619 |

*Chanzo:* Idara ya Mipango ya Watumishi. Wizara ya Kazi na Maendeleo ya Utumishi.

*Ongezeko la kazi linajumuisha nafasi wazi. ongezeo litakalotokana na upanuzi. pamoja na idadi ya wataalam wa kigeni wanaopashwa kukabidhi kazi zao kwa raia.

**Huduma ya Majaribio na Ujenzi wa Tabia:**

17. Mwaka wa 1987 umeonyesha mahitaji zaidi ya huduma hizi ikilinganishwa na hali ilivyokuwa katika kipindi cha mwaka 1986. Maafisa Ustawi wa Jamii waliwahoji washtakiwa 5,689 kote nchini. Kati ya washtakiwa hao watu 606 walionekana wanahitaji majaribio Makosa yaliyoongoza mwaka 1987 ni wizi, mashambulio, kufanya biashara bila leseni, uzururuji pamoja na makosa mengine.

18: Mahabusu za watoto zilizopo Arusha, Dar es Salaam, Moshi na Mbeya ziliendelea kutoa huduma kwa watoto walioshtakiwa. Idadi inafafanuliwa hapa chini:—

| | |
|---|---|
| — Mahabusu mwanzoni mwa mwaka .......... | 177 |
| — Mahabusu wapya .................................. | 454 |
| — Mahabusu waliotoka ............................ | 534 |
| — Mahabusu waliotoroka ......................... | 15 |
| — Mahabusu waliobaki mwishoni ............... | 82 |

Idadi hii ni ndogo ukilinganisha na mahabusu wapya katika mwaka 1986 ambao walikuwa 829.

**Shule ya Maadilisho Iramba:**

19. Shughuli za kuadili watoto wenye tabia sugu ziliendelea katika shule ya Iramba. Watoto walioadiliwa ni kama ifuatavyo:—

| | |
|---|---|
| — Waadiliwa mwanzoni mwa mwaka .......... | 60 |
| — Waadiliwa wapya .................................. | 52 |
| — Waadiliwa waliorejeshwa utoroni ........... | 18 |
| — Jumla ya waadiliwa wote ...................... | 130 |
| — Waadiliwa waliomaliza muda wao ........... | 49 |
| — Waadiliwa waliotoroka ......................... | 12 |
| — Waadiliwa waliobaki mwishoni ............... | 69 |

20. Mwaka wa 1987 umeonyesha sura tofauti ukilinganisha na hali ilivyojitokeza mwaka uliotangulia:

(a) Kumekuwepo na ongezeko kidogo la waadiliwa walioingia shuleni. Mwaka 1986 waadiliwa wapya walikuwa 39.

(b) Utoro ulipungua sana ukilingamsha na hali ilivyokuwa mwaka 1986 ambapo waadiliwa 62 walitoroka.

(c) Idadi ya waadiliwa inaendelea kushuka. Hii haina maana kuwa idadi ya wanaohitaji huduma hizo inapungua. Watoto wengi wanahitaji huduma hii lakini hawaipati.

**Huduma za Marekebisho, Utengemeo na Matunzo kwa walemavu/ wasiojiweza:**

21. Huduma za malazi, chakula, mavazi na matibabu ziliendelea kutolewa kwa wakazi wanaotunzwa katika Makazi 43 ambayo 19 yanaendeshwa na Serikali na 24 yapo chini ya uongozi wa wakala za hiari.

(i) Usambazaji na utengamao kwa walemavu:

Walemavu 728 walisambazwa katika fani zifuatazo:—

| | |
|---|---|
| — Nafasi ya Useremala ............................ | 211 |
| — Nafasi ya Upigaji masbine ...................... | 52 |
| — Nafasi ya Ushonaji viatu ...................... | 71 |
| — Nafasi ya Ushonaji nguo/ufumaji ........... | 246 |
| — Nafasi ya Ufugaji/Kilimo ....................... | 120 |
| — Nafasi ya Uhunzi ................................ | 28 |
| Jumla ya waliosambazwa ... | 728 |

(ii) Utunzaji wa walemavu/wasiojiweza katika makazi:

| | |
|---|---|
| — Wakazi mwanzoni mwa mwaka ............... | 4,849 |
| — Wakazi wapya .................................... | 1,014 |
| — Wakazi waliorejesbwa/fariki/toroka ......... | 1,019 |
| — Wakazi waliobaki mwishoni mwa mwaka . | 4,834 |

22. Idadi ya wakazi wapya katika kipindi cha mwaka 1987 imepungua kidogo ukilinganisha na wale walioingia mwaka 1986 ambao idadi yao walikuwa 1,026. Wakazi waliotoka wameongezeka kidogo kuliko wale waliotoka mwaka 1986 ambao idadi yao ilikuwa 1,001. Pamoja na mabadiliko hayo, walemavu/wasiojiweza wengi bado wanahitaji huduma ya matunzo Serikalini.

(iii) Viwanda vidogo vidogo:

23. Viwanda vya Tujitegemee, Motomoto na Tuungane viliendelea na kazi zake za uzalishaji mali. Viwanda hivyo vilikuwa na Walemavu 38 walioendelea na uzalishaji mali.

(iv) Utoaji wa vifaa vya kujimudu na misaada mingine:

24. Maombi 1,249 yaliyohitaji vifaa vya kujimudu na misaada yalipokelewa katika ofisi ya Ustawi wa Jamii Mikoani na Wilayani. Vifaa vya kujimudu ni pamoja na baiskeli za miguu mitatu, vifaa vya kusikilizia, miguu ya bandia n.k. Misaada ni pamoja na nguo, chakula, matunzo, usafiri n.k. Waombaji 506 kati yao walitekelezewa maombi yao. Maombi

yaliyopokelewa mwaka 1987 ni machache ukilinganisha na yale yaliyopokelewa mwaka 1986 ambayo yalikuwa 1.203. Hata hivyo wale waliopewa misaada mwaka 1987 ni wachache ukilinganisha maombi yaliyopokelewa. Hii imetokana na kupungua kwa uwezo wa Taifa na pia kutokana na kuongezeka kwa bei za vifaa vinavyohitajika.

(v) Mafunzo kwa walemavu:

25. Vyuo vya Yombo (Dar es Salaam), Singida, Manoleo (Tabora) na Mtapika (Masasi) viliendelea kutoa mafunzo ya kujitegemea kwa walemavu 254. Vyuo viliendelea kukabiliwa na upungufu wa waalimu wa ufundi pamoja na uhaba wa nyenzo za kufundishia. Idara iliendelea na jitihada ya kukidhi mahitaji kila ilipowezekana ili kufanikisha lengo lililowekwa. Karakana ya walemavu Kinondoni, bado haikuweza kukamilika na ujenzi wa Karakana ya Mbeya umeanza.

**Huduma kwa Familia na Watoto:**

26. Wananchi waliendelea kupata huduma hizi kwa kiwango cha kuridhisha. Mwaka 1987 mashauri machache ya kifamilia yalipokelewa katika Ofisi za Ustawi wa Jamii kote nchini kwa - kulinganisha na yaliyopokelewa mwaka uliotangulia.

**Makao ya watoto wenye shida:**

27. Makao ya watoto wenye shida 32 yaliendelea kurunza watoto 1.533 kwa kipindi cha mwaka 1987. Mchanganuo wake ni kama ifuatavyo:—

| | |
|---|---|
| —Watoto mwanzoni mwa mwaka .............. | 1.000 |
| —Watoto wapya ........................................ | 533 |
| — Watoto waliotoka/achiliwa/chukuliwa na Jamaa zao .............................................. | 508 |
| — Watoto waliofariki .................................. | 28 |
| — Watoto waliobaki mwishoni ..................... | 996 |

Mwaka 1987 idadi ya watoto waliopokelewa mikoani imeongezeka kuliko mwaka 1986 ambapo watoto 497 wapya walipokelewa. Vile vile kwa upande mwingine watoto wengi walitoka mikoani ukilinganisha na mwaka uliotangulia ambapo watoto 411 walitoka. Pia mwaka jana vifo vilipungua. Mwaka 1986 watoto 40 walifariki ukilinganisha na 28 waliofariki mwaka 1987.

**Baraza la Usuluhishi wa Ndoa la Kamishna wa Ustawi wa Jamii:**

28. Baraza la usuluhishi wa ndoa liliendelea na kazi za kusikiliza matatizo ya familia kwa kipindi cha mwaka 1987. Mashauri 70 yalipokelewa katika Baraza katika kipindi kinachotaarifiwa. Kati ya hayo, 36 yalipelekwa Mahakamani kwa uamuzi wa kisheria. Shauri moja (1) lilisuluhishwa na kumalizika. Hadi mwishoni mwa mwaka mashauri 33 yalibaki yanaendelea kutafutiwa ufumbuzi.

**Huduma za vituo vya kulelea watoto wadogo mchana:**

29. Huduma kwa vituo vya kulelea watoto mchana iliendelea kutolewa kwa watoto kote nchini chini ya ushauri na usimamizi wa Idara ya Ustawi wa Jamii. Kumekuwepo na ongezeko la vituo vipya 346 mwaka jana ukilinganisha na vituo 201 katika kipindi kama hiki mwaka 1986. Huduma hii iliendelea kuathiriwa na tatizo la usafiri kwa ajili ya kufuatilia shughuli za vituo. Mikoa mingi haina usafiri wa kuaminika kutokana na ubovu wa magari na mengineyo kuchakaa na kutoweza kuhudumiwa.

Hapa chini ni mchanganuo wa vituo:

| | |
|---|---|
| — Vituo mwanzoni mwa mwaka | 1,722 |
| — Vituo vipya | 346 |
| — Jumla ya vituo | 2,068 |
| — Vituo vilivyofungwa | 214 |
| — Vituo vilivyoandikishwa | 26 |
| — Vituo visivyoandikishwa | 1,854 |
| — Vituo vilivyobaki mwishoni | 1,854 |

## 12. MAENDELEO VIJIJINI

1. Maendeleo vijijini yametiliwa mkazo na mipango ya awali kwa kutoa msukumo maalum kwa sehemu za vijijini kwa lengo la kupambana na umaskini na kuinua hali ya maisha ya wananchi, ambao wengi wanaishi vijijini. Maelezo ya mambo mbali mbali yaliyofanywa mwaka uliopita kuhusiana na jambo hili yametolewa katika sehemu za sura hii zilizotangulia. Sehemu hii inatoa maelezo ya utekelezaji wa vyombo vingine ambavyo kwa sehemu kubwa vinahusika pia na maendelo vijijini kama halmashauri za wilaya na vyama vya ushirika.

**Mikoa na Halmashauri za Wilaya:**

2. Katika mwaka 1987/88, Mipango ya Mikoa na Halmashauri za Wilaya iliendelea kutilia umuhimu katika kuendeleza miradi mbali mbali kama vile barabara vijijini, maji, elimu na afya inayolenga kutoa huduma muhimu kwa wanavijiji kwa lengo la kuwezesha shughuli za uzalishaji mali vijijini. Serikali kuu ilitoa wataalamu na zana kwa mikoa na Halmashauri za Wilaya.

3. Hadi kufikia Desemba 1987, kulikuwa na shule za msingi 9,603 vijijini kati ya shule 10,280 zilizokuwepo nchini. Idadi ya vituo vya afya vijijini imefikia 260 kwa kulinganisha na vituo 24 mijini. Kwa kulinganisha uwiano kati ya miji na vijiji, vituo vya afya vijijini vilihudumia wastani wa watu 68,322 kwa kila kituo na vile vya mijini vilihudumia wastani wa watu 201,500 kwa kila kituo.

4. Juhudi za kuimarisha Halmashauri za Wilaya ili ziwe vyombo madhubuti vya kuleta maendeleo vijijini ziliendela kutekelezwa. Juhudi hizo zilikuwa ni pamoja na kuajiri wafanyakazi wenye ujuzi na kutoa mafunzo kwa wafanyakazi waliopo.

5. Mchango wa wanavijijini katika kutekeleza miradi kwa mpango wa kujenga taifa iliendelea kuhimizwa. Wananchi walishiriki katika ujenzi na matengenezo ya barabara za vijiji, madarasa na nyumba za walimu, zahanati na miradi ya maji.

**Maendeleo ya Ushirika:**

6. Hadi kufikia Machi 1988, Vyama Vikuu vya Ushirika vipatavyo 25 vilikuwa vimeandikishwa ikilinganishwa na vyama 23 mwaka 1986. Vyama vya msingi vya ushirika vijijini vipatavyo 3,832 vilikuwa vimeandikishwa ilipofika Machi 1988, pamoja na vyama vingine vya ushirika 2,680 vikiwemo vyama vya maduka, viwanda, mikopo na kadhalika. Vyama vya msingi vya ushirika vijijini vilikuwa 1,946 na vyama vingine vilikuwa 2,451 katika mwaka 1986.

7. Katika mwaka 1987/88 Vyama Vikuu vya ushirika vilinunua jumla ya tani 800,707.55 za mazao ya aina mbali mbali yenye thamani ya Sh. 14, 284.8 milioni. Vyama hivi viliweza kununua mazao kwa kutumia mikopo ya muda mfupi (overdraft) kutoka Benki ya Taifa ya Biashara na Benki ya Ushirika na Maendeleo Vijijini. Pamoja na shughuli za ununuzi wa mazao ya wakulima vijijini, Vyama Vikuu vya ushirika viliendesha pia shughuli za usindikaji wa mazao, usafirishaji na usambazaji wa pembejeo. Hata hivyo, matatizo mbali mbali yaliendelea kukumba Vyama Vikuu vya Ushirika, yakiwemo.

(i) Uhaba wa wafanyakazia wenye ujuzi;
(ii) Mikopo iliyotolewa na mabenki haikutosheleza mahitaji kwa ajili ya ununuzi wa mazao kutoka kwa wakulima. Aidba mikopo haikutolewa mapema jambo ambalo lilisababisha ucheleweshaji wa malipo kwa wakulima;
(iii) Uhaba wa maghala ya kuhifadhi mazao na kusababisha mazao kulundikana katika vijiji;
(iv) Uchakavu wa vinu vya kuchambulia baadhi ya mazao hasa pamba ulisababisha zao hilo kukaa kwa muda mrefu vijijini au kwenye magulio bila kuchambuliwa katika muda unaotakiwa;
(v) Uhaba wa vyombo vya usafiri kutoka sehemu za uzalishaji hadi sehemu za wanunuzi na walaji.

8. Katika mwaka 1987/88, Benki ya Ushirika na Maendeleo Vijijini ilipokea maombi ya mikopo kutoka vyombo mbali mbali vikiwemo Vyama Vikuu vya Ushirika ya jumla ya Sh. 2,753.8 milioni. Fedha zilizotolewa na Benki hiyo kwa Vyama vya Ushirika ni Sh. 1,660.●

milioni ambazo zilikuwa ni asilimia 60 ya mikopo iliyoombwa. Tatizo kubwa lililoendelea kukabili utoaji mikopo ya Benki ya Ushirika na Maendeleo Vijijini ni kutolipwa madeni kwa wakati kutoka kwa wateja wake hasa vijiji na vyama vya ushirika.

**Ushirikishaji Wananchi katika Mipango ya Maendeleo:**

9. Katika mpango wa mwaka 1987/88 wananchi waliendelea kushirikishwa katika kutekeleza mipango yao ya maendeleo vijijini hasa katika maeneo yafuatayo:—

(i) Matumizi ya nishati hasa itokanayo na misitu ikiwa ni pamoja na kuelimisha wananchi juu ya athari za kutumia ovyo misitu na juhudi za kupanda miti na kutunza misitu.
(ii) Afya ya msingi, lishe, elimu na maendeleo ya jamii kwa jumla.
(iii) Uendelezaji wa utoaji huduma za maji vijijini.
(iv) Utengenezaji barabara vijijini.

10. Uzoefu unaonyesha kwamba kazi ya kuwashirikisha wananchi inaweza kufanyika kwa ufanisi zaidi pakiwepo taratibu maalum zinazojumuisha:—

(a) Vikundi vya vijana na vile vya wanawake;
(b) Vyama vya hisani (charity organisations);
(c) Makundi yaliyoungana kwa lengo la kutatua matatizo fulani;
(d) Vikundi vya dini, huduma mbali mbali na utamaduni;
(e) Vikundi vya mabingwa ambao wamefanya utafiti katika sehemu hiyo.

Ipo mifano mingi ya miradi iliyotekelezwa kwa njia ya kujitolea, lakini ikilinganishwa na uwezo uliopo, juhudi hizo bado ni ndogo na zinaweza kuongezeka ikiwa taratibu nzuri za kutumia nguvu za wananchi zitaandaliwa na kufuatwa.

8— 86